# Mwongozo wa Kanisa la Waadventista wa Sabato

Mafungu yote yaliyonukuliwa kwa ruhusa kutoka katika
Biblia ya Kiswahili
Union Version 1952 (Ilishahihishwa 1989)

ISBN 978

Haki miliki © 2013
Haki zote zimeifadhiwa hakuna ruhusa ya kunukuu au
kupiga picha bila ruhusa ya wachapaji
Tanzania Adventist Press

# Yaliyomo

**Dibaji ya Toleo la Kiswahili la Mwongozo wa Kanisa (2013) . .9**
Mashemasi wa Kike Kuwekewa Mikono . . . . . . . . . . . . 11

**Kwa nini Kuwe na Mwongozo wa Kanisa?. . . . . . . . . . . . . . . . 12**
Mamlaka na Kazi ya Mwongozo wa Kanisa. . . . . . . . . . . . 14
Kufanya Mabadiliko. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 14
Mahali pa Kupata Ushauri. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16
Istilahi Zilizotumika katika Mwongozo huu wa Kanisa . . . . 16

**Kanisa la Mungu Aliye Hai . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18**
Hakuna Kiambaza Kinachotutenga. . . . . . . . . . . . . . . . . . 18
Kitu Ambacho Kristo Anakijali Kuliko Vyote. . . . . . . . 19
Kamili katika Kristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 20

**Muundo na Mamlaka. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 22**
Msingi wa Kibiblia wa Kuwa na Muundo. . . . . . . . . . . . 22
Umuhimu wa Muundo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23
Makusudi ya Kuwa na Muundo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 24
Mfano wa Agano Jipya. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 24
Muundo wa Sasa wa Kanisa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25
Ngazi za Muundo wa Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 26
Wajibu wa Taasisi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27
Mamlaka katika Kanisa la Awali. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 28
Konferensi Kuu ni Mamlaka ya Juu Kuliko Zote. . . . . . . . 28

**Wachungaji na Watumishi Wengine wa Kanisa . . . . . . . . . . . .30**
Kazi Aliyoagiza Mungu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 30
Vitambulisho na Leseni. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 34

**Kuunda, Kuunganisha na Kuvunja Makanisa na Makundi . .36**
Kuunda Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 36
Kuunda Kundi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 38
Kuunganisha Makanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 39
Kuvunja au Kuondoa Makanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 40
Utunzaji wa Washiriki, Nyaraka, na Pesa. . . . . . . . . . . . . 42

**Ushirika** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **44**
Ubatizo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 44
Kiapo na Ahadi ya Ubatizo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . 46
Kiapo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 46
Kiapo Mbadala. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 48
Ahadi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 49
Kubatizwa Tena. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 51
Kukiri Imani. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 53
Kuhamisha Washiriki. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 54

**Marudi ya Kanisa** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **59**
Kanuni Kuu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 59
Sababu za Marudi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 66
Utaratibu wa Marudi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 66

**Maofisa na Idara za Kanisa Mahalia** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **73**
Sifa kuu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73
Muda wa Uongozi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 77
Wazee. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 78
Mashemasi wa Kiume. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 83
Mashemasi wa Kike. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 86
Karani. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 87
Mhazini. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 89
Mratibu wa Waliovutiwa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . 93
Idara na Taasisi Zingine. . . . . . . . . . . . . . . . . . . 93
Huduma za Watoto. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 94
Mawasiliano. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 95
Huduma za Familia. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 100
Huduma za Afya. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 101
Muziki. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 103
Mambo ya Jamii na Uhuru wa Kidini. . . . . . . . . . . 103
Huduma za Uchapishaji. . . . . . . . . . . . .. . . . . . . 104
Shule ya Sabato na Huduma binafsi. . . . .. . . . . . . 105
Shule ya Sabato. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 105
Huduma Binafsi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 109
Huduma za Uwakili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 111
Huduma za Wanawake. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 112

Huduma za Vijana. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 113
Kuwekwa Wakfu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 119

**Uchaguzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 120**
Kamati ya mapendekezo na Mchakato wa Uchaguzi . . . . . 120
Wajumbe wa Mkutano wa Mkuu wa Konferensi. .. . . . 124

**Huduma na Mikutano Mingine . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 127**
Kanuni za Msingi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 127
Nafasi ya Muziki Katika Ibada. . . . . . . . . . . . . . . . . 129
Mimbari si Jukwaa la Malumbano. . . .. . . . . . . . . . . 129
Umuhimu wa Kudumisha Umoja. . . . . . . . . . . . . . . . 131
Shule ya Sabato na Huduma za Ibada. . . . . . . . . . . . 132
Huduma ya Ushirika Mtakatifu. . . . . . . . . . . .. . . . . 135
Mkutano wa Maombi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 140
Mkutano Mkuu wa Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 141
Baraza la Kanisa na Mikutano Yake. . . . . . . . . . . . . 142
Mikutano ya Bodi ya Shule. . . . . . . . . . . . . . . . . . . 145
Mikutano ya Chama cha Kaya na Shule. . . . . . . . . . . 145
Mikutano ya Vijana. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 145

**Fedha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 148**
Uwakili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .149
Zaka. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 150
Sadaka. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .151
Ushauri wa Jumla wa Kifedha. . . . . . . . . . . . . . . . . 153

**Viwango vya Maisha ya Kikristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 156**
Wito Mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. . . . . . . . . . 156
Usomaji wa Biblia na Maombi. . . . . . . . . . . . . . . .157
Uhusiano katika Jamii. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 158
Ushikaji wa Sabato. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 158
Kicho Mahali pa Ibada. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 160
Afya na Kiasi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 160
Mavazi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 161
Usahili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 163
Vyombo vya Habari vya Kisasa. . . . . . . . . . . . . . . . 163

Starehe na Burudani. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 164
Muziki. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 165
Hitimisho. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 166

**Ndoa, Kuachana na Kuoa/Kuolewa Tena . . . . . . . . . . . . . . . .167**
Uhusiano wa Kijamii. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 167
Uangalizi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 169
Uchumba. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 169
Ndoa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 171
Kuachana. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 174
Msimamo wa Kanisa juu ya Kuachana na Kuoa/Kuolewa Tena. 175
Huduma ya Kanisa Mahalia kwa Familia. . . . . . . . . 178

**Imani za Msingi za Waadventista wa Sabato . . . . . . . . . . . . 180**
1. *Maandiko Matakatifu*. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . *180*
3. *Baba*. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . *181*
4. Mwana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 181
5. Roho Mtakatifu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 181
6. Uumbaji. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 182
7. Silika ya Mwanadamu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 182
8. Pambano Kuu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 183
9. Maisha, Kifo na Ufufuo wa Kristo. . . . . . . . . . . . . 183
10. Kupata Wokovu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 184
11. Kukua katika Kristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 184
12. Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 185
13. Waliosalia na Utume Wao. . . . . . . . . . . . . . . . . . . 185
14. Umoja katika Mwili wa Kristo. . . . . . .. . . . . . . . 186
15. Ubatizo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 186
16. Meza ya Bwana. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 187
17. Karama za Roho na Huduma. . . . . . . . . . . . . . . . . 187
18. Karama ya Unabii. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 188
19. Sheria ya Mungu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 188
20. Sabato. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 188
21. Uwakili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 189
22. Mwenendo wa Kikristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 189
23. Ndoa na Familia. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 190
24. Huduma ya Kristo Patakatifu pa Mbinguni. . . . . . 190

25. Ujio wa Pili wa Kristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 191
26. Kifo na Ufufuo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 192
27. Milenia na Mwisho wa Dhambi. . . . . . .. . . . . . . . 192
28. Nchi Mpya. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 192
Maelezo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 192
Maelezo ya SURA YA 8. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 193
Maelezo ya SURA YA 9. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 198
Maelezo ya SURA YA 11. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 206
Makadirio ya Matimizi-. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 207

**Nyongeza ya Iliyokuwa Divisheni ya Mashariki mwa Afrika 209**
**Nyongeza ya Iliyokuwa Divisheni ya Mashariki Mwa Afrika 210**
Sala ya Baraka. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 215
Viongozi wa Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 218
Ugomvi Kati ya Ndugu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 218
Utunzaji wa Pesa za Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 218
Kitabu cha Orodha ya Washiriki . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 219
Vyeti vya Ushirika. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 220
Kuunda Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 220
Huduma ya Kutawadhana Miguu. . . . . . . . . . . . . . . . . . 221
Huduma ya Meza ya Bwana. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 221
Jinsiyakutengenezamkateusiotiwachachu(kwakanisadogo).222
Jinsi ya Kutengeneza Divai Isiyochachuka. . . . . . . . 222
Utunzaji wa Vyombo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 222
Utaratibu wa lbada ya Meza ya Bwana. . . . . . . . . . . 223
Kuketi Wakati wa Kuomba. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 223
Kipindi cha Idara ya Huduma Mahususi. . . . . . . . . . . 224
Mkutano wa Maombi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 224
Kuhamisha Washiriki. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 224
Mikutano ya Makambi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 225
Huduma ya Mazishi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 226
Muundo wa Kanisa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 228
Pesa za Kundi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 229

# Dibaji ya Toleo la Kiswahili la Mwongozo wa Kanisa (2013)

*Mwongozo wa Kanisa* ambao kwa muda mrefu umekuwa ukichapishwa kama 'Kanuni za Kanisa', ulikuwa haujafanyiwa marekebisho kwa muda mrefu na hasa kwa kuzingatia ukuaji wa lugha ya Kiswahili ongezeko kubwa la istilahi ambao zinafaa zaidi kutafsiri maneno ambayo hapo mwanzo ilikuwa vigumu kuyatafsiri. Lakini pia *mwongozo wa Kanisa* umekuwa ukifanyiwa marekebisho kadhaa wakati wa vikao vya Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato, lakini baadhi ya marekebisho hayo hayakuingizwa ipasavyo katika tafsiri ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, toleo hili la *Mwongozo wa Kanisa* kwa lugha ya Kiswahili, limezingatia matumizi sahihi ya lugha na istilahi za Kiswahili na kuingiza marekebisho yote kama yalivyochapishwa katika toleo la Kiingereza la mwaka 2010.

Kwa hiyo watumiaji wa *mwongozo* huu wataona kuwa maneno au istilahi zilizokuwa zimezoeleka zimeachwa kwa sababu zilizoelezwa hapo juu. Mifano michache ya mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo.

1. Kitabu hiki chenye maelekezo ya uendeshaji wa kanisa mahalia kimezoeleka kuitwa 'Kanuni za Kanisa', lakini kusema kweli hii si tafsiri sahihi ya 'Church Manual', 'manual ni *'mwongozo'* na kwa hiyo tafsiri sahihi ya jina la kitabu hiki ni *Mwongozo wa Kanisa*. Kwa sababu ya mazoea ya muda mrefu na ili watu wasidhani kuwa hiki ni kitabu tofauti, majina yote mawili yamewekwa katika katika jalada la mwongozo huu. Lakini kwa ndani maneno 'kanuni za kanisa' yameachwa kabisa na badala yake kila mahali maneno *'mwongozo wa kanisa'* yametumika.

2. Maneno 'misingi ya imani' yameachwa kwa kuwa si tafsiri sahihi ya 'fundamental beliefs'. Maneno ya Kiingereza yanamaanisha imani (beliefs) 28 za msingi na si misingi

(foundations) 28 ya imani. Msingi ni mmoja ambapo juu yake kuna imani 28, yaani mambo 28 ambayo Waadventista wa Sabato wanayaamini. Kwa hiyo, badala ya ‚misingi ya imani', maneno yaliyotumika ni 'imani za msingi'.

3. Mkutano wa washiriki wote wa kanisa mahalia umekuwa ukiitwa halmashauri au mashauri ya kanisa. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* 'halmashauri' ni 'kikundi cha watu maalum walioteuliwa au kuchaguliwa kuelekeza jambo fulani; bodi.' Kwa hiyo si sahihi kuuuita mkutano wa watu wote halmashauri. Kwa hiyo badala ya halmashauri au mashauri ya kanisa, toleo hili linatumia *Mkutano Mkuu wa Kanisa.*

4. Personal ministries imekuwa ikitafsiriwa kama 'huduma za washiriki' lakini tafsiri sahihi ya neno personal ni '–a mtu binafsi'. Kwa hiyo idara ya 'personal ministries' katika toleo hili imeitwa idara ya 'huduma binafsi.'

5. Neno discipline katika Kiingereza lina maana mbili lakini neno nidhamu katika Kiswahili lina maana moja tu ya 'utaratibu mzuri wa kuendesha jambo, adabu, staha', lakini discipline inapomaanisha hatua zinazochukuliwa dhidi ya mtu aliyekosa nidhamu, neno nidhamu haliwezi kutumika. Neno sahihi katika Kiswahili ni 'marudi'. Kwa hiyo, 'marudi' mahali ambapo hatua za kurudi mtu zinazungumziwa. Hali kama hiyo inajitokeza pia kwenye neno divorce. Katika Kiingereza 'divorce' ina maana ya kuachana lakini pia ina maana ya hati inayotolewa kwa walioachana. Katika Kiswahii 'talaka' ni ile hati na tendo la kuachana haiitwi 'talaka', ni 'kuachana'. Kwa hiyo mahali ambapo divorce ina maana ya kuachana, neno 'kuachana' limetumiwa.

Kuna mifano mingi ambayo haiwezi kuorodheshwa yote katika nafasi hii ndogo ya dibaji lakini mifano hii michache imetolewa kuonesha sababu ya mabadiliko ya istilahi na misemo yaliyo katika toleo hili. Ili kuwasaidia watu kuelewa baadhi ya istilahi na maneno magumu, toleo hili lina orodha ya istilahi maneno hayo pamoja na ufafanuzi wake.

**Mashemasi wa Kike Kuwekewa Mikono (tazama uk. )**

Ingawa kuna vifungu katika mwongozo huu vinavyoelekeza kuwekewa mikono kwa mashemasi wa kike (tazama uk, ), Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati haijalipokea jambo hili na kwa sababu hiyo katika divisheni yetu tutaendelea kuwekea mikono mashemasi wa kiume tu. Mashemasi wa kike wataendelea kuhudumu kama walivyokuwa wanafanya siku zote bila kuwekewa mikono.

SURA YA 1

# Kwa nini Kuwe na *Mwongozo wa Kanisa*?

Kwa nini Kanisa la Waadventista wa Sabato lina *Mwongozo wa Kanisa*?

Mungu ni Mungu wa utaratibu kama ilivyodhihirika katika kazi zake za uumbaji na ukombozi. Vivyo hivyo, utaratibu ni sehemu nyeti ya Kanisa lake. Utaratibu hufikiwa kwa njia ya kanuni na taratibu zinazoliongoza Kanisa katika utendaji wake wa ndani na pia katika kutimiza utume wake duniani. Ili liwe jumuiya ya kikanisa yenye mafanikio katika kumtumikia Bwana na wanadamu, kanisa linahitaji utaratibu, kanuni na nidhamu. Maandiko yanasisitiza kwamba "… mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu." (1 Kor. 14:40).

Ellen G. White alitaja mahitaji hayo mwaka 1875: "Kanisa la Kristo liko hatarini wakati wote. Shetani anajaribu kuwaangamiza watu wa Mungu, kwa hiyo, mawazo ya mtu mmoja, maoni ya mtu mmoja, hayawezi kuaminika vya kutosha. Kristo anataka wafuasi wake wakusanyike kama kanisa, wakifuata taratibu, wakiwa na kanuni na nidhamu, na wote wakiwajibika kwa mwingine, huku wakiwachukulia wengine kuwa bora kuliko wao wenyewe."—3T 445.

Lakini viongozi wa Kanisa hawakutoa haraka kitabu cha kanuni kwa ajili ya uendeshaji wa Kanisa, ingawa Konferensi Kuu ilikuwa inakutana kila mwaka katika miaka ya awali ya Kanisa na wajumbe walikuwa wanaamua juu ya masuala ya utaratibu na uhai wa kanisa. Hatimaye, mwaka 1882, Konferensi Kuu iliamua kuandaa "maelekezo kwa viongozi wa kanisa, ili yachapwe katika Review and Herald au kama kitini." -RH, Des. 26, 1882. Jambo hili lilionesha utambuzi uliokuwa unaongezeka kwamba utaratibu

ulikuwa muhimu kama tulikuwa tunataka uendeshaji ufanye kazi kwa ufanisi na kufanana kwa utaratibu kulikuwa kunahitaji misingi hiyo elekezi iwe katika maandishi.

Hata hivyo, pendekezo la kuziweka ibara hizo katika mfumo wa kudumu kama mwongzo wa kanisa lilipoletwa mbele ya Konferensi Kuu ya mwaka 1883, wajumbe walilikataa wazo hilo. Walikuwa wanahofia kuwa jambo hilo lingefanya kanisa kuwa na utaratibu na kuwaondolea wachungaji uhuru wao binafsi wa kushughulikia masuala ya utaratibu kama waonavyo.

Lakini hofu hiyo—ambayo bila shaka ilikuwa inaakisi upinzani uliokuwepo miaka ishirini kabla dhidi ya muundo wa aina yo yote—ilianza kutoweka. Mikutano ya kila mwaka ya Konferensi Kuu iliendelea kushughulikia masuala ya utaratibu.

Ingawa kanisa lilikuwa limekataa rasmi kuwa na mwongozo, mara kwa mara viongozi walikuwa wanazikusanya na kuziweka katika mfumo wa kitabu au kijitabu, kanuni za uhai wa kanisa zilizokuwa zimekubalika . Pengine kilichokuwa kinavutia zaidi ni kitabu cha kurasa 184 kilichochapishwa mwaka 1907 na mwasisi wa kanisa J. N. Loughborough, kiitwacho *"The Church, Its Organization, Order and Discipline,"* kilichokuwa kinahusu masuala mengi yaliyo katika *mwongozo huu*.

Kanisa lilipokuwa linakua kwa kasi ulimwenguni kote mwanzoni mwa karne ya ishirini, lilizidi kutambua hitaji la kuwa na mwongozo kwa ajili ya kutumiwa na wachungaji na washiriki wake walei ulimwenguni kote. Mwaka 1931 Kamati ya Konferensi Kuu iliamua kuchapisha mwongozo wa kanisa. J. L. McElhany, ambaye baadaye alikuwa mwenyekiti wa Konferensi Kuu, aliandaa muswada, ambao ulichapishwa mwaka 1932.

Sentensi ya kwanza ya utangulizi wa toleo hilo la kwanza ilikuwa inasema, "imedhihirika zaidi kwamba unahitajika mwongozo wa uendeshaji wa kanisa ili kuelezea na kuhifadhi desturi na taratibu za dhehebu letu."

Zingatia neno *kuhifadhi*. Hili halikuwa jaribio la kuunda na kushinikiza haraka utaratibu mzima wa utawala kanisani. Bali ilikuwa juhudi ya kwanza ya *kuhifadhi* uamuzi wote mzuri uliokuwa unafanyika katika miaka yote na kisha

kuongeza kanuni zinazohitajika kwa ajili ya ukuaji na uchangamano wa Kanisa uliokuwa unaongezeka

## Mamlaka na Kazi ya *Mwongozo wa Kanisa*

*Mwongozo wa Kanisa* umekuwa katika mfumo wa sasa tangu mwaka 1932. Unaelezea shughuli na kazi za makanisa mahalia na uhusiano wa makanisa hayo na ngazi zingine za Kanisa ambako yana ushirika. Vilevile, *Mwongozo wa Kanisa* unaelezea jinsi Kanisa linavyoyaelewa maisha ya Kikristo na uendeshaji na nidhamu ya Kanisa kwa kufuata kanuni za Biblia na mamlaka ya Mikutano rasmi ya Konferensi Kuu. "Mungu ameagiza kwamba, wawakilishi wa kanisa lake kutoka pande zote za dunia, wakikutana katika Konferensi Kuu, watakuwa na mamlaka."—9T 261.

*Mwongozo wa Kanisa* umegawanyika katika sehemu mbili. Yaliyomo katika kila sura ni kwa ajili ya kila taasisi ya kanisa, kanisa mahalia, na kila mshiriki. Kwa kutambua haja ya kuwa na tofauti katika sehemu kadhaa, maelezo ya nyongeza, yaliyotolewa kama mwongozo na vielelezo, yapo mwishoni mwa *Mwongozo* huu *wa Kanisa*. Maelezo haya yana na vichwa vidogo vinavyokwenda sambamba na vichwa vidogo vya sura na kurasa za matini ya msingi.

Viwango na desturi za Kanisa zimejengwa katika kanuni za Maandiko Matakatifu. Kanuni hizi, zinazosisitizwa na Roho ya Unabii, zimeelezewa katika *Mwongozo* huu *wa Kanisa.* Hazina budi kufuatwa katika masuala yote yanayohusu utawala na uendeshaji wa makanisa mahalia. *Mwongozo wa Kanisa* pia unafafanua uhusiano kati ya kanisa mahalia na konferensi mahalia au vyombo vingine katika muundo wa dhehebu la Waadventista wa Sabato. Hairuhusiwi kujaribu kuweka viwango vya ushirika au kujaribu kutunga au kutumia, kanuni na taratibu kwa ajili ya uendeshaji wa kanisa mahalia zilizo kinyume na uamuzi huu uliopitishwa katika kikao cha Konferensi Kuu na ambao umeelezewa katika *Mwongozo* huu *wa Kanisa*.

## Kufanya Mabadiliko

Kwa miaka mingi Konferensi Kuu imekuwa ikipitisha mabadiliko muhimu katika *Mwongozo wa Kanisa*. Kwa kutambua

umuhimu wa kuendesha kazi ya Kanisa ulimwenguni kote *"kwa uzuri na kwa utaratibu,"* katika kikao chake cha mwaka 1946, Konferensi Kuu iliamua kwamba "mabadiliko na masahihisho ya sera yatakayofanyika katika *Mwongozo* huu yataidhinishwa na kikao cha Konferensi Kuu." *General Conference Report,* No. 8 uk.197 (Juni 14, 1946).

Kwa kutambua kuwa wakati mwingine hali ya sehemu fulani huhitaji uamuzi maalum, mwaka 1948 Kamati ya Konferensi Kuu iliamua kwamba "kila divisheni duniani, ikiwemo Divisheni ya Kaskazini mwa Amerika, iandae 'Nyongeza' ya *Mwongozo* mpya *wa Kanisa* bila kuubadilisha kwa namna yo yote ile bali uwe na nyongeza inayohusu hali iliyopo katika divisheni husika; rasimu za nyongeza hizo hazina budi kuwasilishwa katika Kamati ya Konferensi Kuu ili zipitishwe. – *Autumn Council Actions,* 1948, uk. 19.

Kikao cha Konferensi Kuu cha mwaka 2000, kiliidhinisha kuainishwa upya kwa baadhi ya maelezo yaliyo katika *Mwongozo wa Kanisa*, na kuyaweka katika sehemu ya Maelezo kama maelekezo na mifano badala ya kuwa mambo ya lazima; pia kiliidhinisha mchakato wa kufanya mabadiliko. Mabadiliko katika *Mwongozo wa Kanisa,* isipokuwa katika sehemu ya maelezo na mabadiliko yatokanayo na uhariri, yanaweza kufanywa kwa uamuzi wa kikao cha Konferensi Kuu tu, ambapo wajumbe wa kanisa la ulimwengu wanaweza kutoa maoni na kupiga kura. Kama kanisa mahalia, konferensi, misheni ya konferensi/union inataka kupendekeza marekebisho ya *Mwongozo wa Kanisa*, haina budi kuwasilisha pendekezo lake kwa ngazi inayofuata kwa ajili ya ushauri na uchunguzi. Kama ngazi hiyo italipitisha pendekezo hilo, itawasilisha mabadiliko yaliyopendekezwa kwa ngazi inayofuata kwa ajili ya tathmini zaidi. Kama ngazi mbalimbali zitalipitisha pendekezo hilo, hatimaye litafika kwenye Kamati ya *Mwongozo wa Kanisa* ya Konferensi Kuu, ambayo huyachunguza mapendekezo yote. Kama Kamati ya *Mwongozo wa Kanisa* itayapitisha mabadiliko hayo, itayaandaa kwa ajili ya kuyawasilisha kwenye Baraza la Mwaka na/au kikao rasmi cha Konferensi Kuu.

Mabadiliko ya maelezo hufuata utaratibu huo huo. Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu inaweza kupitisha mabadiliko ya maelezo katika Kikao cho chote cha Baraza la Mwaka.

Kamati ya *Mwongozo wa Kanisa* itawasilisha taarifa ya mabadiliko yaliyopendekezwa, yatokanayo na uhariri, ambayo hayabadili maana katika *Mwongozo wa Kanisa*, kwenye Baraza la Mwaka la Kamati Kuu ya Utendaji ya Konferensi Kuu, ambalo linaweza kuyaidhinisha. Hata hivyo, Baraza la Mwaka likiamua kwa theluthi moja ya kura, kuwa badiliko hilo la kiuhariri limebadili maana ya ibara husika, basi badiliko hilo lililopendekezwa litapelekwa kwenye kikao cha Konferensi Kuu.

Katika Baraza la Mwaka wa mwisho wa kipindi cha miaka mitano, Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu itapitia mabadiliko yote katika maelezo na kuoanisha mabadiliko hayo na marekebisho yo yote yanayoweza kuwa yamependekezwa katika sehemu ya msingi ya *Mwongozo wa Kanisa.*

Toleo jipya la *Mwongozo wa Kanisa* huchapishwa kila baada ya kikao cha Konferensi Kuu. Toleo jipya kuliko yote halina budi kutumika kila wakati. Toleo hili lina marekebisho yaliyofanywa kwenye kikao cha Konferensi Kuu cha mwaka 2010.

**Mahali pa Kupata Ushauri**

Maofisa wa kanisa na viongozi, wachungaji, na washiriki hawana budi kuwasiliana na konferensi zao kwa ajili ya ushauri juu ya uendeshaji wa makanisa yao au masuala yanayotokana na *Mwongozo* huu *wa Kanisa*. Kama hawatakubaliana, itabidi wawasiliane na misheni/konferensi ya union kwa ajili ya ufafanuzi.

**Istilahi Zilizotumika katika *Mwongozo* huu *wa Kanisa***

*Kanisa*—Kwa sababu za kiuhariri na kiuchapaji, neno "Kanisa," linapoanza na "K" kubwa katika kitabu hiki, litakuwa limetumika badala ya jina kamili la "Kanisa la Waadventista wa Sabato" na litamaanisha muundo mzima wa Kanisa na si kanisa mahalia au kundi, isipokuwa linapotumika katika dondoo.

*Konferensi, misheni, seksheni, ujumbe, field, umoja wa makanisa* – Kwa sababu za kiuhariri na kiuchapaji, katika kitabu hiki "konferensi" inamaanisha "konferensi, misheni, field, seksheni, ujumbe, au umoja wa makanisa," kulingana na muktadha

wa kiutawala. Kwa ujumla, kila kanisa ni sehemu ya jumuiya ya makanisa ijulikanayo kama konferensi, lakini kabla jumuiya hiyo haijawa na hadhi ya konferensi, kulingana na Sera ya Uendeshaji ya Konferensi Kuu, inaweza kuitwa misheni, seksheni, ujumbe, au field. Katika baadhi ya divisheni ulimwenguni, jumuiya za makanisa katika nchi fulani hufanya kazi kama konferensi kwa shughuli za makanisa mahalia na kama union kwa shughuli zingine za kimuundo wa Kanisa. (Tazama Sura ya 3, "Muundo na Mamlaka.")

*Mchungaji*—Wachungaji wanaotajwa ndani ya kanuni hii ni wale walioteuliwa na konferensi kusimamia mambo ya kanisa mahalia au mtaa.

*Vifupisho* vya vitabu vya Ellen G. White vimeelezewa katika uk. 179.

Madondoo ya Maandiko yanatoka katika Biblia ya Kiswahili, Toleo la Union isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

SURA 2

# Kanisa la Mungu Aliye Hai

Maandiko hutumia usemi kama “kanisa lake Mungu” (Mdo. 20:28), “mwili wa Kristo” (Efe. 4:12), “kanisa la Mungu aliye hai” (1 Tim. 3:15).

Kuwa sehemu ya kanisa la Mungu ni fursa ya pekee na ya kuridhisha moyo. Kusudi la Mungu ni kukusanya watu kutoka pande za mbali za dunia ili kuwaunganisha katika mwili mmoja, yaani mwili wa Kristo, ambapo yeye ni kichwa kilicho hai. Wote walio watoto wa Mungu katika Kristo Yesu ni viungo vya mwili huu, na katika uhusiano huo wanaweza kunufaika na ushirika kati yao, na kuwa na ushirika na Bwana wao pia.

Biblia imetumia neno “kanisa” kwa namna zisizopungua mbili: kwa maana ya jumla likimaanisha kanisa ulimwenguni kote (Mat. 16:18; 1 Kor.12:28), na pia kwa maana mahususi likimaanisha kanisa katika mji au jimbo, kama vile kwa wote walioko Rumi (Rum. 1:6, 7), Korintho (1 Kor. 1:2), na Thesalonike (1 Thes. 1: 1), na Galatia (1 Kor. 16:1), Asia (1 Kor. 16:19), na Shamu na Kilikia (Mdo. 15:41).

Kristo, akiwa kichwa cha kanisa na Bwana wake aliye hai, ana upendo mkubwa kwa viungo vya mwili wake. Inampasa kutukuzwa katika kanisa (Efe. 3:21); ataidhihirisha “hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi” (Efe. 3: 10) kwa njia ya kanisa. Yeye hulilisha na kulistawisha kanisa lake siku kwa siku (Efe. 5:29), na shauku yake ni kulifanya liwe “kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi, wala lolote kama hilo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa” (Efe. 5:27).

### Hakuna Kiambaza Kinachotutenga

Kristo alijitahidi, kwa mafundisho na mfano, kufundisha ukweli kwamba kwa Mungu haikupasa kuwe na kiambaza kati ya Israeli na mataifa mengine (Yn. 4:4-42; 10:16; Lk. 9:51-56; Mat. 15: 21-28). Mtume Paulo aliandika, “Mataifa ni warithi pamoja nasi wa urithi mmoja, na wa mwili mmoja na washiriki pamoja nasi wa

ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya injili" (Efe. 3:6).

Wala haipasi kuwa na upendeleo wa tabaka au taifa au jamii au rangi, miongoni mwa wafuasi wa Kristo, kwani wote ni wa damu moja. Wateule wa Mungu, jamii ya ulimwengu mzima, jamii mpya ya wanadamu, wote wamekuwa "mmoja katika Kristo Yesu" (Gal. 3:28).

"Kristo alikuja katika dunia hii akiwa na ujumbe wa rehema na msamaha. Aliweka msingi wa dini ambapo Wayahudi na Watu wa Mataifa, weusi na weupe, walio huru na watumwa, wameunganishwa katika udugu wa pamoja, wakitambuliwa kuwa wako sawa machoni pa Mungu. Mwokozi ana upendo usio na kikomo kwa kila mwanadamu."—7T 225.

"Hakuna tofauti inayotambuliwa na Mungu kwa sababu ya utaifa, rangi, au tabaka. Yeye ndiye Mwumbaji wa wanadamu wote. Wanadamu wote ni wa familia moja kutokana na kuumbwa, na wote ni wamoja kwa njia ya ukombozi. Kristo alikuja kubomoa kila kiambaza kinachotutenga, kuzifungua hema zote za hekalu, ili kila mtu aweze kumfikia Mungu. ... Katika Kristo hakuna Myahudi wala Myunani, hakuna mtumwa wala aliye huru. Wote huvutwa kwa damu yake ya thamani." — COL 386.

**Kitu Ambacho Kristo Anakijali Kuliko Vyote**

Wale walio katika kazi ya Kristo, walioitwa kuwa viongozi, inawapasa "kulitunza kanisa" (1 Tim. 3:5); inawapasa "kulilisha kanisa lake Mungu" (Mdo. 20:28); na kuwa na "maangalizi ya makanisa yote" (2 Kor. 11:28).

"Nawashuhudia ndugu zangu kwamba kanisa la Kristo, japo ni dhaifu na lenye kasoro sana, ni kitu pekee anachokiangalia sana. Anapoita ulimwengu wote uje, kwake upate kuokolewa, huwatuma malaika zake kutoa msaada wa kimbingu kwa kila ajaye kwake kwa toba na majuto, na yeye mwenyewe huja katika kanisa lake kwa njia ya Roho Mtakatifu."—TM 15.

Kama bibi arusi wa Kristo na kitu anachokijali kuliko vyote, kanisa linatarajiwa kuonesha utaratibu na tabia ya yule aliye Mungu katika shughuli zake zote.

"Katika kipindi hiki inalipasa kanisa kuvaa mavazi yake ya

kupendeza—'Kristo aliye haki yetu.' Kuna tofauti za makusudi zilizo wazi ambazo hazina budi kurejeshwa na kuoneshwa kwa ulimwengu katika kuziinua amri za Mungu na imani ya Yesu. Uzuri wa utakatifu hauna budi kuonekana katika mng'ao wake wa asili, tofauti na uharibifu na giza la wasiotii, walioiasi sheria ya Mungu. Kwa hiyo tunamkiri Mungu, na kuitambua sheria yake, ambayo ni msingi wa utawala wake kule mbinguni na katika himaya zake zote duniani. Mamlaka yake inapasa kuwekwa wazi na bayana mbele ya ulimwengu, na sheria zote zinazopingana na sheria za Yehova hazipasi kukubalika. Ulimwengu ukiruhusiwa kuathiri uamuzi na matendo yetu, tunapokaidi mipango ya Mungu, makusudi ya Mungu yatakuwa yameshindwa. Hata kama sababu itakuwa ya kuvutia sana, kanisa likiyumba katika jambo hili, katika vitabu vya mbinguni litakuwa limeandikiwa ukosefu wa uaminifu juu ya dhamana takatifu kuliko zote ambazo lilikabidhiwa, na udanganyifu mkubwa dhidi ya ufalme wa Kristo. Inalipasa kanisa kushika kwa dhati kanuni zake mbele ya mbingu na falme za ulimwengu; uaminifu usiokoma katika kulinda heshima na utakatifu wa sheria ya Mungu utafanya ionekane na kuheshimiwa hata na ulimwengu, na wengi watamtukuza Baba yetu wa mbinguni kutokana na matendo mema watakayoyaona."—TM 16, 17.

Mtume Petro aliandika, "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu." (1 Pet. 2:9).

## Kamili katika Kristo

"Bwana amelipatia kanisa lake uwezo na baraka, ili liwasilishe kwa ulimwengu taswira ya utoshelevu wake, ili liwe kamili katika yeye, yaani liwe udhihirisho endelevu wa ulimwengu mwingine, ambao ni wa milele, udhihirisho wa sheria ambazo ni bora kuliko sheria za duniani. Inalipasa kanisa lake kuwa hekalu lililojengwa kulingana na mfano wa mbinguni, na malaika ambaye ni msanifu wa majengo ameleta mwanzi wake wa dhahabu kutoka mbinguni, ili kila jiwe lichongwe na kusafishwa lipate kung'aa kama kielelezo cha mbingu kilivyo, likiangaza pande zote miali ya Jua la Haki. ...

“Bwana Yesu anaijaribu mioyo ya wanadamu kwa kuonesha rehema na neema yake nyingi. Anafanya mabadiliko ya ajabu ambayo Shetani, pamoja na kujigamba kwake kuwa mshindi, pamoja na mwungano wake wa uovu ulioungana kupingana na Mungu na sheria za serikali yake, amesimama akiyatazama mabadiliko hayo kama ngome isiyoweza kupenyeka kwa hila na uongo wake. Mabadiliko hayo ni fumbo kwake. Malaika wa Mungu, maserafi na makerubi, waliotumwa kushirikiana na binadamu, wanaangalia kwa mshangao na furaha, kwamba wanadamu walioanguka, ambao hapo awali walikuwa watoto wa ghadhabu, wanajenga tabia zao kutokana na mafunzo ya Kristo ili zifanane na tabia ya Mungu, na wawe wana na binti za Mungu, wafanye sehemu muhimu katika shughuli na raha za mbinguni.

“Kristo ametoa zana za kutosha kwa kanisa lake, kusudi ajipatie utukufu mkubwa kutoka kwa milki yake aliyoikomboa na kuinunua. Kanisa likiwa limepewa haki ya Kristo, ni hazina yake, ambamo utajiri wa rehema yake, upendo wake, neema yake, vitaonekana katika ukamilifu na katika udhihirisho wa mwisho. ...

Katika usafi wao usiochafuliwa, na ukamilifu usio na mawaa, Kristo anawaona watu wake kama ujira wa mateso yake, kudhalilishwa kwake, na upendo wake, na nyongeza ya utukufu wake—Kristo, ambaye ni kitovu kikuu ambapo utukufu wote hutokea. ‘Heri walioalikwa katika karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo.’”—TM 15-19.

Kanisa linafuata kwa uaminifu kanuni za umoja wa kiroho wa kanisa la Kristo zilizotajwa hapo juu. Kutokana na amani na uwezo ambao haki ya Kristo huleta, kanisa limedhamiria kushinda kila kizuizi ambacho dhambi imekiweka kati ya wanadamu.

SURA YA 3

# Muundo na Mamlaka

Muundo wa Kanisa unatokana na kanuni za Mungu. "Msiruhusu mawazo ya mtu ye yote yayumbishe imani yenu kuhusu utaratibu na mwafaka unaopasa kuwemo kanisani. ... Mungu wa mbinguni ni Mungu wa utaratibu, na anataka wafuasi wake wote wawe na sheria na kanuni, na kuhifadhi utaratibu."—5T 274.

## Msingi wa Kibiblia wa Kuwa na Muundo

Mungu alipowaita wana wa Israeli kutoka Misri na kuwachagua kuwa watu wake wa pekee, aliwapatia muundo mzuri wa utawala kwa ajili ya kuongoza mwenendo wao katika masuala ya kiraia na kidini.

"Serikali ya Israeli ilikuwa na muundo mkamilifu kabisa, uliokuwa mzuri katika ukamili na usahili wake. Utaratibu ambao unaonekana wazi katika ukamilifu wa mpangilio wa viumbe vyote vya Mungu ulidhihirishwa katika mfumo wa Waebrania. Mungu alikuwa ndiye kiini cha mamlaka na utawala, mfalme wa Israeli. Musa aliteuliwa na Mungu kuwa kiongozi wao anayeonekana, ili asimamie sheria kwa niaba ya Mungu. Baadaye lilichaguliwa baraza la watu sabini miongoni mwa wazee wa makabila kumsaidia Musa katika mambo ya kawaida katika taifa. Baada ya hapo kulikuwa na makuhani, waliokuwa wakiwasiliana na Mungu hekaluni. Machifu, au wakuu, walikuwa wanasimamia makabila. Chini yao kulikuwa na 'wakuu wa maelfu', na wakuu wa mamia, na wakuu wa hamsini, na wakuu wa makumi' na mwishowe, watumishi ambao wangeweza kupewa kazi maalumu."—PP 374

Kanisa la Agano Jipya lilionesha ukamilifu huo huo katika mpangilio wake. Kristo mwenyewe, aliyeanzisha kanisa, (Mt. 16:18) "amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka" (1 Kor. 12:18). Aliwapatia karama na talanta zinazofaa kwa kazi zilizokuwa zinawakabili, na kuwapanga kama mwili ulio hai, utendao kazi, na yeye mwenyewe akiwa kichwa.

“Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja, vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake” (Rum. 12:4, 5). “Naye [Kristo] ndiye kichwa cha mwili, yaani cha Kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote” (Kol. 1: 18).

“Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule. Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule.” (1 Cor. 12:4, 5) “Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja, vivyo hivyo na Kristo.” (1 Cor. 12:4, 5) “Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha.” (1 Kor. 12: 27, 28).

**Umuhimu wa Muundo**

Kama vile isivyowezekana kuwa na mwili wa mtu ulio hai na ufanyao kazi bila viungo vyake kuungana katika mfumo na kufanya kazi pamoja, haiwezekani kuwa na kanisa hai linalokua na kustawi bila washiriki wake kujipanga katika mwili mmoja wa kiroho, wote wakifanya majukumu na kazi walizopewa na Mungu chini ya uongozi wa mamlaka iliyowekwa na Mungu. Hakuna taasisi au kundi linaloweza kufanikiwa bila ya kuwa na muundo. Bila muundo maalum, hakuna taasisi au harakati itakayoweza kustawi. Taifa lisilokuwa na serikali iliyopangwa litakuwa katika machafuko. Biashara isiyokuwa na mpangilio itaanguka. Kanisa lisilokuwa na muundo litasambaratika na kutoweka.

Kristo alilipatia kanisa lake mfumo wa muundo sahili lakini wenye ufanisi kwa ajili ya maendeleo mema ya kanisa na kwa ajili ya kutimiza kazi yake ya kupeleka injili ya wokovu ulimwenguni kote. Mafanikio ya kanisa katika juhudi zake za kumaliza kazi yake, yanategemea kufuata kielelezo hiki cha Mungu kwa uaminifu.

“Baadhi ya watu wamekuwa wakitoa wazo kuwa kadiri tunavyokaribia mwisho wa wakati, kila mtoto wa Mungu atafanya kazi bila kuwa katika muundo wo wote wa kidini. Lakini

nimeelekezwa na Bwana kuwa katika kazi hii, hakuna suala la kila mtu kufanya kazi peke yake."—TM 489.

"Shetani atafurahi sana akifaulu katika juhudi zake kuingia miongoni mwa watu hawa na kuivuruga kazi katika kipindi ambacho mpangilio makini ni wa lazima na utakuwa nguvu kubwa kabisa ya kuzuia harakati za uongo na kukanusha madai yasiyoungwa mkono na Neno la Mungu! Inatupasa kushikilia msimamo bila kusita, ili mfumo wa muundo na mpangilio uliojengwa kwa hekima na uangalifu mkubwa usiporomoke. Tusije, tukaruhusu makundi yasiyo na utaratibu yanayotaka kuidhibiti kazi wakati huu."—TM 489.

**Makusudi ya Kuwa na Muundo**

"Idadi yetu ilipokuwa inaongezeka, ilionekana wazi kuwa bila muundo wa namna fulani kungekuwa na machafuko makubwa, na kazi isingesonga mbele kwa mafanikio. Muundo ulikuwa wa lazima kwa ajili ya kusaidia kazi ya Mungu, kuanzisha kazi katika maeneo mapya, kulinda makanisa na kazi ya Mungu dhidi ya washiriki wasiofaa, kutunza mali ya kanisa, kuchapisha ukweli katika viwanda vya uchapaji, na kwa ajili ya makusudi mengine mengi."—TM 26.

"Kama washiriki wa kanisa linaloonekana, na wafanyakazi katika shamba la Bwana, inawapasa wote wanaodai kuwa Wakristo hawana budi kufanya kila liwezekanalo kudumisha amani, mwafaka na upendo kanisani. Zingatieni ombi la Kristo: 'Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.' Umoja wa kanisa ni ushuhuda wenye ushawishi kuwa Mungu amemtuma Yesu ulimwenguni kama Mkombozi wa ulimwengu."—5T 619, 620.

**Mfano wa Agano Jipya**

Agizo la Mwokozi kwa kanisa kupeleka injili ulimwenguni kote (Mt. 28:19, 20; Mk. 16:15) halikumaanisha kuhubiri injili tu, bali kuhakikisha ustawi wa wale wanaoupokea ujumbe huo. Jambo

hili lilikuwa ni pamoja na kulichunga na kulipatia kundi mahali pa kuishi, na pia kushughulikia matatizo ya uhusiano. Hali hiyo ilikuwa inahitaji muundo.

Mwanzoni, mitume ndio walikuwa baraza lililokuwa linaongoza shughuli za kanisa likiwa Yerusalemu (Mdo. 6:2; 8:14). Kundi hilo lilipokuwa kubwa kiasi cha uendeshaji wa mambo yake kuwa mgumu, kanisa lilichagua mashemasi kwa ajili ya kusimamia shughuli zake (Mdo. 6:2-4).

Baadaye, makundi mengine yakakua, si Asia tu, bali hata Ulaya, na jambo hili lilihitaji hatua zaidi za muundo. Kule Asia Ndogo, wazee walichaguliwa "katika kila kanisa" (Mdo. 14:23). Kupanuka kwa kazi katika majimbo mbalimbali ya Dola ya Kirumi kulihitaji kuyapangilia makanisa katika kile kinachoweza kuitwa konferensi (Gal. 1:2). Kwa njia hiyo, muundo ukawa unaongezeka hatua kwa hatua katika kanisa la awali. Kadiri kulivyokuwa na mahitaji, Mungu alikuwa anawaelekeza viongozi wa kazi yake kwa namna ambayo, kwa kushauriana na kanisa, walijenga mfumo ambao ulikuwa unalinda maslahi ya kazi.

**Muundo wa Sasa wa Kanisa**

Mfumo wa uongozi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ni wakilishi, unaozingatia kuwa mamlaka yako kwa washiriki na yanadhihirishwa kwa kutumia wawakilishi katika kila ngazi ya muundo, ambapo majukumu ya utendaji hukasimiwa kwa vyombo wakilishi na maofisa kwa ajili ya uendeshaji wa Kanisa katika kila ngazi. Mfumo huu wa utawala unatambua pia kuwa kuwekewa mikono kwa ajili ya huduma kunatambuliwa na Kanisa ulimwenguni kote.

"Kila mshiriki wa kanisa ana haki ya kuchagua maofisa wa kanisa. Kanisa huchagua maofisa wa konferensi. Wajumbe waliochaguliwa na konferensi huchagua maofisa wa union, na wajumbe waliochaguliwa na union huchagua maofisa wa Konferensi Kuu. Kwa utaratibu huu, kila konferensi, kila taasisi, kila kanisa, na kila mtu, hupata haki ya kuchagua watu wanaobeba majukumu makubwa ya Konferensi Kuu, ama moja kwa moja au kwa njia ya wawakilishi."—TM 236, 237.

Mfumo wa kimuundo uliopo katika Kanisa ulitokana na ufahamu wa kiteolojia wa kazi ya Kanisa, ongezeko la washiriki, na kuenea kwa Kanisa kijiografia. Wawakilishi wa konferensi walikutana mwaka 1863 kuunda Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato.

Kuna ngazi mbalimbali katika Kanisa kuanzia muumini mmoja mpaka mahali ambapo kazi ya ulimwengu mzima hupangiliwa. Makundi ya washiriki katika kila ngazi hukutana mara kwa mara katika mikutano rasmi ya kujadili shughuli za kanisa ijulikanayo kama vikao. (Kikao cha kanisa mahalia kwa kawaida huitwa Mkutano Mkuu wa Kanisa.) Katika muundo wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, hakuna ngazi inayoweza kuamua yenyewe iwe daraja gani wala kufanya kazi kana kwamba haiwajibiki kwa familia ya Kanisa iliyo nje ya mipaka yake.

**Ngazi za Muundo wa Kanisa**

1. Kanisa Mahalia—Kundi la washiriki walio katika eneo mahususi lililopewa daraja rasmi kama kanisa na kikao cha konferensi.
2. Konferensi Mahalia—Muungano wa makanisa mahalia, katika eneo mahususi la kijiografia, uliopewa daraja rasmi la konferensi mahalia ya Waadventista wa Sabato kwa uamuzi wa kamati kuu ya divisheni katika kikao cha katikati ya mwaka, mwishoni mwa mwaka, au mkutano wa Baraza la Divisheni, na hatimaye kukubaliwa na kikao cha Union kuwa sehemu ya jumuiya ya konferensi/misheni. (tazama uk. 20.)
3. Umoja wa Makanisa—Ni muungano wa makanisa, yaliyo katika eneo mahususi la kijiografia, ambao umepewa, na kikao cha Konferensi Kuu, daraja rasmi la umoja wa wakanisa ulio na hadhi ya konferensi au misheni.
4. Konferensi/Misheni ya Union—Ni muungano wa konferensi katika eneo mahususi la kijiografia, ambao umepewa daraja rasmi la konferensi/misheni ya union na kikao cha Konferensi Kuu.

5. Konferensi Kuu na Divisheni zake—Konferensi Kuu inawakilisha sauti ya Kanisa ulimwenguni kote. Jumuiya zake zimeelezewa katika katiba yake. Ili kurahisisha shughuli zake ulimwenguni kote, Konferensi Kuu imeweka ofisi za kanda, zinazojulikana kama divisheni za Konferensi Kuu, ambazo zimepewa, na mabaraza ya mwaka ya Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu, wajibu wa kusimamia utawala wa kawaida wa muungano wa makundi ya union na vitengo vingine vya Kanisa katika maeneo mahususi ya kijiografia.
6. Biblia ni msingi na chanzo cha imani na mwenendo; kwa msingi huo, kikao cha Konferensi Kuu katika Mkutano wake Mkuu huwa kinabainisha imani za msingi za Kanisa. Vilevile, kikao cha Konferensi Kuu huidhinisha kuundwa kwa union na kuambatanisha field, hurekebisha *Mwongozo wa Kanisa*, huchagua viongozi wa Konferensi Kuu na wa divisheni, hufanya shughuli nyingine kama zilivyoelezwa kwa ufupi katika Katiba na Sheria Ndogo, na hujadili mambo yaliyowasilishwa na Kamati Kuu. Katikati ya vikao vya Konferensi Kuu, Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu inaruhusiwa na Katiba pamoja na Sheria Ndogo Ndogo, kufanya kazi kwa niaba ya maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, jumuiya za Kanisa duniani kote zinakitambua kikao cha Konferensi Kuu kuwa ndiyo sauti ya Kanisa.

**Wajibu wa Taasisi**

Ngazi mbalimbali za kanisa huwa zinaendesha taasisi anuwai za elimu, afya, uchapishaji na zingine zinazohudumia watu katika jina la Kristo kukidhi mahitaji ya ulimwengu uliojaa fadhaa. Katika teolojia na falsafa ya Waadventista wa Sabato, taasisi hizi tangu zilipoanzishwa zimekuwa nyenzo muhimu katika kutimiza kazi ya kiroho ya Kanisa ya kumhudumia mwanadamu katika ujumla wake na kupeleka injili ulimwenguni.

Hakuna jumuiya au taasisi ya Kanisa itakayobeba jukumu kwa ajili ya dhima, madeni, makosa ya kutenda au kutotenda ya jumuiya

nyingine ya Kanisa eti kwa sababu ya kushirikishwa kwake katika kanisa.

## Mamlaka katika Kanisa la Awali

Kama Mwumbaji, Mkombozi na Mruzuku, Bwana na Mfalme wa viumbe vyote, Mungu pekee ndiye chimbuko la mamlaka ya Kanisa. Alikasimu mamlaka kwa manabii wake na mitume (2 Kor. 10:8). Hivyo, walikuwa wanashika nafasi muhimu sana na ya pekee katika kueneza Neno la Mungu na kulijenga kanisa (Efe. 2:20).

Kanisa la awali lilikuwa linawajibika na usafi wa mafundisho na mwenendo. Wazee (au maaskofu) walikuwa na mamlaka makubwa. Moja kati ya kazi zao kubwa ilikuwa mafunzo ya kawaida ya kichungaji (Mdo. 20:17-28; Ebr. 13:17; 1 Pet. 5:1-3), pamoja na kazi maalum kama vile kufundisha mafundisho sahihi na kubainisha uongo wa wale waliokuwa wanayapinga (1 Tim. 3: 1, 2; Tit. 1:5,9). Waliambiwa hivi "zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu" (1 Yoh. 4:1) au, kwa usemi wa Paulo, "jaribuni mambo yote" na "lishikeni lililo jema" (1 The.5:21).

Ndivyo ilivyokuwa katika kutoa marudi (Mt. 18:15-17), yaliyokuwa yanaanzia katika maonyo binafsi na ya malezi (linganisha na Mt. 18: 16; Gal. 6:1) hadi kuondolewa katika ushirika (Mt. 18:18; 1 Kor. 5:11, 13; 2 Kor. 2:5-11).

Kwa hiyo Kanisa lina mamlaka ya kuamua juu ya kanuni za uendeshaji wake.

## Konferensi Kuu ni Mamlaka ya Juu Kuliko Zote

Leo hii katika Kanisa, kikao cha Konferensi Kuu, na Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu katikati ya vikao vya Konferensi Kuu, ndiyo mamlaka ya juu kabisa ya kikanisa, katika uendeshaji wa Kanisa. Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu inaruhusiwa na katiba yake kuunda taasisi ndogo ndogo zenye mamlaka ya kutekeleza majukumu ya taasisi hizo. Kwa hiyo, jumuiya zote zilizo chini yake na taasisi zote katika Kanisa zitakitambua kikao cha Konferensi Kuu, na Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu katikati ya vikao vya Konferensi Kuu, kama mamlaka ya juu kabisa ya kikanisa, iliyo

chini ya Mungu, miongoni mwa Waadventista wa Sabato.

Kukitokea kutokuelewana kati ya makanisa na konferensi au taasisi, kukata rufaa katika ngazi inayofuata ni sahihi hadi itakapofika katika Baraza la Mwaka la Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu au kikao cha Konferensi Kuu. Katikati ya vikao hivyo, Kamati Tendaji ya Konferensi Kuu itakuwa chombo chenye mamlaka ya mwisho katika masuala yote. Uamuzi wa kamati hiyo unaweza kubadilishwa katika kikao cha Konferensi Kuu au Baraza la Mwaka. Jumuiya zinapopitia upya uamuzi wa jumuiya nyingine, haziwajibiki na dhima ya jumuiya nyingine yo yote ile.

"Mara kwa mara nimeelekezwa na Bwana kuwa hakuna uamuzi wa mtu ye yote unaopasa kusalimishwa kwa uamuzi wa mtu mwingine ye yote. Mawazo ya mtu mmoja au ya watu wachache yasichukuliwe kuwa yanatosha katika hekima na uwezo wa kuendesha kazi, na kuamua mipango ya kufuatwa. Lakini, uamuzi wa ndugu waliokusanyika toka sehemu zote za kanisa unapofanyika katika 'Konferensi Kuu,' uhuru binafsi na uamuzi binafsi haupaswi kuendelezwa kikaidi, bali uachwe. Mtenda kazi ye yote asichukulie kuwa jambo jema kung'ang'ania maoni yake ya binafsi, dhidi ya uamuzi wa chombo hicho kikuu." – *Testimonies for the Church, Kitabu cha 9 uk 260.*

SURA YA 4

# Wachungaji na Watumishi Wengine wa Kanisa

### Kazi Aliyoagiza Mungu

"Mungu ana kanisa, nalo lina kazi ambayo limeagizwa na Mungu. 'Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo. ...'

"Watu walioteuliwa na Mungu wamechaguliwa ili walinde kwa uangalifu wenye wivu, na saburi iliyojaa tahadhari ili kanisa lisiangushwe na hila mbaya za Shetani, bali lisimame katika ulimwengu kwa ajili ya kuendeleza utukufu wa Mungu miongoni mwa watu."—T9 52, 53.

***Mwenyekiti wa Konferensi***—Mwenyekiti wa konferensi hana budi kuwa mchungaji aliyewekewa mikono, mwenye uzoefu na sifa njema. Ni msimamizi wa kazi ya injili katika konferensi na ni mzee kiongozi au mwangalizi wa makanisa yote. Hushughulikia ustawi wa kiroho wa makanisa hayo na kuyashauri kuhusu shughuli na mipango yao. Ana haki ya kwenda katika makanisa yote na katika huduma zao, vikao vya mkutano mkuu, pamoja na mabaraza bila kuwa na haki ya kupiga kura kama hajaruhusiwa na kanisa, au kama si mshiriki wa kanisa hilo. Ikibidi anaweza kuwa mwenyekiti wa kikao cho chote cha kanisa lo lote. Ana haki ya kuona nyaraka zote za kanisa.

Mwenyekiti wa konferensi hana mamlaka ya kuondoa maofisa wa kanisa waliochaguliwa kihalali lakini atafanya kazi kwa

kushirikiana nao. Nao kwa upande wao, wakitambua mshikamano wa ushirika wa konferensi, wanatakiwa kushauriana naye, katika mambo yote yanayohusu ustawi wa kanisa. Wasijaribu kumtenga katika utekelezaji halali wa kazi zake.

***Wakurugenzi wa Idara wa Konferensi***—Wakurugenzi wa idara wa Konferensi huhamasisha maeneo muhimu sana ya kazi ya kanisa chini ya uongozi wa kamati ya konferensi ikishauriana na mwenyekiti wa konferensi. Ili wafanye kazi waliyopewa kwa ufanisi, watumishi hawa lazima wawe na fursa ya kwenda makanisani kuwasilisha na kutengeneza mipango yao. Inawapasa watumishi hawa kuzingatia mipango yote ya kanisa, hata iliyo nje, ya idara zao.

Wakurugenzi wa idara hawana mamlaka ya utawala au utendaji, kwa hiyo uhusiano wao na makanisa mahalia ni wa kutoa ushauri. Kazi yao haina uhusiano na makanisa kama ule wa kamati ya konferensi au wa mwenyekiti. Katika kuhamasisha aina mahususi za kazi zao, huwa wanafanya kazi katika konferensi nzima. Hata hivyo, hawategemewi kuyashauri makanisa kuhusu uchaguzi na majukumu mengine ya kiutawala au maeneo mengine ya kazi, kama hawajaagizwa kufanya hivyo na mwenyekiti.

***Wachungaji Waliowekewa Mikono***—Wachungaji waliowekewa mikono walioteuliwa na kamati ya konferensi kuwa wachungaji au viongozi wa mitaa hawachukui nafasi ya mwenyekiti katika maeneo yao. Hawana mamlaka ya kiutawala kama alivyo mwenyekiti, bali hushirikiana naye katika kutekeleza mipango na sera za konferensi.

Mchungaji aliyewekewa mikono akipangwa kwenye kanisa mahalia, husaidiwa na wazee mahalia. Kwa sababu ya kuwekewa mikono, mchungaji anaweza kuhudumu katika kaida za dini na huduma maalum. Inampasa mchungaji kuwa kiongozi na mshauri wa kiroho wa kanisa lake. Wachungaji hawana budi kuwaelekeza maofisa katika katika kazi zao na kupanga pamoja nao katika maeneo yote ya kazi na shughuli za kanisa.

Mchungaji ni mjumbe wa baraza la kanisa na ndiye mwenyekiti wake. Mchungaji akitaka kupunguziwa jukumu la kuwa mwenyekiti wa baraza, mzee wa kanisa huwa mwenyekiti akishirikiana na

mchungaji. (taz. uk. 72.) Mchungaji, akisaidiwa na wazee wa kanisa, anategemewa kupanga na kuongoza huduma zote za kiroho, kama vile ibada ya Siku ya Sabato na mikutano ya maombi, na inampasa kuendesha huduma ya meza ya Bwana na ubatizo. Wachungaji wasiwe na kundi la washauri wa kujichagulia, bali washirikiane na maofisa waliochaguliwa.

Kunapokuwa na mwinjilisti aliyeombwa kufanya mkutano wa injili katika eneo lenye kanisa, konferensi haina budi kumwalika mchungaji kumsaidia mwinjilisti, ili kumpa mchungaji fursa ya kuwafahamu washiriki watarajiwa.

Wachungaji au wachungaji wasaidizi hawapendekezwi au kuteuliwa kushika nafasi hizo na kanisa. Uhusiano wao na kanisa unatokana na uteuzi wa kamati ya konferensi, na uteuzi huo unaweza kubadilishwa wakati wo wote. (tazama uk. 73)

Mchungaji anaweza kuondolewa kazini kwa uamuzi wa kamati ya konferensi bila kuathiri ushirika wake. Lakini, mchungaji akiondolewa katika ushirika wa kanisa na baadaye kurudishwa katika ushirika kama mlei, kurejeshwa kwa ushirika wake hakumaanishi kurejeshwa katika utumishi.

***Wachungaji wenye Leseni***—Ili kuwapa watu fursa ya kuonesha wito wao katika utumishi, hususan katika uongoaji wa roho, wataradhia wa kazi hiyo hupewa leseni ya uchungaji na konferensi. Kutolewa kwa leseni hizo huwapatia fursa ya kukuza karama ya uchungaji.

Wachungaji wenye leseni wana mamlaka ya kuhubiri, kufanya uinjilisti, kuongoza katika kazi ya umisionari, na kusaidia katika shughuli zote za kanisa.

Hata hivyo, kuna mazingira, ambapo huilazimu konferensi kuteua mchungaji mwenye leseni kubeba jukumu la mchungaji au mchungaji msaidizi wa kanisa au jumuiya ya makanisa. Ili kumwezesha mchungaji mwenye leseni kufanya kazi fulani za kichungaji, inabidi kanisa au kundi la makanisa anayoyahudumia yamchague mchungaji huyo kuwa mzee wa kanisa mahalia. Baada ya hapo, kwa kuwa uwezo wa kuruhusu kuongezwa kwa madaraka ya mchungaji mwenye leseni ni wa kamati kuu ya divisheni, inapasa kamati hiyo iidhinishe ongezeko hilo la mamlaka kwa

kubainisha kazi za ziada ambazo mchungaji huyo mwenye leseni anaweza kuzifanya. Kazi hizo za ziada ni katika kanisa au kundi la makanisa ambapo mchungaji huyo mwenye leseni anafanyia kazi na ni mzee wa kanisa. Baada ya kamati ya divisheni kuamua, kamati ya konferensi sasa inaweza kuchukua hatua. (tazama uk. 74)

Kamati ya konferensi haitaongeza kazi za mchungaji mwenye leseni zaidi ya zile zilizoruhusiwa na kamati ya divisheni. Pia haitamruhusu mchungaji mwenye leseni kufanya kazi zilizoongezwa katika kanisa lo lote nje ya mahali ambapo amechaguliwa kama mzee wa kanisa. Uamuzi wa Kamati ya konferensi hauwezi kuwa badala ya uchaguzi wa kanisa au kuwekewa mikono kwa ajili ya kazi ya injili.

***Walimu wa Biblia***—Konferensi inaweza kuajiri walimu wa Biblia na kuwapa kazi katika mikutano ya injili au makanisa na makundi mahalia. Pamoja na kwamba walimu hawa hufanya kazi chini ya konferensi kwa ujumla, mwalimu wa Biblia anayefanya kazi katika mkutano wa injili atakuwa chini ya uongozi wa mwinjilisti anayeendesha mahubiri hayo, na mwalimu anayefanya kazi katika kanisa atakuwa chini ya uongozi wa mchungaji. Mwalimu wa Biblia haruhusiwi kupewa kazi katika kanisa mahalia isipokuwa kwa makubaliano maalum na konferensi, bali inapasa awe huru kufanya kazi ya kuongoa roho.

***Konferensi Husimamia Watumishi wa Kanisa***—Mwenyekiti wa konferensi, kwa kushauriana na kamati ya konferensi husimamia watumishi wote wa konferensi kama vile wachungaji, walimu wa Biblia, na wakurugenzi wa idara, ambao hupata vitambulisho kutoka konferensi na huwajibika kwa konferensi, na si kwa kanisa mahalia. Kanisa linaweza kumwomba mwenyekiti wa konferensi lipate huduma au msaada wa watumishi wa konferensi, lakini kwa hali yo yote ile, uteuzi utafanywa na kamati ya konferensi. Kamati ya konferensi inaweza kubadili kazi za watumishi wakati wo wote inapoona kuwa zinahitajika. Mtumishi au kanisa anaweza kukata rufaa kwa kamati ya konferensi ili kuupima uamuzi wa kuhamishwa kwa mtumishi husika na kamati itaiangalia rufaa hiyo

kwa makini ikizingatia mahitaji ya konferensi nzima. Mtumishi akikataa kushirikiana na kamati na kukataa kutekeleza uamuzi wa kamati, kamati inaweza kuuchukulia mwenendo wa mtumishi huyo kama ukaidi na inaweza kuushughulikia ipasavyo. Kwa namna yo yote ile, mtumishi haruhusiwi kukata rufaa kwa kanisa kuhusu uamuzi kama huo. Kanisa likiunga mkono ukaidi wa mtumishi, nalo litastahili marudi kutoka konferensi.

**Vitambulisho na Leseni**

Kazi ya Mungu haina budi kulindwa kwa wivu na viongozi wawajibikaji kuanzia katika kanisa mahalia hadi Konferensi Kuu. Vitambulisho na leseni rasmi hutolewa kwa watumishi wote wa kudumu walioidhinishwa, navyo hutolewa na kamati za utawala kwa vipindi maalum.

Katika konferensi mahalia, kamati hutoa mamlaka kwa watu kuliwakilisha Kanisa kama wachungaji na wahudumu wa injili. Mamlaka hayo hutolewa kwa kuwapatia vitambulisho na leseni, ambavyo ni maagizo yaliyoandikwa yakiwa na tarehe na kusainiwa ipasavyo na viongozi wa konferensi. Mamlaka inayotolewa kwa njia hiyo, si ya mtu na haitokani na mtu bali ni ya chombo kilichoitoa, ambacho kinaweza kuagiza vitambulisho hivyo virudishwe wakati wo wote, kama aliyepewa atakiuka masharti ya kazi yake. Vitambulisho na leseni si mali yao binafsi na inapasa virudishwe ajira inapositishwa au vikitakiwa na taasisi iliyovitoa.

Ili maadui wa Kanisa wasitumie mimbari zetu, mtu ye yote asiruhusiwe kuhutubia mkutano wo wote wa kanisa asipoonesha kitambulisho au leseni hai ya kanisa. Hata hivyo, inaeleweka kuwa wakati mwingine makanisa yanaweza kuhutubiwa na viongozi wa serikali; lakini watu wote wasioidhinishwa wasiruhusiwe kutumia mimbari.

***Vitambulisho na Leseni Zilizomaliza Muda Wake***—Vitambulisho na leseni hutolewa kwa kipindi maalum kama inavyoelezwa katika katiba ya konferensi pamoja na sheria ndogo ndogo au sera ya uendeshaji, na huwa zinatolewa upya na kikao cha konferensi au kamati kuu. Kuwa na kitambulisho au leseni iliyokwisha muda wake hakumfanyi mtu aliye na vitu hivyo kuwa na madaraka ya namna yo yote ile.

***Watumishi Waliostaafu*****—**Watumishi waliostaafu wanastahili heshima na kufikiriwa kwa ajili ya kusaidia katika ujenzi wa kanisa la Mungu. Wanaweza kuendelea kubariki na kusaidia makanisa ambapo kuna ushirika wao kwa njia ya kuchaguliwa kushika kazi yo yote. Wanaweza pia kufanya kazi za kichungaji wakiongozwa na kamati ya konferensi.

***Wachungaji wa Zamani Wasio na Vyeti***—Watu waliowahi kuwekewa mikono kama wachungaji lakini kwa sasa hawana vitambulisho hai wanaweza kuchaguliwa kuwa wazee wa kanisa na kama kuwekewa kwao mikono hakujabatilishwa, hawahitaji kuwekewa mikono ya uzee wa kanisa. Kazi zao zitakuwa zile za mzee wa kanisa mahalia tu.

SURA YA 5

# Kuunda, Kuunganisha na Kuvunja Makanisa na Makundi

**Kuunda Kanisa**

Kanisa huundwa na mchungaji aliyewekewa mikono kwa pendekezo la kamati kuu ya konferensi. (Angalia uk. 38 kuhusu utaratibu wa kuunda kundi.) Kwa kuwa kuna mambo mengi katika uundaji wa kanisa, inapasa mwenyekiti wa Konferensi aalikwe.

Kundi la waumini waliobatizwa likiwa tayari kubeba majukumu ya kanisa lililoundwa, halina budi kushauriana na mwenyekiti wa Konferensi na kupata kibali cha kamati kuu ya konferensi kabla ya kupanga tarehe ya kufanyika kwa uundaji huo.

Waumini waliobatizwa wanapokutana siku ile iliyopangwa, itampasa mtu anayeendesha shughuli hiyo kutoa muhtasari wa imani za msingi za Waadventista wa Sabato.

Kisha yule anayesimamia shughuli hiyo atatoa wito akiwataka wote wanaokubaliana na kanuni hizo na ambao wanataka kuungana katika ushirika wa kanisa waje, mbele. Jina la kila mtu litaandikwa. Kama kuna watu ambao tayari ni washiriki wa kanisa la konferensi au kanisa lingine, yule anayesimamia shughuli hiyo atawasilisha barua za uhamisho walizopata. Wale wanaohamia watakuwa waanzilishi wa kanisa hilo jipya.

Lakini kama hakuna washiriki wanaohamia, basi washiriki watatu (hasa washika Sabato waliothibitishwa miongoni mwa watu waliopo) watachaguliwa kuwa waanzilishi. Wanaweza kuulizwa maswali yafuatayo: Je, mnamkubali Kristo kuwa Mwokozi wenu? Je, mnakubaliana kikamilifu na kanuni za imani zilizowasilishwa hivi karibuni? Je, mmebatizwa kwa kuzamishwa majini? Je, mna msimamo mzuri na kuaminiana?

Kama wakijibu maswali haya kuwa kukubali, watu hao watatu watatangazwa kuwa waanzilishi wa kanisa hilo jipya. Kisha majina yaliyokuwa yameandikwa yatasomwa moja baada ya lingine, kila mtu ataulizwa maswali yaliyoandikwa katika aya iliyotangulia, na yule msimamizi atapigisha kura miongoni mwa wale waanzilishi, kumpokea kila mtu katika ushirika wa kanisa. Kila mtu atakayepokelewa kwa njia hiyo, atakuwa mshiriki wa kanisa na ana haki ya kulipigia kura jina linalofuata. Tahadhari kubwa inatakiwa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa ushirika kamili na upendo wa udugu unakuwepo miongoni mwa wale wanaopokelewa katika ushirika. Endapo kutatokea tatizo lo lote juu ya suala lo lote, ama la mafundisho, au ushirika, inapasa hatua ziahirishwe isipokuwa kama suala hilo linaweza kusuluhishwa kwa upole na busara.

Baada ya waanzilishi kuwapigia kura washiriki watarajiwa wote, kanisa litakuwa taasisi kamili likiwa tayari kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi. Washiriki watachagua kamati ya mapendekezo na mchungaji anayesimamia atakuwa mwenyekiti. Kamati ya mapendekezo italeta mapendekezo ya kujaza nafasi mbalimbali za uongozi kanisani. Maofisa hao wakisha kuchaguliwa, wazee hawana budi kuwekewa mikono kama watakuwa wahajawahi kuwekewa. Huduma kama hiyo, lakini fupi zaidi itapasa kufanyika kwa ajili ya kuwawekea mikono mashemasi wa kiume na wa kike. Hapo kanisa litakuwa limeundwa kikamilifu na kuwa tayari kwa ajili ya huduma.

Kabla ya mkutano wa uundaji wa kanisa kumalizika, washiriki watapiga kura ya kuiomba konferensi kulipokea kanisa hilo lililotoka kuundwa katika jumuiya ya makanisa katika kikao cha konferensi kitakachofuata.

Ili kuhakikisha mafanikio makubwa ya kanisa hilo jipya, inawapasa viongozi wa konferensi na wa kanisa mahalia kuhakikisha kwamba viongozi wote wamefundishwa vyema kuhusu kazi zao. Kanisa halina budi pia kuwa na vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya Meza ya Bwana, ambayo, ikiwezekana, ifanyike kama sehemu ya mkutano huo wa uundaji wa kanisa. Itampasa mhazini, karani, na viongozi wengine kupokea nyaraka zote muhimu au vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao.

**Kuunda Kundi**

Mahali ambapo kuna waumini kadhaa walio mbali na kanisa, wanaokaa katika eneo moja au walio katika kundi dogo, wanaoabudia nyumbani au kundi la waongofu wapya, inawapasa kufikiria kuunda kundi la waumini kwa ajili ya ushirika, ibada na utume kwa lengo la kukua na kuwa kanisa lililoundwa au kuzaa makanisa mengine ya nyumbani katika eneo hilo la kijiografia.

Hadhi ya kuwa kundi huidhinishwa kwa uamuzi wa kamati ya konferensi, ambayo ikibidi, inaweza kulivunja kundi hilo. Inapasa divisheni na/au konferensi iwe na mwongozo ulioandikwa kwa ajili ya kuunda makundi katika eneo lake.

Washiriki wa kanisa ambao ni sehemu ya makundi madogo au makundi ya nyumbani wanaweza kuwa waanzilishi wa kundi jipya. Ushirika wa watu wanaotaka kuwa sehemu ya kundi, utakuwa ama katika kanisa la konferensi au katika kanisa mahalia (kanisa mama). Kama ushirika wa wale wanaotaka kuwa sehemu ya kundi itabidi uwe katika kanisa la konferensi, kamati ya konferensi itapitisha uhamisho wa ushirika wao kwenda kwenye kanisa la konferensi na kuonesha kuwa wao ni sehemu ya kundi hilo jipya.

Kamati ya konferensi inapoidhinisha kuanzishwa kwa kundi jipya, timu ya viongozi haina budi kuteuliwa, ikiwa ni pamoja na mkuu wa kundi, karani, na mhazini. Uteuzi huo hauna budi kufanywa na mchungaji wa mtaa, au mchungaji mwingine aliyechaguliwa na kamati ya konferensi, kwa kushauriana na kundi linaloanzishwa.

Uteuzi mwingine wote katika kundi hilo utafanywa kwa kura za watu wanaounda kundi hilo. Mchungaji wa mtaa au mtu mwingine ye yote aliyeidhinishwa na kamati ya konferensi atakuwa mwenyekiti katika kikao hicho. Washiriki hai wa kanisa la Waadventista wa Sabato tu ndio wanaweza kuteuliwa.

Mkuu wa kundi hatawekewa mikono kwa ajili ya kazi hiyo na hatakuwa na mamlaka ya kufanya kazi ambazo hufanywa na mzee wa kanisa. Hata hivyo, mazingira yasiyo ya kawaida yakilazimisha kamati ya konferensi inaweza kuteua mtu mwenye uzoefu kanisani na uwezo wa uongozi kuwa mzee wa kanisa wa kundi hilo.

Karani wa kundi ataweka kumbukumbu ya shughuli na mikutano yote ya kundi na atatuma taarifa za mara kwa mara za takwimu kwa kanisa mama au kwa katibu mkuu wa konferensi. Taarifa hizo

hazina budi kuwa na takwimu za mahudhurio na shughuli za kundi, ikiwa ni pamoja na huduma za jamii zinazofanywa katikati ya juma au siku ya Sabato.

Mhazini wa kundi ataweka kumbukumbu za pesa zote zilizopokelewa na kutumika na atatuma zaka na sadaka zote ambazo hazikukusanywa kwa ajili ya matumizi mahalia mara moja, au kwa wakati uliopangwa na konferensi, kwa mhazini wa konferensi ambaye pia ni mhazini wa kanisa la konferensi.

Kama washiriki wa kundi lililoundwa ni washiriki wa kanisa la konferensi, kundi hilo halitakuwa na haki ya kufanya marudi au kuhamisha na kupokea washiriki. Masuala hayo yote yatapelekwa kwenye kamati ya konferensi, ambayo ndiyo baraza la kanisa la konferensi. Mwenyekiti wa konferensi ndiye mzee wa kanisa la konferensi.

Kama konferensi itaunda kundi kwa njia ya kanisa mama la jirani badala ya kanisa la konferensi, kazi zilizoorodheshwa hapo juu (kama vile kutoa taarifa na ushirika) zitashughulikiwa na/kupitia kanisa mama.

Kwa kuwa kundi halina budi kutaka kukua na hatimaye kutambuliwa kama kanisa, uongozi wake hauna budi kuwaandaa washiriki kwa ajili ya kuwa na hadhi ya kanisa kwa kuhamasisha shughuli zote zinazofanywa na kanisa.

**Kuunganisha Makanisa**

Inapoonekana kuwa ni vyema kuunganisha makanisa mawili, kamati ya konferensi haina budi kupendekeza jambo hilo. Italipasa kila kanisa kuamua kwa kura juu ya suala la kuungana katika kikao kilichoitishwa rasmi kikiongozwa na mwenyekiti wa konferensi au mchungaji wa mtaa au mchungaji mwingine aliyewekewa mikono. Uamuzi wa kukubaliana na jambo hilo ukisha kufanywa na makanisa yote mawili, itabidi uandaliwe mkutano wa pamoja, ukiongozwa na mwenyekiti wa konferensi, na kama hayupo, mchungaji aliyewekewa mikono atakayechaguliwa na konferensi.

Tamko lililoandikwa kwa makini litaandaliwa likieleza sababu za kuungana na mambo mengine muhimu au masharti yatakayokuwapo, kama vile matumizi, mgawanyo au namna ya kushughulikia rasilimali, na uwajibikaji juu ya madeni. Linapaswa

kutaja jina jipya la kanisa lililounganishwa na kusitisha kazi za voingozi wa makanisa yote mawili.

Kukubaliwa kwa tamko hilo na mkutano wa pamoja utakuwa mwanzo wa mwungano wa makanisa hayo mawili. Baada ya hapo itawapasa washiriki wa kanisa jipya kuchagua kamati ya kupendekeza maofisa watakaohudumu kwa sehemu ya mwaka huo itakayokuwa imebakia.

Nakala ya tamko hilo itahifadhiwa na konferensi.

Washiriki wote wa makanisa hayo mawili wataungana katika jumuiya hiyo mpya. Hairuhusiwi kuondoa mshiriki ye yote kwa kukosa kumweka katika orodha ya washiriki wakati wa kuungana. Jumuiya iliyoungana itawajibika kwa ajili ya utaratibu na marudi ya washiriki wote. Washiriki walio chini ya marudi watakuwa hawana budi kushughulikiwa kama ilivyoelezwa mahali pengine katika mwongozo huu.

Kumbukumbu zote za makanisa yote mawili zitakuwa sehemu ya kumbukumbu za kanisa la muungano. Konferensi mahalia itajulishwa ili ichukue hatua stahiki katika mkutano mkuu unaofuata.

**Kuvunja au Kuondoa Makanisa**

". . . Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na waa. ... Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake" (Efe. 5:25-30).

Moyo huo ndio upasao kutawala katika juhudi za kusaidia kanisa lililokosa na aina zote za marudi yanayoweza kufanyika—wakati wote kusaidia na kuokoa kwa ajili ya kazi ya Mungu.

Hadhi ya kuwa kanisa si lazima iwe ya kudumu. Kanisa linaweza kuvunjwa au kuondolewa katika jumuiya ya makanisa kwa sababu zifuatazo:

***1. Kupoteza Washiriki***—Licha ya juhudi za kulilinda kanisa, wakati mwingine, washiriki wengi hupotea kwa kuhama au kwa kifo au kwa uasi kiasi kwamba kuwepo kwa kanisa huwa hatarini.

Katika hali kama hiyo, itabidi konferensi ipendekeze uwezekano wa kuvunjwa kwa kanisa hilo.

Kabla kanisa halijafanya uamuzi wa mwisho wa kuvunjwa, washiriki waliobaki wataombwa kuhamishia ushirika wao kwenye makanisa mengine.

Kama watakuwa wamebaki washiriki wa kutosha, kanisa linaweza kuitisha mkutano mkuu chini ya uongozi wa mwenyekiti wa konferensi au mchungaji atakayechaguliwa na mwenyekiti wa konferensi, kupitisha barua zinazoomba uhamisho wa washiriki wote hai ili wajiunge na makanisa mengine. Kwa njia hiyo kanisa litakuwa limejivunja lenyewe kwa mapendekezo ya kamati ya konferensi, na itakuwa imefunguliwa njia kwa kamati ya konferensi kuchukua hatua ya kuandika taarifa za kuvunjwa kwa kanisa hilo.

Kama, kulingana na maoni ya kamati ya konferensi, kuna washiriki wachache mno kufanya mkutano mkuu, kamati ya konferensi itakuwa na mamlaka ya kupitisha uhamisho wa washiriki hai kwenda makanisa mengine au kwenye kanisa la konferensi. Kwa njia hiyo kanisa hilo litakuwa limevunjwa.

Kama wakati wa kuvunjwa kwa kanisa hilo kutakuwa na washiriki walio katika marudi na hivyo hawawezi kupewa barua zinazosema kuwa wako hai, ushirika wao utahifadhiwa kwa muda katika kanisa la konferensi wakati uongozi wa konferensi unahakikisha kuwa kila juhudi imefanyika kuwasaidia washiriki hao haraka iwezekanavyo kuwa na Ukristo wa kuridhisha. Juhudi hizo zikifanikiwa, ushirika wao unaweza kuthibitishwa wakati huo katika kanisa la konferensi au barua za uhamisho zitatolewa ili wahamie katika makanisa mengine. Kama hawataweza kurejeshwa, itabidi waondolewe katika ushirika kwa uamuzi wa kamati ya konferensi.

***2. Marudi***—Matukio ya kuondoa makanisa kwa sababu za kinidhamu ni machache sana, kwa sababu kazi ya kanisa ni kutafuta na kuokoa. Kunapokuwa na matatizo makubwa kama vile uasi, kukataa kuenenda kulingana na *Mwongozo wa Kanisa*, au uasi dhidi ya Konferensi ukiendelea, juhudi za dhati hazina budi kufanyika kuepuka haja ya kuondoa kanisa. Inampasa mchungaji kujitahidi kuimarisha hali ya kiroho ya kanisa kwa njia ya mahubiri na huduma ya kuwatembelea washiriki. Konferensi

haina budi kuhimiza mfululizo wa mikutano ya uamsho kuwafanya washiriki wafanye upya agano na Bwana wao. Kama juhudi hizo hazitafanikiwa, mchungaji, atashauriana na uongozi wa kanisa, kwa kushirikana na konferensi, akijaribu kuleta suluhu na upatanisho na kulinusuru kanisa.

Hatua hizo za suluhu ni bora kuliko kuruhusu kudorora kwa uhusiano, jambo ambalo litasababisha kuondolewa kwa kanisa.

Lakini kama juhudi zote za kulinusuru kanisa zikishindwa, kamati ya konferensi italiangalia kwa makini suala la kuondolewa kwa kanisa husika. Kama itaamuliwa hatua hiyo ichukuliwe, konferensi itafuata hatua zifuatazo:

a. Uamuzi wa kupendekeza kuondolewa kwa kanisa, pamoja na sababu zake, utawasilishwa kwa kanisa lenyewe katika mkutano mkuu kwa ajili ya taarifa na kufikiria kwa makini.
b. Kama kanisa halitakubaliana na pendekezo hilo, linaweza kujibu kwa njia moja kati ya hizi zifuatazo:

1) Kurekebisha mambo yaliyosababisha marudi na kukubaliana na maagizo ya konferensi, kuiomba konferensi itangue pendekezo la kulivunja au kuliondoa kanisa.
2) Kukata rufaa kwenye kamati tendaji ya union, au divisheni kama ni suala la jumuiya ya makanisa, ili ifanye usuluhishi kwa niaba ya kanisa hilo.

c. Kama kanisa hilo litaendelea kuasi, kamati kuu ya konferensi itatoa pendekezo la kuvunjwa kwa kanisa hilo katika mkutano mkuu wa kawaida wa konferensi au mkutano mkuu maalum wa konferensi.
d. Kama mkutano mkuu huo utatoa uamuzi wa kuliondoa kanisa hilo, konferensi itatekeleza uamuzi huo.

**Utunzaji wa Washiriki, Nyaraka, na Pesa**

Washiriki waaminifu wa kanisa lililovunjwa au kuondolewa wanaweza kutaka kendelea na ushirika katika Kanisa. Ili kuhakikisha ustawi wao, ushirika wao utahifadhiwa kwa muda wa hadi mwaka mmoja katika kanisa la konferensi kutoa fursa kwa

wale wanaotaka, kuwa na ushirika katika kanisa la konferensi au kuuhamishia katika kanisa lingine. Uaminifu wao utatathminiwa na kamati ya konferensi, na ukiridhisha, kamati ya konferensi inaweza kupendekeza wapewe ushirika katika kanisa la konferensi au makanisa watakayotaka wenyewe.

Majina ya washiriki wa kanisa lililovunjwa au kuondolewa ambao watakuwa katika marudi yatapelekwa kwa katibu wa konferensi kwa ajili uangalizi wa kamati ya konferensi tangu mwanzo kama ilivyoelezwa katika "Kupoteza washiriki," hapo juu.

Kanisa likivunjwa au kuondolewa kwa sababu ya kupoteza washiriki au sababu za kinidhamu, sadaka zote, mahesabu ya fedha, na mali zisizohamishika au zinazohamishika, ziwe katika jina la kanisa mahalia au la konferensi au jumuiya nyingine halali ya kikanisa, zitakuwa katika dhamana ya konferensi. Kwa hiyo, konferensi itakuwa na haki, mamlaka na wajibu wa kusimamia, kulinda au kutumia mali na pesa hizo. Nyaraka zote za kanisa hilo zitakuwa katika uangalizi wa katibu na/au mhazini wa konferensi.

Endapo hakutakuwa na suala la kinidhamu, njia nyingine badala ya kulivunja au kuliondoa kanisa ni kulirudisha katika hadhi ya kundi. Uamuzi huo utafanywa kwa zaidi ya nusu ya kura zitakazopigwa katika kamati ya konferensi, baada ya kushauriana na mchungaji wa mtaa pamoja na washiriki, na kuwasilishwa kwa kanisa na mchungaji au mwakilishi wa konferensi.

Barua za uhamisho wa washiriki wote waaminifu zinaweza kupitishwa katika mkutano mkuu kwenda kwenye kanisa la konferensi au makanisa mengine endapo washiriki wengine watataka kuhama. Katika mkutano huo huo, mchungaji, akishauriana na washiriki mahalia, atateua timu ya viongozi miongoni mwa washiriki wa kundi hilo jipya, ikiwa ni pamoja na mkuu wa kundi, karani, na mhazini. Kwa maelezo ya masuala mengine yanayohusu uundaji wa kundi, tazama "Uundaji wa Kundi" uk. 38

SURA YA 6

# Ushirika

Wajibu nyeti unaoambatana na ushirika katika mwili wa Kristo unapasa kueleweka vyema kwa kila mtu anayetaka ushirika wa Kanisa. Wale tu waliooonesha kuwa wamezaliwa upya na kunufaika na hali ya kiroho ndani ya Bwana Yesu, watakuwa tayari kupokelewa katika ushirika. Inawapasa wachungaji kuwafundisha wale wanaotaka kuingia katika ushirika, mafundisho ya msingi pamoja na desturi zinazohusiana na mafundisho hayo, ili waingie katika Kanisa wakiwa na msingi imara wa kiroho. Ingawa hakuna umri uliotajwa kwa ajili ya ubatizo, inapendekezwa kwamba watoto wadogo watakaoonesha nia ya kubatizwa watiwe moyo na kuingizwa katika mpango wa mafunzo utakaowawezesha kubatizwa.

Mtume Paulo anaandika: "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." (Rum. 6:3, 4).

Luka pia anaeleza: "Petro akawaambia, 'Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo,' … Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. (Mdo. 2:38-41).

"Washiriki wa kanisa, wale aliowaita kutoka gizani waingie katika nuru yake ya ajabu, hawana budi kuonesha utukufu wake. Kanisa ni hazina ya utajiri wa neema ya Kristo; na kwa njia ya kanisa, hatimaye litadhihirishwa, hata kwa 'falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho' onesho kamili na la mwisho la upendo wa Mungu."—AA 9.

### Ubatizo

***Sharti la Kuingia katika Ushirika*—**"Kristo ameufanya ubatizo kuwa ishara ya kuingia katika ufalme wake wa kiroho. Ameufanya

kuwa sharti bayana linalopasa kutimizwa na wote wanaotaka kutambuliwa kuwa wako chini ya mamlaka ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. …

"Ubatizo ni tendo nyeti kabisa la kuukataa ulimwengu. Wale waliobatizwa katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, mwanzoni kabisa mwa maisha yao ya Kikristo hutangaza hadharani kwamba wameacha kumtumikia Shetani na wamekuwa sehemu ya ukoo wa kifalme, watoto wa mfalme wa mbinguni. Wamelitii agizo lisemalo: 'Tokeni kati yao, mkatengwe nao, … msiguse kitu kilicho kichafu,' nao hutimiziwa ahadi isemayo 'Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi.' 2 Wakorintho 6:17, 18."—6T 91.

Ubatizo ni njia ya kusimikwa kanisani. Kimsingi ni ahadi ya kuingia katika Agano la Kristo linalookoa na hauna budi kuchukuliwa kama ukaribisho nyeti, lakini wa furaha katika familia ya Mungu.

Ushirika katika Kanisa unawezekana katika makanisa yaliyo katika jumuiya ya makanisa yanayotambuliwa na konferensi fulani tu.

***Aina ya Ubatizo*—**Kanisa linaamini ubatizo wa kuzamishwa na huwapokea katika ushirika wale waliobatizwa kwa njia hiyo tu. (Tazama sura ya 14, "Imani za Msingi za Waadventista wa Sabato.") Wale wanaokiri hali yao ya kupotea kama wenye dhambi, wakatubu dhambi zao na kuongoka kwa dhati baada ya kufundishwa vyema, wanaweza kukubaliwa kama wataradhia wa ubatizo na ushirika wa Kanisa.

***Mafundisho Kamili na Kupimwa Hadharani Kabla ya Ubatizo*—**Inawapasa wataradhia, ama mmoja mmoja au katika darasa la ubatizo, kufundishwa kutoka katika maandiko, juu ya imani za msingi na desturi za Kanisa pamoja na wajibu wa washiriki. Inampasa mchungaji kuliridhisha kanisa, kwa kuwapima hadharani, kwamba wataradhia wamefundishwa vizuri, wamedhamiria kuchukua hatua hiyo muhimu na kwa mwenendo na tabia wanaonesha ukubali wa hiari wa mafundisho ya Kanisa na

kanuni za mwenendo ambazo ni udhihirisho wa nje, wa mafundisho hayo, kwani “kwa matunda yao mtawatumbua” (Mt. 7:20).

Kama haiwezekani kuwapima hadharani, basi wataradhia watasailiwa na baraza la kanisa, au kamati itakayochaguliwa na baraza, kama vile baraza la wazee, ambao watatoa taarifa kwa kanisa kabla ya ubatizo.

“Upimaji wa uanafunzi haufanyiki kwa umakini kama ipasavyo kwa wanaojitoa kwa ajili ya ubatizo. Ni vyema ikaeleweka kama wanataka kuitwa Waadventista wa Sabato, au wanasimama upande wa Bwana, ili watoke katika ulimwengu na kutengwa nao, wasiguse kitu kilicho kichafu. Kabla ya ubatizo inapasa kuwe na uchunguzi wa kina juu ya hali ya wataradhia. Uchunguzi huu usifanyike bila upendo na uchangamfu, bali ufanyike kwa ukarimu, upole ukiwaelekeza waumini wapya kwa Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya dunia. Yafanye matakwa ya injili yaeleweke kwa wataradhia wa ubatizo.”—6T 95, 96.

**Kiapo na Ahadi ya Ubatizo**

***Kiapo cha Ubatizo*—**Wataradhia wa ubatizo na wale wanaopokelewa katika ushirika kwa kukiri imani watathibitisha kukubaliana kwao na imani za msingi mbele ya kanisa mahalia au chombo kingine kitakachochaguliwa ipasavyo. (tazama uk. 45)

Mchungaji au mzee wa kanisa atawauliza wataradhia maswali yafuatayo, ambao watajibu ama kwa kutamka, kunyosha mkono au njia nyingine inayofaa kitamaduni.

**Kiapo**

1. Je, unaamini kwamba kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, umoja wa Nafsi Tatu za milele?
2. Je, unakikubali kifo cha Yesu Kristo pale Kalvari kama dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zako, na unaamini kwamba, kwa neema ya Mungu, kwa kuiamini damu yake iliyomwagika, umeokolewa kutoka katika dhambi pamoja na adhabu yake?

3. Je, unamkubali Yesu Kristo kama Bwana wako na Mwokozi wako mahususi ukiamini kwamba, Mungu amekusamehe dhambi zako na kukupa moyo mpya katika Kristo, na unazikataa njia za dhambi za ulimwengu?
4. Je, unaikubali kwa imani haki ya Kristo, ambaye ni Mwombezi wako katika patakatifu pa mbinguni, na unaikubali ahadi ya kukupatia neema ibadilishayo na uwezo wa kuishi maisha ya upendo yaliyojengwa katika Kristo nyumbani kwako na mbele za ulimwengu?
5. Je, unaamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, kanuni pekee ya Mkristo kwa ajili ya imani na mwenendo? Je, unaazimu kuwa na muda wa maombi na kusoma Biblia mara kwa mara?
6. Je, unazikubali Amri Kumi kuwa ni andiko la tabia ya Mungu na, ufunuo wa mapenzi yake? Je, unakusudia kuishika sheria hii kwa uwezo wa Kristo aliye ndani yako, ikiwa ni pamoja na amri ya nne inayoagiza kuiadhimisha siku ya saba ya juma kama Sabato ya Bwana na kumbukumbu ya Uumbaji?
7. Je, unangoja kwa hamu kuja upesi kwa Yesu pamoja na tumaini lenye baraka ambapo "huu wa kufa utakapovaa kutokufa" [1 Kor. 15:54]? Unapojiandaa kukutana na Bwana, je, utaushuhudia wokovu wake wa upendo kwa kutumia talanta zako katika juhudi mahususi za kuongoa roho na kuwasaidia wengine kuwa tayari kwa ajili ya kuonekana kwake katika utukufu?
8. Je, unalikubali fundisho la Biblia la karama za Roho, na je, unaamini kwamba karama ya unabii ni moja kati ya alama za kulitambua kanisa la waliosalia?
9. Je, unakubaliana na muundo wa kanisa? Na je, unakusudia kumwabudu Mungu na kulisaidia kanisa kwa njia ya zaka na sadaka zako na kwa juhudi zako binafsi na ushawishi wako?
10. Je, unaamini kuwa mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu; na je, utamheshimu Mungu kwa kuutunza,

kuepuka kutumia vitu vyenye madhara; kuacha kula vyakula vyote najisi; kuacha kutumia, kutengeneza, au kuuza vileo; kuacha kutumia, kutengeneza, au kuuza tumbaku katika aina zake zote kwa ajili ya matumizi ya binadamu; na kuacha matumizi mabaya au biashara haramu ya dawa za kulevya au dawa zingine?

11. Je, unazijua na kuzielewa kanuni kuu za Biblia kama zinavyofundishwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato? Na je, unakusudia, kuyafanya mapenzi ya Mungu kwa neema yake, kwa kuishi maisha yanayolingana na kanuni hizo?
12. Je, unalikubali fundisho la Agano Jipya kuhusu ubatizo wa kuzamishwa majini na unataka kubatizwa hivyo kama udhihirisho wa hadhara imani yako kwa Kristo na msamaha wake kwa dhambi zako?
13. Je, unakubali na kuamini kwamba Kanisa la Waadventista wa Sabato ndilo kanisa la waliosalia linalotajwa katika unabii wa Biblia na kwamba watu wa kila taifa, jamaa, na lugha wanakaribishwa na kupokelewa katika ushirika wa Kanisa hilo? Je, unataka kuwa mshiriki wa kanisa hili mahalia ambalo ni sehemu ya jumuiya ya Kanisa la ulimwengu?

**Kiapo Mbadala**

1. Je, unampokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako binafsi, na je, unataka kuishi ukiwa na uhusiano naye unaookoa?
2. Je, unayakubali mafundisho ya Biblia kama yanavyo-elezwa katika Tamko la Imani za Msingi za kanisa la Waadventista wa Sabato, na unaahidi kuishi kuli-ngana na mafundisho hayo kwa neema ya Mungu?
3. Je, unataka kubatizwa kama udhihirisho wa hadhara wa imani yako kwa Yesu Kristo, kupokelewa katika ushirika wa kanisa la Waadventista wa Sabato, na kulisaidia kanisa na kazi yake kama wakili mwaminifu kwa ushawishi wako, zaka na sadaka, na maisha ya utumishi?

Agano la Ubatizo—Kanisa limezifasiri imani zake 28 za msingi, pamoja na kiapo cha ubatizo na Cheti cha Ubatizo na Ahadi, kama agano la ubatizo.

Nakala iliyochapwa ya agano hili pamoja na Cheti cha Ubatizo na Ahadi iliyojazwa ipasavyo, itatolewa kwa wote wanaopokelewa katika ushirika kwa njia ya ubatizo. Cheti stahiki kitatolewa kwa wale wanaopokelewa kwa njia ya kukiri imani yao.

Cheti cha Ubatizo pamoja na Ahadi zina nafasi ya kutia sahihi kwa mshiriki mpya kama njia ya kuzikubali ahadi hizo. Baada ya ubatizo, Cheti cha Ubatizo na Ahadi vitakabidhiwa kwa wataradhia kama hati ya agano. Ahadi zinasomeka ifuatavyo:

**Ahadi**

1. Ninaamini kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ambao ni umoja wa Nafsi Tatu za milele.
2. Ninaikubali mauti ya Yesu Kristo pale Kalvari kama dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zangu, na ninaamini kwamba nimeokolewa kwa neema, kutoka katika dhambi pamoja na adhabu yake, kwa njia ya imani kwa damu yake iliyomwagika.
3. Ninampokea Yesu Kristo kama Bwana wangu na Mwokozi wangu binafsi, na ninaamini kwamba, ndani ya Kristo Mungu amenisamehe dhambi zangu na amenipa moyo mpya, nami ninaziacha njia mbaya za ulimwengu huu.
4. Ninaipokea kwa imani haki ya Kristo, ambaye ni Mwombezi wangu patakatifu pa mbinguni, na ninaipokea ahadi yake ya neema inayoweza kubadilisha, pamoja na uwezo wa kuishi maisha ya upendo yaliyojengwa katika Kristo nyumbani mwangu na mbele za ulimwengu.
5. Ninaamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, yaani kanuni pekee ya imani na mwenendo wa Kikristo. Ninaahidi kutumia muda mara kwa mara katika maombi na kusoma Biblia.
6. Ninazikubali Amri Kumi kuwa ni andiko la tabia ya Mungu, na ni ufunuo wa mapenzi yake. Ninakusudia, kwa uwezo wa Kristo akaaye ndani yangu, kuishika sheria hii, pamoja na amri ya nne inayoagiza kuiadhimisha siku ya saba ya juma kama Sabato ya Bwana na kumbukumbu ya Uumbaji.

7. Ninasubiri kwa hamu ujio wa Yesu uliokaribia pamoja na tumaini lenye baraka “huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika” [1 Kor. 15:54]. Ninapojiandaa kukutana na Bwana, nitakuwa ninashuhudia wokovu wake utokanao na upendo kwa kutumia talanta zangu katika juhudi zangu za kuongoa roho na kuwasaidia wengine kujiandaa kwa ajili ya kuonekana kwake katika utukufu.
8. Ninalikubali fundisho la Biblia la karama za Roho, na ninaamini kwamba karama ya unabii ni moja kati ya vigezo vya kulitambua kanisa la waliosalia.
9. Ninaukubali muundo wa kanisa. Ninakusudia kumwabudu Mungu na kulisaidia Kanisa kwa zaka na sadaka zangu na kwa juhudi na ushawishi wangu binafsi.
10. Ninaamini kwamba mwili wangu ni hekalu la Roho Mtakatifu; na nitamheshimu Mungu kwa kuutunza, nikiepuka matumizi ya vitu vinavyodhuru, na kuacha kutumia vyakula vyote vilivyo najisi; kuacha kutumia, kutengeneza, au kuuza vileo; kuacha kutumia, kutengeneza au kuuza tumbaku katika aina zake zote; na kuacha matumizi mabaya au biashara haramu ya dawa za kulevya au dawa zingine.
11. Ninazijua na kuzielewa kanuni kuu za Biblia kama zinavyofundishwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato. Ninakusudia kuyatekeleza mapenzi ya Mungu, kwa neema yake, kwa kuendesha maisha yangu kulingana na kanuni hizo.
12. Ninalikubali fundisho la Agano Jipya kuhusu ubatizo wa kuzamishwa na ninataka kubatizwa kama udhhirisho wa hadhara wa imani yangu kwa Kristo na msamaha wake kwa dhambi zangu.
13. Ninakubali na kuamini kwamba, Kanisa la Waadventista wa Sabato ndilo kanisa la waliosalia linalotajwa katika unabii wa Biblia na kwamba watu wa kila taifa, jamaa, na lugha wanakaribishwa na kupokelewa katika ushirika wa kanisa hilo. Ninataka kuwa mshiriki wa kanisa hili mahalia ambalo ni sehemu ya jumuiya ya kanisa la ulimwengu.

***Kura ya Kuwapokea Huthibitishwa kwa Ubatizo***—Baada ya wataradhia kujibu maswali ya kiapo kwa kukubali mbele

ya washiriki wa kanisa au chombo kingine kilichoteuliwa, au uthibitisho kutolewa kwa kanisa kwamba wamefanya hivyo, kanisa litapiga kura ya kuwapokea katika ushirika utakaoanza rasmi baada ya ubatizo, ambao haupasi kucheleweshwa kupita kiasi.

***Kupokea Washiriki Wasiojulikana***—Wakati wa kuwaandaa kwa ajili ya ubatizo wale walioongoka, inampasa mwinjilisti amwalike mchungaji au mzee wa kanisa kulitembelea darasa la ubatizo ili afahamiane na wataradhia. Mawasiliano kama hayo yataliwezesha kanisa kujiandaa vizuri zaidi kuwapokea washiriki wapya.

***Maandalizi ya Ubatizo***—Katika hafla ya ubatizo, mashemasi wa kiume watafanya maandalizi muhimu na kuwasaidia wataradhia wa kiume kuingia na kutoka majini. Mashemasi wa kike watawasaidia wataradhia wa kike.

Inapasa kuwe na uangalifu kuhakikisha kwamba mavazi stahiki yanatolewa kwa wataradhia, hasa majoho ya kitambaa kizito kinachofaa. Kama hakuna majoho, wataradhia hawana budi kuvaa mavazi ya staha.

Ubatizo hauna budi kufuatiwa na hafla fupi ya kuwakaribisha.

**Kubatizwa Tena**

Ubatizo wa kurudia unatajwa bayana katika Matendo 19:1-7 tu, ambapo Paulo aliuidhinisha kwa ajili ya kundi la waumini ambao ubatizo wao wa kwanza wa toba ulikuwa umefanywa na Yohana. Pamoja na toba, ubatizo wa Kikristo unaambatana na weledi na dhamira ya kuifuata injili na mafundisho ya Yesu na kupokea Roho Mtakatifu. Mahali ambapo kuna ongezeko la aina hiyo la weledi na dhamira, ubatizo mwingine unakubalika.

***Watu Kutoka Katika Jumuiya Nyingine za Kikristo***—Kwa kufuata Biblia, watu kutoka jumuiya nyingine za Kikristo ambao wamepokea imani za Kanisa la Waadventista wa Sabato na ambao wamewahi kubatizwa kwa kuzamishwa kabla ya hapo wanaweza kuomba kubatizwa tena.

Mifano ifuatayo, hata hivyo, inaonesha kuwa ubatizo wa kurudia unaweza usihitajike. Ni wazi kwamba tukio la Matendo 19 lilikuwa

la pekee, kwani Apolo anaelezewa kuwa alibatizwa ubatizo wa Yohana (Mdo. 18:25), na hakuna maelezo kwamba alibatizwa tena. Ni wazi kuwa baadhi ya mitume walibatizwa ubatizo wa Yohana (Yn. 1:35-40), lakini hakuna maelezo kwamba walibatizwa tena.

Ellen G. White anakubaliana na ubatizo wa kurudia kama muumini mpya amepata ukweli mpya wa msingi, kwa kadiri Roho atakavyomwongoza kuuomba. Hii ni kulingana na mtiririko wa matukio ya Matendo 19. Inampasa mtu aliyewahi kubatizwa kwa kuzamishwa kutathmini hali yake mpya ya kiroho na kuamua kama anataka ubatizo. Kusiwe na ushawishi wo wote.

"Hili (ubatizo wa pili) ni suala ambalo inampasa kila mtu kuamua kwa uangalifu katika hofu ya Mungu. Suala hili halina budi kuelezwa kwa roho ya upole na upendo. Kisha kazi ya kushawishi si ya mtu ye yote isipokuwa Mungu; mpatieni Mungu nafasi ya kufanya kazi katika mioyo kwa Roho wake Mtakatifu, ili mtu awe ameshawishika kikamilifu na kuridhika juu ya hatua hii kubwa."—Ev 373.

***Uasi na Ubatizo wa Pili*****—**Ingawa kulikuwa na uasi katika kanisa la mitume (Ebr. 6:4-6), Maandiko hayazungumzii suala la kubatizwa tena. Ellen G. White anakubaliana na ubatizo wa pili kama muumini ameasi na kisha akaongoka upya na kutaka kujiunga na kanisa. (tazama uk. 66, 67, 154.)

"Bwana anataka matengenezo ya thabiti. Na mtu anapokuwa ameongoka upya kwa dhati, basi abatizwe. Afanye upya agano lake na Mungu, na Mungu atafanya upya agano lake naye."—Ev 375.

***Ubatizo wa Kurudia Usiofaa*****—**Kulingana na mafundisho ya Biblia na uongozi wa Ellen G. White, ubatizo mwingine hauna budi kufanyika kutokana na mazingira maalum tu na inapasa uwe nadra. Kurudia rudia ubatizo au kubatiza kutokana na mihemko huhafifisha maana ya ubatizo na humaanisha kukosa weledi wa uzito na umuhimu ambao Maandiko yanaupatia ubatizo. Mshiriki ambaye hali yake ya kiroho imepoa anahitaji moyo wa toba ambao utaleta uamsho na matengenezo. Hali hiyo itafuatiwa na kushiriki katika huduma ya meza ya Bwana kuonesha utakaso mpya na ushirika katika mwili wa Kristo, jambo ambalo linafanya ubatizo mpya usiwe wa lazima.

**Kukiri Imani**

Watu ambao wamezikubali imani za msingi za Kanisa la Waadventista wa Sabato na ambao wanataka kuwa na ushirika katika Kanisa kwa kukiri imani wanaweza kukubaliwa katika moja ya mazingira manne yafuatayo:

1. Mkristo mwaminifu kutoka katika jumuiya nyingine ya Kikristo ambaye amekwisha kubatizwa kwa kuzamishwa kama ilivyo katika Kanisa la Waadventista wa Sabato. (tazama uk. 45.)
2. Mshiriki wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ambaye, kwa sababu zisizozuilika, ameshindwa kupata barua ya uhamisho kutoka katika kanisa lake. (tazama uk. 53)
3. Mshiriki wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ambaye ombi lake la uhamisho halijapata majibu kutoka mahali ulipo ushirika wake. Katika hali kama hiyo kanisa litaomba msaada wa konferensi husika.
4. Mtu ambaye alikuwa mshiriki, lakini ambaye ushirika wake umepotea au umeondolewa kwa kuwa alikuwa mshiriki asiyejulikana aliko, lakini ambaye ameendelea kuwa mwaminifu kwa ahadi zake za Kikristo.

Uangalifu mkubwa unatakiwa kuwepo katika kupokea washiriki kama wamewahi kuwa washiriki wa kanisa lingine. Mtu anapoomba ushirika kwa kukiri imani, upelelezi ufanywe juu ya hali ya nyuma ya mwombaji. Viongozi wa kanisa hawana budi kuomba ushauri wa mwenyekiti wa konferensi. Muda wa kutosha unatakiwa kutumika kupeleleza mambo yanayomhusu.

Mtu anapoomba ushirika kwa kukiri imani na ikaonekana kwamba bado ni mshiriki wa kanisa lingine, isichukuliwe hatua yo yote ya kumpokea mtu huyo katika ushirika mpaka kanisa lililo na ushirika wake litoe barua ya uhamisho.. Kama, baada ya kufuata mchakato wa uhamisho (tazama uk. 52), kanisa fulani limekataa kutoa barua ya uhamisho, na mshiriki huyo anaona kuwa barua hiyo imezuiliwa isivyostahili, mshiriki huyo anaweza kukata rufaa katika kamati ya konferensi. Kufuata utaratibu huu kutasababisha kuthaminiwa zaidi kwa utakatifu wa ushirika wa Kanisa na

urekebishaji wa makosa. Hakuna kanisa lenye haki ya kuzuia ushirika kama mtu huyo hayuko chini ya marudi.

Mtu ambaye ushirika wake umeondolewa akitaka kurejeshwa katika ushirika wa kanisa, kurejeshwa huko kwa kawaida hutanguliwa na ubatizo mpya. (Tazama uk 66, 67.)

**Kuhamisha Washiriki**

Mshiriki anapohamia mahali pengine, inampasa karani wa kanisa lenye taarifa za ushirika wake kumwandikia katibu wa konferensi husika akiomba mchungaji wa eneo hili jipya amtembelee mshiriki huyo ili kufanikisha uhamisho wa ushirika wake kwenda katika kanisa lingine.

Karani wa kanisa lililo na taarifa za ushirika huo pia hana budi kumjulisha mshiriki anayehama juu ya kusudi lake la kutoa anuani yake mpya kwa konferensi.

Washiriki wanaohamia kwenye eneo lingine kwa zaidi ya miezi sita hawana budi kuomba barua ya uhamisho mara moja. Washiriki wanaohamia kwenye maeneo ya pembezoni yasiyokuwa na kanisa jirani hawana budi kuomba kujiunga na kanisa la konferensi.

***Utaratibu wa Kutoa Barua za Uhamisho*—**Inampasa mshiriki kuomba barua ya uhamisho kwa karani wa kanisa analotaka kujiunga nalo. Karani wa kanisa atatuma ombi kwa karani wa kanisa ambalo mshiriki huyo anatoka. (tazama uk. 53 kwa ajili ya utaratibu mwingine.)

Karani wa kanisa analotoka akipata ombi hilo, ataliwasilisha kwa mchungaji au mzee wa kanisa, ambaye ataliwasilisha kwenye baraza. Baada ya tafakari stahiki, baraza litapiga kura kupendekeza kwa kanisa, kukubali au vinginevyo. (tazama uk. 37-39, 41, 49-55, 65-67, 80.) kisha mchungaji au mzee wa kanisa ataliwasilisha pendekezo hilo mbele ya kanisa kusomwa kwa mara ya kwanza. Uamuzi wa mwisho utafanyika juma linalofuata, pendekezo hilo litakapowasilishwa kwa ajili ya kura.

Kusudi la kipindi cha juma moja ni kuwapa washiriki furasa ya kupinga kutolewa kwa barua hiyo. Kwa kawaida mapingamizi hayapasi kutolewa hadharani bali yawasilishwe kwa mchungaji au mzee wa kanisa, ambaye atayawasilisha mbele ya baraza kwa

ajili ya uchunguzi. Inalipasa baraza kumpatia kila anayepinga fursa ya kuja kuwasilisha pingamizi lake. Kama pingamizi hilo halina sababu za msingi, mtu aliyeweka pingamizi atatakiwa kuliondoa. Kama pingamizi lina sababu za msingi, ni wajibu wa baraza kupeleleza. Uamuzi wa mwisho kuhusu utoaji wa barua ya uhamisho utaahirishwa mpaka suala hilo litakapowekwa sawa kikamilifu.

Kama pingamizi lihahusu uhusiano baina ya watu, juhudi zote zifanyike kuleta mapatano. Kama kuna makosa yaliyofanywa hadharani, hatua za kinidhamu zinaweza kuhitajika. Kama kuna uzembe wa kiroho, juhudi za kumrejesha mshiriki huyo hazina budi kufanyika.

***Karani Aandae Barua***—Kanisa likiridhia barua hiyo ya uhamisho, karani atajaza fomu ya uhamisho na kuituma kwa karani wa kanisa litakalompokea yule mshiriki. Karani wa kanisa analohamia atawasilisha barua hiyo kwa mchungaji au mzee wa kanisa, ambaye ataipeleka kwenye baraza kwa ajili ya mapendekezo, na baada ya hapo pendekezo hilo litawasilishwa mbele ya kanisa wakati wa huduma ya ibada inayofuata. Kura ya kumpokea mtu huyo katika ushirika kwa kawaida hupigwa wakati wa ibada juma moja baadaye. Karani wa kanisa analohamia ataandika jina la mshiriki huyo na tarehe ya kupokelewa katika kumbukumbu za washiriki. Karani pia atajaza sehemu ya majibu ya ile barua ya uhamisho, akithibitisha kuwa yule mshiriki amepokelewa na kuirejesha kwa karani wa kanisa alilotoka yule mshiriki.

***Barua ya Uhamisho ni Halali kwa Miezi Sita***—Barua ya uhamisho itakuwa halali kwa miezi sita kuanzia siku ilipotolewa.

***Njia Nyingine ya Kuhamisha Ushirika***—Divisheni inaweza kuidhinisha njia nyingine ya kuhamisha washiriki kati ya makanisa yaliyo ndani ya divisheni husika, lakini washiriki wanapoomba uhamisho kwenda kanisa lililo katika divisheni nyingine, Njia iliyo hapo juu “Utaratibu wa Kutoa Barua za Uhamisho” haina budi kufuatwa.

***Ushirika Wakati wa Uhamisho*****—**Kwa hali yo yote ile, karani wa kanisa analotokea mshiriki, hataliondoa jina la mshiriki katika kumbukumbu za washiriki mpaka ipokelewe sehemu ya barua ya uhamisho inayothibitisha kuwa mshiriki huyo amepokelewa katika ushirika wa kanisa analohamia. Kufanya hivyo kutamkosesha mtu huyo ushirika wakati wa uhamisho. Karani, wazee, mchungaji na mwenyekiti wa konferensi wote wanawajibika kuhakikisha kuwa makanisa yote yanafuata utaratibu huu.

***Kupokea Washiriki Wakati wa Matatizo*****—**Wakati mwingine hali ya ulimwengu huzuia mawasiliano juu ya uhamisho wa ushirika. Katika hali kama hiyo, italipasa kanisa linalopokea mshiriki kujiridhisha, kwa kushauriana na konferensi, juu ya uhai wa mwombaji na kisha kumpokea katika ushirika kwa kukiri imani. Kama baadaye njia ya kuwasiliana na kanisa analotoka au koferensi ambako kanisa hilo lipo itafunguka, italipasa kanisa analohamia kutuma barua inayoeleza lilivyofanya.

***Ajumuishwe Katika Taarifa za Takwimu*****—**Taarifa za takwimu za robo na za mwaka zinapoandaliwa, mshiriki ambaye amepewa barua ya uhamisho, lakini barua yake ya kupokelewa haijapokelewa, atahesabiwa kuwa mshiriki wa kanisa analotoka. Barua ya kupokelewa itakapofika, jina lake litaondolewa katika kumbukumbu za washiriki wa kanisa analotoka, na hataingizwa katika taarifa zitakazofuata.

***Kama Mshiriki Hatapokelewa*****—**Kanisa analohamia halina budi kumpokea mshiriki huyo kama halijui sababu yo yote halali ya kumnyima fursa ya kuwa mshiriki. Kama kanisa halitampokea mshiriki huyo, karani atairudisha barua hiyo kwa kanisa analotoka pamoja na maelezo kamili ya sababu za kumkataa. Wakati huo ushirika wa mtu huyo utabaki katika kanisa analotoka, ambalo litakuwa halina budi kushirikiana na mshiriki huyo kutatua tatizo hilo.

***Barua Zitolewe kwa Washiriki Hai Tu*****—**Barua za uhamisho hutolewa kwa washiriki walio hai tu, na si kwa washiriki walio

chini ya marudi. Maelezo ya ziada hayakubaliki isipokuwa pale mchungaji au baraza la kanisa analotoka mtu huyo linajua kwa hakika kuwa mshiriki huyo amehusika katika kosa la kunajisi watoto. Katika hali hiyo, kwa ajili ya usalama wa watoto, itampasa mchungaji au mzee kutoa maelezo ya siri kumwarifu mchungaji au mzee wa kanisa analohamia mshiriki huyo.

Kama mshiriki aliyehamia kwenye kanisa lingine amepoa, mchungaji au mzee wa kanisa analotoka anaweza kuongea na mchungaji au mzee wa kanisa analohamia ili jambo hilo liwe wazi kabla uhamisho haujatolewa.

***Barua Isitolewe Bila Idhini ya Mshiriki*****—**Kwa hali yo yote ile kanisa haliwezi kupiga kura ya kutoa barua ya uhamisho kinyume na matakwa ya mshiriki, wala kanisa haliwezi kupokea mshiriki kwa barua iliyotolewa katika mazingira hayo. Ushirika ni uhusiano mahususi wa mtu na mwili wa Kristo, na inalipasa kanisa kuutambua uhusiano huo na kuepuka tendo lo lote linaloweza kuchukuliwa kama la kulazimisha.

Kwa upande mwingine, mshiriki hana budi kuutambua ustawi wa kanisa na kufanya kila juhudi kulipunguzia kanisa matatizo yanayotokana na washiriki wasiojulikana waliko. Mshiriki anapohama, inampasa kuomba barua ya uhamisho mara moja.

Inapotokea kanisa limeondolewa kutoka katika jumuiya ya makanisa kwa uamuzi wa kikao cha konferensi, ushirika wa washiriki wote waaminifu, isipokuwa wale watakaokataa, utachukuliwa kuwa umehamia katika kanisa la konferensi kwa muda. Baada ya hapo kanisa la konferensi linaweza kutoa barua za uhamisho kwa ajili ya washiriki waaminifu na kushughulikia ushirika wa watu wengine kadiri itakavyokuwa lazima. (tazama uk. 40-43.)

***Baraza la Kanisa Haliwezi Kutoa Barua*****—**Baraza halina mamlaka ya kuamua juu ya barua za uhamisho au kupokea washiriki kwa barua. Mamlaka ya baraza yanaishia katika kutoa mapendekezo kwa kanisa. Uamuzi juu ya uhamisho wote wa ushirika, wa kukubali au kukataa, hauna budi kufanywa na kanisa. (tazama uk. 52.) Karani hana mamlaka ya kuondoa au kuingiza

majina katika kumbukumbu za washiriki isipokuwa kwa kura ya kanisa. Mshiriki akifa, karani ataingiza tarehe ya kifo katika kumbukumbu za washiriki, na hauhitajiki uamuzi wa kanisa.

***Ushirika Katika Kanisa la Konferensi*****—**Washiriki wanaokaa mahali pasipo na kanisa/kundi, hawana budi kujiunga na kanisa la Konferensi, ambalo ni jumuiya iliyoundwa kwa ajili ya washiriki wasiokuwa na bahati ya kuwa na kanisa. Washiriki vikongwe na wasiojiweza wanaoishi karibu na kanisa na maofisa na wafanyakazi wengine wa konferensi, pamoja na wachungaji, hawana budi kuwa washiriki wa kanisa mahalia, na si kanisa la konferensi.

Mwenyekiti wa konferensi ndiye mzee kiongozi wa kanisa la konferensi, na kazi ambayo kwa kawaida hufanywa na karani na mhazini itafanywa na katibu na mhazini wa konferensi. Kwa kuwa kanisa hili halina baraza, shughuli zote ambazo kwa kawaida hufanywa na baraza la kanisa mahalia hufanywa na kamati ya konferensi, ambayo pia huchagua wawakilishi wa kanisa hili katika mkutano mkuu wa konferensi.

***Kumbukumbu za Washiriki*****—**Kanisa halina budi kuwa na kitabu kimoja cha ushirika. Majina huingizwa au kuondolewa kwa kura ya kanisa tu au kwa kifo. (tazama uk. 80.) Kwa hali yo yote ile kanisa lisiwe na orodha ya watu ambao ushirika wao umekoma.

SURA YA 7

# Marudi ya Kanisa

**Kanuni Kuu**

Biblia na Roho ya Unabii vinaeleza kwa lugha bayana isiyoweza kukosewa unyeti wa wajibu walio nao watu wa Mungu kudumisha usafi wao, unyoofu na ari yao ya kiroho. Washiriki wakipoa au kutanga mbali, kanisa halina budi kuwarejesha kwa ajili ya Bwana.

Kushuhgulikia Washiriki Waliokosa—“Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza hao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni” (Mat. 18:15-18).

“Katika kushughulikia washiriki waliokosa, inawapasa watu wa Mungu kufuata kwa makini maelekezo yaliyotolewa na Mwokozi katika sura ya kumi na nane ya Kitabu cha Mathayo.

“Wanadamu ni mali ya Kristo, aliowanunua kwa gharama isiyopimika, wakaunganishwa naye kwa upendo ambao yeye na Baba yake wameuonesha kwa ajili yao. Basi, inatupasa kuwa makini sana tunaposhughulikia mambo yetu sisi kwa sisi! Watu hawana haki ya kuhisi uovu dhidi ya wanadamu wenzao. Washiriki wa kanisa hawana haki ya kufuata misukumo na matakwa yao katika kushughulikia matatizo ya washiriki wenzao waliokosa. Haiwapasi hata kueleza maoni yao juu ya wakosaji, kwani kwa kufanya hivyo huwa wanatia chachu ya uovu katika mioyo mingine. …

“‘Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu.’ … Usiwaeleze watu wengine kosa hilo. Mtu mmoja akiambiwa, kisha mwingine, na hata mwingine tena; na habari hizo

huendelea kuenea, na uovu huzidi, mpaka kanisa lote huathirika. Malizeni tatizo hilo ‘wewe na yeye peke yenu.’ Huo ndio mpango wa Mungu.”—7T 260.

***Mpango wa Mungu—***“Hata kama kosa ni la aina gani, hiyo haibadilishi mpango ambao Mungu ameuandaa kwa ajili ya kusuluhisha migongano na maudhi binafsi. Kuongea peke yenu na yule aliyekosa, tena katika roho ya Kristo kutaondoa tatizo. Mwendee aliyekosa kwa moyo uliojaa upendo na huruma ya Kristo, na ujaribu kurekebisha lile tatizo. Hojiana naye kwa upole na utulivu. Usiruhusu maneno ya ukali kutoka katika mdomo wako. Ongea katika njia ambayo itabadili mtazamo wake. Kumbuka usemi huu: ‘Yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika njia ya upotevu, ataokoa roho na mauti, na kufunika wingi wa dhambi.’ Yakobo 5:20. …

“Mbingu yote hufuatilia mazungumzo kati ya yule aliyeudhiwa na yule aliyekosa. Yule mkosaji anapopokea maonyo yaliyotolewa kwa upendo wa Kristo, na kukiri kosa lake akiomba msamaha kwa Mungu na kwa ndugu yake, nuru ya mbinguni hujaa moyoni. . . Roho wa Mungu huunganisha moyo na moyo, na huwa kuna muziki mbinguni kwa ajili ya umoja uliopatikana. . .

“‘La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike.’ . . . Chukua pamoja nawe watu wenye moyo wa kiroho na mwongee na yule mkosaji juu ya lile kosa. . . Akiona mwafaka walio nao katika suala hilo, moyo wake unaweza kuangaziwa.

“‘Na asipowasikiliza hao,’ kufanyike nini sasa? Je, watu wachache katika baraza wabebe jukumu la kumwondoa mkosaji katika ushirika? ‘Na asipowasikiliza hao, liambie *kanisa*.’ . . .Liachie kanisa lichukue hatua juu ya washiriki wake.

“Na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru.’ . . Asipoisikia sauti ya kanisa, akizikataa juhudi zote zilizofanyika kumwongoa,

kanisa lina wajibu wa kumtenga na ushirika. Jina lake halina budi kufutwa katika vitabu.

"Ofisa ye yote wa kanisa haruhusiwi kushauri, kamati yo yote ile hairuhusiwi kupendekeza, wala kanisa lo lote haliruhusiwi kupiga kura, kwamba jina la mkosaji liondolewe katika vitabu vya kanisa, mpaka maelekezo yaliyotolewa na Kristo yamefuatwa kwa uaminifu. Maelekezo haya yakifuatwa, kanisa litakuwa halina hatia mbele za Mungu. Uovu huo sasa utakuwa hauna budi kudhihirishwa kama ulivyo na kuondolewa, ili usienee zaidi na zaidi. Uhai na usafi wa kanisa hauna budi kuhifadhiwa, ili liweze kusimama mbele ya Mungu bila mawaa, likiwa limevikwa mavazi ya haki ya Kristo. …

Kristo akaendelea, "'Amin, nawaambia, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.' …

"Kauli hii ina nguvu katika vizazi vyote. Uwezo wa kuchukua hatua kwa niaba ya Kristo umewekwa kwa kanisa. Ni chombo cha Mungu kwa ajili ya kuhifadhi utaratibu na nidhamu miongoni mwa watu wake. Bwana amelipatia uwezo wa kuamua mambo yanayohusu ustawi, usafi, na utaratibu wa kanisa. Kanisa lina wajibu wa kuondoa watu wasiofaa katika ushirika wake, wanaoudhalilisha ukweli kwa tabia yao isiyofanana na ya Kristo. Jambo lo lote ambalo kanisa litafanya kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa katika Neno la Mungu litaidhinishwa mbinguni."—7T 260-263.

***Mamlaka ya Kanisa*—**"Mkombozi wa ulimwengu alilipatia uwezo mkubwa kanisa lake. Anaelezea kanuni za kufuatwa katika mashauri ya washiriki wake. Baada ya kutoa maelekezo dhahiri kuhusu njia ipasayo kufuatwa, Anasema: 'Amin, nawaambia, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua [katika marudi ya kanisa] duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni. Kwa njia hiyo, hata mamlaka ya mbinguni huidhinisha marudi ya kanisa kwa washiriki wake kama kanuni ya Biblia imefuatwa.

"Neno la Mungu haliruhusu mtu mmoja kung'ang'ania maoni yake yanayopingana na uamuzi wa kanisa, wala haruhusiwi kusisitiza maoni yake dhidi ya yale ya kanisa."—3T 428.

***Wajibu wa Kanisa*—**“Mungu huwawajibisha watu wake, kama jumuiya, kwa ajili ya dhambi zilizo ndani ya watu binafsi walio miongoni mwao. Viongozi wa kanisa wakipuuza kuchunguza kwa makini dhambi zinazoleta hasira ya Mungu dhidi ya jumuiya, watawajibika kwa ajili ya dhambi hizo.”—3T 269.

“Kusingekuwa na marudi na utawala wa kanisa, kanisa lingepasuka vipande vipande; lisingeweza kushikamana kama jumuiya.”—3T 428.

***Watu Wasiotakasika Hupinga Marudi*—**“Wapo wengi wasiokuwa na uwezo wa kuamua kama Joshua na ambao hawajishughulishi kuchunguza makosa na kushughulikia ipasavyo dhambi zilizo miongoni mwao. Watu kama hao wasiwazuie wale wanaoona kuwa wana wajibu wa kazi hii; wasiwe kizuizi kwa wale wanaoifanya kazi hii. Wengine wanaona ni muhimu kuhoji na kutilia mashaka na kutafuta kasoro kwa sababu wengine wanaifanya kazi ambayo Mungu hakuwatuma wao. Hawa huwa wanawakwamisha moja kwa moja wale ambao Mungu amewapa wajibu wa kukemea na kurekebisha dhambi zinazoendelea ili hasira yake iondolewe kwa watu wake. Suala kama la Akani lingekuwa miongoni mwetu, wapo wengi ambao wangewashutumu wale ambao wangechukua nafasi ya Joshua katika kuchunguza lile kosa, kwamba wana roho mbaya ya kutafuta kasoro. Mungu hawezi kuchezewa na maonyo yake kupuuzwa na watu wakaidi bila kutarajia adhabu. …

“Wale wanaojishughulisha kwa kicho cha Mungu kuliondolea kanisa vikwazo na kusahihisha makosa makubwa, ili watu wa Mungu waone umuhimu wa kuchukia dhambi na kukua katika usafi, na ili jina la Mungu litukuzwe, watakutana na nguvu kinzani kutoka kwa wale wasiotakasika.”—3T 270, 271.

***Kulinda Umoja wa Kanisa*—**Inawapasa Wakristo kufanya kila juhudi kuepuka mitazamo inayoweza kuwagawa na kuziaibisha harakati zao. “Kusudi la Mungu ni kwamba, watoto wake waungane katika umoja. Je, hawatarajii kuishi pamoja katika mbingu moja? … Wale wanaokataa kufanya kazi kwa umoja humfedhehesha sana Mungu.”—8T 240. Inalipasa kanisa kuzuia matendo yanayotishia umoja miongoni mwa washiriki wake na inalipasa kuhimiza umoja

siku zote.

Ingawa washiriki wana haki sawa ndani ya kanisa, hakuna mshiriki, au kikundi kinachoruhusiwa kuanzisha harakati au kuanzisha jumuiya au kutaka kupata wafuasi kwa ajili ya kutimiza lengo au kwa ajili ya kufundisha fundisho au ujumbe usioafikiana na makusudi ya msingi ya kidini na mafundisho ya kanisa. Kitendo cha namna hiyo kitasababisha kujenga moyo wa faraka, kusambaratika kwa ushuhuda wa Kanisa, na kwa njia hiyo, kuzuia Kanisa kutekeleza majukumu yake kwa Bwana na kwa ulimwengu.

Matatizo baina ya ndugu yasingewekwa wazi kwa watu wengine, ila yakaongelewa kwa uaminifu kati yao wenyewe katika roho ya upendo wa Kikristo, uovu mwingi sana ungezuiwa! Mizizi mingi ya uchungu ingeangamizwa, na wafuasi wa Kristo wangeungana katika upendo wake kwa ukaribu na wema mkubwa.

***Kusuluhisha Ugomvi***—Kila juhudi haina budi kufanyika kusuluhisha ugomvi miongoni mwa washiriki wa kanisa na kudhibiti migogoro ikiwa katika hatua inayohusisha watu wachache kadiri iwezekanavyo. Suluhu ya ugomvi katika kanisa, mara nyingi inawezekana bila kupelekwa ama katika mchakato wa usuluhishi utolewao na kanisa au vyombo vy sheria.

"Ugomvi, mivutano na daawa kati ya ndugu hudhalilisha harakati za kueneza ukweli. Wanaochukua hatua hiyo hulisababishia kanisa dhihaka kutoka kwa maadui wake na kuzifanya nguvu za giza zishinde. Wanayachoma majeraha ya Kristo upya na kumfedhehi kwa dhahiri. Kwa kupuuza mamlaka ya kanisa wanaonesha dharau yao kwa Mungu, ambaye amelipa kanisa mamlaka yake."—5T 242, 243.

Mara nyingi madai ya mahakamani hufanywa kwa moyo wa mashindano ambao hutokana na ubinafsi na hudhihirisha ubinafsi. Kesi zenye uhasama kama hizo hazina budi kupingwa na kanisa linalotaka kudhihirisha moyo wa Kristo. Hali ya Kikristo ya kutokuwa na ubinafsi itawafanya wafuasi wa Kristo wakubali kudhulumiwa (1 Kor. 6:7) kuliko "kushitaki mbele ya wasio haki, wala si mbele ya watakatifu" (1 Kor 6:1).

Ingawa katika ulimwengu wa kisasa, kuna wakati inapobidi kutafuta uamuzi wa mahakama, inawapasa Wakristo kuchagua suluhu ndani ya mamlaka ya Kanisa, na watafute uamuzi wa

mahakama katika masuala ambayo mahakama hizo zina uwezo nayo na ambayo yako nje ya uwezo wa Kanisa, au ambayo kanisa linaona kwamba halina nyenzo za kutosha kupata suluhu inayofaa. Kesi kama hizo katika mahakama, zisiwe za uhasama wa kulipiza kisasi lakini zijenge shauku ya kutafuta suluhu na kumaliza ugomvi kwa amani.

Mifano ya kesi kama hizo inaweza kuwa pamoja, ingawa haiishii kwenye kuamua kuhusu madai ya bima, kufanya uamuzi juu ya mipaka na umiliki wa mali isiyohamishika, kuamua juu ya usimamizi wa mirathi, na kutoa dhamana ya uangalizi wa watoto walio chini ya umri wa mtu mzima.

Pamoja na kwamba inalipasa Kanisa kuweka taratibu za kuepuka aina ya kesi zilizoelezwa katika 1 Wakorintho 6 bila kukiuka mipaka ya sheria, kanisa halina budi kuwa macho wakati wote lisije likaacha kazi yake ya injili na kufanya kazi za hakimu. (Tazama Luka 12:13, 14 na 9T 216-218.)

Mpango wa Mungu kwa ajili ya watu wake ni kuishi "kwa amani na watu wote" (Rum. 12:18) kama yamkini kwa upande wao. Inalipasa Kanisa kutumia utaratibu wake upatikanao kirahisi na kwa haraka unaoweza kusaidia kusuluhisha ugomvi mwingi baina ya washiriki. Kanisa likishindwa kuchukua hatua baada ya kuombwa kusuluhisha ugomvi fulani, au kama Kanisa likikiri kwamba aina hiyo ya tatizo iko nje ya mamlaka yake, ieleweke kwamba mshiriki huyo atakuwa ametumia uwezekano wote wa mchakato wa kusuluhisha ugomvi ulioelezwa katika Biblia na kwamba atakachofanya baada ya hapo kitategemea dhamiri yake. (Tazama *The SDA Bible Commentary,* vol. 6, uk. 698.

Hata hivyo, kanisa linapojaribu kusaidia katika kupata suluhu ya ugomvi kati ya washiriki kwa wakati na kwa njia ya amani na kupendekeza ufumbuzi, washiriki wasiukatae ufumbuzi huo bila kutafakari kwa kina. Kama 1 Wakorintho 6:7 inavyosema, si jambo dogo kwa mshiriki kupeleka shauri dhidi ya mshiriki mwingine nje ya utaratibu wa kanisa.

Washiriki wanaoonesha kukosa uvumilivu na kuonesha ubinafsi kwa kutokuwa tayari kusubiri na kukubaliana na mapendekezo ya Kanisa katika kusuluhisha malalamiko yao dhidi ya washiriki wengine, wanaweza kuwekwa chini ya marudi ya kanisa kihalali

(tazama uk. 58, 59), kwa sababu ya usumbufu kwa Kanisa na kukataa kwao kutambua mamlaka ya Kanisa iliyowekwa kihalali.

***Usuluhishi wa Malalamiko ya Washiriki Dhidi ya Kanisa***—Kanuni zile zile zinazotumika kuleta suluhu ya ugomvi kati ya washiriki zitatumika kusuluhisha malalamiko ya washiriki dhidi ya Kanisa na taasisi zake.

Washiriki wasichukue hatua za kisheria dhidi ya kitengo cho chote cha kanisa isipokuwa katika mazingira ambapo kanisa halijatoa utaratibu unaofaa kushughulikia vizuri malalamiko hayo au ambapo ni bayana kuwa aina ya tatizo hilo iko nje ya uwezo wa Kanisa kusuluhisha.

***Usuluhishi wa Malalamiko ya Kanisa Dhidi ya Washiriki***—Wakati mwingine jumuiya au taasisi za kanisa zinaweza kuwa na malalamiko dhidi ya washiriki. Katika hali kama hiyo, viongozi wa Kanisa hauna budi kuzingatia kwa uvumilivu ushauri wa Biblia katika kutatua migogoro kati ya Wakristo na kutumia ushauri huo kusuluhisha malalamiko ya Kanisa dhidi ya washiriki wake. Inalipasa kanisa kufanya kila juhudi inayowezekana, kwa kushirikiana na mshiriki husika kuandaa mchakato utakaotumika kusuluhisha vizuri tatizo hilo badala ya kushitaki katika mahakama za kiraia.

Kanisa linatambua haja ya kuwa na uangalifu mkubwa kulinda maslahi ya juu kabisa ya kiroho kwa washiriki wake, kuhakikisha wanatendewa haki, na kulinda jina la Kanisa. Kanisa haliwezi kuchukulia kwa wepesi dhambi kama hizo au kuruhusu mawazo binafsi kuathiri shughuli zake, na wakati huo huo halina budi kuwatafuta na kuwarejesha waliokosa.

"Yule aliyekosa akitubu na kutii marudi ya Kristo, hana budi kujaribiwa tena. Na hata asipotubu, hata akibaki nje ya kanisa, watumishi wa Mungu bado wana kazi ya kufanya kwa ajili yake. Inawapasa kujitahidi sana kumfanya atubu. Hata kama kosa lake ni kubwa sana, akijisalimisha chini ya nguvu ya Roho Mtakatifu, na akaonesha toba kwa kuungama na kuiacha dhambi yake, hana budi kusamehewa na kukaribishwa tena katika zizi. Ndugu zake hawana budi kumtia moyo kwa njia sahihi, wakimtendea vile

ambavyo wangependa kutendewa kama wangekuwa mahali pake, wakijiangalia wao wenyewe wasijaribiwe pia"—7T 263.

**Sababu za Marudi**

Sababu zitakazofanya washiriki wawekwe chini ya marudi ni:

1. Kukana imani juu ya misingi ya injili na juu ya imani za msingi za Kanisa au kufundisha mafundisho yaliyo kinyume.
2. Kuvunja sheria ya Mungu, kama vile kuabudu sanamu, kuua, kuiba, mwenendo mbaya au tabia chafu, kucheza kamari, kuvunja Sabato, na udanganyifu wa makusudi na wa mara kwa mara.
3. Kuvunja amri ya saba ya sheria ya Mungu kuhusu ndoa, nyumba ya Kikristo, na viwango vya Biblia vya tabia ya uadilifu.
4. Kunajisi watoto, vijana, na watu wazima wasioweza kujilinda, uasherati, ufuska, kujamiiana kwa maharimu, ushoga, kutengeneza, kutumia au kusambaza ponografia au upotovu mwingine katika ngono.
5. Kuoa/kuolewa kwa mtalaka, isipokuwa mwanandoa aliyeendelea kuwa mwaminifu kwa ahadi za ndoa aliyeachana kwa sababu ya uzinzi au upotovu katika ndoa.
6. Kipigo, ikiwa ni pamoja na kipigo ndani ya familia.
7. Kughushi au kudanganya katika biashara.
8. Tabia mbaya iletayo fedheha kwa kanisa
9. Kuwa mfuasi au kushiriki katika kikundi au jumuiya iletayo utengano au iliyoasi (tazama uk. 59).
10. Kuendelea kukataa kutambua mamlaka ya kanisa iliyowekwa kihalali au kukataa kutii agizo au marudi ya kanisa.
11. Kutumia, kutengeneza au kuuza vileo
12. Kutumia, kutengeneza au kuuza tumbaku katika aina zake zote kwa ajili ya matumizi ya binadamu.
13. Kutumia au kutengeneza dawa haramu au matumizi mabaya au biashara haramu ya dawa za kulevya au dawa zingine.

**Utaratibu wa Marudi**

Kunapokuwa na dhambi kubwa, kanisa lina njia mbili za kuchukua hatua za kinidhamu.

1. Kwa kupiga kura ya karipio
2. Kwa kupiga kura ya kuondoa katika ushirika

***Marudi kwa Njia ya Karipio*—**Mahali ambapo kosa halionekani kuwa zito kwa kanisa kiasi cha kuchukua hatua ya kuondoa katika ushirika, kanisa linaweza kuonesha kutokuridhia kosa hilo kwa kura ya karipio.

Karipio lina makusudi mawili: (1) Kuliwezesha kanisa kuonesha kutoridhia kosa kubwa lililoleta aibu kwa kazi ya Mungu na (2) Kuwaonesha washiriki waliokosa haja ya kubadili maisha yao na kurekebisha tabia na kuwapa kipindi cha rehema ili wafanye mabadiliko hayo.

Uamuzi wa karipio ni kwa kipindi kitakachoelezwa kuanzia kipindi kidogo kabisa cha mwezi mmoja hadi kipindi cha juu kabisa cha miezi 12. Husitisha uchaguzi au uteuzi wa mshiriki aliyekosa katika wadhifa wo wote na kumwondolea haki ya kuchaguliwa katika kipindi hicho. Mshiriki aliye katika karipio hana haki ya kushiriki kwa kauli au kura katika masuala ya kanisa au kuongoza katika shughuli za kanisa, kama vile kufundisha darasa la Shule ya Sabato. Hata hivyo hanyang’anywi haki yake ya kushiriki baraka za Shule ya Sabato, ibada, na meza ya Bwana. Ushirika hauwezi kuhamishwa katika kipindi cha karipio.

Uamuzi wa karipio usiwe na vipengele vinavyohusu kuondolewa kwa ushirika endapo atashindwa kutimiza masharti yaliyowekwa. Tathmini itafanyika mwishoni mwa kipindi cha karipio kuona kama mshiriki aliyerudiwa amebadili mwenendo. Tabia yake ikiwa ya kuridhisha, anaweza kuhesabiwa kuwa hai bila hatua nyingine na atajulishwa kuwa karipio limekwisha. Tabia yake isiporidhisha, kanisa litafikiria tena marudi yanayofaa. Kurejea katika wadhifa wo wote wa kanisa itakuwa kwa kuchaguliwa.

***Marudi kwa Kuondoa Katika Ushirika*—**Kuondoa watu katika ushirika kanisani, yaani mwili wa Kristo, ni hatua ya mwisho kabisa ambayo kanisa linaweza kuchukua. Baada tu ya maelekezo yaliyotolewa katika sura hii kufuatwa, baada ya ushauri kutoka

kwa mchungaji, na baada ya juhudi zote zinazowekana za kumpata na kumrejesha mshiriki katika njia sahihi kufanyika, ndipo ataondolewa katika ushirika.

***Hakuna Kipimo cha Ziada cha Ushirika*****—**Hakuna mchungaji, kanisa au konferensi iliyo na mamlaka ya kuweka vipimo vya ushirika. Mamlaka hayo yako katika kikao cha Konferensi Kuu. Ye yote anayetaka kutumia kipimo kingine zaidi ya vile vilivyotajwa katika mwongozo huu, atakuwa haliwakilishi kanisa ipasavyo. (Tazama 1T 207.)

***Wakati Mwafaka wa Marudi*****—**Kanisa halina budi kushughulikia mchakato wa marudi katika muda mwafaka na kueleza uamuzi wake kwa huruma na upesi. Kuchelewa kushughulikia marudi kunaweza kuongeza usumbufu na uchungu kwa yule mshiriki na kanisa lenyewe.

***Angalizo Juu ya Kuhukumu Tabia na Dhamira*****—**"Kristo amefundisha wazi kuwa inawapasa wale wanaoendelea kufanya dhambi ya wazi kutengwa na ushirika, lakini hajatupatia kazi ya kuhukumu tabia na dhamira. Anajua sana tulivyo kiasi kwamba hawezi kutukabidhi kazi hiyo. Tukijaribu kuwatoa kanisani wale tunaodhani kuwa ni Wakristo wa bandia, bila shaka tutafanya makosa. Mara nyingi watu ambao Kristo anawavuta waje kwake, sisi huwa tunawaona kuwa hawaponyeki. Tungewashughulikia watu hawa kulingana na uamuzi wetu wenye dosari, pengine tungezimisha tumaini lao la mwisho. Wengi wanaojiona kuwa ni Wakristo, hatimaye wataonekana kuwa wamepungua. Mbinguni watakuwepo watu wengi ambao majirani zao walidhani wasingeingia huko. Mwanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo. Magugu na ngano havina budi kukua pamoja mpaka wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno ndio mwisho wa muda wa rehema. Katika maneno haya ya Mwokozi kuna somo lingine, somo la uvumilivu wa ajabu na upendo. Kama mizizi ya magugu inavyoingiliana na ile ya ngano ndivyo ndugu wa uongo walivyo na uhusiano wa karibu na wanafunzi wa kweli. Tabia halisi ya waumini hawa wa bandia haijadhihirika kikamilifu. Wakitengwa

na kanisa, wengine ambao wangeweza kusimama imara, wanaweza kukwazwa"—COL 71, 72.

***Katika Kikao Kilichoitishwa Kihalali*—**Washiriki wanaweza kurudiwa kwa sababu za kutosha, lakini iwe katika mkutano mkuu ulioitishwa kihalali (tazama uk. 123, 124) baada ya baraza la kanisa kupitia suala husika. Mkutano huo utaongozwa na mchungaji aliyewekewa mikono, au mchungaji mwenye cheti aliyewekewa mikono kama mzee wa kanisa husika, au kama mchungaji hayupo, mzee wa kanisa mahalia kwa kushauriana na mwenyekiti wa konferensi.

***Kwa Zaidi ya Nusu ya Kura*—**Washiriki wanaweza kuondolewa katika ushirika au kurudiwa vinginevyo kwa zaidi ya nusu ya kura za washiriki waliohudhuria na kupiga kura katika mkutano ulioitishwa kihalali tu. "Zaidi ya nusu ya kanisa ni nguvu inayopasa kutawala washiriki wake mmoja mmoja."—5T 107.

***Baraza la Kanisa Haliwezi Kuondoa Washiriki*—**Baraza linaweza kupendekeza kwa mkutano mkuu kuondoa washiriki, lakini kwa hali yo yote ile, baraza halina haki ya kufanya uamuzi wa mwisho. Isipokuwa katika suala la kifo cha mshiriki, karani hawezi kuondoa jina katika kitabu kabla ya uamuzi wa kanisa katika mkutano mkuu.

***Haki za Msingi za Washiriki*—**Washiriki wana haki ya msingi ya kujulishwa kabla ya mkutano wa marudi na haki ya kusikilizwa wakijitetea, kutoa ushahidi na kuleta mashahidi. Kanisa lo lote lisipige kura ya kumwondoa mshiriki katika mazingira yanayomnyima mshiriki husika haki hizo. Taarifa ya maandishi lazima itolewe angalao majuma mawili kabla ya mkutano na iwe na sababu za mkutano huo wa nidhamu.

***Wanasheria Wasiwakilishe Washiriki*—**Kazi ya Kanisa katika kusimamia utaratibu na nidhamu ni jukumu la kikanisa ambalo halina uhusiano wo wote na taratibu za kiraia au kisheria kwa namna yo yote ile. Kwa hiyo, Kanisa halitambui haki ya washiriki kuleta

wanasheria kuwawakilisha katika mkutano wo wote ulioitishwa kushughulikia utaratibu au nidhamu au kushughulikia jambo lingine lo lote la kanisa. Mshiriki anayetaka kuleta mwanasheria katika mkutano hana budi kuarifiwa kuwa hatasikilizwa aking'ang'ania kuleta mwanasheria.

Kanisa pia halina budi kutohusisha wasio washiriki katika mkutano wo wote wa kanisa ulioitishwa kushughulikia utaratibu na nidhamu ya kanisa, isipokuwa pale wanapoitwa kama mashahidi.

***Kuhamisha Washiriki Walio Katika Karipio*****—**Kanisa lo lote lisipokee katika ushirika mtu aliye katika karipio la kanisa lingine, kwani jambo hilo litakuwa ni kukubaliana na makosa yaliyofanya arudiwe. Kupokea mshiriki aliye katika karipio ni ukiukaji mkubwa wa sera ya Kanisa kiasi kwamba kanisa litakalokiuka linaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na ngazi ya konferensi.

***Washiriki Wasiondolewe kwa Kutohudhuria*****—**Inawapasa viongozi wa kanisa kuwatembelea washiriki wasiofika kanisani na kuwatia moyo kuendelea kuja na kufaidi baraka za ibada pamoja na kanisa.

Inapotokea mshiriki ameshindwa kuja kanisani mara kwa mara kwa sababu ya umri, ulemavu, au sababu nyingine isiyozuilika, inampasa kuwa na mawasiliano na uongozi wa kanisa kwa barua au njia nyingine. Hata hivyo, kama mshiriki anaendelea kuwa mwaminifu kwa mafundisho ya Kanisa, kutohudhuria hakutachukuliwa kuwa sababu ya kutosha kumwondoa katika ushirika.

***Washiriki Wanaohama Bila Taarifa*****—**Mshiriki akihama hana budi kumwarifu karani au mzee juu ya makazi yake mapya. Akiwa anaendelea kuwa mshiriki wa kanisa hilo, inampasa kutoa taarifa na kutuma zaka na sadaka yake japo mara moja kwa robo. Hata hivyo, endapo mshiriki atahama bila kuacha anuani ya makazi yake mapya na bila kufanya juhudi yo yote ya kuwasiliana au kutoa taarifa kwa kanisa, na kanisa likashindwa kumpata kwa angalao miaka miwili, basi kanisa linaweza kuthibitisha kuwa limejitahidi kumpata mshiriki huyo bila mafanikio na anaweza kuondolewa kwa kura ya kanisa. Karani anaweza kuandika katika kitabu cha ushirika: "Hajulikani aliko. Imeamuliwa kumhesabu kuwa hayupo."

***Washiriki Wasiondolewe kwa Sababu za Kifedha***—Ingawa washiriki hawana budi kusaidia kazi ya kanisa kwa kadiri wanavyoweza, wasiondolewe kwa sababu ya kushindwa kwao kulichangia kanisa kifedha.

***Kuondoa Wahiriki kwa Maombi Yao***—Inapasa kuwe na uangalifu mkubwa wakati wa kushughulikia washiriki wanaoomba kuondolewa katika ushirika. Ingawa kanisa linatambua haki ya mshiriki kuamua kuwa sehemu ya Kanisa, inabidi utolewe muda wa kutosha kwa mshiriki wa aina hiyo kufikiria na kutafakari, na juhudi zote zifanyike kumrejesha katika hali ya kuridhisha.

Barua za kujitoa hazina budi kuwasilishwa kwa baraza, ambalo litaziwasilisha katika mkutano mkuu. Kwa kuzingatia moyo wa Kikristo, uamuzi utafanyika bila mjadala wa hadhara.

***Taarifa kwa Walioondolewa katika Ushirika***—Kanisa linaloondoa mshiriki halina budi kumjulisha kwa maandishi juu ya hatua iliyochukuliwa lakini pamoja na kumhakikishia kumjali kiroho na kama binadamu. Ikiwezekana taarifa hii ipelekwe na mchungaji mwenyewe au na mtu aliyechaguliwa na baraza. Mshiriki wa zamani hana budi kuhakikishiwa kuwa kanisa linatumaini kuwa atarudi kanisani na kwamba siku moja kutakuwa na ushirika wa milele katika ufalme wa Mungu.

***Kurejesha Waliokuwa Wameondolewa katika Ushirika***—Mtu akiisha kuondolewa, ikiwezekana kanisa lidumishe mawasiliano na kuonesha moyo wa urafiki na upendo, likijaribu kumrudisha kwa Bwana.

Mshiriki aliyeondolewa anaweza kupokelewa tena katika ushirika wa kanisa muda uliopangwa na kanisa katika mkutano mkuu ukiisha, baada ya kuungama makosa yaliyokuwa yamefanywa, ushahidi wa toba na mabadiliko ya kweli umeoneshwa, na mwenendo unakubaliana na viwango vya Kanisa na ni bayana kuwa mshiriki huyo atajitiisha kikamilifu chini ya utaratibu na marudi ya kanisa. Urejeshwaji wa jinsi hiyo ni vema ukifanyika katika kanisa ambalo mshiriki huyo aliondolewa. Hata hivyo, ikiwa jambo hili haliwezekani, kanisa ambako mtu huyo anaomba kurejeshwa,

halina budi kutafuta habari kutoka katika kanisa la awali juu ya sababu za kuondolewa kwake katika ushirika.

Wakati wa kushughulikia wanaojihusisha na udhalilishaji wa kingono ikumbukwe kuwa urejeshwaji katika ushirika hauondoi athari zote za makosa makubwa kama hayo. Ingawa kuhudhuria katika shughuli za kanisa kunaweza kuruhusiwa kwa maelekezo yaliyowekwa kihalali, mtu mwenye hatia au aliyerudiwa kwa udhalilishaji wa kingono asiwekwe katika kazi itakayomfanya akutane na watoto, vijana, na watu wengine wasioweza kujilinda. Wala asipewe wadhifa wo wote utakaowafanya watu wanaoweza kunajisiwa wamwamini.

Kwa kuwa kuondolewa katika ushirika ni marudi makali kuliko yote, muda unaowekwa na mkutano mkuu wa kanisa, upasao kupita kabla ya mshiriki kurejeshwa, hauna budi uwe wa kutosha kuonesha kuwa matatizo yaliyosababisha kuondolewa katika ushirika yamesuluhishwa kikamilifu. Inatarajiwa kwamba kurejeshwa katika ushirika kutafanyika sambamba na ubatizo.

***Haki ya Kukata Rufaa ya Kurejeshwa*—**Pamoja na kwamba ni haki ya kanisa kusimamia nidhamu, hiyo haina maana kupuuza haki za washiriki kutafuta haki. Mshiriki akiamini kuwa ameonewa na kanisa mahalia, au hakuwa na haki ya kusikilizwa ipasavyo, na kanisa haliko tayari kufikiria upya shauri husika au kama maofisa hawataki kushugulikia ombi lake la kurejeshwa, mshiriki huyo wa zamani atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa maandishi kwa kanisa ili asikilizwe. Kanisa lisipuuze au kukataa kumsikiliza. Likikataa au kupuuza, au mshiriki huyo wa zamani akiona bado anaonewa na kanisa baada ya rufaa hiyo, ana haki ya kukata rufaa asikilizwe na kamati tendaji ya konferensi.

Kama baada ya uchunguzi kamili usio na upendeleo, kamati ya konferensi itaona kuwa uonevu umefanywa na kanisa, kamati inaweza kupendekeza arejeshwe katika ushirika. Lakini kama bado atakataliwa na kanisa, basi kamati ya konferensi inaweza kupendekeza awe na ushirika katika kanisa lingine. Kwa upande mwingine, kamati ikiona sababu nzuri za kuliunga mkono kanisa katika kukataa kumrejesha mshiriki huyo wa zamani, itaandika uamuzi wake.

SURA YA 8

# Maofisa na Idara za Kanisa Mahalia

Kuchagua viongozi bora ni muhimu kwa ustawi wa kanisa ambalo halina budi kuwa na uangalifu mkubwa kabisa linapowaita watu kushika nafasi zenye majukumu matakatifu.

### Sifa kuu

***Kufaa Kimaadili na Kiroho—***“Zaidi ya hayo utajipatia katika watu hawa watu walio na uwezo, wenye kumcha Mungu, watu wa kweli, wenye kuchukia mapato ya udhalimu; ukawaweka juu yao, wawe wakuu wa maelfu, na wakuu wa mia, na wakuu wa hamsini, na wakuu wa kumi” (Kut. 18:21).

“Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili” (Mdo. 6:3).

“Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi” (1 Tim. 3:7).

“Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine” (2 Tim. 2:2).

“Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi.

“Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu” (1 Tim. 3:2-13: tazama pia Tito 1:5-11 na 2:1, 7, 8).

“Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi. Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha. Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee. Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia” (1 Tim. 4:12-16).

***Kulilisha na Kulilinda Kundi***—Mtume Paulo aliwaita “wazee wa kanisa” na kuwaasa: “Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe. Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu, usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi” (Mdo. 20:28-31; tazama pia 1 Petro 5:1-3).

***Kuheshimu Wachungaji na Maofisa*—**“Lakini, ndugu, tunataka mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu, na kuwasimamia ninyi katika Bwana, na kuwaonyeni; mkawastahi sana katika upendo, kwa ajili ya kazi zao. Iweni na amani ninyi kwa ninyi” (1 Thess. 5:12, 13; see also 1 Tim. 5:17 and Heb. 13:7, 17).

Waumini wa Thesalonike walikuwa wanakerwa sana na watu waliokuwa wanatokea kati yao wakiwa na mawazo na mafundisho yenye itikadi kali. Wengine walikuwa ‘waendao bila utaratibu, hawana shughuli zao wenyewe, lakini wanajishughulisha na mambo ya wengine.’ Kanisa lilikuwa limeundwa kihalali, na maofisa walikuwa wamechaguliwa kuwa wachungaji na mashemasi. Lakini walikuwapo wengine waliokuwa wakaidi, wasiofikiri, waliokuwa hawataki kuwa chini ya wale waliokuwa na mamlaka kanisani. Pamoja na kudai kuwa na haki ya kuwa na uamuzi wao wenyewe, walikuwa pia wanadai hadharani kuwa na haki ya kushinikiza mawazo yao kwa kanisa. Kutokana na hali hiyo, Paulo aliwakumbusha Wathesalonike juu ya heshima na staha iwapasayo wale waliochaguliwa kushika nafasi zenye mamlaka kanisani.”—AA 261, 262.

Wale wenye vyeo vyenye majukumu katika kanisa wanaweza kuwa na kasoro kama walivyo watu wengine na wanaweza kukosea katika uamuzi wao; lakini pamoja na hayo, kanisa la Kristo duniani limewapa mamlaka yasiyoweza kupuuzwa.”—4T 17.

***Wasiharakishwe Katika Kazi*—**Katika sehemu nyingi tunakutana na watu waliowekwa haraka katika nafasi zenye majukumu kama vile wazee wa kanisa wakati hawafai kwa kazi hiyo. Hawawezi kujitawala wenyewe. Mvuto wao si mzuri. Kanisa huwa na matatizo siku zote kwa sababu ya tabia yenye kasoro ya kiongozi. Mikono imewekwa haraka mno juu ya watu hawa.”—4T 406, 407. (Tazama pia 5T 617 na 1 Tim. 5:22.)

***Wanaopinga Umoja Hawafai Kazini*—**"Siku hizi wametokea watu miongoni mwetu wanaodai kuwa watumishi wa Kristo, huku wakipinga umoja ambao Bwana wetu aliuanzisha kanisani. Wana mipango na mbinu mpya za kazi. Wanataka kuleta mabadiliko kanisani kulingana na mawazo yao ya ustawi wakidhani kwamba matokeo makubwa yatapatikana. Watu hawa wanahitaji kuwa wanafunzi badala ya kuwa walimu katika shule ya Kristo. Siku zote hawatulii, wakitaka kufanya kazi kubwa, kufanya jambo litakalowaletea sifa wao wenyewe. Wanahitaji kujifunza lile somo lenye manufaa kuliko yote, yaani unyenyekevu na imani kwa Yesu. …

Walimu wa ukweli, wamisionari, maofisa kanisani, wanaweza kufanya kazi nzuri kwa ajili ya Bwana wakiitakasa mioyo yao kwa kuutii ukweli."—5T 238.

***Si Salama Kuchagua Wanaokataa Kushirikiana*—**"Mungu ameweka kanisani wasaidizi wake aliowachagua, watu wenye talanta mbalimbali, ili kwa kuunganisha hekima ya wengi, nia ya Roho iweze kutimia. Watu wanaoenenda kwa kufuata tabia zao shupavu, wakikataa kushikamana na wengine walio na uzoefu mkubwa katika kazi ya Mungu, watapofushwa kwa kujiamini, wasiweze kutofautisha yale ya uongo na ya kweli. Si salama kwa watu kama hao kuchaguliwa kuwa viongozi kanisani; kwani watafuata uamuzi na mipango yao wenyewe, bila kujali uamuzi wa ndugu zao. Ni rahisi kwa yule adui kufanya kazi kwa njia ya wale ambao, licha ya wao wenyewe kuhitaji ushauri katika kila hatua, huamua kuongoza watu kwa nguvu zao wenyewe, bila kujifunza kwanza unyenyekevu wa Kristo."—AA 279. (tazama uk. 34, 35, 114-116.)

***Ushirika Mahalia*—**Washiriki hai wana haki ya kuchaguliwa kushika nafasi za uongozi katika kanisa lenye ushirika wao. (tazama uk. 106-109.) Kuna tofauti

kwa hawa wafuatao:

Wanafunzi ambao ni washiriki hai lakini wanaishi mbali na nyumbani kwa ajili ya masomo na huhudhuria mara kwa mara katika kanisa lililo katika eneo wanaloishi kwa muda.

Mfanyakazi wa konferensi aliyekwa na konferensi kama mchungaji/kiongozi wa makanisa mawili au zaidi. (tazama uk. 110, 111.)

Mzee ambaye, inapolazimu na kwa mapendekezo ya kamati ya konferensi, anaweza kuchaguliwa kuhudumia zaidi ya kanisa moja katika mtaa mmoja. (tazama uk. 73.)

Hali zingine zisizo za kawaida zinaweza kuangaliwa na kamati ya konferensi.

***Kuwa Mfano Katika Utoaji wa Zaka***—Maofisa wote watakuwa mfano katika suala la kurudisha zaka kwa Kanisa kwa uaminifu. Ye yote atakayeshindwa kuwa mfano wa aina hiyo asichaguliwe katika kazi ya kanisa.

***Si Wajumbe kwa Wadhifa Wao***—Ofisa ye yote wa kanisa hawezi kuwa mjumbe wa mkutano mkuu wa konferensi kwa wadhifa wake. Kama kanisa linataka ofisa awe mjumbe, itabidi limchague kuwa mjumbe.

***Kugawa Majukumu***—Kanisa lisiweke majukumu mengi kupita kiasi kwa kundi dogo la maofisa walio tayari, wakati wengine hawatumiki ipasavyo. Kama hali hailazimishi, uchaguzi wa mtu mmoja kushika nyadhifa nyingi hauna budi kupingwa.

***Kuondoa na Kurejesha***—Ofisa anapoondolewa katika ushirika na baadaye kurejeshwa, kurejeshwa huko hakumrejeshi mtu huyo katika kazi yake ya kwanza.

**Muda wa Uongozi**

Muda wa uongozi kwa maofisa wa kanisa na jumuiya zake utakuwa mwaka mmoja, isipokuwa pale ambapo kanisa limeamua katika mkutano mkuu kuwa na uchaguzi kila baada ya miaka miwili ili kurahisisha mwendelezo wa kazi na kukuza karama za roho na kupunguza kazi ya kuwa na uchaguzi wa kila mwaka.

Ingawa haishauriwi mtu mmoja kuhudumu bila kikomo katika nafasi fulani, maofisa wanaweza kuchaguliwa tena.

**Wazee**

***Viongozi wa Kiroho wa Kanisa*****—**Wazee hawana budi kutambuliwa na kanisa kama viongozi imara wa kiroho na inapasa wawe na sifa njema kanisani na katika jamii. Mchungaji asipokuwapo, wazee ni viongozi wa kiroho wa kanisa na hawana budi kujitahidi kuliongoza kanisa kuwa na ukristo wa kina na mkamilifu zaidi kwa mafundisho na kwa kuonesha mfano.

Wazee hawana budi kuwa na uwezo wa kuendesha huduma za ibada na kuhudumu katika Neno wakati mchungaji aliyepangwa hayupo. Hata hivyo wazee wasichaguliwe kwa sababu ya nafasi yao katika jamii au uwezo wao wa kuhubiri, bali wachaguliwe kwa sababu ya maisha yao matakatifu na uwezo wa kuongoza.

Wazee wanaweza kuchaguliwa tena, lakini haishauriwi watumike bila kikomo. Kanisa halilazimiki kuwachagua tena na linaweza kuchagua wengine ikionekana kuwa mabadiliko yanafaa. Baada ya kuchaguliwa wazee wapya, wazee wa zamani hawatatumika tena kama wazee lakini wanaweza kuchaguliwa katika nafasi zingine.

***Kuwekewa Mikono kwa Wazee*****—**Kuchaguliwa kuwa mzee peke yake hakumfanyi mtu kuwa mzee. Kuwekewa mikono kunahitajika kabla mzee hajawa na mamlaka ya kufanya kazi. Katika kipindi kati ya kuchaguliwa na kuwekewa mikono, mzee aliyechaguliwa anaweza kufanya kazi kama mzee wa kanisa lakini hawezi kuhudumu katika huduma maalum za kanisa.

Huduma ya kuwekea mikono hufanywa na mchungaji aliyewekewa mikono mwenye vyeti hai kutoka konferensi. Mchungaji mgeni aliyewekewa mikono anaweza kukaribishwa kusaidia kama njia ya kuonesha staha. Hata hivyo mchungaji mgeni aliyewekewa mikono au mchungaji mstaafu aliyewekewa mikono anaweza kuendesha huduma ya kuwekea mikono kwa ombi maalum toka kwa maofisa wa konferensi.

Huduma takatifu ya kuwekea mikono haina budi kufanyika kwa usahili mbele ya kanisa na inaweza kuwa na maelezo mafupi ya kazi ya mzee, sifa zinazotakiwa, na kazi za msingi ambazo mzee

ataruhusiwa kuzifanya. Baada ya mausia, mchungaji aliyewekewa mikono na/au wazee wanaoshiriki katika huduma hiyo, watawawekea mikono wazee kwa maombi na kuweka mikono juu yao. (tazama uk. 38.)

Baada ya kuwekewa mikono, wazee hawana haja ya kuwekewa mikono tena wakichaguliwa tena, au wakichaguliwa kuwa wazee katika makanisa mengine, ili mradi wameendeleza uhai wa ushirika wao. Wanaweza pia kutumika kama mashemasi.

***Uhusiano na Mchungaji***—Kamati ya konferensi ikimpanga mchungaji kwenye kanisa, mchungaji huyo au mchungaji mwandamizi kama wako zaidi ya mmoja, atakuwa ofisa mkuu na wazee watakuwa wasaidizi wake. Kwa kuwa kazi yao inahusiana sana, inawapasa kufanya kazi pamoja kwa kupatana. Mchungaji asichukue majukumu yote, bali agawane na wazee pamoja na maofisa wengine. Mchungaji anayehudumu katika kanisa husika atakuwa mwenyekiti wa baraza. (tazama uk. 33, 125, 126.) Hata hivyo, inaweza kutokea hali ambapo itakuwa vyema mzee kuwa mwenyekiti. Kazi ya kuchunga kanisa ifanywe kwa pamoja kati ya mchungaji na wazee. Inawapasa wazee, kwa kushauriana na mchungaji, kutembelea washiriki, kuhudumia wagonjwa, kuhamasisha huduma ya maombi, kuandaa huduma za kuwekea mikono na kuweka watoto wakfu, kutia moyo waliokata tamaa na kusaidia katika majukumu mengine ya kichungaji. Kama wachungaji wasaidizi, wazee hawana budi kuliangalia kundi wakati wote.

Kama mchungaji ni mwenye cheti, kanisa au makanisa anayoyahudumia hayana budi kumchagua kuwa mzee wa kanisa. (tazama uk. 34.)

Kwa kuwa mchungaji huteuliwa na konferensi kushika nafasi hiyo kanisani, mchungaji hulihudumia kanisa kama mfanyakazi wa konferensi, akiwajibika kwa kamati ya konferensi, na kudumisha uhusiano mzuri na wa kushirikiana na kufanya kazi kulingana na mipango na sera za kanisa mahalia. Wazee waliochaguliwa na kanisa, huwajibika kwa kanisa na baraza lake. (Tazama hapa chini.)

***Kazi ya Wazee ni Mahalia***—Mamlaka na kazi ya wazee yanaishia katika kanisa walilochaguliwa. Kamati ya konferensi

hairuhusiwi kupiga kura ya kumpa mzee hadhi apewayo mchungaji aliyewekewa mikono ya kuhudumia makanisa mengine kama mzee. Kama kuna hitaji hilo, kamati ya konferensi inaweza kulipendekezea kanisa linalohitaji mzee, limwalike mzee wa kanisa la jirani kuhudumu. Kwa hiyo, mtu mmoja anaweza kuhudumia zaidi ya kanisa moja kwa kuchaguliwa. Utaratibu huo hauna budi kufanywa kwa kushuriana na kamati ya konferensi tu. Mamlaka ya kuchagua wazee wa kanisa yako katika kanisa mahalia na si katika kamati ya konferensi. Njia pekee ya kumfanya mtu ahudumie kanisa kwa ujumla ni kuwekewa mikono ya huduma ya injili. (tazama uk. 33, 72, 73.)

***Kuendesha Huduma za Ibada***—Mzee, kwa kuongozwa au kusaidiana na mchungaji, anawajibika katika huduma za ibada na inampasa kuziendesha au kupanga mtu aendeshe. Huduma ya meza ya Bwana haina budi kuendeshwa na mchungaji aliyewekewa mikono au mzee mahalia siku zote. Kwa kawaida mchungaji ndiye mwenyekiti wa mkutano mkuu. Mchungaji asipokuwapo, mzee anaweza kuwa mwenyekiti kwa kuruhusiwa na mwenyekiti wa konferensi.

***Huduma ya Ubatizo***—Pasipokuwa na mchugaji aliyewekewa mikono, mzee atamwomba mwenyekiti wa konferensi aandae ubatizo wa wale wanaotaka kujiunga na kanisa. (tazama uk. 46-49.) Mzee hawezi kufanya huduma hiyo bila kuruhusiwa kwanza na mwenyekiti wa konferensi.

***Sherehe ya Ndoa***—Katika sherehe ya ndoa, agizo, nadhiri na tangazo la ndoa, hutolewa na mchungaji aliyewekewa mikono tu, isipokuwa katika maeneo ambapo kamati za divisheni zimeruhusu, wachungaji kadhaa wenye vyeti, au wachugaji wateule, waliowekewa mikono kama wazee mahalia wanaweza kuendesha huduma hiyo. (tazama uk. 34.) Sheria mahalia zinaweza kuhitaji mtu anayeendesha huduma ya ndoa awe pia na leseni/kibali cha serikali kufanya hivyo. Mchungaji aliyewekewa mikono, mchungaji mwenye cheti au mteule, au mzee anaweza kutoa hubiri, kuomba, na kutoa baraka. (Tazama maelezo #1, uk. 167.)

***Kuhimiza Utoaji wa Zaka*—**Kwa kurudisha zaka kwa uaminifu, wazee husaidia sana kuhamasisha washiriki wengine kurudisha zaka kwa uaminifu. (tazama uk. 130, 131, 163.) Wazee wanaweza kuhimiza utoaji wa zaka kwa kuelezea fursa na wajibu wa uwakili ulio katika Maandiko na kwa kuwashauri washiriki kwa hekima.

***Kuhimiza Usomaji wa Biblia, Maombi na Uhusiano na Yesu*—** Kama viongozi wa kiroho, wazee wana wajibu wa kuwahimiza washiriki kujenga uhusiano binafsi na Yesu kwa kuimarisha mazoea yao ya kujisomea Biblia na kuomba. Inawapasa wazee kuwa mfano katika uaminifu wa kusoma Biblia na kuomba. Maisha yenye ufanisi katika maombi kwa kila mshiriki na kusaidia huduma na programu za kanisa mahalia, kutaimarisha utume wa kanisa. Wazee wanaweza kuliomba baraza kuchagua kamati ya kusaidia katika kazi ya ukuaji na uhamasishaji.

***Kuendeleza Kazi Zote*—**Kwa uongozi wa mchungaji na kwa kusaidiana naye, wazee ni viongozi wa kiroho wa kanisa na wana wajibu wa kuendeleza idara zote na shughuli zote za kazi ya Mungu. Inawapasa wazee kudumisha uhusiano saidizi na maofisa wengine.

***Kushirikiana na Konferensi*—**Mchungaji, wazee na maofisa wote hawana budi kushirikiana na maofisa wa konferensi na wakurugenzi wa idara katika kutekeleza mipango iliyopitishwa. Inawapasa kuliarifu kanisa juu ya sadaka zote za kawaida na sadaka maalum, kuhamasisha programu na shughuli zote za kanisa, na kuhimiza maofisa wote kuunga mkono mipango na sera za konferensi.

Wazee hawana budi kufanya kazi kwa kushirikiana na mhazini na kuhakikisha kwamba pesa za konferensi zinawasilishwa kwa wakati uliopangwa na konferensi kwa mhazini wa konferensi. Inawapasa wazee kuhakikisha kuwa taarifa ya karani imetumwa kwa katibu wa konferensi mwishoni mwa kila robo.

Inawapasa wazee kuchukulia mawasiliano yote kutoka konferensi kuwa ya muhimu. Barua zinazohitaji matangazo hazina budi kuwasilishwa kwa wakati mwafaka.

Kama mchungaji hayupo, mzee kiongozi (tazama uk. 110) hana

budi kuhakikisha kanisa linachagua wajumbe wa mkutano mkuu wa konferensi na kwamba karani anatuma majina ya wajumbe hao katika ofisi ya konferensi.

***Kuendeleza Kazi ya Ulimwengu Mzima*****—**Pia inawapasa wazee kuhamasisha kazi ya utume ulimwenguni kwa kuchunguza vizuri kazi ya kanisa ulimwenguni na kuwahimiza washiriki kusaidia kazi ya utume. Mtazamo wao wa upole na hekima, utaleta moyo wa utoaji kwa washiriki katika huduma ya ibada na katika Shule ya Sabato.

***Mafunzo na Maandalizi ya Wazee*****—**Chama cha Wachungaji, kwa kushirikiana na idara, huhamasisha mafunzo na maandalizi ya wazee. Hata hivyo, mchungaji ana jukumu kubwa la kuwafundisha wazee. (Tazama maelezo, #2, uk. 167.)

***Wasipewe Majukumu Mengi ili Wafanye Kazi kwa Ufanisi*****—**Wazee hasa hawana budi kupunguziwa majukumu mengine ili wafanye kazi zao nyingi kwa ufanisi. Katika hali fulani inaweza kuwa vyema kuwaomba wazee wasaidie kuongoza kazi ya huduma (utume) kanisani, lakini hata jambo hilo halina budi kuepukwa kama kuna watu wengine wenye talanta hiyo.

***Mzee kiongozi*****—**Inaweza kuwa vyema, kulingana na ukubwa wa kanisa, kuchagua zaidi ya mzee mmoja kwa kuwa majukumu ya kazi hiyo ni makubwa mno kwa mtu mmoja. Kanisa likichagua zaidi ya mzee mmoja, mmoja kati yao hana budi kuwa "mzee kiongozi." Kazi igawanywe kati ya wazee kulingana na uzoefu na uwezo.

***Mipaka ya Mamlaka*****—**Wazee hawana mamlaka ya kupokea na kuondoa washiriki. Mambo hayo hufanywa kwa kura ya kanisa tu. Baraza tu ndilo linaloweza kupendekeza kwamba kanisa lipige kura ya kupokea au kuondoa mshiriki. (tazama uk. 49, 54, 55.)

***Viongozi wa Makanisa*****—**Wakati fulani huwa hakuna mtu mwenye uzoefu na sifa za kuwa mzee. Katika hali hiyo kanisa

halina budi kuchagua mtu atakayejulikana kama "kiongozi." Asipokuwapo mchungaji au mchungaji aliyewekwa na konferensi, kiongozi atawajibika na huduma za ibada, pamoja na mkutano mkuu. Kiongozi hana budi kufanya mambo hayo au kuandaa mtu mwingine kufanya hivyo.

Kiongozi hawezi kuendesha huduma yo yote maalum ya kanisa, kuendesha ubatizo, kuendesha meza ya Bwana, kuendesha huduma ya ndoa, au kuwa mwenyekiti wa mkutano mkuu ambapo washiriki wanarudiwa. Inabidi ombi lipelekwe kwa mwenyekiti wa konferensi ili alete mchungaji aliyewekewa mikono kuja kuendesha mikutano hiyo.

## Mashemasi wa Kiume

Agano jipya linaitaja kazi ya ushemasi kwa neno la Kigiriki *diakonos,* ambapo neno la Kingereza "deacon" limetoholewa. Neno hilo la Kigiriki hufasiriwa kwa namna mbalimbali kama "mtumishi, mchungaji, mwandishi, mhudumu" na katika mazingira ya Kikristo limekuwa na maana maalum ya "shemasi."

Watu hao saba waliokuja kujulikana kama mashemasi wa kanisa la mitume walikuwa wamechaguliwa na kuwekewa mikono kufanya shughuli za kanisa. (Tazama Matendo 6:1-8.) Sifa hizi, ambazo ni nyepesi kidogo kuliko za wazee zimeorodheshwa katika 1 Timotheo 3:8-13.

"Ukweli kwamba ndugu hawa walikuwa wamewekewa mikono kwa kazi maalum ya kuangalia mahitaji ya maskini haukuwazuia kufundisha imani. Kinyume chake, walikuwa wanaweza kabisa kuwafundisha wengine ukweli, na waliifanya kazi hiyo kwa ari na ufanisi mkubwa."—AA 90.

"Kuchaguliwa kwa wale saba kusimamia maeneo fulani ya kazi kulikuwa baraka kubwa kwa kanisa. Maofisa hawa walichunguza kwa makini mahitaji ya watu na pia maslahi ya kifedha ya kanisa, na kwa usimamizi wao makini na mfano wa utauwa walikuwa msaada muhimu kwa maofisa wenzao katika kuunganisha shughuli mbalimbali za kanisa na kuwa kitu kimoja."—AA 89.

Siku hizi uteuzi wa mashemasi kwa uchaguzi huleta baraka kama hizo katika uongozi wa kanisa kwa kuwapunguzia wachungaji,

wazee na maofisa wengine kazi ambazo mashemasi wanaweza kuzifanya vizuri.

"Muda na nguvu za wale ambao kwa majaliwa ya Mungu wamewekwa katika nafsi za juu za majukumu ya kanisa havina budi kutumika katika kushughulikia masuala mazito yanayohitaji hekima maalum na ukuu wa moyo. Si mpango wa Mungu kwamba watu kama hao waombwe kushughulikia masuala madogo madogo ambayo wengine wanaweza kuyashughulikia."—AA 93.

***Baraza la Mashemasi wa Kiume--***Mahali ambapo kanisa lina mashemasi kadhaa, halina budi kuunda baraza la mashemasi wa kiume linalosimamiwa na shemasi mkuu wa kiume na shemasi mwingine akiwa katibu. Chombo hicho husaidia kugawa majukumu na kuratibu mchango wao katika ustawi wa kanisa. Pia hutoa fursa ya mafunzo ambapo mashemasi wapya kufundishwa kazi zao.

***Mashemasi wa Kiume Lazima Wawekewe Mikono*—**Mashemasi waliotoka kuchaguliwa hawawezi kuanza kazi zao mpaka kwanza wawekewe mikono na mchungaji aliyewekewa mikono mwenye vyeti hai kutoka konferensi.

Ibada takatifu ya kuwekea mikono haina budi kuwa sahili na ifanyike mbele ya kanisa. Mchungaji anaweza kutoa maelezo mafupi ya kazi ya shemasi kibiblia, sifa zinazohitajika kwa huduma hiyo na kazi za msingi ambazo mashemasi wanaruhusiwa kuzifanya. Baada ya mausia mafupi ya uaminifu katika huduma, mchungaji atawawekea mikono mashemasi kwa ombi na kuweka mikono juu yao akisaidiwa na mzee kama inafaa.

Mashemasi wakidumisha ushirika wao, wakisha kuwekewa mikono, hawana haja ya kuwekewa tena wakihamishia ushirika katika makanisa mengine. Muda waliochaguliwa ukiisha, inawapasa kuchaguliwa tena, ndipo waendelee kutumika kama mashemasi.

Wazee ambao baadaye huchaguliwa kuwa mashemasi hawana haja ya kuwekewa mikono kama mashemasi kwani mikono ya uzee inahusisha kazi ya ushemasi.

***Mashemasi Hawaruhusiwi Kusimamia*—**Mashemasi hawaruhusiwi kuendesha huduma yo yote maalum ya kanisa au mkutano

mkuu na hawawezi kuendesha huduma ya ndoa au kuwa wenyeviti wakati wa kupokea au kuhamisha washiriki.

Kama kanisa halina mtu mwenye mamlaka ya kufanya shughuli hizo, liwasiliane na konferensi kwa ajili ya msaada.

***Kazi za Mashemasi wa Kiume*****—**Kazi ya ushemasi inahusisha huduma nyingi kwa kanisa ikiwa pamoja na:

*Kusaidia katika Ibada na Mikutano*—Kwa kawaida mashemasi wanawajibika kukaribisha washiriki na wageni wanapoingia kanisani na ikibidi, kuwasaidia kupata mahali pa kuketi. Pia hushirikiana na mchungaji na wazee katika uendeshaji mzuri wa mikutano yote.

*Kutembelea Washiriki*—Katika makanisa mengi utembeleaji hupangwa kwa kuwagawa washiriki katika maeneo na kupanga shemasi kwa kila eneo ikitarajiwa kwamba shemasi huyo atatembelea kila nyumba japo mara moja kwa robo.

*Maandalizi ya Huduma ya Ubatizo*—Mashemasi wa kiume hufanya maandalizi muhimu kwa ajili ya huduma ya Ubatizo. (tazama uk. 49.)

*Kusaidia Katika Huduma ya Meza ya Bwana*—Katika huduma ya kuoshana miguu, mashemasi wa kiume au wa kike hutoa kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya huduma hiyo kama vile vitambaa, maji na ndoo. Baada ya huduma huwa wanahakikisha kuwa vyombo vyote na vitambaa vimeoshwa/vimefuliwa na kutunzwa ipasavyo.

Mikate na divai iliyobaki isiliwe au kunywewa, bali itupwe na mashemasi kwa heshima baada ya Meza ya Bwana.

*Kutunza Wagonjwa na Kusaidia Maskini na Wenye Shida*—Mashemasi wa kiume na wa kike wana kazi ya kusaidia wagonjwa, maskini na wenye shida na hawana budi kulijulisha kanisa wakati wote mahitaji yao na kuomba msaada wa washiriki. Pesa za kazi hiyo zitatolewa katika mfuko wa maskini na wahitaji. Kwa mapendekezo ya baraza, mhazini atawapatia mashemasi cho chote kitakachohitajika kwa ajili ya matumizi ya wahitaji.

*Kutunza na Kukarabati Mali*—Katika makanisa ambayo utunzaji na ukarabati wa mali za kanisa haujawekwa chini ya kamati ya majengo, mashemasi wa kiume na wa kike wana jukumu hilo. (Tazama maelezo, #3, uk. 167.)

**Mashemasi wa Kike**

Mashemasi wa kike walikuwa wanajumuishwa katika watendakazi rasmi wa makanisa ya awali ya Kikristo. "Namkabidhi kwenu Fibi, ndugu yetu, aliye mhudumu wa kanisa lililoko Kenkrea; kwamba mmpokee katika Bwana, kama iwapasavyo watakatifu; mkamsaidie katika neno lo lote atakalohitaji kwenu; kwa sababu yeye naye amekuwa msaidizi wa watu wengi, akanisaidia mimi pia" (Rum. 16:1. 2).

Mashemasi wa kike wachaguliwe kwa sababu ya kujitoa kwao pamoja na sifa zingine zinazowafanya wafae kwa ajili ya majukumu ya kazi hiyo.

***Baraza la Mashemasi wa Kike*—**Kama kanisa limechagua mashemasi wengi wa kike, halina budi kuunda baraza la mashemasi wa kike, likisimamiwa na shemasi mkuu wa kike na mwingine akiwa katibu. Baraza hili lina mamlaka ya kuwapangia kazi mashemasi wa kike na kushirikiana kwa karibu na baraza la mashemasi wa kiume, hasa katika kuwakaribisha washiriki na wageni na katika kutembelea nyumba. (tazama uk. 76, 77.) Pia hutoa fursa ya mafunzo ambapo mashemasi wapya hufundishwa kazi zao.

***Huduma ya Kuwekea Mikono Mashemasi wa Kike*—**Huduma hiyo haina budi kufanywa na mchungaji aliyewekewa mikono mwenye vyeti hai kutoka konferensi. Huduma ya kuwekea mikono haina budi kuwa sahili na ifanywe mbele ya kanisa.

Mashemasi wa kike wakidumisha ushirika wao, wakisha kuwekewa mikono, hawana haja ya kuwekewa tena wakihamishia ushirika katika makanisa mengine. Muda waliochaguliwa ukiisha, inawapasa kuchaguliwa ndipo waendelee kutumika kama mashemasi wa kike.

***Kazi za Mashemasi wa Kike*—**Mashemasi wa kike hulitumikia kanisa katika shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

*Kukaribisha Wageni na Washiriki*—Katika makanisa mengi, mashemasi wa kike husaidia kukaribisha wageni na washiriki katika mikutano na kutembelea washiriki majumbani mwao wanapokuwa hawawezi kuja kanisani.

*Kusaidia Katika Ubatizo*—Mashemasi wa Kike huhakikisha kwamba wataradhia wa kike wanahudumiwa kabla na baada ya ubatizo. Pia huwa wanatoa ushauri na kusaidia kadiri itakavyohitajika kuhusu mavazi yanayofaa kwa ajili ya ubatizo. Majoho ya kitambaa kinachofaa hayana budi kutolewa. Endapo majoho yatatumika, mashemasi wa kike watahakikisha kuwa yamefuliwa na kutunzwa vizuri. (tazama uk. 49.)

*Maandalizi ya Huduma ya Meza ya Bwana*—Mashemasi wa kike na wa kiume huandaa kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya huduma hii na kuhakikisha kwamba kila kitu kilichotumika kinatunzwa vizuri baada ya hapo. (tazama uk. 121.)

Kabla ya kuanza kwa huduma ya meza ya Bwana, mashemasi wa kike hufanya maandalizi ya meza, ikiwa pamoja na kuandaa mkate na divai, kupanga meza ya huduma, kumimina divai, kuweka sahani za mikate isiyotiwa chachu, na kufunika meza kwa kitambaa maalum kwa shughuli hiyo.

Mashemasi wa kike husaidia katika huduma ya kutawadhana miguu, wakitoa msaada wa pekee kwa wageni wa kike na washiriki wapya.

*Kutunza Wagonjwa na Maskini*—Mashemasi wa kike huwasaidia mashemasi wa kiume katika kutunza wagonjwa, wahitaji na wenye shida. (tazama uk. 78.)

*Kutunza na Kukarabati Mali*—Katika makanisa ambayo utunzaji na ukarabati wa mali za kanisa haujawekwa chini ya kamati ya majengo, mashemasi wa kiume na wa kike wana jukumu hilo. (Tazama maelezo, #3, uk. 167.)

## Karani

Sehemu kubwa ya ufanisi wa shuhguli za kanisa hutegemea karani. Kutokana na umuhimu na upekee wa majukumu ya ofisi hii, ni vyema kuchagua mtu ambaye anaweza kuchaguliwa tena ili kuwe na mwendelezo katika uhifadhi na utoaji wa taarifa. Makanisa makubwa yanaweza kuchagua makarani wasaidizi kulingana na mahitaji. Endapo karani, hataweza kuhudhuria mkutano mkuu kama katibu, itampasa kumwandaa msaidizi kwa ajili ya kuandika kumbukumbu. (Tazama maelezo, #4, uk. 168.)

***Majina Yasiingizwe au Kuondolewa Bila Kura***—Isipokuwa katika suala la kifo cha mshiriki, karani hana mamlaka ya kuingiza au kutoa majina katika kitabu cha ushirika bila kura ya kanisa, ambalo siku zote, halina budi kupiga kura kuingiza au kuondoa jina. Mshiriki akifa, karani ataandika tarehe ya kifo hicho katika kitabu cha ushirika. (tazama uk. 55.)

***Kuhamisha Washiriki***—Karani hushughulikia mawasiliano kati ya washiriki na makanisa katika kuhamisha ushirika. (tazama uk. 52-55.)

***Kuwasiliana na Washiriki***—Inampasa karani kuwa na mawasiliano na washiriki wasiofika kanisani. (Tazama maelezo, #5, uk. 168.)

***Taarifa Kuhusu Wajumbe wa Vikao vya Konferensi***—Kwa kuidhinishwa na baraza, karani ataiarifu konferensi juu ya wajumbe waliochaguliwa kuliwakilisha kanisa katika kikao cha konferensi, kwa kutumia karatasi au fomu maalum.

***Ripoti Zitolewe kwa Wakati***—Inampasa karani kutoa ripoti zinazotakiwa na konferensi kwa wakati. Baadhi ya ripoti ni za kila robo, zingine ni za mwaka. Ni muhimu ripoti hizo zitumwe kwa katibu wa konferensi katika kipindi kilichowekwa kwa sababu ni za muhimu kwa ajili ya usahihi wa ripoti zinazoandaliwa na Kanisa la ulimwengu. Karani hukusanya taarifa kwa ajili ya ripoti hizo kutoka kwa maofisa wengine na viongozi wa idara.

***Kumbukumbu za Kanisa***—Karani huandika kumbukumbu za kanisa, ambazo hazina budi kuhifadhiwa vizuri. Kumbukumbu zote na vitabu vya mahesabu ya maofisa wote ni mali ya kanisa na zinapasa kukabidhiwa kwa karani mpya mwishoni mwa kipindi cha uongozi wa karani wa zamani, au kwa kanisa wakati wo wote katikati ya kipindi kwa kuombwa na mchungaji au wazee.

**Mhazini**

Kwa sababu ya kazi muhimu za mhazini, ni vyema kuchagua mtu ambaye anaweza kuchaguliwa tena ili kuwe na mwendelezo katika uhifadhi na utoaji wa taarifa. Makanisa makubwa yanaweza kuchagua wahazini wasaidizi kulingana na mahitaji.

Mhazini anaweza kuhamasisha kwa kiasi kikubwa uaminifu katika kurudisha zaka na kuimarisha moyo wa kutoa kwa washiriki. Ushauri unaotolewa katika moyo wa Bwana utasaidia washiriki kumtolea Bwana zaka na sadaka zake kwa uaminifu, hata wakati wa hali ngumu kifedha.

***Mhazini ni Mtunzaji wa Pesa Zote*****—**Mhazini ndiye mtunzaji wa pesa zote za kanisa. Pesa hizo ni pamoja na (1) pesa za konferensi, (2) pesa za kanisa mahalia na (3) pesa za taasisi saidiziza kanisa mahalia.

Pesa zote (za konferensi, kanisa mahalia na taasisi saidiziza kanisa mahalia) huwekwa katika akaunti ya benki au taasisi ya kifedha na mhazini kwa jina la kanisa, isipokuwa kama konference mahalia itaidhinisha mfumo mwingine.

Pesa za ziada za kanisa, zinaweza kuwekwa katika akaunti ya akiba kwa idhini ya baraza. Mahali ambapo pesa nyingi huchukuliwa kwa ajili ya ujenzi au miradi maalum, baraza linaweza kuidhinisha akaunti tofauti za benki. Hata hivyo, akaunti hizo zitasimamiwa na mhazini na zitatolewa taarifa kwa kanisa pamoja na pesa zingine za kanisa.

Akaunti zote za kanisa ni kwa ajili ya pesa za kanisa tu na haziwezi kuchanganywa na akaunti au pesa zingine za binafsi.

***Pesa za konferensi*****—**Pesa za konferensi, ambazo ni pamoja na zaka, pesa zote za utume wa kawaida, pesa zote za miradi maalum na tasisi za konferensi ni amana. Mwisho wa kila mwezi, au kabla ya hapo kulingana na matakwa ya konferensi, mhazini atatuma kwa mhazini wa konferensi pesa zote zilizopokelewa katika kipindi hicho. Kanisa haliruhusiwi kukopa, kutumia, au kubaki na pesa hizo za konferensi kwa makusudi yo yote yale.

***Pesa za Shule ya Sabato*****—**Sadaka zote za Shule ya Sabato hazina budi kukabidhiwa na karani-mhazini wa Shule ya Sabato kwa mhazini kila juma na mhazini aandike vizuri kumbukumbu ya sadaka zote za aina hiyo. Pesa hizo za utume hupelekwa katika ofisi ya konferensi kama ilivyoelezwa katika aya iliyotangulia. Pesa za matumizi ya Shule ya Sabato hutunzwa kama amana, zikingoja maagizo ya baraza la Shule ya Sabato (tazama uk. 94, 95), kugharimia matumizi ya kawaida ya Shule ya Sabato.

***Pesa za Kanisa Mahalia*****—**Pesa za kanisa mahalia ni pamoja na zile za matumizi ya kanisa, pesa za ujenzi na ukarabati na pesa kwa ajili ya maskini na wahitaji. Pesa hizi ni za kanisa mahalia na hutolewa na mhazini kwa idhini ya baraza au mkutano mkuu tu. Hata hivyo, mhazini atalipa bili zote za matumizi mahalia yaliyoidhinishwa na baraza kwa kutumia pesa za matumizi.

***Pesa za Taasisi Saidizi*****—**Pesa za jumuiya saidizi ni pamoja na pesa kama za programu za huduma, kaya na familia, Chama cha Vijana Waadventista, Huduma za jamii/Chama cha Dorkas, matumizi ya shule ya Sabato na sehemu ya pesa za huduma za afya ambazo ni za kanisa, na zinaweza kuwa pamoja na pesa za shule ya kanisa. Pesa zote zinazopokelewa na taasisi na kwa ajili ya taasisi hizo huwasilishwa mara moja kwa mhazini wa kanisa na katibu-mhazini wa taasisi husika, mashemasi au ye yote aliyepokea pesa hizo. Pesa hizo ni mali ya jumuiya hizo ndogo-ndogo. Zinaweza kutolewa kwa maagizo ya taasisi saidizi zinazozimiliki.

Mhazini atatoa stakabadhi kwa ajili ya pesa zilizopokelewa. Wakati wa kupokea pesa kutoka kwa mhazini, katibu wa taasisi saidizi atampa mhazini stakabadhi halali.

***Kulinda Makusudi ya Pesa*****—**Sadaka inapokusanywa kwa ajili ya utume ulimwenguni au kwa ajili ya mradi wo wote wa pamoja au mahalia, pesa zote zilizowekwa kwenye sahani (isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo na mtoaji) zitahesabiwa kuwa sehemu ya sadaka hiyo husika. Sadaka na zawadi zote zinazotolewa na watu kwa ajili ya mfuko au makusudi mahususi hazina budi kutumiwa kwa makusudi hayo. Mhazini au baraza hawana mamlaka ya

kubadili matumizi ya pesa zo zote kutoka katika makusudi yaliyofanya zitolewe.

Pesa za taasisi saidizi, ambazo mara nyingi hutolewa kwa ajili ya makusudi maalum, hukusanywa kwa ajili ya sehemu hiyo ya kazi ya kanisa ambayo ilifanya jumuiya hiyo ianzishwe. Pesa hizo hutunzwa na mhazini kama amana, na hizo pia haziwezi kukopwa au kubadilishwa matumizi na mhazini au baraza nje ya makusudi yaliyofanya zikusanywe.

Taasisi saidizi inapositishwa, kanisa litafanya uamuzi katika mkutano mkuu likionesha jinsi pesa zo zote zilizobaki katika akaunti ya taasisi hiyo zitakavyotumika.

***Pesa za Oda Binafsi za Maandiko Mbalimbali***—Pesa za uagizaji binafsi wa maandishi mbalimbali, vitabu, makabrasha, magazeti, na pesa za kuagizia majarida yatolewayo kwa kipindi maalum, hutunzwa na mhazini mahali ambapo hakuna Kituo cha Vitabu vya Waadventista. (Tazama maelezo, #6, uk. 168.)

***Njia Sahihi ya Washiriki Kulipa Pesa***—Mhazini hana budi kuhimiza pesa zote zinazotolewa na washiriki, nje ya makusanyo ya kawaida ya kanisa, ziwekwe katika bahasha za zaka na sadaka, isipokuwa kama kuna njia nyingine iliyowekwa na konferensi. Inawapasa washiriki kuandika maelezo na kiasi cha pesa juu ya bahasha kama ilivyooneshwa na kuhakikisha kuwa pesa iliyomo ni sawa na jumla inayooneshwa. Inawapasa pia kuandika majina na anuani zao, na kuweka bahasha hizo katika chombo cha sadaka au wazikabidhi kwa mhazini, ambaye atatunza zile bahasha zikitumika kama vocha mpaka mahesabu yote yatakapokaguliwa na mkaguzi wa conference.

Washiriki wanaorudisha zaka na sadaka kwa hundi au hati za posta hawana budi, pale inapowezekana kisheria, kuziandika hundi au hati hizo kwa jina la kanisa, badala ya mtu binafsi.

***Stakabadhi kwa Washiriki***—Inapasa stakabadhi zitolewe mara moja kwa ajili ya pesa zote zilizopokelewa kutoka kwa washiriki hata kama ni pesa kidogo sana, na hesabu sahihi ya stakabadhi zote lazima iandikwe na mhazini. Sadaka zote za kawaida zisizokuwa

katika bahasha hazina budi kuhesabiwa na mhazini mbele ya ofisa mwingine, hasa shemasi, na itolewe stakabadhi kwa ofisa huyo.

***Njia Sahihi ya Kuwasilisha Pesa Konferensi***—Wakati wa kutuma pesa kwa mhazini wa konferensi, hundi zote, hati za benki, na hawala zote za posta hazina budi kulipwa kwa taasisi kila inapowezekana kisheria na siyo kwa mtu binafsi. Nakala ya kumbukumbu za mhazini lazima ziambatanishwe na malipo hayo. Fomu za malipo hutolewa na konferensi. (tazama uk. 130, 131.)

***Utunzaji wa Nyaraka za Fedha***—Nyaraka za fedha, vocha, au ankara zenye stakabadhi, kwa ajili ya pesa zote zilizopokelewa au kulipwa, lazima zihifadhiwe kulingana na utaratibu ulioidhinishwa na konferensi mahalia.

***Vitabu Lazima Vikaguliwe***—Mhazini wa konferensi, au mtu mwingine aliyechaguliwa na kamati ya konferensi, hukagua vitabu vya mahesabu vya kanisa, kwa kawaida kila mwaka.

Vitabu vya mhazini pamoja na vitabu vingine vya fedha vinavyohusiana na kazi ya mhazini, mhazini wa shule ya kanisa, na mhazini wa taasisi nyingine yo yote vinaweza kutakiwa na kukaguliwa wakati wo wote na mkaguzi wa konferensi au na mchungaji, kiongozi wa mtaa, mzee kiongozi au na watu wengine wo wote walioidhinishwa na baraza la kanisa, lakini visitolewe kwa watu wasioidhinishwa. (tazama uk. 135.)

Taarifa za pesa zote zilizopokelewa na kutolewa lazima ziwasilishwe katika mkutano mkuu wa kawaida wa kanisa. Nakala ya taarifa hizo inapasa kutolewa kwa maofisa wote walio katika uongozi.

Idadi ya watu wanaorudisha zaka katika kanisa inapotolewa, mume, au mke au watoto wadogo wasio na kipato lakini ni washiriki wa kanisa hawana budi kujumuishwa katika kundi hilo, pamoja na yule mwenye kipato katika familia.

***Uhusiano na Washiriki ni Siri***—Inampasa mhazini kukumbuka kila wakati kwamba uhusiano na washiriki ni wa siri sana. Haimpasi mhazini kusema cho chote juu ya zaka iliyorejeshwa na mshiriki

ye yote au kuhusu kipato au jambo lo lote juu ya kipato hicho, isipokuwa kwa wale anaoshirikiana nao katika majukumu ya kazi. Madhara makubwa yanaweza kusababishwa kwa kutokufuata kanuni hii.

**Mratibu wa Waliovutiwa**

Inapasa achaguliwe mratibu wa waliovutiwa kuhakikisha kuwa waliovutiwa wote kutokana na huduma ya utume wa kanisa, wanahudumiwa kwa wakati. Mtu huyu ni mjumbe wa baraza la kanisa na baraza la huduma na hufanya kazi moja kwa moja na mchungaji na mwenyekiti wa baraza la huduma.

Kazi za mratibu wa waliovutiwa ni pamoja na:

Kuandaa orodha ainifu ya watu wote waliovutiwa ambao wamepokelewa na kanisa.

Kumsaidia mchungaji na mwenyekiti wa baraza la huduma katika kuandikisha washiriki wenye sifa kwa ajili ya huduma ya ufuatiliaji.

Kutoa taarifa kwa baraza la kanisa kila mwezi juu ya idadi na ufuatiliaji wa waliovutiwa. Mtu aliyevutiwa akifundishwa vya kutosha, mchungaji ajulishwe.

**Idara na Taasisi Zingine**

Muundo wa kanisa, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, ni muhimu kwa ajili ya ukuaji wa kiroho wa washiriki na kwa ajili ya utekelezaji wa utume wa Kanisa. Muundo huo ni mhimili wa jumuiya ya kikanisa. “Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo” (Efe. 4:16).

Vipengele muhimu kabisa vya muundo na mfumo wa kanisa ni maofisa (tazama uk. 71-84) na idara pamoja na taasisi zingine. Sehemu hii inaelezea makusudi, uongozi na kazi za vipengele hivyo.

Kazi ya idara na taasisi saidizi inahusiana sana na kazi ya mchungaji kwani wote wanashughulika katika huduma ya injili. Mchungaji hufanya kazi kama mshauri wa taasisi hizo, nazo kwa

upande wake husaidia katika programu za huduma za kanisa zima. Wakati wa dharura, au ikibidi, mchungaji anaweza kuitisha mkutano wa kamati au taasisi yo yote.

Kila kanisa halina budi kutumia huduma za idara na taasisi kulea washiriki wake na kutimiza utume uliotolewa na Kristo (Tazama Mat. 28:19; Ufu. 10:11; 14:6).

## Huduma za Watoto

Huduma za watoto hukuza imani ya watoto tangu kuzaliwa mpaka umri wa miaka 14, zikiwaelekeza katika umoja na Kanisa. Hujaribu kutoa huduma mbalimbali zitakazowaelekeza watoto kwa Yesu na kuwafundisha kutembea naye kila siku. Hushirikiana na Shule ya Sabato na idara zingine kutoa elimu ya dini kwa watoto na hutimiza utume wake kwa kuanzisha huduma mbalimbali za watoto zenye mwelekeo wa neema zinazojumuisha watoto wote, zenye mwelekeo wa huduma, zinazojenga uwezo wa kuongoza, zilizo salama na za uinjilisti.

"Mafunzo ya awali ya watoto yana umuhimu usiopimika. Mambo ambayo mtoto hujifunza katika miaka saba ya kwanza ya maisha yana mchango mkubwa zaidi katika kujenga tabia yake kuliko yote anayojifunza katika miaka inayofuata."—CG 193.

"Bado ni kweli kwamba watoto huguswa zaidi na mafundisho ya injili; mioyo yao iko tayari kupata ushawishi wa Mungu, na ina nguvu ya kuhifadhi mambo waliyojifunza. Watoto wadogo wanaweza kuwa Wakristo, wakiwa na hisia za Kikristo kulingana na miaka yao. Wanahitaji kuelimishwa katika mambo ya kiroho, na wazazi hawana budi kuwapatia kila fursa, ili wajenge tabia zinazofanana na tabia ya Kristo."—DA 515.

"Watoto wa miaka minane, kumi, au kumi na miwili ni wakubwa kiasi cha kutosha kufundishwa somo la dini mahususi. ... Wakifundishwa vizuri, watoto wadogo sana wanaweza kuwa na mtazamo sahihi juu ya hali yao kama wenye dhambi na juu ya njia ya wokovu katika Kristo."—1T 400.

"Yesu alipowaambia wanafunzi wake wasiwazuie watoto kuja kwake, alikuwa anazungumza na wafuasi wake katika enzi zote—na maofisa wa kanisa, wachungaji, wasaidizi, na Wakristo wote.

Yesu anawavuta watoto, na anatuambia, Waacheni waje kwangu; kana kwamba anasema, Msipowazuia, watakuja."—DA 517

***Mratibu wa Huduma za Watoto na Kamati*—**Kanisa huchagua mratibu wa huduma za watoto kustawisha huduma ambazo hujenga imani ya watoto. Inapasa mratibu huyo awe na uwezo wa kuongoza na pia uzoefu na upendo wa kuhudumia watoto.

Mratibu wa huduma za watoto hufanya kazi pamoja na mchungaji na baraza kuanzisha kamati ya huduma za watoto ili kutoa huduma kwa watoto. Kamati hiyo itakuwa na watu wanaopenda na wenye uzoefu wa kuhudumia watoto. Wajumbe wa kawaida ni pamoja na viongozi wa vitengo vya Shule ya Sabato, kiongozi wa Shule ya Biblia Wakati wa Likizo, viongozi wa Vijana Wadogo wa Kiadventista, na watu wengine wawili au watatu walio na shauku ya kuhudumia watoto.

Kama kanisa lina idara ya huduma za watoto, Shule za Biblia Wakati wa Likizo, matawi ya Shule ya Sabato ya Watoto, Vilabu vya Biblia kwa Majirani na Saa za Visa, vitakuwa chini ya uongozi wa huduma za watoto (Tazama uk, 85.)

Kila anayehusika katika kuhudumia watoto hana budi kukidhi vigezo na matakwa ya kisheria na ya Kanisa, kama vile kuchunguza historia yake au kuwa na cheti. Viongozi wa kanisa mahalia hawana budi kuwasiliana na konferensi ambayo itawahakikishia na kuwashauri kuhusu uchunguzi wa historia na vyeti vinavyoweza kupatikana. (Tazama maelezo, #7, uk. 168, 169.)

***Miongozo*—**Kuhusu miongozo ya huduma za watoto tazama Maelezo, #8, uk. 169.

## Mawasiliano

Huduma ya mawasiliano inahitaji msaada wa kila mlei, kila mfanyakazi wa Kanisa na kila taasisi ya kanisa. Idara ya mawasiliano huhamasisha utumiaji wa programu thabiti ya uhusiano na mbinu zote za kisasa za mawasiliano, tekinolojia endelevu na vyombo vya habari katika kueneza injili. Inalipasa kanisa kuchagua katibu wa mawasiliano na kamati ya mawasiliano kama inahitajika.

“Inatupasa kutumia kila njia iliyo halali kuleta nuru kwa watu. Vyombo vya habari vitumike, na kila shirika la matangazo litakalovuta usikivu juu ya kazi ya Mungu.”—6T 36.

“Njia zitabuniwa za kuifikia mioyo. Baadhi ya njia zitumikazo katika kazi hii zitakuwa tofauti na njia zilizokuwa zinatumika zamani.”—Ev 105.

***Katibu wa Mawasiliano*—**Katibu wa mawasiliano hana budi kuwa na uwezo wa kukutana na watu na kuliwakilisha vyema Kanisa, awe na hekima, mipangilio mizuri, ujuzi wa uandishi, na awe tayari kutekeleza kazi.

Katibu hukusanya na kusambaza habari kwa vyombo mahalia vya habari, hushirikiana na mkurugenzi wa mawasiliano wa konferensi na hutoa taarifa zitolewazo kwa vipindi maalum kwa mkutano mkuu. Idara ya mawasiliano ya konferensi kutoa maelekezo stahiki na msaada kwa makatibu wa mawasiliano.

Mchungaji, ambaye ana jukumu hasa la programu ya mawasiliano ya kanisa, atafanya kazi kwa karibu na katibu au kamati ya mawasiliano kama mshauri.

Idara au taasisi yo yote inaweza kuchagua mtu wa kumpatia habari katibu au kamati juu ya matukio yanayostahili kutangazwa.

***Kamati ya Mawasiliano*—**Katika kanisa kubwa kamati ya mawasiliano inaweza kushughulikia kwa ukamilifu zaidi nyanja nyingi za uhusiano na programu ya mawasiliano. Kanisa huchagua kamati hiyo na katibu wa mawasiliano huwa mwenyekiti. Wajumbe wa kamati wanaweza kupewa majukumu mahususi ya mawasiliano, kama vile kuwasiliana na vyombo vya habari, watengenezaji wa vitu vinavyohifadhi sauti na picha na watu wa mtandao, pamoja na taasisi za habari za ndani ya kanisa. Kama kuna taasisi ya kanisa jirani, mjumbe wa kamati ya uhusiano au mawasiliano ya taasisi hiyo, hana budi kukaribishwa katika kamati ya mawasiliano ya kanisa.

***Kamati ya Pamoja ya Mawasiliano*—**Makanisa kadhaa yaliyo katika eneo moja yakiunda kamati ya pamoja ya mawasiliano, katibu wa mawasiliano wa kila kanisa atakuwa mjumbe na itampasa

kufanya kazi sambamba na mpango wa pamoja utakaoratibu vizuri zaidi masuala ya habari na mambo mengine yanayohusu vyombo vya habari kwa makanisa hayo yanayoshirikiana. Kuundwa kwa kamati hii kutaanzishwa na mkurugenzi wa mawasiliano wa konferensi. Mikutano ya kamati ya pamoja itaitishwa na kusimamiwa na mwenyekiti atakayechaguliwa na kundi hilo.

## Elimu

Taasisi za kanisa huendesha shule kuanzia chekechea hadi chuo kikuu kwa makusudi ya kuwapatia wanafunzi kanuni za maisha, imani, mitazamo, maadili, tabia na desturi za Kanisa. Chanzo, mbinu na makusudi ya elimu ya Kiadventista ni elimu halisi ya Mungu, ushirika na uhusiano na Mungu katika masomo na huduma, na kufanana naye katika kujenga tabia.

***Katibu wa Elimu*—**Kanisa huchagua katibu wa elimu kuhamasisha na kukuza uungaji mkono wa elimu ya Kikristo. Katibu huyo ni mjumbe wa kamati tendaji ya Chama cha Kaya na Shule na hufanya kazi kwa kushirikiana na chama hicho.

***Chama cha Kaya na Shule*—**Kanisa lenye shule litaanzisha Chama cha Kaya na Shule, ambacho kitakuwa na kazi ya kutoa elimu kwa wazazi na kuunganisha kaya, shule na kanisa katika juhudi za kutoa elimu ya Kikristo kwa watoto. Wazazi wa wanafunzi, walezi wa shule, na washiriki hawana budi kuhamasishwa kuwa wanachama hai wa chama hicho.

Maofisa wa Chama cha Kaya na Shule watakuwa ni pamoja na kiongozi, kiongozi msaidizi, katibu-mhazini, mkutubi, na katibu wa elimu. (tazama uk. 172.) Ili kuwe na mwendelezo, inapasa baadhi ya maofisa wachaguliwe kwa kipindi cha pili. Wote wawe washiriki wa kanisa.

Kiongozi wa chama awe mshiriki mwenye mafanikio katika kufundisha watoto, ambaye moyo wake uko tayari kupokea mawazo mapya, na anayeona umuhimu wa elimu ya Kikristo.

Katibu-mhazini huandika kumbukumbu zote za chama na kutoa

taarifa kwa mkurugenzi wa idara ya elimu wa konferensi mwanzoni na mwishoni mwa kila mwaka wa masomo. Pesa za chama hupitia kwa mhazini wa kanisa/shule, huwekwa katika akaunti tofauti na hukaguliwa kulingana na sera ya Kanisa.

Mkuu wa shule ni mjumbe wa kamati ya Chama cha Kaya na Shule kwa wadhifa wake.

***Bodi ya Shule ya Kanisa*****—**Bodi ya shule ya kanisa iliyochaguliwa na kanisa au kamati ya shule iliyoteuliwa na baraza, itakuwa ndiyo, chombo cha utawala wa kila shule ya msingi na sekondari inayoendeshwa na kanisa moja. Kwa hiyo chombo hicho kinaweza kuwa bodi ya shule isiyokuwa sehemu ya baraza la kanisa, baraza la kanisa lenyewe au kamati ya baraza la kanisa inayoshughulikia shule iliyochaguliwa kwa lengo hilo. Sera za divisheni zinafafanua kazi za bodi za shule.

Wajumbe wa bodi hawana budi kuchaguliwa kwa ajili ya utauwa wao, imani na uaminifu wao kwa kanuni za elimu ya Kikristo, busara na hekima, uzoefu katika masuala ya shule, na hekima na uwezo wao katika masuala ya kifedha. Inawapasa wawe wanakubaliana na wawe tayari kufuata sera za elimu na mapendekezo ya Kanisa.

Kama makanisa mawili au zaidi yanaendesha shule ijulikanayo kama shule ya makanisa mengi, chombo cha utawala kitatokana na makanisa husika.

Mjumbe mmoja au zaidi wa bodi ya shule atachaguliwa kutoka katika baraza la kanisa, ili bodi ya shule ihusiane kwa karibu na baraza la kanisa.

Mchungaji hana budi kuwa mjumbe wa bodi ya shule. Kama shule inaendeshwa na zaidi ya kanisa moja, kwa kawaida wachungaji wa makanisa husika huwa wajumbe wa bodi.

Katika shule za sekondari na shule za msingi, mwalimu mkuu atakuwa mjumbe wa bodi.

Baadhi ya wajumbe wa bodi wanaweza kuwa wazazi wa watoto wanaosoma katika shule husika, ili bodi inufaike na maoni ya wazazi na ushauri unaotokana na uangalizi wa karibu na uzoefu.

Maofisa wa bodi ya shule watakuwa mwenyekiti na katibu. Kama shule inaendeshwa na kanisa moja, kanisa hilo litachagua mwenyekiti.

Katika bodi za shule za makanisa mengi, maofisa wa ziada watakuwa pamoja na mhazini, naibu mwenyekiti, na mhazini msaidizi. Baada ya kuchaguliwa, katika kikao chake cha kwanza, bodi ya pamoja itachagua mwenyekiti miongoni mwa wajumbe wake. Endapo hautapatikana mwafaka kati ya makanisa husika, uteuzi utafanywa na bodi ya elimu ya konferensi au kamati ya konferensi. Kwa kawaida mkuu wa shule huchaguliwa kuwa katibu wa bodi.

Uamuzi wo wote wa bodi ya shule ya makanisa mengi unaoyaingiza makanisa husika katika majukumu ya kifedha, hauna budi kuwasilishwa kwenye mabaraza husika ili upate idhini.

Mahali ambapo bodi ya shule isiyokuwa sehemu ya baraza la kanisa itachaguliwa, mmoja kati ya taratibu zifuatazo utafuatwa katika kuamua wakati wa kufanya uchaguzi na muda wa uongozi: (1) wajumbe wote wanaweza kuchaguliwa mwisho mwa mwaka wa kawaida au mwaka wa fedha na kufanya kazi kwa mwaka mmoja; (2) wajumbe wa bodi ya kwanza wanaweza kuchaguliwa kwa vipindi vya mwaka mmoja, miwili na mitatu na wa kuwapokea wakichaguliwa kila mwaka kwa vipindi vya miaka mitatu. Kusudi la mpango huu ni kuwa na wajumbe wenye uzoefu katika bodi kuhakikisha kuwa kuna mwendelezo wa sera. Wakati wa kujaza nafasi katikati ya muda wa uongozi, mjumbe mpya atatumikia kipindi kilichobaki cha muda wa uongozi.

Katika mwaka wa masomo, Bodi au kamati ya shule inatakiwa kukutana angalao mara moja kwa mwezi katika muda na mahali pa kawaida.

Mwenyekiti wa bodi ya shule ndiye anayeitisha mikutano, huwa mwenyekiti, na huhakikisha kuwa uamuzi wa bodi unatekelezwa, na hutia saini kuidhinisha malipo yote ya pesa yanayofanywa na katibu. Mwenyekiti ni mjumbe wa kamati ya ukaguzi ya shule ya msingi au sekondari, ambayo huchunguza na kutathmini shule husika na kazi zake.

Katibu huandika taarifa za kudumu za mikutano, huomba pesa za kulipia madeni na faradhi, na hufanya mawasiliano kwa niaba ya bodi.

Mahali ambapo kanisa moja linaendesha shule, kazi ya mhazini kwa kawaida hufanywa na mhazini wa kanisa au mhazini msaidizi

wa kanisa, ambaye hupokea ada na pesa zingine, hulipa kwa maagizo ya katibu (yaliyoidhinishwa kwa saini ya mwenyekiti), hutunza mahesabu sahihi ya malipo yote, na katika mkutano wa kila mwezi hutoa taarifa ya kina kwa bodi. Katika bodi ya makanisa mengi, mhazini huchaguliwa na bodi ya pamoja.

**Huduma za Familia**

Madhumuni ya huduma za familia ni kuimarisha ndoa na familia. Familia ilianzishwa kwa uumbaji wa Mungu na ndoa ikiwa kiini chake. Kama mahali pa awali ambapo maadili hufundishwa na uwezo wa kuhusiana na Mungu na watu wengine hujengwa, ustawi wake ni muhimu kwa kazi ya Kanisa ya kufanya watu wawe wanafunzi.

Huduma za familia hudumisha fundisho la Biblia kuhusu familia na huinua kiwango cha maisha ya familia kilichowekwa na Mungu. Wakati huo huo, huleta huruma wakati wa huzuni inayowapata watu na familia katika ulimwengu ulioanguka. Idara hii hufanya kuwe na huruma, umoja, na upendo nyumbani na katika familia ya Mungu. Huhamasisha mwafaka kati ya vizazi ambao umeahidiwa katika ujumbe wa Eliya wa Malaki 4:5, 6 na huleta tumaini na msaada kwa wale waliosononeshwa na unyanyasaji, kuvunjika kwa familia na kuvunjika kwa uhusiano. Fursa za kukua katika uhusiano hutolewa kwa njia ya elimu na ustawishaji wa maisha katika familia. Watu binafsi, wanandoa na familia husaidiwa ili wawe tayari kuonana na washauri nasaha inapobidi.

Huduma kwa familia katika kanisa mahalia huzingatia uongozi kwa watu wanaotarajia kuoana, programu za kuimarisha ndoa na elimu kwa wazazi. Huduma kwa familia pia huangalia mahitaji maalum ya wazazi wasio katika ndoa na familia za kambo na kutoa mafunzo ya uinjilisti wa familia kwa familia.

"Kazi tunayomfanyia Kristo haina budi kuanzia katika familia, yaani nyumbani. … Hakuna eneo la umisionari lililo muhimu kuliko hilo. … Eneo hili la nyumbani limepuuzwa na wengi kiasi cha kutia aibu, na sasa ni wakati wa kuwasilisha nyenzo na ufumbuzi wa Mungu ili hali hii ya uovu irekebishwe."—AH 35.

"Mungu anakusudia familia za duniani ziwe mfano wa familia

ya mbinguni. Nyumba za Kikristo, zilizoanzishwa na kuendeshwa kulingana na mpango wa Mungu, ni miongoni mwa njia za Mungu zifaazo kwa ajili ya kujenga tabia ya Kikristo na kwa ajili ya kuendeleza kazi yake."—6T 430.

"Kazi ya familia huenda mbali zaidi ya wanafamilia. … Ushawishi wa familia halisi juu ya mioyo na maisha ya watu, una nguvu zaidi kuliko hubiri lo lote linaloweza kuhubiriwa.

***Kiongozi/Viongozi wa Huduma za Familia***—Mtu mmoja au wanandoa (Tazama uk, 148-150 kuhusu ufafanuzi wa kanisa juu ya ndoa) anaweza/wanaweza kuchaguliwa kuhudumu kama kiongozi/viongozi wa huduma za familia. Inawapasa wawe kielelezo cha uhusiano wa ndoa ulio imara na unaokua na kuonesha shauku ya dhati ya kuhamasisha ustawi wa familia zote. Ili awe/wawe na ufanisi, kiongozi/viongozi hana/hawana budi kuuelewa vizuri mpango wa ukombozi uliowekwa na Mungu kwa ajili ya kushughulikia kuvunjika kwa uhusiano ambako dhambi imesababisha. Kiongozi/viongozi huyo/hao pia hana/hawana/budi kudumisha usiri stahiki na kujua wakati na namna ya kuwahimiza watu walio katika hali ngumu watafute ushauri wa kitaalamu.

***Kamati ya Huduma za Familia***—Baraza liweza kuunda kamati ya huduma za familia itakayokuwa chini ya uenyekiti wa kiongozi/viongozi wa huduma za familia.

***Miongozo***—Tazama Maelezo, #9, uk. 169, kwa ajili ya miongozo ya huduma za familia.

**Huduma za Afya**

Kanisa linaamini kuwa wajibu wake wa kumfanya Kristo ajulikane ni pamoja na wajibu wa kimaadili wa kuhifadhi utu wa mtu kwa kuhimiza viwango vya juu vya afya ya kimwili, kiakili na kiroho.

Pamoja na kuwahudumia wanaougua, jukumu hili linakwenda mpaka kwenye uzuiaji wa magonjwa kwa kutumia elimu ya afya inayofaa na uongozi katika kuhimiza afya murua bila kutumia tumbaku, vileo, dawa zingine za kulevya na vyakula najisi.

Inapowezekana, washiriki watahimizwa kimsingi kutokula vyakula vya nyama.

***Kongozi wa Huduma za Afya*—**Kanisa huchagua kiongozi wa huduma za afya na ikibidi kiongozi msaidizi kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza programu yenye ufanisi. Kiongozi huyo hana budi kuwa mtu anayejali afya na anayependa kuhamasisha viwango vya Kanisa vya kuishi kiafya miongoni mwa washiriki na katika jumuiya kwa kutumia programu za huduma za afya zinazoendeshwa na kanisa. Kiongozi huyo ni lazima aweze kuchuja programu na habari zinazowakilisha maadili na falsafa ya Kanisa na kuziingiza katika ushuhuda wa kiroho na kimwili wenye ufanisi.

***Baraza la Huduma za Afya*—**Inapowezekana, kanisa linaweza kuteua baraza la huduma za afya ili kuwe na uongozi kwa washiriki na katika jamii katika masuala ya kuishi kwa afya na kusaidia katika shughuli za pamoja za kuokoa roho kwa kutumia programu mwafaka ya afya na kiasi na kusisitiza mambo ya kiroho. Baraza hilo, kwa kusaidiana na baraza la huduma binafsi, litasimamia uandaaji wa ratiba ya shughuli za huduma za afya ambazo ni pamoja na programu kama za kuacha kuvuta, mafunzo ya upishi, mafunzo ya afya, programu za kudhibiti fadhaa, na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kama hatakuwa mwenyekiti, mchungaji atakuwa mjumbe kwa wadhifa wake

***Chama cha Huduma za Afya au Kiasi*—**Katika maeneo mengine kinaweza kuanzishwa chama cha huduma za afya na kiasi kama chombo kingine tofauti na taasisi za Kanisa. Mkurugenzi wa huduma za afya wa konferensi hana budi kuhusika katika uanzishaji wa chombo hicho.

***Sadaka ya Sabato ya Huduma za Afya Ulimwenguni*—**Sadaka ya Sabato ya Huduma za Afya Ulimwenguni kote hutumwa konferensi ili igawiwe kulingana na sera. Hadi asilimia 25 ya sadaka hiyo iliyopokelewa kanisani inaweza kurudi kwa kanisa husika kwa ajili ya programu za huduma za afya endapo kutakuwa na ombi la kanisa kwa konferensi.

*Miongozo*—Tazama Maelezo #10, uk. 169 kwa ajili ya miongozo ya huduma za afya.

**Muziki**

***Kuchagua Waratibu wa Muziki***—Inalipasa kanisa kuwa na tahadhari kubwa katika kuchagua viongozi wa muziki, likichagua wale waliojitoa kikamilifu tu na kutoa muziki unaofaa kwa ajili ya huduma zote za ibada na mikutano. Muziki wa kidunia au ule uletao mashaka kwa namna ulivyo, usiingizwe katika ibada zetu.

Viongozi wa muziki hawana budi kufanya kazi kwa karibu na mchungaji au wazee ili uchaguzi wa muziki uende sambamba na mada ya hubiri. Kiongozi wa muziki huwa chini ya uongozi wa mchungaji au wazee na hayuko huru kufanya kazi kama apendavyo. Kiongozi wa muziki hana budi kushauriana nao juu ya muziki wa kupiga na uchaguzi wa waimbaji na wapiga muziki.

***Kuchagua Wapiga Muziki***—Muziki mtakatifu ni sehemu muhimu ya ibada ya pamoja. Inalipasa kanisa kuwa na uangalifu katika kuchagua waimbaji na wapiga muziki wengine ambao watawakilisha vyema maadili ya Kanisa. Hawana budi kuwa washiriki wa kanisa, Shule ya Sabato, au Chama cha Vijana wa Kiadventista. Kwa kuwa wanashika nafasi inayoonekana katika ibada, inawapasa kuwa mfano wa staha na adabu katika kuonekana na mavazi yao. Majoho ya kwaya yanaweza kutumika.

Makanisa yanaweza kuwa na kwaya zaidi ya moja. Kwaya ya watoto ni njia ya malezi ya kiroho, ikiwafungamanisha na familia ya kanisa na uinjilisti.

**Mambo ya Jamii na Uhuru wa Kidini**

Idara ya mambo ya jamii na uhuru wa dini hukuza na kudumisha uhuru wa kidini, ikiwa na msisitizo juu ya uhuru wa dhamiri. Uhuru wa kidini ni pamoja na haki ya binadamu kuwa na au kufuata dini aliyoichagua, kubadili imani ya kidini kulingana na dhamiri, kudhihirisha imani kwa mtu binafsi au katika jumuiya pamoja na waumini wenza, katika ibada, maadhimisho, desturi, ushuhuda na kufundisha kwa sharti la kuheshimu haki sawa kwa wengine.

***Kiongozi wa Uhuru wa Kidini***—Kiongozi wa uhuru wa kidini aliyechaguliwa hushirikiana na mchungaji pamoja na idara ya mambo ya jamii na uhuru wa kidini ya konferensi au union. Kiongozi huyo lazima awe na mvuto chanya wa kiroho, aweze kukutana na umma wa kawaida, apendaye masuala ya jamii, mwandishi stadi na awe na shauku ya kuhifadhi uhuru wa watu wa Mungu.

***Vyama vya Uhuru wa Kidini***—Kila kanisa huchukuliwa kuwa ni chama cha uhuru wa kidini kisicho rasmi, na kila mshiriki wa kanisa huchukuliwa kuwa mwanachama wa chama hicho. Mchungaji au mzee ni mwenyekiti.

***Miongozo***—Tazama Maelezo, #11, uk. 170 kuhusu miongozo ya mambo ya jamii na uhuru wa kidini

## Huduma za Uchapishaji

Huduma za uchapishaji huratibu na kukuza uinjilisti wa vitabu chini ya usimamizi wa baraza la huduma za uchapishaji pamoja na taasisi husika katika eneo hilo. Husaidia idara zingine katika kutangaza, kuuza na kusambaza majarida yanayolipiwa kabla ya kuchapwa pamoja na machapisho mengine ya utume. Idara hii hufanya kazi na mchungaji na idara zingine katika kuandaa utaratibu wa kuwashirikisha washiriki katika huduma za uchapishaji.

"Kuna mahali pengi ambako sauti ya mchungaji haiwezi kusikika, mahali ambako kunaweza kufikiwa na machapisho yetu tu—vitabu, magazeti, na vitini vilivyojaa ukweli wa Biblia ambao watu wanauhitaji."—CM 4.

Kazi ya huduma za uchapishaji ni uinjilisti na malezi ya washiriki. Ellen G. White aliwahimiza washiriki "kuuza au kugawa bure machapisho yetu."—CM 91.

***Uuzaji kwa Kutumia Wainjilisti wa Vitabu***—"Mungu anahitaji wafanyakazi kutoka katika kila kanisa kati yetu waingie katika kazi yake kama wainjilisti wanaokwenda nyumba kwa nyumba [wainjilisti wa vitabu]."—CM 20.

***Washiriki Kugawa Bure*****—**"Kila muumini atawanye vitini na vipeperushi na vitabu vyenye ujumbe wa wakati huu."—CM 21.

***Mratibu wa Huduma za Uchapishaji*****—**Kanisa huchagua mratibu wa huduma za uchapishaji ili kuwe na uongozi katika shughuli za uinjilisti wa vitabu.

***Baraza la Huduma za Uchapishaji*****—**Baraza la kanisa huteua baraza la huduma za uchapishaji linalofanya kazi chini ya uongozi wake. Mratibu wa huduma za uchapishaji ndiye mwenyekiti wa baraza la huduma za uchapishaji. Mchungaji, kiongozi wa huduma binafsi na katibu wa huduma binafsi, ni wajumbe kwa wadhifa wao. Inawapasa wajumbe kupenda na kuwa na uzoefu wa uinjilisti wa vitabu.

***Miongozo*****—**Tazama Maelezo, #12, uk. 170 kuhusu miongozo ya huduma za uchapishaji.

### Shule ya Sabato na Huduma binafsi

#### Shule ya Sabato

Shule ya Sabato ambayo ni programu ya msingi ya elimu katika Kanisa, ina malengo manne: kusoma maandiko, ushirika, huduma kwa jamii na kusisitiza utume ulimwenguni. Idara ya Shule ya Sabato na Huduma Binafsi ya Konferensi Kuu husambaza miongozo ya kusoma Biblia kwa viwango vyote vya umri, hutoa miundo ya programu za shule ya Sabato katika muktadha wa utamaduni mbalimbali wa divisheni za ulimwengu, hutoa miongozo na mifumo ya mafunzo kwa ajili ya walimu wa shule ya Sabato, na huhamasisha utoaji wa sadaka za shule ya Sabato kwa ajili ya utume wa ulimwengu.

"Shule ya Sabato ni tawi muhimu la kazi ya umisionari, siyo kwa sababu tu hutoa maarifa ya Neno la Mungu kwa vijana na wazee, lakini kwa sababu huchochea ndani yao, moyo wa kuupenda ukweli mtakatifu wa Neno hilo, na shauku ya kuusoma wao wenyewe; zaidi ya yote, huwafundisha kuendesha maisha yao kulingana na mafundisho matakatifu ya ukweli huo."—CSW 10, 11.

"Shule ya Sabato, ikiendeshwa vizuri, ni moja kati ya zana kuu za Mungu za kuwafanya watu wauelewe ukweli."—CSW 115.

***Maofisa wa Baraza la Shule ya Sabato*—**Kanisa huchagua maofisa wa shule ya Sabato na wajumbe wa baraza la shule ya Sabato. Maofisa ni pamoja na Mrakibu na warakibu wo wote wasaidizi; katibu na makatibu wo wote wasaidizi; kiongozi wa kila kitengo ikiwa pamoja na vitengo vya watu wazima na utandaaji; mratibu wa huduma za watoto na/au mkurugenzi wa Shule ya Biblia Wakati wa Likizo na katibu wa uwekezaji.

Maofisa hao, walimu na washiriki wote wa shule ya Sabato hawana budi kushirikiana na idara zingine katika kazi ya umisionari, na kuendesha uinjilisti wa shule ya Sabato kwa njia ya vikosi vya kawaida na shughuli zingine kama vile Siku za Uamuzi, madarasa ya Mchungaji ya Biblia, Sabato za Wageni, Shule za Biblia Wakati wa Likizo, na Shule za Sabato za matawi, ikiwa ni pamoja na Vilabu vya Biblia kwa majirani na simulizi za visa.

Baraza la shule ya Sabato ndiyo chombo cha utawala cha Shule ya Sabato. Linaundwa na Mrakibu (ambaye ni mwenyekiti), warakibu wo wote wasaidizi, katibu (ambaye ni katibu wa baraza la shule ya Sabato), makatibu wo wote wasaidizi, viongozi wa vitengo, katibu wa uwekezaji, kiongozi wa huduma binafsi, mratibu wa huduma za watoto na/au mkurugenzi wa Shule ya Biblia Wakati wa Likizo, mzee mmoja (aliyechaguliwa na baraza la kanisa au na la wazee) na mchungaji.

Mrakibu hana budi kuitisha kikao cha baraza haraka iwezekanavyo mara baada ya maofisa hao kuchaguliwa ili kiteue maofisa wengine kadiri watavyohitajika kwa ajili ya vitengo mbalimbali, ambao si wajumbe wa baraza. Hawa wanaweza kuwa pamoja na viongozi wasaidizi wa vitengo, makatibu wa vitengo, waimbishaji, wapiga piano/au ogani na wakaribishaji.

Pamoja na viongozi wanaoteuliwa walioorodheshwa hapo juu, baraza la shule ya Sabato huangalia mahitaji ya vitengo na makundi yote na kuteua walimu ambao majina yao huwasilishwa kwa baraza la kanisa ili yaidhinishwe. Ili kudumisha hadhi ya mtaala wa masomo ya shule ya Sabato na ubora wa ufundishaji, baraza la shule ya Sabato halina budi kuwa na uangalifu mkubwa katika

kuchagua walimu. Hasa katika kuchagua walimu wa vitengo vya watoto, inabidi baraza lishauriane na viongozi wa vitengo. Walimu wote hawana budi kuwa washiriki hai wa kanisa.

Baraza la shule ya Sabato linawajibika na uendeshaji fanisi wa shule ya Sabato yote kupitia kwa mrakibu. Baraza la shule ya Sabato litakutana mara kwa mara kama itakavyohitajika. Inalipasa baraza la shule ya Sabato kuhakikisha kwamba vifaa vya kutumia katika programu na masomo ikiwa pamoja na mwongozo wa kusoma Biblia wa Shule ya Sabato unaoandaliwa na Konferensi Kuu, vinapatikana vya kutosha.

***Mrakibu wa Shule ya Sabato na Maofisa Wengine wa Shule ya Sabato*—**Mrakibu ni ofisa kiongozi wa shule ya Sabato na inampasa kuanza kupanga mipango ya ufanisi na uendeshaji wake mzuri wenye ufanisi mara baada ya kuchaguliwa. Mrakibu hana budi kusaidia mipango na mambo yanayotiliwa mkazo na idara ya shule ya Sabato ya konferensi na inampasa kutekeleza uamuzi wa baraza la shule ya Sabato kuhusu uendeshaji wa shule ya Sabato. Kanisa linaweza kuchagua mrakibu msaidizi mmoja au zaidi.

Katibu atajaza taarifa ya robo katika fomu maalum mara baada ya Sabato ya mwisho ya robo na kuituma kwa wakurugenzi wa shule ya Sabato na huduma binafsi, kabla ya siku ya mwisho iliyowekwa. Katibu hana budi pia kuweka nakala katika faili la kudumu la katibu, kuwapa nakala mrakibu na mchungaji, na kuiwasilisha katika mkutano mkuu wa kanisa.

Katibu wa uwekezaji huhamasisha mpango wa uwekezaji kwa ajili ya kusaidia utume katika vitengo vyote vya shule ya Sabato na kuwaarifu washiriki jinsi mpango huo unavyoendelea.

Mkurugenzi wa Shule ya Biblia Wakati wa Likizo huongoza katika kupanga, kuhamasisha, na kuanzisha uinjilisti katika jamii kwa kutumia Shule ya Biblia Wakati wa Likizo kila mwaka. Kanisa linaweza kuweka jukumu hili kwa mratibu wa huduma za watoto.

Baraza linaweza kuteua mwimbishaji wa shule ya Sabato kwa kushauriana na viongozi wa vitengo. Muziki ambao ni njia ya kuonesha ibada, hauna budi kumtukuza Mungu. Waimbaji na wapiga muziki wengine hawana budi kuchaguliwa kwa uangalifu kama ilivyo kwa viongozi wa sehemu zingine za huduma ya shule

ya Sabato na inabidi wapimwe kwa vipimo hivyo hivyo. (tazama uk. 92, 144.) Baraza pia linaweza kuteua wapiga piano na wapiga ogani kwa ajili ya vitengo.

***Viongozi wa Vitengo vya Shule ya Sabato*—**Baraza la kanisa huchagua kiongozi wa kila kitengo. Baraza la shule ya Sabato linaweza kuteua viongozi wasaidizi wa vitengo kama itakavyohitajika. *Mwongozo wa Shule ya Sabato* unaopatikana katika maduka ya vitabu ya Waadventista au idara ya shule ya Sabato ya konferensi, una maelezo juu ya vitengo vyote, kuanzia kitengo cha awali hadi kitengo cha watu wazima na kitengo ya utandaaji ambacho huhudumia wasioweza kuhudhuria katika shule ya Sabato.

***Walimu wa Shule ya Sabato*—**Baraza la shule ya Sabato huchagua walimu wa shule ya Sabato na baraza la kanisa huwaidhinisha. Inawapasa wawe na uwezo wa kufundisha na kuwa tayari kujifunza njia za kuboresha uwezo wao wa kufundisha. Inawapasa kuwa makini katika maandalizi, wahudhuriaji wazuri wanaofika kwa wakati, na wawe mfano katika usomaji wa kila siku wa mwongozo wa kusoma Biblia wa shule ya Sabato.

Baraza halina budi kufanya juhudi maalum kuchagua walimu wa watoto na vijana walio na mapenzi na umri huo na uwezo wa kukidhi mahitaji yao. Kila anayehusika na shughuli za vitengo vya watoto hana budi kukidhi viwango vya Kanisa na vya kisheria, kama vile uchunguzi wa historia zao au kuwa na vyeti. Viongozi wa kanisa mahalia hawana budi kushauriana na konferensi ambayo itahakikisha na kushauri juu ya uchunguzi wa historia na vyeti vinavyoweza kupatikana na/au kuhitajika. (Tazama Maelezo, #7, uk. 168. 169.) Walimu wote hawana budi kuhimizwa kushiriki katika mafunzo yapatikanayo kupitia idara ya shule ya Sabato ya konferensi.

Kila shule ya Sabato haina budi kuwa na mkutano wa walimu wa kila juma.

Wakitambua kuwa “hakuna watakaosimama katika pambano kuu la mwisho isipokuwa wale walioimarisha mioyo kwa ukweli wa Biblia” (GC 593, 594), viongozi wa shule Sabato hawana

budi kuhimiza kwa nguvu usomaji wa Neno kwa mpango, desturi ambayo imesaidia sana kudumisha umoja katika Kanisa lote. Inapasa kila mshiriki aweze kupata mwongozo wa shule ya Sabato wa kusoma Biblia unaofaa kwa umri wake ambao huchapishwa na Konferensi Kuu na/au divisheni. Vivyo hivyo, inapasa kila kiongozi na mwalimu aweze kupata vitendea kazi vinavyotengenezwa na Konferensi Kuu na/au divisheni kwa ajili ya vitengo mbalimbali vya shule ya Sabato.

Inawapasa walimu kuwa na dakika zisizopungua 30 kwa ajili ya kufundisha madarasa yao.

***Sadaka za Shule ya Sabato*—**Katibu wa shule ya Sabato hana budi kuandika kwa usahihi sadaka za shule ya Sabato na kuzipeleka kwa mhazini wa kanisa mara moja. Sadaka za kitengo cha utandaaji hazina budi kujumlishwa kwenye sadaka za kawaida za shule ya Sabato. Shule nyingi za Sabato hukusanya sadaka kwa ajili ya matumizi ya shule ya Sabato. Ukitoa mfuko huo wa matumizi, sadaka zote za shule ya Sabato ni kwa ajili ya kusaidia maeneo ya utume na hazina budi kupelekwa kama zilivyo kwa mhazini wa konferensi. Pesa hizo ni pamoja na sadaka ya kawaida ya shule ya Sabato kila juma, sadaka ya Sabato ya kumi na tatu, uwekazaji wa shule ya Sabato na sadaka ya shukurani ya sherehe ya kuzaliwa. Kila moja lazima ianishwe kama fungu tofauti katika mfumo wa fedha wa kanisa. Pesa za utume hugawiwa kulingana na sera. Hakuna pesa za utume zinazoweza kubakia kanisani au katika konferensi.

Mahali ambapo kalenda ya sadaka hutumika, sadaka ya matumizi ya shule ya Sabato na sadaka ya utume, zisikusanywe kama sadaka moja na kugawanywa kulingana na fomula au asilimia iliyokubaliwa. Sadaka hizi zinaweza kukusanywa pamoja mahali ambapo kanisa linatumia mpango ulioidhinishwa na divisheni wa sadaka ya pamoja.

***Miongozo*—**Tazama Maelezo, #13, uk. 17, kuhusu miongozo ya shule ya Sabato na huduma binafsi.

## Huduma Binafsi

Huduma mahususi hutoa zana na kufundisha washiriki kuunganisha juhudi zao na zile za mchungaji na maofisa katika

huduma ya kuongoa roho. Pia ina jukumu kubwa kwa ajili ya programu za kusaidia wahitaji.

***Baraza la Huduma Mahususi***—Baraza la huduma mahususi huongoza juhudi za utume za kanisa na kufanya kazi chini ya uongozi wa baraza la kanisa. Baraza la huduma mahususi litakutana japo mara moja kila mwezi na litakuwa na mchungaji, mzee mmoja, mhazini, na viongozi wa idara zingine na huduma saidizi zilizo katika kanisa husika. Baraza la huduma mahususi linaweza kuunda kamati ndogo-ndogo kwa ajili ya kazi maalum. Kamati ndogo-ndogo zote huwajibika kwa baraza la huduma mahususi. Baraza la huduma mahususi na kiongozi wana wajibu wa kuanzisha huduma za vikundi vidogo-vidogo.

***Maofisa wa Huduma Mahususi***—Kanisa huchagua maofisa wa huduma mahususi ikiwa pamoja na kiongozi, wasaidizi (kadiri watakavyohitajika), na katibu.

Kiongozi huwafundisha na kuwaelekeza washiriki katika umisionari, na ni mwenyekiti wa baraza la huduma mahususi. Kiongozi hutoa taarifa katika ibada ya huduma ya kila mwezi kuhusu shughuli zote za utume za kanisa. Wasaidizi wanaweza kupewa kazi ya kuratibu Shule ya Biblia kwa njia ya posta, uinjilisti wa Biblia, ugawaji wa machapisho, mavuno (au wito mwingine kama huo), huduma za vikundi vidogo-vidogo, kufundisha washiriki, na programu zingine za kuongoa roho.

Katibu hufanya kazi kama mwakilishi wa duka la vitabu la Waadventista kwa ajili ya idara zote za kanisa na hufanya kazi na kiongozi katika kuandaa programu za utume za kanisa.

***Wanaume wa Kiadventista***—Wanaume wa Kiadventista ni kitengo cha idara ya huduma mahususi. Huduma za wanaume wa kiadventista hujumuisha mikutano ya mahubiri, huduma magerezani, na huduma za Jamii.

***Mratibu wa Shule ya Biblia***—Mratibu wa shule ya Biblia hupanga na kuratibu huduma ya kanisa ya shule ya Biblia kwa jamii. Mratibu hana budi kufanya kazi na mchungaji, mratibu wa waliovutiwa na kiongozi wa huduma mahususi.

***Kiongozi wa Huduma za Jamii/Chama cha Dorkas*—**Kanisa huchagua kiongozi wa Huduma za Jamii/Chama cha Dorkas, viongozi wasaidizi (kadiri watakavyohitajika), na katibu-mhazini. Asasi hii hukusanya na kuandaa nguo, chakula, na mahitaji mengine kwa ajili ya wahitaji na kufanya kazi kwa karibu na mashemasi wa kike na wa kiume. Hata hivyo, Huduma za Jamii/Dorkas ni zaidi ya kutoa msaada wa mali. Hujumuisha elimu ya watu wazima, kutembelea, huduma za nyumbani, uuguzi majumbani, ushauri nasaha na huduma zingine.

Kama kanisa lina kituo cha Huduma za Jamii, baraza la huduma mahususi litakuwa chombo chake cha utawala. Baraza hilo litateua mkurugenzi wa kituo hicho, ambaye ni mjumbe wa baraza la huduma mahususi.

***Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu*—**Huduma hii hufanya kazi chini ya baraza la huduma mahususi na huandaa programu kwa ajili ya washiriki na watu wengine wenye ulemavu. Haina budi kuandaa programu za ushuhudiaji, kupendekeza namna ya kufanya huduma za kanisa zipatikane kwa urahisi zaidi, kusaidia kutatua matatizo ya usafiri, na kupendekeza njia za kuwashirikisha washiriki wenye ulemavu. Mratibu wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu hufanya kazi kama kiungo na asasi zingine zinazotoa huduma kwa walemavu kama vile ***Christian Record Services*** na huhamasisha programu za ***Christian Record Services***.

***Miongozo*—**Tazama Malezo, #13, uk. 170 kwa ajili ya miongozo ya shule ya Sabato na huduma mahususi

**Huduma za Uwakili**

Huduma za uwakili huhimiza washiriki kuitikia neema ya Mungu kwa kuweka wakfu kwake vyote walivyo navyo. Majukumu ya uwakili ni zaidi ya pesa. Ni pamoja na utunzaji na utumiaji bora wa mwili, akili, muda, uwezo, karama za roho, na uhusiano, ushawishi, lugha, mazingira na mali. Idara hii husaidia washiriki katika ushirika wao na Mungu katika kumaliza kazi yake kwa kutumia vizuri karama na raslimali zote za Mungu.

Roho wa Mungu anapotawala maisha ya mtu, "wale ambao mioyo yao imejaa upendo wa Kristo watafuata mfano wake ambaye alikuwa maskini kwa ajili yetu, ili kwa njia ya umaskini wake, tufanywe kuwa matajiri. Pesa, muda, ushawishi—karama zote walizopata kutoka mkononi mwa Mungu, watazithamini tu kama nyenzo za kuendeleza kazi ya injili."—AA 71.

***Kiongozi wa Huduma za Uwakili***—Kiongozi wa huduma za uwakili hana budi kutimiza kanuni za uwakili wa Kikristo na inampasa kuielewa huduma ya kiroho ya kifedha ifanywayo na Kanisa. Kiongozi huyo atafanya kazi kwa kushirikiana na mkurugenzi wa huduma za uwakili wa konferensi, mchungaji, na baraza la kanisa. Kiongozi huyo hufanya kazi kama kiungo kati ya idara ya huduma za uwakili ya konferensi na kanisa.

***Miongozo*****—**Tazama Maelezo, #14, uk. 170 kwa ajili ya miongozo ya huduma za uwakili

**Huduma za Wanawake**

Huduma za wanawake huendeleza, huhimiza, na kuwapa changamoto wanawake katika kutembea kwao kila siku kama wanafunzi wa Yesu Kristo na washiriki wa kanisa lake.

Malengo yake ni kuhamasisha ukuaji wa kiroho na uamsho; kusisitiza kuwa wanawake wana thamani isiyopimika kwa sababu ya kuumbwa na kukombolewa kwao, kuwaandaa kwa ajili ya huduma na kueleza mitazamo ya wanawake katika masuala ya kanisa; kuhudumia upeo wote wa mahitaji ya wanawake kwa kuzingatia mitazamo ya utamaduni na makabila mbalimbali; kushirikiana na idara zingine kurahisisha huduma za wananawake na kwa wanawake; kujenga mapenzi mema miongoni mwa wanawake, kuhimiza kusaidiana na kubadilishana mawazo kwa ubunifu; kuwashauri na kuwatia moyo wanawake na kutengeneza njia kwa ajli ya ushiriki wao katika kanisa; na kutafuta njia na namna ya kumpa changamoto kila mwanamke kutumia karama zake kuendeleza utume ulimwenguni.

***Kiongozi na Kamati ya Huduma za Wanawake***—Kiongozi wa huduma za wanawake aliyechaguliwa huanzisha huduma maalum kulea wanawake na kuwaandaa kwa ajili ya huduma. Yeye ni mwenyekiti wa kamati ya huduma za wanawake na huhamasisha mawazo na mipango inayokuza mchango wa wanawake katika kazi ya Kanisa.

Kiongozi huyo hulisaidia baraza la kanisa kwa kujumuisha shughuli na programu za wanawake katika programu kuu ya kanisa. Hulipatia kanisa taarifa ya mchango wa huduma za wanawake katika uhai wa kanisa. Mtu wa kuwasiliana na kiongozi huyo kuhusu mafunzo na vitendea kazi ni mkurugenzi wa huduma za wanawake wa konferensi.

Kiongozi wa huduma za wanawake hana budi awe mwanamke makini anayejali ambaye anawiwa na huduma ya wanawake na matatizo yao, mwenye ulingano katika mitazamo yake, mwenye uwezo wa kuwatia moyo wanawake wengine kukuza karama zao za kiroho na mwenye uwezo wa kuhudumia vizuri wanawake, akishirikiana na mchungaji na baraza la kanisa.

Kamati ya huduma za wanawake huhamasisha huduma kwa wanawake katika kanisa. Kamati hii haina budi kuundwa na watu wanaopenda kuhudumia upeo wote wa mahitaji na huduma za wanawake na wenye talanta na uzoefu mbalimbali.

***Miongozo***—Tazama Maelezo, #15, uk. 170 kuhusu miongozo ya huduma za wanawake.

**Huduma za Vijana**

Vyama mbalimbali vya vijana kanisani havina budi kufanya kazi kwa karibu na idara ya huduma za vijana ya konferensi.

***Chama cha Vijana wa Kiadventista (CVK)***—Kanisa huhudumia vijana na kufanya nao kazi kwa kutumia CVK. Inawapasa vijana kufanya kazi pamoja chini ya kiongozi wa chama cha vijana katika kujenga huduma imara ya vijana inayojumuisha ustawi wa kila mmoja kiroho, kiakili na kimwili, shughuli za kijamii za Kikristo na programu hai ya ushuhudiaji inayosaidia mipango mikuu ya kanisa ya uongoaji wa roho. Lengo la chama cha vijana liwe kuwahusisha

vijana wote katika shughuli zitakazowaunganisha na kanisa na kuwafundisha kwa ajili ya huduma ya Kikristo.

Mungu alimwambia Musa, "Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako" (Kum. 6:6-9).

Mtume Paulo aliongeza kusema, "Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi" (1 Tim. 4:12).

"Tuna jeshi la vijana leo ambao wanaweza kufanya makubwa wakielekezwa vizuri na kutiwa moyo. … Tunataka wabarikiwe na Mungu. Tunataka wafanye sehemu katika mipango iliyopangwa vizuri kwa ajili ya kuwasaidia vijana."—GCB, Jan. 29, 30, 1893, uk. 24.

"Vijana wanapotoa mioyo yao kwa Mungu, wajibu wetu kwa ajili yao hauishi. Inapasa wasaidiwe kuipenda kazi ya Bwana na kufanywa waone kwamba anatarajia wachangie kuendeleza kazi yake. Haitoshi kuonesha kiasi cha kazi kipasacho kufanyika, na kuwahimiza vijana kufanya sehemu fulani. Hawana budi kufundishwa kumfanyia kazi Bwana. Inabidi wafundishwe, waadibishwe na kuzoeshwa katika njia bora za kuongoa roho kwa ajili ya Kristo. Wafundisheni kujaribu kuwasaidia vijana wenzao katika njia ya utulivu usiokuwa na unafiki. Nyanja mbalimbali za shughuli za utume ambazo wanaweza kushiriki zielezewe, na wapewe maelekezo na msaada. Kwa njia hiyo watajifunza kumtumikia Mungu."—GW 210.

"Tukiwa na jeshi la watenda kazi, kama lile ambalo vijana wetu, waliofundishwa vizuri wanaweza kuunda, ujumbe wa Mwokozi aliyesulibiwa, akafufuka na anayekuja hivi karibuni utapelekwa ulimwenguni kote haraka sana!"—MYP 196.

Wakati inapasa kuwe na chama hai cha vijana katika kila kanisa, ni muhimu programu za vijana zisitengwe na kanisa lote. P amoja na ushiriki wao katika chama cha vijana, inapasa vijana wahusishwe katika uongozi wa kazi na katika nyanja zote za kazi ya kanisa.

Kwa mfano, wakiwa wazee wa kanisa vijana, mashemasi wa kiume na wa kike, wanaweza kufanya kazi pamoja na kujifunza kutoka kwa maofisa wenye uzoefu.

"Ili kazi isonge mbele katika nyanja zake zote, Mungu anahitaji nguvu, ari na ujasiri wa ujana. Amewachagua vijana wasaidie kuendeleza kazi yake. Kupanga kwa akili angavu na kutenda kwa mkono wa ujasiri kunahitaji nguvu mpya zisizolemaa. Vijana wa kike na wa kiume wanaalikwa kutoa nguvu za ujana wao kwa Mungu, ili kwa kutumia nguvu zao, kwa fikra makini na ushupavu waweze kuleta utukufu kwa Mungu na wokovu kwa wanadamu wenzao."—GW 67.

***Kamati ya Huduma za Vijana*****—**Kamati ya huduma za vijana ni asasi kuu katika kanisa kwa ajili ya kupanga mipango mikuu ya programu ya huduma za vijana. (Tazama uk, 127, 128.) Inajumuisha maofisa wa chama cha vijana waliochaguliwa pamoja na kiongozi wa huduma mahususi, kiongozi wa kitengo cha vijana cha shule ya Sabato, kiongozi wa huduma za afya, mkurugenzi wa klabu ya mabalozi, mkurugenzi wa klabu ya watafuta njia, mkurugenzi wa klabu ya wagunduzi, mkuu wa shule, mdhamini, na mchungaji. Kiongozi wa chama cha vijana ambaye ni mjumbe wa baraza la kanisa ni mwenyekiti wa kamati hiyo. Kamati haina budi kukutana kadiri inavyohitajika kuweka malengo ya muda mfupi na mrefu na mipango ya huduma yenye mafanikio.

***Kamati ya Chama cha Vijana*****—**Kamati ya chama cha vijana inawajibika katika shughuli za vijana wakubwa na kufanya kazi kwa kushirikiana na asasi zingine kwa njia ya kamati ya huduma za vijana wa Kiadventista. Kama hakuna programu za mabalozi, watafuta njia na wagunduzi, chama cha vijana kitawajumuisha wanachama hawa wadogo katika chama kidogo.

***Maofisa wa Chama cha Vijana*****—**Kanisa huchagua maofisa wafuatao wa chama cha vijana: kiongozi wa vijana, kiongozi msaidizi wa vijana, katibu-mhazini, katibu-mhazini msaidizi, mwimbishaji, mpiga piano au ogani, mdhamini (ambaye anaweza kuwa mzee wa kanisa). Kwa kuwa mziki huchangia sana katika ujenzi wa

tabia kwa vijana, wapiga muziki hawana budi kuchaguliwa kwa uangalifu kama maofisa wengine wa chama cha vijana. (tazama uk. 92, 96.) Kundi hili huunda mhimili wa kamati ya chama cha vijana, ambayo huchagua maofisa wengine kwa kushauriana na vijana. Katika makanisa madogo mtu mmoja anaweza kubeba majukumu kadhaa.

Kiongozi wa chama cha vijana hana budi kuwa mfano kwa kuwa na neema za Kristo na kuwiwa na uongoaji wa roho na ari iambukizayo. Katika kuwahamasisha vijana kufanya kazi pamoja na kubeba majukumu, kiongozi huyo atakuwa kichocheo—akielekeza, kushauri na kuwatia moyo vijana, akiwasaidia kupata uzoefu na furaha ya mafanikio. Kiongozi huyo hana budi kuyaelewa makundi ya vijana katika kanisa na kujitahidi kumshirikisha kila kijana katika chama cha vijana.

Kiongozi huyo atakuwa anawasiliana na mchungaji, mdhamini, na mkurugenzi wa huduma za vijana wa konferensi, akitumia vizuri fursa za mafunzo kazini na kukiongoza chama katika uhusiano wa ushirikiano na kanisa na konferensi.

Kiongozi msaidizi (kama atahitajika) atamsaidia kiongozi na atakuwa mwenyekiti wa kamati ya chama cha vijana na kufanya kazi za uongozi wakati kiongozi hayupo. Kamati ya chama cha vijana inaweza kumpa kiongozi msaidizi kazi zingine.

Katibu-mhazini ataandika kumbukumbu za shughuli za chama cha vijana, kutoa taarifa kila mwezi katika form zitolewazo na mkurugenzi wa konferensi, na kuwahimiza vijana kutoa taarifa za shughuli zao za ushuhudiaji katika kipindi cha dakika kumi cha huduma mahususi.

Katibu-mhazini msaidizi (akihitajika) husaidia katika kazi ya katibu-mhazini kama atakavyopangiwa.

***Mdhamini wa Chama cha Vijana***—Mdhamini wa chama cha vijana anaweza kuwa mzee wa kanisa au mtu mwingine katika baraza la kanisa anayeyaelewa madhumuni ya chama cha vijana, anayewaelewa vijana na ushiriki wao katika huduma za kanisa, na atafanya kazi kama mshauri muhimu kwa vijana. Mdhamini hufanya kazi kama mshauri wa maofisa wa chama cha vijana na huungana nao kila mara katika mikutano ya kamati ya chama cha

vijana. Mdhamini atashirikiana na kiongozi wa chama cha vijana kuwasilisha mahitaji ya chama kwa baraza la kanisa.

Inampasa mdhamini kuwasiliana na mkurugenzi wa huduma za vijana wa konferensi na kumpatia taarifa za mabadiliko ya maofisa na mambo mengine ya chama cha vijana. Mdhamini atahudhuria pamoja na maofisa wa chama cha vijana kwenye mikutano ya mafunzo ya vijana ili awe anajua mabadiliko yanayotokea katika huduma za vijana.

Ikiwezekana, kwa ajili ya kuwa na mwendelezo, mdhamini afanye kazi kwa vipindi vingi vya uongozi.

***Mgawanyo wa Vijana wa Kiadventista*—**Ili kusaida vijana wakue katika uhusiano wao na Yesu Kristo, idara ya huduma za vijana huandaa mpangilio kwa kufuata umri ambao hutoa mazingira ya ukuaji wa karama za kiroho.

***Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista*—**Madhumuni ya chama cha vijana wadogo ni kuwafundisha vijana wadogo uongozi na huduma ya Kikristo na kuwakuza wanachama hadi upeo wa uwezo wao.

Katika makanisa yenye shule, chama cha vijana wadogo ni sehemu ya mtaala na mwalimu mmoja ni kiongozi au mdhamini wa chama cha vijana wadogo. Chama cha vijana wadogo kinapoendeshwa katika shule, kila darasa huchukuliwa kuwa ni chama, na wanafunzi walio katika madarasa ya chini katika shule ya msingi huchukuliwa kama wanachama wanaoandaliwa. Wanafunzi wa madarasa ya juu ya shule ya msingi ni wanachama wa kawaida.

Kila mtu anayehusika na vijana lazima akidhi vigezo vya kanisa na vya kisheria, kama vile uchunguzi wa historia yake au kuwa na cheti cha uthibitisho. Viongozi wa kanisa mahalia hawana budi kushauriana na konferensi ambayo itahakikisha na kushauri juu ya uchunguzi wa historia na vyeti vinavyoweza kupatikana na/au kuhitajika. (Tazama Maelezo, #7, uk. 168. 169.)

***Klabu ya Mabalozi*—**Klabu ya mabalozi hutoa programu mahususi kukidhi mahitaji ya vijana wa kuanzia miaka 16 hadi 21. Huwapatia vijana wa umri huo utaratibu na muundo, na

kuhamasisha ushiriki wao katika shughuli za kanisa mahalia na ulimwenguni. Klabu hiyo imekusudiwa kuimarisha huduma ya Kanisa ya vijana wakubwa/watu wa umri wa katiwatu wa umri wa kati. Huwapa changamoto ya kuwa na uhusiano na Kristo na kuelezea uhusiano huo, huwasaidia kuwa na mtindo wa maisha unaolingana na mfumo wa imani yao na kupenda kazi, na huwapatia uwanja ulio salama wa kujenga urafiki wa kufaa wa maisha yote. Shughuli zake zitaendeshwa kwa kufuata sera za konferensi na kwa kushirikiana na huduma zingine za vijanawatu wa umri wa kati katika kanisa mahalia. Klabu ya mabalozi ina mkurugenzi na mkurugenzi/wakurugenzi msaidizi/wasaidizi. Mkurugenzi/wakurugenzi msaidizi/wasaidizi wanaweza pia kufanya kazi kama katibu na mhazini. Mkurugenzi ni mjumbe wa Kamati ya Chama cha Vijana wa Kiadventista.

***Klabu ya Watafuta Njia*****—**Klabu ya watafuta njia hutoa fursa ya kukidhi moyo wa uvumbuzi na utafiti ulio ndani ya vijana wadogo. Hii ni pamoja shughuli zilizobuniwa mahususi za maisha ya kupiga kambi, kuchunguza viumbe, ustadi, burudani, au ufundi ambao ni nje ya uwezo wa chama cha vijana wadogo cha kawaida. Katika mazingira hayo, mambo ya kiroho hupokelewa vizuri, na Klabu ya Watafuta Njia imeonesha mvuto wake wa kuongoa roho. Katika makanisa mengi Klabu ya Watafuta Njia imechukua nafasi ya chama cha vijana wadogo kilichozoeleka. Kama kuna shule, Klabu ya Watafuta Njia itafanya kazi ya chama cha vijana wadogo.

Mkurugenzi wa Klabu ya Watafuta Njia na wakurugenzi wasaidizi huchaguliwa na kanisa. (tazama uk. 105, 172.) Wakichaguliwa wakurugenzi wasaidizi wawili, inapasa watoke katika kila jinsia. Mmoja wa wakurugenzi wasaidizi pia atafanya kazi kama mwandishi na mhazini wa klabu. Mkurugenzi ni mjumbe wa baraza la kanisa na kamati ya huduma za vijana.

Watendakazi wengine wa Watafuta Njia wanaweza kuwa pamoja na walimu wa madarasa ya ustadi na elimu ya viumbe na washauri ambao kila mmoja anashughulikia kikundi cha Watafuta Njia sita hadi wanane.

Makabrasha ya miongozo hupatikana kwa mkurugenzi wa huduma za vijana wa konferensi.

Kila mtu anayehusika na watoto wadogo lazima akidhi vigezo vya kanisa na vya kisheria, kama vile uchunguzi wa historia yake au kuwa na cheti cha uthibitisho. Viongozi wa kanisa mahalia hawana budi kushauriana na konferensi ambayo itahakikisha na kushauri juu ya uchunguzi wa historia na vyeti vinavyoweza kupatikana na/ au kuhitajika. (Tazama Maelezo, #7, uk. 168. 169.)

***Klabu ya Wavumbuzi*****—**Klabu ya Wavumbuzi kutoa programu za nyumbani na kanisani kwa wazazi wenye watoto wa umri wa miaka 6 hasi 9. Inakusudiwa kuamsha udadisi wa watoto na shughuli zizonafaa kwa umri husika ambazo huhusisha mzazi na mtoto katika shughuli za burudani, stadi sahili, kufurahia viumbe vya Mungu na shughuli zingine zinazovutia umri huo. Yote hayo hufanyika kwa mtazamo wa kiroho, yakiweka mazingira ya kushiriki katika kanisa kama Mtafuta Njia.

Kanisa huchagua mkurugenzi na wasaidizi. (tazama uk. 104, 172.) Watenda kazi zaidi huchaguliwa na viongozi wa klabu. Mkurugenzi ni mjumbe wa kamati ya huduma za vijana. Makabrasha ya miongozo hupatikana kwa mkurugenzi wa huduma za vijana wa konferensi.

Kila mtu anayehusika na watoto wadogo lazima akidhi vigezo vya kanisa na vya kisheria, kama vile uchunguzi wa historia yake au kuwa na cheti cha uthibitisho. Viongozi wa kanisa mahalia hawana budi kushauriana na konferensi ambayo itahakikisha na kushauri juu ya uchunguzi wa historia na vyeti vinavyoweza kupatikana na/ au kuhitajika. (Tazama Maelezo, #7, uk. 168. 169.)

***Miongozo*****—**Tazama Maelezo #17, uk. 17 kuhusu miongozo ya huduma za vijana.

## Kuwekwa Wakfu

Maofisa wote wapya wa kanisa mahalia wanaweza kujumuishwa katika huduma ya kuwekwa wakfu itakayofanywa na mchungaji mwenye leseni au cheti hai. Kama hakuna mchungaji, mzee wa kanisa anaweza kuendesha huduma hiyo kwa maofisa wengine isipokuwa wazee na mashemasi wa kiume na wa kike. Kanisa likiendesha huduma ya kuweka wakfu kwa maofisa wapya, ijumuishe viongozi wa idara na asasi zote.

SURA YA 9

# Uchaguzi

Uchaguzi wa maofisa wa kanisa watakaotekeleza majukumu yao kwa maombi, kwa umakini na kwa ustadi ni kazi muhimu. Sura hii inaelezea taratibu za uchaguzi kuanzia kamati ya mapendekezo mpaka kujaza nafasi katikati ya kipindi cha uongozi.

**Kamati ya mapendekezo na Mchakato wa Uchaguzi**

Maofisa huchaguliwa kila baada ya mwaka mmoja au miwili (tazama uk. 71) kwa kutumia kamati ya mapendekezo iliyoteuliwa. Kamati hii huleta taarifa kwa kanisa, ambalo hupigia kura majina yaliyowasilishwa. Utaratibu huu huliwezesha kanisa kuchunguza kila jina kwa makini kabla ya uchaguzi na huepusha moyo wa ushindani unaoweza kutokea kama majina yatapendekezwa na washiriki.

Kamati ya mapendekezo itaangalia mahitaji ya kanisa na kupeleleza uwezo wa washiriki kutumikia nafasi mbalimbali. Hii ni sababu nyingine inayofanya maofisa wasipendekezwe na washiriki au kwa kura ya kanisa zima.

Ukubwa wa kamati ya mapendekezo utakuwa kati ya wajumbe watano katika kanisa dogo hadi idadi kubwa zaidi katika kanisa kubwa. Idadi ya wajumbe imeachiwa uamuzi wa kila kanisa na haina budi kuangaliwa na baraza la kanisa. Kisha pendekezo la kufaa litaletwa mbele ya kanisa, kwa kutumia muda mfupi kadiri iwezekanavyo katika ibada ya Sabato.

***Wakati na Namna ya Kuteua Kamati ya Mapendekezo***—Kamati ya mapendekezo haina budi kuteuliwa mapema katika robo ya mwisho ya mwaka wa kanisa na inatakiwa kutoa taarifa angalao majuma matatu kabla ya Sabato ya mwisho ya mwaka wa kanisa.

Mchungaji au kiongozi wa mtaa, au mzee kama hakuna mchungaji au kiongozi wa mtaa, ataleta suala hilo mbele ya kanisa. Ndipo kanisa litateua kamati ya maandalizi itakayopendekeza kamati ya

mapendekezo. Kamati hii ya maandalizi inaweza kuchaguliwa kwa kutumia moja kati ya njia mbili.

Kwa kupendekeza, kwa washiriki kutamka au kuandika. Endapo mapendekezo yatatolewa kwa kutamka, mshiriki mmoja asipendekeze zaidi ya mtu mmoja. Juhudi za mtu mmoja au kikundi kidogo kuamrisha washiriki wote hazikubaliki. Kila juhudi zifanyike kuhakikisha uwakilishi wa haki katika muundo wa kamati ya maandalizi. Jambo lo lote lenye mtazamo wa kisiasa halina budi kuepukwa. Mchungaji au kiongozi wa mtaa atakuwa mwenyekiti wa kamati ya maandalizi. Kama hakuna mchungaji au kiongozi wa mtaa, mwenyekiti wa kamati hii ya maandalizi atateuliwa na baraza la kanisa kutoka miongoni mwa wajumbe wa kamati ya maandalizi. Ukubwa wa kamati ya maandalizi utakuwa watu watano hadi saba zaidi ya wajumbe wa baraza la kanisa.

Kwa kanisa kuidhinisha baraza pamoja na watu wengine watano hadi saba waliochaguliwa na kanisa (Tazama ibara iliyotangulia), kufanya kazi ya kamati ya maandalizi. Njia hii ikitumika, kwa kawaida mwenyekiti wa baraza la kanisa atakuwa mwenyekiti wa kamati ya maandalizi (tazama uk. 33).

***Jinsi Mchakato Huo Unavyofanya Kazi*—**Hatua za uteuzi ni:

Kanisa litachagua kamati ya maandalizi kwa kura, kwa kutumia moja ya njia mbili zilizoorodheshwa hapo juu.

Kamati ya maandalizi itapendekeza majina ya kamati ya mapendekezo kwa kanisa, ikiwa pamoja na pendekezo la katibu. Kila juhudi ifanyike kuhakikisha kuwa kuna uwakilishi wa kufaa katika muundo wa kamati ya mapendekezo.

Kanisa litapiga kura kuteua kamati ya mapendekezo na katibu wake.

Mchungaji au kiongozi wa mtaa ni mjumbe kwa wadhifa wake na ni mwenyekiti wa kamati ya mapendekezo. Endapo mchungaji au kiongozi wa mtaa ataamua kutokuwa mwenyekiti, au kama mchungaji au kiongozi wa mtaa hajateuliwa kuhudumia kanisa hilo, kamati ya maandalizi itapendekeza mtu kutoka katika kamati ya mapendekezo iliyopendekezwa ili awe mwenyekiti.

Kamati ya mapendekezo itakutana kuandaa orodha ya maofisa ambayo itaiwasilisha kwa kanisa ili ipitishwe.

Kanisa litateua maofisa wake kwa kura kwa ajili ya mwaka unaofuata

***Watu Gani Wanaweza Kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mapendekezo*—**Washiriki hai tu ndio watakaochaguliwa kuingia katika kamati ya mapendekezo. Inapasa wawe watu wenye hekima wanaojali ustawi na ufanisi wa kanisa.

***Kazi ya Kamati ya Mapendekezo*—**Mwenyekiti ataitisha kikao cha kamati hiyo mara baada ya kuchaguliwa. Kwa maombi ya dhati, kamati itaanza kuandaa orodha ya watakaopendekezwa kwa nafasi zote. Watakaopendekezwa lazima wawe washiriki hai wa kanisa linalofanya uchaguzi. Orodha ya waliopendekezwa itawasilishwa kwa kanisa katika ibada ya Sabato au katika mkutano mkuu ulioitishwa kwa sababu hiyo. Katika uchaguzi wake, kamati inaweza kushauriana na wengine walio na taarifa zaidi. Kamati hii haipendekezi mchungaji au mchungaji/wachungaji msaidizi/wasaidizi ambao huteuliwa na konferensi.

Orodha ya maofisa watakaopendekezwa na kamati ya mapendekezo itatofautiana kulingana na wingi wa washiriki. Kanisa dogo linaweza kuwa na wachache. Kamati itashughulikia nafasi zote za uongozi isipokuwa walimu wa shule ya Sabato, ambao hupendekezwa na baraza la shule ya Sabato na kuidhinishwa na baraza la kanisa. Tazama Maelezo, #1, uk. 171, 172, ili upate orodha ya maofisa wanaoweza kupendekezwa.

***Kamati ya Mapendekezo Lazima Ipate Ukubali wa Maofisa Watarajiwa*—**Baada ya kupendekeza watu waaminifu, washiriki watiifu wa kanisa husika mahalia, isipokwa mahali ambapo konferensi imeidhinisha vinginevyo (tazama uk. 73, "Kazi ya Wazee ni Mahalia"), wajumbe stahiki wa kamati watawaarifu juu ya kupendekezwa kwao na kupata ukubali wao wa kufanya kazi.

***Washiriki Wanaweza Kujitokeza Mbele ya Kamati ya Mapendekezo*—**Washiriki wanaotaka kufika mbele ya kamati kutoa mapendekezo au pingamizi hawana budi kupewa fursa ya kufanya hivyo. Baada ya kutoa maelezo yao mbele ya kamati na kuondoka

katika chumba cha mkutano, kamati haina budi kuyafikiria maoni yao na kutoa taarifa yake kwa kanisa.

***Mijadala ya Kamati ya Mapendekezo ni Siri*****—**Uchunguzi na mijadala yote ya kamati ya mapendekezo ni ya siri. Kwa mjumbe wa kamati kutoa nje ya kamati ya mapendekezo taarifa zo zote nyeti za binafsi zilizojadiliwa ni uvunjaji wa maadili ya Kikristo na madhumuni ya kanuni ya msingi. Kukiuka katika jambo hili ni sababu ya kutosha kumzuia mshiriki kuingia katika kamati ya mapendekezo siku za usoni. Kukiwa na haja ya kufanya uchunguzi nje ya kamati, mwenyekiti atafanya uchunguzi huo.

***Kutoa Taarifa kwa Kanisa*****—**Taarifa ya kamati ya mapendekezo hutolewa kwa kanisa zima na si kwa baraza la kanisa, ambalo halina mamlaka katika mchakato huo. Taarifa hiyo inaweza kutolewa wakati wa ibada ya Sabato au katika mkutano mkuu maalum utakaoitishwa kwa ajili hiyo.

Kamati ya mapendekezo ikiwa tayari kutoa taarifa, mwenyekiti hana budi kutoa maelezo stahiki kwa kanisa. Nakala ya taarifa hiyo haina budi kutolewa kwa washiriki au kusomwa kwa sauti na katibu wa kamati. Inampasa mwenyekiti kutangaza kuwa kanisa litapigia kura taarifa hiyo juma moja au mawili baadaye.

Kila mshiriki inampasa kupiga kura katika uchaguzi wa maofisa. Uchaguzi utafanyika kwa zaidi ya nusu ya kura za wale waliopo na kupiga kura.

***Pingamizi Dhidi ya Taarifa ya Kamati ya Mapendekezo*****—**Washiriki wanaweza kuipinga taarifa ya kamati ya mapendekezo na hawana budi kuwasilisha pingamizi lao wao wenyewe mbele ya kamati kabla ya taarifa hiyo kusomwa mara ya pili kwa kuomba kukutana na kamati kupitia kwa mwenyekiti au mchungaji. Au, wakati wa kusomwa kwa taarifa mara ya pili, mshiriki anaweza kuomba taarifa yote irejeshwe kwa kamati bila kujadiliwa ili ikachunguzwe zaidi. Ni utaratibu wa kawaida kwa mwenyekiti kuruhusu urejeshwaji huo. Hata hivyo, ombi hilo likiwa pendekezo, halina majadala na litaamuliwa kwa wingi wa kura.

Mwenyekiti wa kamati hana budi kutangaza wakati na mahali

ambapo kamati itakutana kusikiliza pingamizi. Wakati huo washiriki wenye pingamizi au mshiriki mwingine ye yote anayetaka kufanya hivyo, anaweza kufika mbele ya kamati. Kama uchaguzi utaahirishwa kwa sababu ya pingamizi, litakuwa kosa kubwa kwa walioweka pingamizi kushindwa kufika mbele ya kamati.

Kamati haina budi kuzifikiria ipasavyo pingamizi zilizowasilishwa. Zikionekana kuwa halali, kamati itachagua majina mengine badala ya yale yaliyowekewa pingamizi. Taarifa itakapowasilishwa tena, kanisa litapigia kura taarifa ya kamati.

Mapingamizi madogo-madogo yasiyo na msingi dhidi ya jina lo lote haipasi yawekwe, lakini kukiwa na sababu za msingi za kubadilisha pendekezo lo lote, sababu hizo hazina budi kutolewa kwa kamati ya mapendekezo.

***Kujaza Nafasi Katikati ya Vipindi vya Uchaguzi*—**Nafasi ya uongozi wa kanisa ikiwa wazi katikati ya kipindi cha uongozi kwa sababu ya kifo, kuondolewa, kujiuzulu, au sababu yo yote nyingine, baraza la kanisa litapendekeza mtu wa kujaza nafasi hiyo kwa kipindi kilichosalia cha muda wa uongozi na kuwasilisha pendekezo hilo kwa kanisa kwa ajili ya uchaguzi.

## Wajumbe wa Mkutano wa Mkuu wa Konferensi

Mamlaka ya kiutawala ya konferensi yanatokana na uwakilishi wake. Makanisa ya konferensi huchagua wajumbe wa mkutano mkuu wa konferensi kwa ajili ya kuyawakilisha katika mabaraza ya konferensi. Mkutano mkuu wa konferensi kuchagua wafanyakazi wa konferensi, hutoa vyeti na leseni (isipokuwa pale ambapo katiba ya konferensi inaipa kamati tendaji jukumu hilo), hurekebisha katiba na sheria zake ndogo ndogo ikilazimu, na hufanya mambo mengine. Moja ya kazi zake muhimu zaidi ni uchaguzi wa kamati tendaji, ambayo hufanya kazi badala ya mkutano mkuu katikati ya mkutano mkuu mmoja na mwingine. Uwezo na mamlaka ya makanisa yote ya konferensi unaokasimiwa hutolewa kwa kamati hii.

***Kuchagua Wajumbe*—**Mpango wa Mungu ni kwamba wachaguliwe wajumbe waaminifu waliojaribiwa na kuthibitishwa, "wanaoweza kuangalia jambo toka chanzo hadi athari zake," kwani

inawapasa kuweka mipango itakayofuatwa katika kuendeleza kazi."—9T 262.

Idadi ya wajumbe kutoka kila kanisa kwenda kwenye mkutano mkuu wa konferensi itaamuliwa na katiba ya konferensi. Wakati wa kuchagua wajumbe ukifika, mchungaji, au mzee kiongozi kwa kushirikiana na mchungaji, atalileta jambo hilo mbele ya kanisa. Inaweza kuteuliwa kamati ya kupendekeza wajumbe, au baraza la kanisa linaweza kuombwa kuwapendekeza. Jambo lo lote lenye mtazamo wa kisiasa lisiruhusiwe kuingia katika kazi hii. Watu wenye utauwa, uaminifu unaojulikana na wanaoweza kuhudhuria mkutano mkuu hawana budi kupendekezwa kuwa wajumbe. (tazama uk. 80.)

Kamati au baraza la kanisa likimaliza kazi yake, litatoa taarifa ya waliopendekezwa kwa kanisa. Kisha kanisa litawapigia kura waliopendekezwa. Hakuna ofisa wa kanisa anayeweza kuwa mjumbe kwa wadhifa wake. Baada ya uchaguzi, karani atajaza fomu za vyeti vya wajumbe na kuzirudisha kwa katibu wa konferensi. Wajumbe hao watakuwa wawakilishi wa kanisa, wakiungana na wawakilishi wa makanisa mengine kushughulikia mambo yote yanayokuja mbele ya mkutano mkuu wa konferensi.

Wajumbe wa mkutano mkuu wa konferensi/misheni ya union huchaguliwa na konferensi, na si makanisa. Wajumbe wa mkutano mkuu wa konferensi kuu huchaguliwa na divisheni na konferensi/misheni za union.

***Kazi ya Wajumbe*—**Wajumbe wa mkutano mkuu wa konferensi hawachaguliwi kuwakilisha kanisa au konferensi tu. Inawapasa kuitazama kazi yote, wakikumbuka wajibu wao juu ya ustawi wa kazi ya Kanisa ulimwenguni. Hairuhusiwi wajumbe wa kanisa au konferensi kupanga au kujaribu kupiga kura zao kwa umoja. Wala hairuhusiwi kwa wajumbe kutoka katika kanisa kubwa au konferensi kudai kuwa na mamlaka ya kuamua jinsi mambo yanavyotakiwa kuwa katika mkutano mkuu wa konferensi. Kila mjumbe hana budi kuwa tayari kuongozwa na Roho Mtakatifu na kupiga kura kulingana na maoni yake binafsi. Ofisa ye yote wa kanisa au konferensi atakayejaribu kudhibiti kura za kundi fulani la wajumbe atachukuliwa kuwa hafai kuwa kiongozi.

***Wajibu wa Maofisa wa Konferensi***—Kanisa mahalia halina mamlaka nje ya usharika wake. Huungana na makanisa mengine katika konferensi katika kukasimu mamlaka na majukumu kwa maofisa wa konferensi na kamati tendaji kuendeleza kazi ya konferensi katikati ya mkutano mkuu mmoja na mwingine. Maofisa wa konferensi wanawajibika kwa konferensi nzima na si kwa kanisa moja lo lote.

***Kamati Kuu ya Konferensi***—Wajumbe wa kamati kuu ya konferensi huchaguliwa kuwakilisha kazi ya konferensi nzima, na siyo ya kanisa moja, mtaa mmoja au taasisi. Kila mjumbe hana budi kusimamia maslahi ya kazi katika sehemu zote za eneo na kufanya uamuzi baada ya uchunguzi makini na maombi. Uamuzi wa kamati haipasi utawaliwe au kufanyika kwa ushawishi wa kanisa, kundi, au mtu ye yote.

SURA YA 10

# Huduma na Mikutano Mingine

**Kanuni za Msingi**

Mtume Yohana alisema kwamba "waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu" (Yn. 4:23).

"Ingawa Mungu hakai katika nyumba zilizojengwa kwa mikono, lakini huiheshimu mikutano ya watu wake kwa kuwepo kwake. Ameahidi kwamba wanapokusanyika kumtafuta, kukiri dhambi zao na kuombeana, atakutana nao kwa njia ya Roho wake. Lakini wale wanaokutana kwa ajili ya kumwabudu hawana budi kujitenga na kila jambo baya. Wasipomwabudu katika roho na kweli na katika uzuri wa utakatifu, kukusanyika kwao kutakuwa bure."—PK 50.

***Kusudi la Huduma na Mikutano***—Kusudi la huduma na mikutano yote ni kumwabudu Mungu kwa ajili ya kazi yake ya uumbaji na kwa ajili ya fadhili za wokovu wake; kulielewa Neno lake, mafundisho yake, na makusudi yake; kujumuika katika imani na upendo; kushuhudia imani yetu mahususi juu ya dhabihu ya upatanisho iliyotolewa na Kristo pale msalabani; na kujifunza namna ya kutimiza agizo la injili la kufanya wanafunzi ulimwenguni kote. (Mat. 28:19, 20).

***Kicho kwa Nyumba ya Ibada***—Kwa mtu mnyenyekevu anayeamini, nyumba ya Mungu duniani ni lango la mbingu. Wimbo wa sifa, ombi, na maneno yasemwayo na wawakilishi wa Kristo, ni nyenzo zilizoteuliwa na Mungu kuwaandaa watu kwa ajili ya kanisa la juu, kwa ajili ya ibada ya juu zaidi ambako ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge.

Kutoka katika utakatifu uliokuwa anaambatana na patakatifu pa duniani, Wakristo wanaweza kujifunza inavyowapasa kupaheshimu mahali ambapo Bwana hukutana na watu wake.. . . Mungu mwenyewe alitoa utaratibu wa huduma yake, akiinua juu kuliko vitu vyote vya duniani.

"Nyumba ni patakatifu pa familia, na chumba au kwenye miti ni mahali patulivu kabisa kwa ajili ya ibada ya binafsi; lakini kanisa ni patakatifu pa usharika. Inapasa kuwe na kanuni kuhusu wakati, mahali, na namna ya kuabudu. Jambo lo lote lililo takatifu, jambo lo lote linalohusu ibada ya Mungu, lisifanywe kwa uzembe au bila kujali."—5T 491.

***Wafundisheni Watoto Kicho*—"**Wazazi, inueni viwango vya Ukristo katika akili za watoto wenu; wasaidieni kumhusisha Yesu katika maisha yao; wafundisheni kuwa na kicho cha juu kabisa kwa ajili ya nyumba ya Mungu na kuelewa kwamba wanapoingia katika nyumba ya Mungu inawapasa kuingia na mioyo iliyolainika na kutawaliwa na mawazo kama haya: 'Mungu yupo hapa, hii ni nyumba yake. Inanipasa kuwa na mawazo safi kabisa na dhamira takatifu. Inanipasa nisiwe na kiburi, kijicho, wivu, dhana mbaya, chuki, au udanganyifu moyoni mwangu, kwani nipo mbele za Mungu mtakatifu. Hapa ndipo mahali ambapo Mungu hukutana na watu wake na kuwabariki. Yeye aliye juu na mtakatifu aishiye milele ananitazama, anaupeleleza moyo wangu, na kuyasoma mawazo na matendo ya siri kabisa ya maisha yangu.'"—5T 494.

***Adabu na Utulivu Mahali pa Ibada*—**"Wanaoabudu wakiingia mahali pa mkutano, inawapasa kufanya hivyo kwa adabu, wakitembea kwa utulivu kwenda kwenye viti vyao. … Maongezi ya kawaida, kunong'ona, na kucheka visiruhusiwe katika nyumba ya ibada, ama kabla au baada ya ibada. Ucha Mungu wa hali ya juu wa vitendo hauna budi kuonekana kwa wanaoabudu.

Endapo itawalazimu wengine kungoja kwa dakika chache kabla ya mkutano kuanza, basi wadumishe moyo wa kweli wa ibada kwa kuwa na tafakari ya kimya kimya, wakiendelea kuinua mioyo kwa Mungu katika kuomba kwamba ibada iwe na manufaa kwa mioyo yao wenyewe na kuleta ushawishi na uongofu kwa watu wengine. Inawapasa kukumbuka kuwa wajumbe kutoka mbinguni wamo ndani ya nyumba. Watu wakija kwenye nyumba ya ibada wakiwa na kicho halisi kwa Bwana na kukumbuka kuwa wako mbele yake, kutakuwa umbuji mzuri katika ukimya. Minong'ono na kucheka na kuongea ambako kunaweza kusiwe dhambi mahali pa shughuli za kawaida

kusiendekezwe katika nyumba ambayo Mungu anaabudiwa. Akili haina budi kuwa tayari kusikia Neno la Mungu, ili liwe na uzito stahiki na kugusa moyo kwa namna ifaayo."—5T 492

***Ukarimu***—"Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua" (Ebr. 13:2). Inalipasa kila kanisa kujenga moyo wa ukarimu, ambao ni kipengele muhimu cha maisha ya Kikristo. Hakuna jambo linalofisha uhai wa kiroho wa kanisa kama hali ya kupoa na ushupavu ambayo huondoa ukarimu na ushirika wa Kikristo. Wakaribishaji waliochaguliwa mahususi hawana budi kuwakaribisha kwa uchangamfu, wageni ambao wanaweza pia kukaribishwa wakati wa huduma ya ibada.

## Nafasi ya Muziki Katika Ibada

***Nguvu ya Muziki***—Muziki unaweza kuwa nguvu kubwa sana kwa ajili ya wema, lakini hatukitumii ipasavyo kipengele hiki cha ibada. Mara nyingi uimbaji hufanyika kutokana na msisimko au kukidhi hitaji fulani, na wakati mwingine wanaoimba huachwa wakiboronga, na muziki hupoteza mguso wake unaotakiwa katika akili za watu waliopo. Muziki hauna budi kuwa na uzuri, kuchochea hisia na nguvu. Sauti ziinuliwe katika nyimbo za sifa na ibada. Ikiwezekana tumieni muziki wa ala, na mwafaka wenye utukufu utapanda kwenda kwa Mungu kama sadaka iliyokubalika."—4T 71.

***Imbeni kwa Roho na kwa Akili Pia***—"Katika juhudi zao za kuwafikia watu, haiwapasi wajumbe wa Mungu kufuata njia za ulimwengu. Katika mikutano inayofanyika, wasitegemee waimbaji wa kidunia na maonesho kama ya waigizaji kuleta usikivu. Wale wasiopenda Neno la Mungu, ambao hawajawahi kusoma Neno lake kwa shauku ya dhati ya kuuelewa ukweli wake, wanawezaje kutegemewa kuimba kwa roho na kwa akili pia? … Kwaya ya mbinguni inawezaje kujiunga na muziki ambao ni wa kuigiza tu? …

"Uimbaji usifanywe na wachache tu kila wakati. Kanisa lote lishiriki mara nyingi iwezekanavyo."—9T 143, 144.

## Mimbari si Jukwaa la Malumbano

Kanisa halimpatii mchungaji, mzee au mtu mwingine ye yote haki ya kugeuza mimbari kuwa jukwaa la kutolea hoja zinazobishaniwa kuhusu mafundisho au taratibu za kanisa.

***Kupima Nuru Mpya***—Washiriki wanaoona kuwa wamepata nuru mpya inayopingana na mitazamo ya kanisa inayotambulika, hawana budi kutafuta ushauri wa viongozi waadilifu.

"Kuna maelfu ya majaribu yaliyofichika ambayo yameandaliwa kwa ajili ya wale walio na nuru ya ukweli; na usalama pekee kwa ye yote kati yetu ni kutopokea fundisho lo lote jipya, fasiri yo yote mpya ya Maandiko, bila kuiwasilisha kwanza kwa ndugu wenye uzoefu. Iweke mbele yao kwa moyo mnyenyekevu unaofundishika, kwa maombi ya dhati; na wasipoona nuru ndani yake, ukubaliane na busara yao; kwani 'kwa wingi wa washauri huja wokovu.'"—5T 293. (Tazama pia Mdo. 15:1-32.)

Mpango huu ulikuwa unafuatwa katika kanisa la awali. Kulipotokea tofauti ya maoni kule Antiokia kuhusu suala nyeti, waumini walituma wawakilishi Yerusalemu kuwasilisha suala hilo kwa mitume na wazee. Waumini wa Antiokia waliupokea kwa furaha uamuzi wa Baraza la Yerusalemu, na hivyo wakadumisha umoja na upendo wa kindugu.

Ushauri wa kupima nuru mpya usichukuliwe kuwa unamzuia mtu kuchunguza Maandiko kwa makini, bali ni ulinzi dhidi ya kuingia kwa nadharia potovu na mafundisho ya uongo katika Kanisa. Mungu anataka watoto wake watafute nuru na ukweli katika Neno lake kwa uaminifu, lakini hataki wapotoshwe na mafundisho ya uongo.

"Tumeona kwa mbali tu utukufu wa Mungu na kutokuwa na kikomo kwa ujuzi na hekima; kwa namna fulani, tumekuwa tukipapasa juu ya mgodi, wakati mawe yaliyojaa dhahabu yako chini ya udongo kwa ajili ya kumtunuku yule atakayechimba. Mtaimbo hauna budi kuzamishwa chini zaidi na zaidi katika mgodi na matokeo yake yatakuwa hazina tukufu. Kwa njia ya imani sahihi, ujuzi wa Mungu utakuwa ujuzi wa wanadamu.—COL 113.

"Siku zote nuru mpya juu ya Neno la Mungu itadhihirishwa kwa yule aliye katika uhusiano hai na Jua la Haki. Mtu ye yote asije akadhani kuwa hakuna ukweli zaidi unaoweza kuonekana. Mtu atafutaye ukweli kwa makini na maombi atapata miali muhimu ambayo ilikuwa haijawahi kuangaza kutoka katika Neno la Mungu. Vito vingi bado vimesambaa vinavyotakiwa kukusanywa na kuwa mali ya watu wa Mungu waliosalia."—CSW 34.

Nuru mpya inapoangaza kutoka katika kurasa takatifu kumtunuku mtafutaji makini wa ukweli, haibatilishi ukweli wa zamani. Badala yake huungana na ule wa zamani, ikiufanya uwe angavu zaidi kwa mng'ao ulioongezeka. Kwa hiyo "njia ya wenye haki ni kama nuru ing'aayo, ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu" (Mit. 4:18).

Ingawa mtoto wa Mungu hana budi kuwa tayari kupokea nuru endelevu, mtu asisikilize sauti yo yote, ambayo itasababisha kuyaacha mafundisho ya msingi ya Biblia hata ikionekana kuwa takatifu na yenye kukubalika sana.

"Tusije tukapokea maneno ya wale wanaokuja na ujumbe unaopingana na hoja mahususi za imani yetu. Huwa wanakusanya Maandiko mengi, na kuyaleta kama ushahidi wa nadharia zao wanazozing'ang'ania. Mambo haya yamekuwa yakifanyika tena na tena katika miaka hamsini iliyopita. Pamoja na kwamba Maandiko ni Neno la Mungu na inapasa yaheshimiwe, matumizi yake yakiondoa nguzo moja kutoka katika msingi ambao Mungu ameusimamisha kwa miaka hii hamsini, litakuwa kosa kubwa. Mtu atumiaye Maandiko kwa jinsi hiyo haujui udhihirisho wa ajabu wa Roho Mtakatifu ulioupa nguvu na kani ujumbe uliotangulia ambao uliwajia watu wa Mungu."—CW 32.

**Umuhimu wa Kudumisha Umoja**

Ni muhimu tuudumishe "umoja wa imani" (Efe. 4:13), na ni muhimu vilevile "kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani" (aya ya 3). Umoja wa jinsi hiyo unahitaji tahadhari na ushauri wa viongozi wa kanisa.

Mungu anaongoza watu ili watoke ulimwenguni kwa kutumia ukweli wa milele, yaani amri za Mungu na imani ya Yesu. Atawarudi watu wake na kuwafanya wafae. Hawatatofautiana, mmoja akiamini jambo moja na mwingine akiwa na imani na maoni yaliyo kinyume kabisa, kila mmoja akienda mwenyewe bila kuambatana na mwili. Kwa kutumia tofauti za karama na utawala aliouweka kanisani, watakuwa katika umoja wa imani. Mtu mmoja akiwa na maoni yake juu ya ukweli wa Biblia bila kujali maoni ya ndugu zake, na kuhalalisha hatua yake, akidai kuwa ana haki ya kuwa na maoni yake binafsi, na kisha kuyashinikiza kwa wengine, atakuwa anatimiza vipi ombi la Kristo? …

"Ingawa tuna kazi ya kila mmoja na wajibu wa kila mmoja mbele za Mungu, hatutakiwi kufuata maoni yetu wenyewe bila kujali maoni ya ndugu zetu; kwani hatua hiyo itasababisha vurugu katika kanisa. Ni kazi ya wachungaji kuheshimu uamuzi wa ndugu zao; lakini uhusiano kati yao na mafundisho wanayofundisha lazima vipimwe kwa sheria na ushuhuda; kisha kama mioyo inafundishika, hakutakuwa na migawanyiko kati yetu. Wengine wana mwelekeo wa kuwa na vurugu, na wanatanga mbali na mambo muhimu yanayoitambulisha imani; lakini Mungu anawavuvia wachungaji wake kuwa wamoja katika mafundisho na katika roho."—TM 29, 30.

Kwa kuzingatia mambo hayo, ni wazi kwamba mimbari lazima ihifadhiwe kwa ajili ya mahubiri ya ukweli wa Neno la Mungu na kuwasilisha mipango na sera za kanisa kwa ajili kuendeleza kazi ya Mungu, na si mitazamo na maoni binafsi. (tazama uk. 35, 114, 115.)

***Wahutubu Wasioruhusiwa*—**Kwa hali yo yote ile mchungaji, mzee au ofisa mwingine hawezi kukaribisha wageni au watu wasioruhusiwa kuendesha huduma. Watu walioondolewa katika uchungaji au walioondolewa katika ushirika mahali pengine, wasioidhinishwa na kanisa, wazuiwe kutumia mimbari. Wale wanaostahili kuaminiwa wataweza kujitambulisha kwa kuonesha vyeti halali.

Wakati mwingine inakubalika kwa maofisa wa serikali au viongozi wa mji kuongea na kanisa, lakini wengine wote wazuiwe kutumia mimbari bila kuwa na ruhusa kutoka konferensi. Kila mchungaji, mzee, na mwenyekiti wa konferensi hana budi kusimamia kanuni hii. (tazama uk. 35, 114, 115.)

## Shule ya Sabato na Huduma za Ibada

***Shule ya Sabato*—**Shule ya Sabato, moja ya huduma zetu muhimu kabisa, ni kanisa mafunzoni. Kila Sabato washiriki wetu na maelfu ya marafiki wanaopenda hukutana katika shule ya Sabato kujifunza Neno la Mungu kwa mpangilio. Washiriki wote wa kanisa hawana budi kuhimizwa kuhudhuria shule ya Sabato na kuleta wageni.

Kila shule ya Sabato haina budi kujitahidi kutoa programu zinazofaa kwa kila daraja la umri. Masomo na miongozo hupatikana konferensi, union na divisheni.

Shule ya Sabato haina budi kuhamasisha shughuli za utume mahalia na ulimwenguni kote; sadaka ya utume, na kuwa na muda wa kutosha wa kujifunza Biblia. (Tazama Maelezo, #1 uk. 172.)

***Matangazo na Uhamasishaji wa Idara*—**Inapasa kuwe na tafakari ya kina juu ya urefu na aina ya matangazo na uhamasishaji wa idara wakati wa huduma za shule ya Sabato. Kama yanahusu mambo yasiyohusiana moja kwa moja na ibada ya Sabato au kazi ya kanisa, wachungaji na maofisa wa kanisa wayazuie, wakidumisha hata katika suala hili moyo stahiki wa ibada na uadhimishaji wa Sabato.

Makanisa mengi hutoa matangazo yaliyochapwa yakieleza utaratibu wa ibada na pia matangazo ya juma husika. Mahali ambapo jambo hili hufanyika kuna haja kidogo sana au haipo kabisa ya matangazo ya mdomo. Mahali ambapo hakuna matangazo yaliyochapwa kama hayo, makanisa mengi hufanya matangazo kabla ya kuanza kwa huduma ya ibada. (Tazama Maelezo, #2, uk. 172, 173.)

Inapasa itolewe fursa stahiki pia kwa ajili ya idara kuhamasisha programu zao, lakini kuwe na uangalifu mkubwa kulinda muda wa kujifunza na kuhubiri Neno la Mungu.

***Huduma ya Ibada*—**Huduma ya ibada siku ya Sabato ni mkutano wa kanisa ulio muhimu kuliko yote. Hapo ndipo washiriki hukutana kila juma kujumuika katika kumwabudu Mungu kwa moyo wa sifa na shukurani, kusikia Neno la Mungu, kukusanya nguvu, kupambana na taabu za maisha, na kuyajua mapenzi ya Mungu kwa ajili yao katika huduma ya kuongoa roho. Kicho, usahili, na kufanya mambo kwa wakati vinatakiwa kuonekana katika ibada.

***Ujuzi, Utafiti na Mipango Vinahitajika*—**"Je, si wajibu wako kutumia ujuzi, utafiti, na mipango katika uendeshaji wa mikutano ya kidini—itakavyoendeshwa ili ilete tija zaidi na kuacha fikra nzuri kabisa kwa wote waliohudhuria?"—RH Apr. 14, 1885.

Mungu ni Baba mpole mwenye huruma. Huduma yake isitazamwe kama zoezi la kuhuzunisha, linalosikitisha. Inapasa iwe furaha kumwabudu Bwana na kushiriki katika kazi yake. … Kristo, naye akiwa amesulibiwa hana budi kuwa jambo la taamuli, la kuzungumzia, na la hisia zetu za furaha kabisa. … Tunapotoa shukurani zetu tunakaribia ibada ya majeshi ya mbinguni. "Atoaye dhabihu za kushukuru, ndiye' amtukuzaye Mungu. Zaburi 50:23. Tuje mbele za Muumba wetu tukiwa na furaha yenye kicho, kwa 'kushukuru, na sauti ya kuimba.' Isaya 51:3."—SC 103, 104.

***Muundo wa Ibada*—**Huduma ya Sabato asubuhi ina sehemu mbili: mwitikio wa kanisa kwa sifa na kuabudu, kwa njia ya nyimbo, maombi, na matoleo, na ujumbe kutoka katika Neno la Mungu. (Tazama Maelezo, #3, uk, 173, 174.)

Hakuna muundo au utaratibu uliowekwa wa ibada ya pamoja. Utaratibu mfupi kwa kawaida hufaa kwa moyo halisi wa ibada. Shughuli ndefu za awali ziepukwe. Zoezi la mwanzo lisichukue muda unaohitajika kwa ajili ya mahubiri ya Neno la Mungu. (Tazama Maelezo, #2, uk. 172, 173, kwa ajili ya utaratibu wa ibada unaopendekezwa.)

***Huduma ya Utume wa Kanisa*—**Sabato ya kwanza ya kila mwezi ni Sabato ya Utume wa Kanisa. Huduma hii ya ibada huzingatia uinjilisti wa walei na inaweza kuhusisha mipango na shuhguli za idara mbalimbali. "Mungu ametupatia kazi takatifu kuliko zote, na tunahitaji kukutana ili tupate maelekezo ili tufae kuifanya kazi yake."—6T 32, (Tazama Maelezo, #4, uk. 174, 175.)

***Maombi ya Pamoja*—**Kristo aliwaonesha wanafunzi wake kuwa maombi yao hayana budi kuwa mafupi, yanayoeleza kile wanachotaka tu, na si zaidi. … Dakika moja au mbili zinatosha sana kwa ombi la kawaida."—2T 581.

"Wale wanaoomba na wale wanaohubiri watamke maneno yao sawasawa na kusema kwa sauti dhahiri iliyo wazi. Maombi, yakitolewa ipasavyo, ni uwezo uletao tija. Ni moja kati ya njia zinazotumiwa na Bwana kuwasilisha kwa watu hazina za kweli. . . . Watu wa Mungu wajifunze kusema na kuomba katika

namna ambayo itawakilisha ukweli mkuu walio nao. Ushuhuda unaotolewa na maombi yanayoombwa yawe dhahiri na ya wazi. Mungu atatukuzwa kwa njia hiyo."—6T 382.

***Kutoa Machapisho Siku ya Sabato***—Kwa kawaida Sabato ni wakati mwafaka kwa ajili ya katibu wa Huduma Binafsi kuwapa washiriki machapisho. Njia zisizokubalika zinazohamisha usikivu kutoka kwenye ibada na kicho halisi, hazina budi kuepukwa.

**Huduma ya Ushirika Mtakatifu**

Huduma ya ushirika mtakatifu kwa kawaida husherehekewa mara moja kwa robo. Huduma hiyo huhusisha huduma maalum ya kutawadhana miguu ikifuatiwa na Meza ya Bwana. Inapasa kuwa tukio takatifu na la furaha kuliko yote kwa kanisa, mchungaji na wazee. Kwa kawaida huduma hii hufanyika wakati wa huduma ya ibada lakini inaweza kupangwa wakati mwingine.

***Agizo la Kutawadhana Miguu***—"Basi, baada ya kuwatawadha miguu wanafunzi wake alisema, 'nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.' Katika maneno hayo Kristo alikuwa haagizi kufanyika kwa desturi ya ukarimu. Kulikuwa na maana zaidi kuliko kuosha miguu ya wageni kuondoa vumbi la safarini. Kristo alikuwa anaanzisha huduma ya kidini hapa. Kwa kitendo cha Bwana wetu, hii … kaida ilifanywa kuwa agizo takatifu. Ilipasa kuadhimishwa na wanafunzi, ili wakumbuke kila wakati somo lake la unyenyekevu na utumishi.

"Agizo hili ni maandalizi yaliyopangwa na Yesu kwa ajili ya Meza ya Bwana. Wakati kiburi, tofauti, mivutano vinaendekezwa, moyo hauwezi kuwa na ushirika na Kristo. Tunakuwa hatujawa tayari kushiriki mwili wake na damu yake. Kwa hiyo Yesu aliamua kumbukumbu ya kudhalilishwa kwake iadhimishwe kwanza."—DA 650.

Katika tendo la kutawadha miguu ya wanafunzi, Kristo alifanya utakaso wa kina zaidi, wa kuosha doa la dhambi kwenye moyo. Wanaoshiriki huona kutostahili kupokea mkate na divai kabla ya kupata utakaso uwafanyao kuwa "safi mwili wote" (Yn. 13:10). Yesu alikuwa anataka kuosha "mifarakano, wivu, na kiburi kutoka

katika mioyo yao. … Kiburi na ubinafsi huleta mifarakano na chuki, lakini Yesu aliyaosha yote hayo. … Akiwatazama, Yesu aliweza kusema, 'Mmekuwa safi.'"—DA 646.

Mguso wa kiroho ambao ni kiini cha kutawadhana miguu huiinua huduma hiyo kutoka kuwa desturi ya kawaida na kuwa agizo takatifu. Inatoa ujumbe wa msamaha, ukubali, uhakika, na mshikamano, utokao kimsingi kwa Kristo kwenda kwa muumini, lakini pia kati ya waumini wao kwa wao. Ujumbe huo hutolewa katika mazingira ya unyenyekevu.

***Meza ya Bwana*—**Malaika wanatangaza kuwa, Yesu, Mkombozi wa ulimwengu huu, ni mtakatifu. Vivyo hivyo, ishara zinazowakilisha mwili wake na damu yake ni takatifu. Kwa kuwa Bwana mwenyewe alichagua ishara zenye maana nzito za mkate usiotiwa chachu na tunda la mzabibu lisilochachuka na kutumia njia sahili kabisa kuosha miguu ya wanafunzi, ni lazima kuwa na tahadhari kubwa kuanzisha ishara na njia zingine, isipokuwa katika hali ya dharura, ili umuhimu wa awali wa huduma hiyo usipotee. Vivyo hivyo, katika mpangilio wa huduma na majukumu yaliyozoeleka kufanywa na mchungaji, wazee, mashemasi wa kiume na wa kike, inapasa kuwa na tahadhari ili mabadiliko na uboreshaji visije vikafanya kilicho kitakatifu kuwa cha kawaida.

Huduma ya Meza ya Bwana leo, ni takatifu kama ilivyokuwa wakati ilipoanzishwa na Yesu Kristo. Yesu huwa anakuwepo wakati kaida hii takatifu inapoadhimishwa. "Ni katika mambo haya, aliyoyachagua mwenyewe, ambapo Kristo hukutana na watu wake na kuwatia nguvu kwa kuwepo kwake."—DA 656.

***Mkate Usiotiwa Chachu na Divai Isiyochachuka (Juisi ya Zabibu)*—**"Kristo huwa anakuwapo katika meza ambapo mlo wa pasaka umewekwa. Mikate isiyotiwa chachu itumikayo wakati wa Pasaka huwa mbele yake. Divai ya Pasaka, isiyoguswa na chachu, huwa inakuwapo mezani. Yesu huzitumia ishara hizi kuwakilisha dhabihu yake mwenyewe isiyokuwa na waa. Cho chote kilichoharibiwa na chachu, ambayo ni ishara ya dhambi na mauti, kisingeweza kumwakilisha 'mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa.' 1 Pet. 1:19."—DA 653.

Divai na Mkate havikuwa na chachu kwa kuwa jioni ya siku ya kwanza ya Pasaka ya Kiebrania, chachu yote ilikuwa imeondolewa kutoka katika nyumba zao (Kut. 12:15, 19; 13:7). Kwa hiyo juisi ya zabibu isiyotiwa chachu na mkate usiotiwa chachu tu ndiyo vinafaa kutumika katika huduma ya ushirika mtakatifu, na ni lazima kuwe na uangalifu mkubwa katika kuandaa vitu hivi. Katika maeneo ya pembezoni ambapo juisi ya zabibu haipatikani, konferensi itashauri au itasaidia.

***Kumbukumbu ya Kusulibiwa*—**"Tunapopokea mkate na divai vinavyowakilisha mwili wa Kristo uliovunjika na damu yake iliyomwagika, huwa tunajumuika kana kwamba tuko kule orofani kwenye Ushirika Mtakatifu. Tunakuwa kama vile tunapita katika ile bustani iliyotakaswa kwa uchungu wake aliyechukua dhambi za ulimwengu. Tunashuhudia pambano lililofanya upatanisho wetu na Mungu upatikane. Kristo huwa anadhihirishwa kati yetu akiwa amesulibiwa."—DA 661.

***Tangazo la Ujio wa Pili*—**"Huduma ya Ushirika Mtakatifu huelekeza kwenye ujio wa pili wa Kristo. Ilikuwa imekusudiwa kufanya tumaini hilo liendelee kuwa dhahiri katika akili za wanafunzi. Kila walipokutana pamoja kuadhimisha mauti yake, walikuwa wakielezea jinsi alivyokitwaa 'kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.' Katika mateso yao walipata faraja katika tumaini la kurudi kwa Bwana wao. Fikra isemayo, 'Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo' 1 Kor. 11:26, ilikuwa na umuhimu usioelezeka kwao."—DA 659.

***Kuitangaza Huduma ya Ushirika Mtakatifu*—**Huduma ya ushirika mtakatifu inaweza kujumuishwa kihalali kama sehemu ya huduma yo yote ya ibada ya Kikristo. Hata hivyo, kuipatia msisitizo stahiki na kuifanya huduma ya ushirika mtakatifu iwezekane kwa

washiriki wengi zaidi kushiriki, kwa kawaida huwa sehemu ya huduma ya ibada katika Sabato ya pili kutoka mwisho wa kila robo.

Katika Sabato inayotangulia inapasa litolewe tangazo juu ya huduma hiyo likielezea umuhimu wa ushirika mtakatifu unaokuja, ili washiriki waandae mioyo yao na kutatua migogoro yo yote ambayo haijatatuliwa kati yao. Wanapokuja katika meza ya Bwana Sabato inayofuata, waweze kupokea baraka zilizokusudiwa. Wale wasiokuwapo wakati wa tangazo hawana budi kualikwa pia.

***Kuendesha Huduma ya Ushirika Mtakatifu***—*Urefu wa Huduma*—Muda si kigezo muhimu sana katika huduma ya ushirika mtakatifu. Hata hivyo mahudhurio yanaweza kuboreshwa na mguso wa kiroho kuongezeka kwa (1) Kuondoa mambo ya ziada katika huduma ya ibada katika sikukuu hii. (2) kuepuka ucheleweshaji kabla na baada ya kutawadhana miguu, na (3) kuwafanya mashemasi wa kike waandae vitu katika meza ya ushirika mtakatifu kabla.

*Utangulizi*—Sehemu ya utangulizi wa huduma iwe fupi, ikiwa na matangazo mafupi, wimbo, ombi, sadaka, na hubiri fupi kabla ya kugawanyika kwenda kutawadhana miguu na kurudi tena kwa ajili ya Meza ya Bwana.

*Kutawadhana Miguu*—Kila kanisa liwe na utaratibu wa kukidhi mahitaji ya washiriki wake kwa ajili ya huduma ya kutawadhana miguu. (Tazama Maelezo, #5, uk. 175.)

*Mkate na Divai*—Baada ya kutawadhana miguu, kanisa hukusanyika tena pamoja kula mkate na kunywa divai. (Tazama Maelezo #6, uk, 175, 276.)

*Sherehe*—Ushirika mtakatifu hauna budi kuwa tukio makini, na si la huzuni. Makosa yamesahihishwa, dhambi zimesamehewa, na imani imethibitishwa. Ni wakati wa kusherehekea. Muziki uwe mchangamfu na wa furaha. Huduma hiyo imalizike kwa furaha, kama vile kwa kipande cha muziki au wimbo wa pamoja, ukifuatiwa na kutawanyika.

Mara nyingi, sadaka kwa ajili ya maskini hukusanywa wakati watu wanatoka.

Baada ya huduma hiyo, mashemasi wa kike na wa kiume wataondoa vitu mezani, watakusanya vyombo na kumwaga kwa staha mabaki yote ya mkate na divai. Mkate na divai hiyo visiliwe

wala kunywewa kwa hali yo yote, na wala visirejeshwe kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

***Wanaoweza Kushiriki*****—**Kanisa huwa linafanya ushirika mtakatifu wa wazi. Watu wote waliotoa maisha yao kwa Mwokozi wanaweza kushiriki. Watoto hujifunza umuhimu wa huduma hii kwa kuangalia wengine wakishiriki. Baada ya kupata mafunzo rasmi katika madarasa ya ubatizo na kujitoa kwa Yesu kwa njia ya ubatizo, huwa wanakuwa tayari kushiriki katika huduma hiyo wao wenyewe.

"Mfano wa Yesu unakataza kuzuia watu kushiriki katika Meza ya Bwana. Ni kweli kwamba dhambi ya wazi humzuia mkosaji. Roho Mtakatifu anafundisha wazi jambo hili. 1 Kor. 5:11. Lakini zaidi ya hapo, mtu ye yote asitoe hukumu. Mungu hajawaruhusu wanadamu kuamua nani ajihudhurishe katika matukio haya. Kwani ni nani awezaye kuusoma moyo? Ni nani anayeweza kutofautisha magugu na ngano? 'Mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe.' Kwani 'kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.' 'Alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili.' 1 Kor. 11:28, 27, 29. … Wanaweza kuja katika kundi la watu wasiokwa watumishi wa ukweli na utakatifu, lakini wakataka kushiriki katika huduma hiyo. Wasizuiwe. Kulikuwa na mashahidi wakati Yesu anatawadha miguu ya wanafunzi na ya Yuda. Macho yaliyokuwa zaidi ya macho ya wanadamu yalikuwa yanatazama tukio hilo."—DA 656.

***Kila Mshiriki Hana Budi Kushiriki*****—**Mtu ye yote asiondoke kwenye Ushirika Mtakatifu kwa sababu kuna watu wasiostahili. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki hadharani, na hivyo kushuhudia kwamba anamkubali Kristo kama Mwokozi wake binafsi. Ni katika miadi hii aliyoiweka yeye mwenyewe ambapo Kristo hukutana na watu wake na kuwatia nguvu kwa kuwepo kwake. Mioyo na mikono isiyostahili inaweza kuhudumu katika huduma hiyo, lakini Kristo atakuwapo kuwahudumia watoto wake. Wote watakaokuja na imani iliyoelekezwa kwake watabarikiwa

sana. Wote watakaopuuza matukio haya, watapata hasara. Hao wanaweza kuambiwa, '… mmekuwa safi, lakini si nyote.'

***Wanaoweza Kuendesha Ushirika Mtakatifu—***Huduma ya Ushirika Mtakatifu itaendeshwa na mchungaji aliyewekewa mikono au mzee aliyewekewa mikono. Mashemasi, hata wakiwa wamewekewa mikono, hawawezi kuendesha huduma hii.

***Ushirika Mtakatifu Kwa Ajili ya Wasioweza Kuhudhuria—*** Kama mshiriki ni mgonjwa au hawezi kuja katika huduma ya ushirika mtakatifu kwa sababu nyingine, mchungaji au mzee anaweza kuendesha huduma maalum nyumbani kwa mshiriki huyo, ikiwezekana afuatane na kusaidiwa na shemasi wa kiume au wa kike.

**Mkutano wa Maombi**

***Mikutano ya Maombi Iwe ya Kupendeza—***"Mikutano ya maombi haina budi kuwa mikutano ya kupendeza kuliko yote inayofanyika, lakini mara nyingi mikutano hii huendeshwa vibaya. Wengi huja kwenye mahubiri lakini hupuuza mkutano wa maombi. Hapa tena, unahitajika umakini. Inapasa hekima itafutwe kwa Mungu na mipango ifanywe ya kuendesha mikutano hii kwa namna itakayokuwa ya kupendeza na kuvutia. Watu wana njaa ya mkate wa uzima. Wakiuona katika mkutano wa maombi watakwenda kuupokea.

"Mahubiri na maombi marefu yasiyovutia hayafai mahali po pote, na hasa katika mkutano wa pamoja (maombi). Wale wepesi na walio tayari kusema kila wakati huwa wanaachiwa kuziba nafasi ya wale wasiojiamini na wenye haya. Mara nyingi wale wenye mambo ya juu juu tu, huwa wana mengi ya kusema. Maombi yao huwa marefu na si ya kina. Huwachosha malaika na watu wanaoyasikiliza. Maombi yetu hayana budi kuwa mafupi na yanayotoa hoja moja kwa moja. Kama mtu ana maombi marefu yanayochosha, basi yafanyike chumbani. Ruhusuni Roho wa Mungu ainge mioyoni mwenu na ataondoa utaratibu mkavu wote."—4T 70, 71

Inapasa zifanyike juhudi zisizokuwa za kawaida kuhakikisha kuwa mikutano ya maombi inakuwa na mafanikio. Mkutano hauna

budi kuanza kwa wakati, hata kama kuna watu wawili au watatu tu. Kuwe na somo fupi la Maandiko au somo kutoka katika roho ya unabii, likifuatiwa na maombi, ushuhuda, na ombi la baraka. Badilisheni mpangilio wa huduma kila juma.

Kama washiriki hawawezi kukutana mahali pa kawaida kwa ajili ya maombi, mikutano ya nyumbani inaweza kuwa na manufaa makubwa.

**Mkutano Mkuu wa Kanisa**

Kanisa mahalia hufanya kazi katika dhima zilizo bayana katika muundo wa Kanisa la Waadventista wa Sabato. Katika muktadha wa dhima hizo, mkutano mkuu wa kanisa ndio chombo kikuu cha utawala wa kanisa mahalia. Washiriki hai wanahimizwa kuhudhuria na wana haki ya kupiga kura. Mshiriki aliye na karipio hana haki ya kushiriki kwa kusema wala kupiga kura.

Mkutano mkuu utafanyika angalao mara moja kwa mwaka. Mchungaji au baraza la kanisa kwa kushauriana na kusaidiwa na mchungaji, ataitisha mkutano huo. Kwa kawaida mkutano mkuu wa kanisa hutangazwa juma moja au mawili kabla katika ibada ya kawaida ya siku ya Sabato, ikiwa pamoja na muda na mahali pa kukutania. Mchungaji, au mzee aliyepangiwa na mchungaji au katika masuala kadhaa, mwenyekiti wa konferensi atakuwa mwenyekiti wa mkutano mkuu wa kanisa.

Kila kanisa litaamua koramu iweje katika mikutano ijayo.

Kura wakilishi au za barua haziruhusiwi.

Masuala makubwa hayana budi kuamuliwa katika mkutano mkuu wa kawaida au mkutano mkuu maalum.

Mkutano mkuu wa kanisa una mamlaka juu ya baraza la kanisa na unaweza kukasimu kwa baraza majukumu zaidi ya yale yaliyoelezwa tayari kwenye *Mwongozo wa Kanisa.* (Tazama Maelezo, #7, uk. 176, 177.)

Ili kudumisha moyo wa ushirikiano kati ya kanisa na konferensi, kanisa litaomba ushauri kwa maofisa wa konferensi katika masuala makubwa yote.

Maofisa wa konferensi na union (mwenyekiti, katibu na mhazini) au watu waliowachagua, wanaweza kuhudhuria mkutano

mkuu wa kanisa lo lote katika eneo lao bila kupiga kura (isipokuwa wakiruhusiwa na kanisa). Kura ya kuwaruhusu kupiga kura si ya lazima kama maofisa hao ni washiriki wa kanisa husika.

**Baraza la Kanisa na Mikutano Yake**

***Ufafanuzi na Kazi Zake*—**Kila kanisa halina budi kuwa na baraza linalofanya kazi ambalo wajumbe wake wamechaguliwa katika mkutano mkuu wa kanisa. Shughuli yake kubwa ni malezi ya kiroho ya kanisa na kazi ya kupanga na kuendeleza uinjilisti katika sura zake zote.

Katika majukumu ya baraza la kanisa kuna:

1. Kulea kiroho.
2. Uinjilisti katika sura zake zote.
3. Kudumisha usafi wa mafundisho.
4. Kuhifadhi viwango vya Kikristo.
5. Kupendekeza mabadiliko ya ushirika.
6. Pesa za kanisa.
7. Ulinzi na utunzaji wa mali ya kanisa.
8. Kuratibu idara za kanisa.

Agizo la Yesu kuhusu injili linaufanya uinjilisti, yaani kutangaza habari njema ya injili, kuwa kazi ya msingi ya baraza la kanisa, ambalo hufanya kazi kama kamati kuu ya kanisa. Baraza la kanisa linapoelekeza shauku zake kuu na nguvu zake zote katika uinjilisti wa kila mshiriki, matatizo mengi yatazuiwa na mvuto chanya wenye nguvu utaonekana katika uhai na ukuaji wa kiroho wa washiriki.

Baraza huchaguliwa na washiriki wakati wa uchaguzi wa kawaida wa maofisa. (tazama uk. 70, 71.0

***Wajumbe*—**Pamoja na wachungaji waliochaguliwa na konferensi, kanisa halina budi kuchagua baraza wakilishi ambalo lina maofisa wafuatao:

Wazee
Shemasi mkuu wa kiume
Shemasi mkuu wa kike
Mhazini
Karani

Mratibu wa waliovutiwa
Mratibu wa Wanaume wa Kiadventista
Kiongozi wa Chama cha Vijana
Mkurugenzi wa Klabu ya Wavumbuzi
Mkurugenzi wa Klabu ya Mabalozi
Mratibu wa shule ya Biblia
Kiongozi wa huduma za watoto
Mratibu wa muziki wa kanisa
Mwenyekiti wa kamati ya mawasiliano au katibu wa mawasiliano
Kiongozi wa huduma za jamii na/au Chama cha Dorkas
Katibu wa elimu
Kiongozi wa huduma za familia
Kiongozi wa huduma za afya
Kiongozi wa Chama cha Kaya na Shule
Mkurugenzi wa Klabu ya Watafuta Njia
Kiongozi na katibu wa huduma binafsi
Mratibu wa huduma za uchapishaji
Kiongozi wa uhuru wa kidini
Mrakibu wa shule ya Sabato
Kiongozi wa huduma za uwakili
Kiongozi wa huduma za wanawake

Katika mazingira fulani, kulingana na wingi wa washiriki, baraza linaweza lisiwe na wote walio katika orodha hii au linaweza kuongeza wajumbe wengine. Mchungaji aliyechaguliwa na konferensi kuhudumia kanisa husika siku zote ni mjumbe wa baraza.

***Maofisa*—**Mwenyekiti wa baraza ni mchungaji aliyeteuliwa na konferensi. Mchungaji akiamua kutofanya kazi hiyo au akiwa hawezi kuhudhuria, anaweza kupanga mzee asimamie kama mwenyekiti.

Karani hufanya kazi kama katibu wa baraza na ana wajibu wa kuandika, kuwasilisha na kuhifadhi kumbukumbu za mikutano.

***Mikutano*—**Kwa kuwa kazi ya baraza ni nyeti kwa uhai, ustawi, na ukuaji wa kanisa, inapendekezwa kwamba likutane japo mara

moja kila mwezi, na mara nyingi zaidi ikihitajika. Ni vyema kupanga muda wa mkutano wa kila mwezi ili uwe katika juma lile lile na siku ile ile ya juma kila mwezi.

Mkutano wa baraza hutangazwa katika ibada ya kawaida ya Sabato, na wajumbe wote wa baraza wanatakiwa kuhudhuria.

Kila kanisa halina budi kuamua katika mkutano mkuu wa kanisa, idadi ya wajumbe ambao ni lazima wawepo ili kuwe na koramu katika mikutano ya baadaye.

Kura wakilishi au za barua haziruhusiwi.

***Kazi ya Baraza***—1. Kipengele muhimu kuliko vyote katika ajenda lazima kiwe uenezaji wa injili katika eneo la umisionari la kanisa. Zaidi ya hapo, mara moja kila robo mkutano mmoja mzima hauna budi kujielekeza katika mipango ya uinjilisti. Baraza litachunguza mapendekezo ya konferensi kuhusu programu na njia za uinjilisti na namna inavyoweza kutekelezwa kikanisa mahalia. Mchungaji na baraza wataanzisha kuweka mipango ya mikutano ya hadhara ya uinjilisti.

Kuratibu programu za umisionari za idara. Baraza la kanisa lina wajibu wa kuratibu kazi za idara zote za kanisa. Kila idara hupanga mipango yake ya umisionari katika eneo lake. Ili kuepuka migongano ya wakati na mashindano katika kupata watu wa kujitolea na kupata matokeo mazuri, uratibu ni wa lazima. Kabla ya kukamilisha na kutangaza mipango ya programu yo yote, kila idara haina budi kuwasilisha mipango yake kwenye baraza kwa ajili ya kuidhinishwa. Idara pia hutoa taarifa kwa baraza juu ya maendeleo na matokeo ya programu zao za umisionari. Baraza linaweza kupendekeza jinsi mipango ya idara inavyoweza kuchangia katika maandalizi, uendeshaji na ufuatiliaji wa kampeni ya hadhara ya uinjilisti.

Kuihimiza idara ya huduma binafsi kuhusisha washiriki wote, pamoja na watoto katika namna fulani ya huduma ya umisionari binafsi. Inapasa madarasa ya mafunzo yaendeshwe katika nyanja mbalimbali za huduma ya umisionari.

Kumhimiza mratibu wa waliovutiwa kuhakikisha kuwa kila mtu aliyevutiwa anafuatiliwa binafsi na haraka na mlei aliyepangiwa.

Kuhimiza kila idara kutoa taarifa kwa baraza japo kwa robo na

kwa washiriki katika mkutano mkuu wa kanisa au katika mkutano wa Sabato

Kupokea taarifa za mara kwa mara. Baraza halina budi kuangalia vipengele vya shughuli za kanisa na kupokea taarifa za mara kwa mara za mhazini juu ya pesa za kanisa. Inalipasa kanisa kuangalia kumbukumbu za washiriki na kupeleleza juu ya hali ya kiroho ya washiriki wote na kuandaa utaratibu wa kutembelea washiriki wanaoumwa, waliokata tamaa, au waliorudi nyuma. Maofisa wengine hawana budi kutoa taarifa kwa vipindi maalum.

***Kamati za Baraza***—Baraza lisiruhusu shughuli zingine kuingilia upangaji wa uinjilisti. Shughuli zingine zikiwa zinachukua muda mrefu kupita kiasi, inalipasa baraza kuteua kamati kushughulikia maeneo mahususi ya shughuli za kanisa, kama vile fedha au miradi ya ujenzi. Kamati hizo zitatoa mapendekezo kwa baraza. (Tazama Maelezo, #8, uk. 177.)

**Mikutano ya Bodi ya Shule**

Kwa kawaida shule ya kanisa husimamiwa na bodi ya shule. Kanisa huchagua mwenyekiti wa kuendesha mikutano na katibu wa kuandika kumbukumbu na uamuzi wa mikutano hiyo. Bodi hii haina budi kukutana kwa vipindi maalum. Mikutano maalum inaweza kuitishwa na mwenyekiti. Makanisa mengine huamua baraza la kanisa au kamati ndogo ya baraza la kanisa itumike pia kama bodi ya shule. (Tazama pia uk. 88, 89.)

**Mikutano ya Chama cha Kaya na Shule**

Chama cha kaya na shule hakina budi kukutana kila mwezi na kuratibu shughuli za kaya, shule na kanisa. Inapasa kuwe na msisitizo katika kuelimisha wazazi, na kuisaidia shule kupata raslimali inazozihitaji, kama vile wasimamizi wa vyumba, vitabu, vifaa vya kufundishia, na vyombo. Miongozo ya kusaidia viongozi wa Kaya na Shule hupatikana katika idara ya elimu ya konferensi.

**Mikutano ya Vijana**

Viongozi wa makundi mbalimbali ya vijana hawana budi kupanga mikutano ya mara kwa mara itakayowahusisha vijana

wa kanisa katika shughuli za maana ambazo zitawafanya wawe karibu zaidi na kanisa na kuwafundisha kwa ajili ya huduma zenye manufaa.

***Mikutano ya Chama cha Vijana***—Mikutano ya Chama cha Vijana haina budi kufanyika kwa kufuata ratiba ya vipindi maalum na kuzingatia ujenzi wa sifa za kiroho, kiakili, na kimwili kwa vijana wa kanisani. Mikutano hiyo pia huwawezesha kuwa na uhusiano wa Kikristo na kuwa na programu za ushuhudiaji zinazochangia katika mipango ya kanisa ya kuongoa roho. Kamati ya huduma za vijana wa Kiadventista huhimiza na kuratibu shughuli za Chama cha Vijana wa Kiadventista na za asasi zingine za vijana. (Tazama uk. 102.) Tazama Maelezo, #9, uk. 177 kwa ajili ya miongozo.

***Mikutano ya Chama cha Vijana Wadogo***—Mikutano ya Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista ni sawa na ile ya Chama cha Vijana wa Kiadventista lakini huwahusisha vijana wadogo. Kama kuna shule ya kanisa, Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista kitakuwa sehemu ya mtaala wa kiroho wa shule. (Tazama Maelezo, #10, uk. 177.)

***Mikutano ya Klabu ya Mabalozi***—Mikutano ya Klabu ya Mabalozi hutoa programu maalum kukidhi mahitaji ya vijana wa umri wa miaka 16 hadi 21, na kuhamasisha ushiriki wao katika kanisa. Mikutano yake na shughuli zingine zitafanyika kulingana na sera za konferensi na kwa kushirikiana na huduma zingine za vijana/watu wa umri wa kati wa kanisa mahalia.

***Mikutano ya Klabu ya Watafuta Njia***—Mikutano ya Klabu ya Watafuta Njia hutoa programu maalum kwa ajili ya vijana wadogo na katika maeneo mengine imechukua nafasi ya mikutano ya Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista. Makanisa ambapo vyama vyote viwili vinafanya kazi, hayana budi kuratibu shughuli zao.

***Mikutano ya Klabu ya Wavumbuzi***—Mikutano ya Klabu ya Wavumbuzi hutoa programu maalum kwa ajili ya watoto wa shule za msingi/awali zilizokusudiwa kuongezea na kuimarisha

ushiriki wa wazazi katika ukuaji wa awali wa mtoto. Mikutano na shughuli zingine zitafanyika kulingana na sera za konferensi kama zilivyoainishwa katika miongozo ya klabu na kwa kushirikiana na asasi zingine za kanisa zinazohusiana na vijana na familia.

SURA YA 11

# Fedha

Mpango wa Biblia kwa ajili ya kusaidia kazi ya Mungu ni kwa njia ya zaka na sadaka za watu wake. Bwana anasema, “Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu” (Mal. 3:10). Kanisa limekuwa likifuata mpango huu tangu siku za awali kabisa.

“Utaratibu wa zaka na sadaka ulikusudiwa kufikisha ukweli mkuu katika mioyo ya watu—Kwamba Mungu ni chanzo cha kila baraka kwa viumbe vyake, na kwamba anastahili shukurani za wanadamu kwa ajili ya zawadi nzuri za majaliwa yake.”—PP 525.

“Zaka na Sadaka kwa ajili ya Mungu ni kutambua stahili yake juu yetu inayotokana na kutuumba, na pia ni kukiri stahili yake inayotokana na kutukomboa. Kwa kuwa uwezo wetu wote unatoka kwa Kristo, sadaka hizi hazina budi kutoka kwetu kwenda kwa Mungu. Zinapasa kutukumbusha wakati wote stahili yake itokanayo na ukombozi, stahili kubwa kuliko stahili zote, na ambayo inahusisha stahili zingine zote.”—6T 479.

“Zaka ni takatifu, imetengwa na Mungu kwa ajili yake yeye mwenyewe. Inatakiwa kuletwa katika hazina yake ili itumike kukimu watenda kazi wa injili katika kazi zao.”—9T 249.

“Amewapa watu wake mpango wa kukusanya kiasi cha kutosha kufanya kazi yake ijitosheleze. Mpango wa Mungu katika mfumo wa zaka ni mzuri katika usahili na usawa wake. Watu wote wanaweza kuufuata katika imani na ujasiri, kwani chanzo chake ni Mungu. Ndani yake kuna usahili na kufaa. … Kila mwanamume, mwanamke na kijana anaweza kuwa mhazini wa Bwana na anaweza kuwa wakala wa kukidhi mahitaji ya pesa. Mtume Paulo anasema: ‘kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake.’”—3T 388, 389.

“Mungu ameufanya utangazaji wa injili utegemee kazi na matoleo kutoka kwa watu wake. Sadaka za hiari na zaka ndizo zinazounda hazina ya kazi ya Bwana. Mungu anadai sehemu ya mali iliyokabidhiwa kwa mwanadamu—sehemu ya kumi. Amewapa

uhuru wa kuamua kama watampa zaidi ya hapo."—AA 74.

Mungu ametoa maelekezo maalum juu ya matumizi ya zaka. Hakusudii kazi yake izorote kwa kukosa pesa. … Sehemu ambayo Mungu ameitenga kwa ajili yake isichepushwe kwenda katika matumizi mengine zaidi ya yale yaliyotajwa. Mtu ye yote asije akajisikia huru kubaki na zaka yake, ili aitumie kulingana na uamuzi wake mweyewe. Asiitumie kwa ajili yake katika dharura, wala kuitumia kama anavyoona inafaa katika jambo analoweza kulichukulia kuwa ni kazi ya Bwana."—9T 247.

**Uwakili**

Wakristo ni mawakili wa Mungu, waliokabidhiwa mali zake kama washirika wake wenye jukumu la kuzisimamia kulingana na maelekezo na kanuni zake. Ushauri wa Mungu ni kwamba, kama wakili wake; "mtu aonekane kuwa mwaminifu" (1 Kor. 4:2). Ingawa suala la uwakili linahusu nyanja nyingi za maisha ya Kikristo, bila shaka uwakili wa mali zetu ni muhimu sana. Unahusu familia yote ya Kanisa na unajumuisha kuitambua mamlaka ya Mungu, umiliki wake wa vitu vyote, na ukarimu wa neema yake kwa mioyo yetu.

Ingawa kipengele hiki cha uwakili wa Kikristo kinahusu mali zetu, kinatokana na hali ya Ukristo wetu. Bwana anataka mambo kadhaa kutoka kwetu ili aweze kutufanyia mambo fulani. Utii wetu wa kukubaliana na matakwa ya Baba yetu wa mbinguni huiweka sura hii ya uwakili katika kiwango cha juu cha kiroho. Halazimishi tumtumikie au tumtambue kwa matoleo yetu. Lakini ameweka utaratibu ili tukienenda kwa kuafikiana naye katika mambo hayo baraka nyingi za kiroho zitamiminika katika mioyo yetu.

"Mungu anataka mawakili wake wote wawe sahihi katika kufuata utaratibu wake. Hawatakiwi kufidia utaratibu wa Mungu kwa kufanya jambo lingine la kujitolea au kutoa zawadi au sadaka fulani kwa wakati na namna ambayo wao ambao ni mawakala wa kibinadamu, wataona inafaa. Ni sera isiyofaa kabisa kwa wanadamu kujaribu kuboresha utaratibu wa Mungu na kubuni utaratibu wa muda, wakitazama nia zao nzuri katika jambo hili na lile na kuziweka mahali pa matakwa ya Mungu. Mungu anawataka watu wote watumie ushawishi wao kwa ajili ya utaratibu wake."—9T 248.

**Zaka**

Kwa kuutambua utaratibu wa Biblia na fursa na wajibu nyeti uliopo kwa washiriki kama watoto wa Mungu na sehemu ya mwili wake, yaani Kanisa, washiriki wote wanahimizwa kurejesha katika hazina ya Kanisa kwa uaminifu zaka, yaani moja ya kumi ya maongeo au mapato binafsi.

Zaka haitatumiwa na kanisa mahalia kwa namna yo yote ile, bali itatunzwa kama amana na kutumwa kwa mhazini wa konferensi. Kwa njia hiyo zaka kutoka makanisa yote huingia katika hazina ya konferensi, na asilimia fulani hutumwa kwenye ngazi ya juu zaidi kulingana na sera za Konferensi Kuu na divisheni kwa ajili ya kugharimia uendeshaji wa kazi ya Mungu katika maeneo ya wajibu na shughuli zao.

Sera hizi zimewekwa kwa ajili ya kukusanya na kugawa pesa ulimwenguni kote na kwa ajili ya kuendesha shughuli za kazi ya Mungu. Nyanja za fedha na mwenendo wake katika kazi ni za muhimu sana. Haziwezi kutenganishwa na uenezaji wa ujumbe wa wokovu. Kwa kweli nyanja hizo ni sehemu ya uenezaji wa ujumbe wa wokovu.

***Utoaji wa Mpango na Umoja*****—**Mpango wa fedha wa Kanisa hukidhi kusudi kubwa zaidi kuliko inavyoonekana katika taarifa zake za fedha na takwimu. Mfumo wa kushirikiana na maeneo ya ulimwengu katika matumizi ya pesa kama unavyoainishwa katika *Sera za Kazi* za Konferensi Kuu, unakidhi kusudi zuri la kuunganisha kazi ya kiroho ya Kanisa ulimwenguni kote.

***Jinsi Zaka Inavyotumika*****—**Zaka inachukuliwa kuwa ni takatifu kwa ajili ya kazi ya uchungaji, kwa kufundisha Biblia na kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa konferensi katika kusimamia makanisa na shughuli za umisionari. Zaka isitumike kwa kazi nyingine, katika kulipia madeni ya kanisa au taasisi, au program za majengo, isipokuwa pale ilipoidhinishwa na *Sera ya Kazi* ya Konferensi Kuu. Kwa maelezo zaidi juu ya matumizi ya zaka, tazama Maelezo, #1, uk. 177.

"Nimepewa ujumbe bayana, ulio fasaha, kwa ajili ya watu wetu. Nimeagizwa kuwaambia kuwa wanafanya kosa kutumia

zaka kwa mambo mbalimbali ambayo, japo ni mema jinsi yalivyo, si mambo ambayo Bwana amesema zaka itumike kuyagharimia. Wale wanaotumia zaka namna hiyo wanatoka katika mpango wa Mungu. Mungu atahukumu kwa ajili ya Mambo hayo."—9T 248.

***Jinsi Zaka Inavyoshughulikiwa***—Zaka ni mali ya Bwana na haina budi kuletwa katika hazina ya Konferensi kama tendo la ibada kupitia kanisa ambapo ushirika wa mhusika upo. Kunapokuwa na mazingira yasiyokuwa ya kawaida, washiriki wawasiliane na maofisa wa konferensi.

***Maofisa wa Kanisa na Konferensi Waoneshe Mfano***—Wazee na maofisa wengine, pamoja na mchungaji na watumishi wa konferensi na taasisi, wanatarajiwa kuonesha mfano mzuri wa uongozi kwa kurudisha zaka. Hakuna mtu atakayeendelea kuwa ofisa wa kanisa au mfanyakazi wa konferensi kama haendi sawa na kipimo hiki cha uongozi.

**Sadaka**

Pamoja na zaka, Maandiko yanasisitiza wajibu wetu wa kuleta sadaka kwa Bwana. Kutokutoa sadaka kumewekwa pamoja na kutokutoa zaka na kunaitwa wizi (Mal. 3:8). Tangu siku za mwanzo kabisa za kanisa, washiriki wamekuwa wakitoa sadaka kubwa ambazo zimebariki na kustawisha kazi ya Mungu.

Pamoja na kalenda iliyozoeleka ya mpango wa sadaka, ambapo kila sadaka hukusanywa kwa kusudi maalum, Konferensi kuu imeruhusu mfumo wa sadaka ya pamoja na mpango mahususi wa utoaji. Kamati ya divisheni inaruhusiwa kuamua mpango/mipango upi/ipi utumike/itumike katika eneo lake.

***Sadaka ya Shule ya Sabato***—Njia ya kanisa inayotumika sana na iliyofanikiwa zaidi ya utoaji wa mpango kwa vipindi maalum ni ile ya sadaka za shule ya Sabato, ambazo hutengwa kwa ajili ya kazi ya umisionari ulimwenguni.

***Sadaka Zingine***—Sadaka zingine hukusanywa nyakati mbalimbali kwa ajili ya kazi ya umisioanari ulimwenguni na kwa

ajili ya miradi ya jumla na mahalia. Inapotolewa sadaka yo yote, pesa yote iliyokusanywa, itahesabiwa kama sehemu ya sadaka hiyo mahususi isipokuwa kama mtoaji atakuwa ameelekeza vinginevyo.

***Matoleo Maalum kwa Maeneo ya Kazi***—Msaada wa kifedha kwa kazi ya Kanisa ulimwenguni umejengwa katika mfumo wa bajeti. Pesa hutolewa kwa maeneo mbalimbali kwa msingi wa mahitaji yaliyotengewa bajeti. Hii ni njia ya haki na isiyo na upendeleo ya kugawa pesa.

Pale ambapo matoleo maalum nje ya bajeti ya kawaida yametolewa kwa eneo maalum, kutakuwa na tofauti itakayoleta madhara kwa maeneo mengine. Matoleo kama hayo yakitolewa kwa ajili ya kuanzisha kazi mpya, kazi iliyoanzishwa kwa njia hiyo inaweza kukwama sadaka hiyo itakapokwisha, au inaweza kujumuishwa katika bajeti kwa ajili ya kusaidiwa siku za usoni. Kwa njia hiyo maeneo mengine ambayo huenda yana mahitaji makubwa zaidi lakini hayana fursa ya kufanya yajulikane, yatakosa sehemu yake ya haki katika pesa za jumla ambazo zitachepushwa kwenda kwenye kazi iliyoanzishwa kwa sadaka maalum.

Historia imeithibitisha hekima ya washiriki kutoa sadaka na matoleo yao kwa ukarimu na uaminifu kwa kutumia njia zilizokubaliwa na wakijua kuwa kila eneo hunufaika kwa kutoa kwao.

***Kusaidia Maskini na Wahitaji***—Sadaka kwa ajili ya maskini na wahitaji hukusanywa kusaidia washiriki wanaohitaji msaada. Mfuko wa akiba hauna budi kuwepo kwa ajili ya dharura kama hizo. Pamoja na hayo, kanisa halina budi kuwa na mtazamo wa ukarimu kwa wote walio wahitaji, na baraza linaweza kutoa pesa katika mfuko huo kusaidia kazi ya kanisa ya afya na ustawi wa familia katika jamii.

***Bajeti ya Kanisa kwa Ajili ya Matumizi Mahalia***—Njia nzuri kabisa ya kugharimia mambo ya kanisa ni mpango wa bajeti. Kabla ya kuanza kwa mwaka mpya, baraza litaandaa bajeti ya matumizi kwa ajili ya shughuli za kanisa kwa mwaka unaofuata. Bajeti hiyo itakuwa na mapato na matumizi yote, ikiwa ni pamoja na yale

yanayohusu idara. Haina budi kueleza matumizi yanayotarajiwa kama vile, matumizi ya huduma mbalimbali kama umeme, maji, bima, ukarabati, ulinzi, pesa kwa ajili ya maskini na wahitaji na matumizi ya shule ya kanisa. (Tazama Maelezo, #2, uk. 177, 178, kwa ajili ya bajeti ya mfano.)

Bajeti haina budi kuwasilishwa kwa kanisa ili liiangalie na kuipitisha, na kwa ajili ya mipango ya kuhakikisha kwamba pesa zitatolewa kulingana na bajeti katika mwaka unaokuja. Pesa za kugharimia bajeti ya matumizi ya kanisa zinaweza kupatikana kwa sadaka au michango. Washiriki hawana budi kuhimizwa kusaidia kanisa lao mahalia kulingana na hali zao za kifedha.

### Ushauri wa Jumla wa Kifedha

***Kanuni za Kuchangisha Pesa*—**Zifuatazo ni kanuni kwa ajili ya kuchangisha pesa:

Hakuna konferensi, kanisa, au taasisi, itakayopanga kazi inayohitaji kuchangisha pesa nje ya mipaka yake bila kushauriana na kufanya mipango maalum. Michango yo yote ndani ya mipaka yake itafanyika kulingana na sera za union mahalia, divisheni na Kuonferensi Kuu. Hakuna ruhusa kwa watumishi wa kanisa wanaowakilisha maslahi maalum katika sehemu moja ya eneo kuomba misaada katika eneo lingine lo lote la eneo hilo au katika konferensi nyingine bila makubaliano na idhini ya maandishi kutoka kwa maofisa wa konferensi ambako uchangishaji huo utafanyika.

Kanuni zifuatazo zinalinda makanisa dhidi ya michango ya udanganyifu isiyoidhinishwa na isiyokuwa ya kikanisa:

Wachungaji na maofisa hawatatoa fursa ya kutumia mimbari kwa watu kwa ajili ya kuchangisha pesa ambao hawajatambuliwa na kupendekezwa na konferensi. (tazama uk. 116, 117.) Ruhusa haitatolewa kuchangisha pesa ama hadharani au kwa mtu mmoja mmoja bila kutambuliwa na konferensi

Pesa zote zitakazochangishwa kwa ajili ya jambo lo lote kutokana na ombi kama hilo, zitapita katika mkondo wa kawaida wa kanisa.

Maofisa wa konferensi na kanisa watachukua hatua zitakazolazimu kuzuia uchangishaji wa hadhara ulio kinyume cha sheria.

Hakuna kampeni zaidi ya Wito wa Mwaka (Mavuno au wito kama huo), unaohusisha vipeperushi vya wito na vyombo vyenye lebo za wito zilizoidhinishwa, itakayoendeshwa kwa ajili ya kuchangisha pesa kwa ajili ya kazi ya umisionari wa ndani ya nchi au nchi za nje. Union na konferensi hazina budi kuzuia ukiukwaji wa kanuni hii.

Watumishi wanaofanya kazi nje ya divisheni zao wanapotembelea makanisa yao ya nyumbani au kuwasiliana na sehemu wanazotoka wanaombwa kuchangisha pesa kwa ajili ya shughuli zilizo katika bajeti ya matumizi tu, wakifanya kazi kwa kushirikiana na makanisa na konferensi kuchangisha pesa zinazotakiwa kufanya malipo ambayo kazi yetu ya umisionari ulimwenguni inayategemea. Pesa zote za aina hiyo zitapita katika mkondo wa kawaida.

***Njia Zisizofaa za Kuchangisha Pesa*—**Kanisa mahalia halina budi kuwa na msimamo thabiti dhidi ya njia zisizofaa za kuchangisha pesa.

"Pesa zinapochangishwa kwa makusudi ya kidini, makanisa mengi hutumia njia gani? Minada, chakula, maonesho, na hata bahati nasibu na mambo mengine kama hayo. Mara nyingi mahali palipotengwa kwa ajili ya kumwabudu Mungu hunajisiwa kwa kula sana na kunywa, kununua, kuuza na shamra shamra. Heshima kwa nyumba ya Mungu na kicho kwa ibada yake hupungua katika akili za vijana. Uwezo wa kujitawala hudhoofishwa. Ubinafsi, uchu, kupenda kujionesha, huamshwa na kuimarika vinapoendekezwa."—9T 91.

Kadiri kazi ya Mungu inavyopanuka, maombi ya misaada yatakuja kwa wingi zaidi. … Wanaodai kuwa Wakristo wakileta zaka na sadaka zao kwa Mungu kwa uaminifu, hazina yake itajaa. Hakutakuwa tena na haja ya kutumia maonesho, bahati nasibu au tafrija za anasa kupata pesa za kusaidia injili."—AA 338.

***Zaka na Sadaka si Amana za Watu*—**Zaka na Sadaka zinazotolewa na washiriki kwa kanisa hazifanyi mfuko wa amana kwa ajili ya matumizi ya badaye ya watoaji. Pesa hizi zitatumiwa kwa ajili ya makusudi yaliyopo ambayo yanafanya zitolewe.

***Kugharimia Mipango ya Ujenzi*****—**Makanisa yanayofikiria kununua au kujenga makanisa au majengo mengine, au kuwa na deni la aina yo yote, hayana budi kushauriana na konferensi kabla ya kubeba majukumu ya kifedha kama hayo. Katika kununua au kujenga majengo ya kanisa, kwa hali yo yote zisitolewe ahadi au ujenzi kuanza mpaka idhini itolewe na kamati za konferensi na union. Kamati hizi zitaidhinisha tu baada ya kujiridhisha kuwa mipango ya kifedha inakubaliana na sera zilizopo. Katika kutoa ushauri wa kifedha, kamati ya konferensi itaangalia idadi ya washiriki, uwezo wa kifedha wa kanisa husika na mahali pa jengo hilo.

***Kushughulikia na Kutoa Hesabu ya Pesa*****—**Kukusanya na kushughulikia pesa za kazi ya Bwana ni dhamana takatifu. Mkondo sahihi wa kupitia pesa hizo ni kwanza kutoka kwa washiriki kwenda kwa kanisa mahalia, ambapo mhazini huzipokea. (tazama uk. 80-84.) Mhazini hugawa pesa zilizokusudiwa kwa matumizi ya kanisa. Mhazini hutunza kama amana pesa zilizokusudiwa kwa ajili ya konferensi au matumizi ya jumla na kuzituma kwa mhazini wa konferensi. Mhazini wa kanisa mahalia hufanya kazi kwa maelekezo ya baraza. Wahazini wa ngazi yo yote (kanisa mahalia, konferensi, union au divisheni/Konferensi Kuu) hawafanyi kazi kama wapendavyo wenyewe. Hulipa pesa kwa uamuzi au mamlaka ya kamati husika.

***Ukaguzi*****—**Kila seti ya vitabu vya mahesabu, kuanzia vile vya kanisa mahalia, mpaka vile vya Konferensi Kuu, hukaguliwa na wakaguzi walioteuliwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Kanuni hii, ambayo pia hutumika katika kila taasisi shiriki ya kanisa, inatoa usalama wa hali ya juu katika kushughulikia pesa. (Tazama uk. 83.)

SURA YA 12

# Viwango vya Maisha ya Kikristo

### Wito Mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu

Maisha ya Mkristo si badiliko au uboreshaji mdogo, bali ni badiliko la hulka. Hii inamaanisha kuifia nafsi na dhambi na kufufuka katika uzima mpya kama mtu mpya katika Kristo Yesu.

Moyo wa Mkristo huwa makazi ya Kristo kwa imani. Jambo hili husababishwa na "kumtafakari Kristo, kumtazama Kristo, wakati wote tukimthamini Mwokozi mpendwa kama rafiki yetu mkubwa anayeheshimika kuliko wote, kiasi kwamba hatuwezi kumwudhi na kumkasirisha"—TM 387. Kwa njia hiyo Wakristo huambatana na kuwepo kwa Mungu," na tunapotambua kuwepo huko, "mawazo yetu hutekwa na Yesu Kristo" (TM 388) na mwenendo wetu hufanywa upatane na kiwango cha Mungu.

Inatupasa kukumbuka kwamba "hakuna mvuto mwingine unaoweza kulingana na hisia za kuwepo kwa Mungu kama ngao dhidi ya majaribu na kichocheo cha usafi na ukweli,."—Ed 255.

"Hakuna sehemu ya mwenendo wetu inayopita bila kuangaliwa. Hatuwezi kuzificha njia zetu Aliye Juu asizione. … Kila tendo, kila neno, kila wazo, liko bayana kana kwamba kuna mtu mmoja tu katika ulimwengu wote, na macho ya Mungu yameelekezwa kwake."—PP 217, 218.

Upendo wa Mungu humfikia kila mtu, na hasa watoto wake. Sikio lake husikia kusihi kwa watu wake waliouacha ulimwengu na kujitoa kwake. Kutokana na uhusiano huu mtakatifu huja heshima na kicho ambavyo huonekana kila siku na kila mahali.

Kama Wakristo sisi ni sehemu ya familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa mbinguni. Kwa hiyo inatupasa tusiseme neno na tusifanye tendo linaloweza kusababisha "jina lile zuri mliloitwa" likatukanwa. (Yak. 2:7). Sisi ni wanamatengenezo. Katika kila

awamu ya maisha, inatupasa kuichunguza kwa makini tabia ya yule Mwanadamu-mungu na kujiuliza kila wakati, 'Je, Yesu angefanya nini kama angekuwa mahali pangu?' Hiki ndicho kinapasa kuwa kipimo cha wajibu wetu."—MH 491.

Kwa njia ya Kanisa la waliosalia, Mungu ataonesha kwa Ulimwengu wote utoshelevu wa injili katika kuwaokoa watu kutoka katika nguvu ya dhambi. Kama washiriki wa Kanisa hilo, inatupasa kusisitiza tena viwango vikuu vya Biblia na kufanya upya utii kwa kanuni hizo zilizotolewa na Mungu. Inatupasa kufikia katika viwango vya juu vya maisha ya Kikristo na kuwa tofauti na ulimwengu. Kwa kusudi hilo inatupasa kutii onyo la Bwana: "Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake" (1 Yoh. 2:15).

**Usomaji wa Biblia na Maombi**

Uhai wa kiroho hudumishwa kwa chakula cha kiroho. Inatupasa kudumisha tabia ya usomaji wa Biblia kwa taamuli na maombi kama tunataka kukamilisha utakatifu. Wakati mafuriko ya mawasiliano yakimiminika kutoka katika machapisho, redio, televisheni, intaneti, na vyombo vingine vya habari vya kisasa, wakati maelfu ya sauti zinataka kusikilizwa, inatupasa kufumba macho na masikio yetu dhidi ya mambo mengi yanayotaka kuingia katika akili zetu na badala yake tujitoe kwa ajili ya Kitabu cha Mungu, Kitabu cha vitabu, Kitabu cha uzima—yaani Biblia. Tukikoma kuwa watu wa Kitabu, tutapotea, na utume wetu utakuwa umeanguka. Ni pale tu tunapoongea na Mungu katika maombi na kusikia sauti yake kila siku, tunaweza kutumaini kuwa na uhai ambao "umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu" (Kol. 3:3) na kuimaliza kazi yake.

Maombi ni mazungumzo ya pande mbili ambapo huwa tunamsikiliza Mungu na kuzungumza naye. "Maombi ni kuufungua moyo kwa Mungu kama rafiki."—SC 93. "Kwa maombi ya dhati huwa tunaunganishwa na moyo wake asiye na ukomo," na bila maombi yasiyokoma na kukesha kwa makini tuko katika hatari ya kuwa wazembe na kuiacha njia sahihi."—SC 97, 95.

Kaya ni jiwe la pembeni la Kanisa. Nyumba ya Kikristo ni nyumba ya sala. "Akina baba na akina mama, hata kama shughuli zenu

zikiwabana sana, msiache kukusanya familia zenu katika madhabahu ya Mungu. . . .Wale wanaotaka kuishi maisha ya uvumilivu, upendo, na uchangamfu imewapasa kuomba."—MH 393.

**Uhusiano katika Jamii**

Pamoja na kwamba "wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo" (Flp. 3:20), bado tuko katika ulimwengu kama sehemu ya jamii ya wanadamu na inatupasa kugawana na raia wenzetu majukumu kadhaa katika matatizo ya kawaida ya maisha. Po pote tulipo kama watoto wa Mungu, inatupasa kutambuliwa kama raia wema katika unyofu wetu wa Kikristo na katika kushughulikia maslahi ya wote.

Licha ya wajibu wetu mkuu kuwa kwa Kanisa na agizo la injili, inatupasa kusaidia juhudi za kuleta utulivu na kuboresha jamii, kwa huduma zetu na mali zetu, kadiri inavyowezekana na kadiri inavyokubaliana na imani zetu. Ingawa inatupasa kujitenga na migogoro ya kisiasa na kijamii, inatupasa kila wakati, kwa utulivu na uthabiti, kudumisha msimamo usiotikisika kwa ajili ya haki na usahihi katika mambo ya kijamii, sambamba na kushika kikamilifu imani zetu za kidini. Ni wajibu wetu mtakatifu kuwa raia watiifu wa mataifa tunayotoka, tukimpa "Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu" (Mt. 22:21).

**Ushikaji wa Sabato**

Sabato ni ishara ya upendo wa Mungu kwa wanadamu. Ni kumbukumbu ya uwezo wa Mungu katika uumbaji wa mwanzo na pia ishara ya uwezo wake wa kuumba upya na kutakasa maisha yetu (Eze: 20:12), na uadhimishaji wake ni ushahidi wa utii wetu kwake na wa ushirika wetu na yeye.

Sabato ina nafasi maalum katika maisha yetu. Siku ya saba ya juma, tangu machweo ya Ijumaa hadi machweo ya Jumamosi (Law. 23:32), ni zawadi kutoka kuwa Mungu, ishara ya neema yake katika wakati. Ni fursa, yaani miadi maalum na yule atupendaye na tumpendaye, muda mtakatifu uliotengwa na sheria ya Mungu ambayo ni ya milele, siku ya furaha kwa ajili ya kumwabudu Mungu na kujumuika na wengine (Isa. 58:13). Tunaikaribisha Sabato kwa furaha na shukurani.

“Siku ya Sabato—ah!—ifanyeni kuwa tamu, yenye baraka kuliko siku zote za juma zima.”—FLB 36.

“Siku ya Sabato … ni muda wa Mungu, si wetu; tunapoikanyaga tunamwibia Mungu. … Mungu ametupatia siku sita zote za kufanya kazi zetu, na ametenga siku moja tu kwa ajili yake. Siku hii haina budi kuwa ya baraka kwetu—siku ambapo inatupasa kuacha mambo yetu yote ya kidunia na kuelekeza mawazo yetu kwa Mungu na mbingu. …

“Tusiwafundishe watoto wetu kuwa haiwapasi kuwa na furaha siku ya Sabato, kwamba si sahihi kwenda nje ya malango. Ah!, hapana. Kristo aliwapeleka wanafunzi wake kando ya ziwa siku ya Sabato na kuwafundisha. Mahubiri yake ya siku ya Sabato mara nyingi yalikuwa hayahubiriwi ndani ya majengo.”—HP 152.

Upendo wa Mungu umeweka kikomo cha shinikizo la kazi ngumu. Mungu huweka mkono wake wa rehema juu ya Sabato. Katika siku yake mwenyewe, amehifadhi fursa ya familia kuwa na ushirika naye, na viumbe, na sisi kwa sisi.”—Ed 251.

Saa za Sabato ni mali ya Mungu na hazina budi kutumika kwa ajili yake tu. Anasa zetu, maneno yetu, shughuli zetu na mawazo yetu yasipate nafasi katika kuiadhimisha siku ya Bwana (Isa. 58:13). Tukusanyike katika familia wakati wa machweo na kuikaribisha Sabato kwa maombi na nyimbo, na tuhitimishe siku hiyo kwa maombi na maneno ya shukurani kwa ajili ya upendo wake wa ajabu. Sabato ni siku maalum kwa ajili ya ibada katika nyumba na makanisa yetu, siku ya furaha kwetu na kwa watoto wetu, siku ambapo tunaweza kujifunza zaidi kuhusu Mungu kwa njia ya Biblia na viumbe ambavyo ni kitabu kikuu cha mafunzo. Ni muda ambao tunaweza kuwatembelea wagonjwa na kujishughulisha na wokovu wa watu. Inatupasa kuyaacha mambo ya kawaida ya zile siku sita za kazi na kutokufanya kazi yo yote isiyokuwa ya lazima. Tusiruhusu vyombo vya habari vya kidunia kuchukua muda wetu katika siku takatifu ya Mungu.

“Sabato haikusudiwi kuwa siku ya kukaa bila shughuli. Sheria hiyo inakataza kazi za kidunia katika siku ya Mungu ya kupumzika; kazi ngumu inayoleta riziki lazima ikome; hakuna kazi yo yote ya anasa au maslahi ya kidunia iliyo halali katika siku hiyo; lakini kama Mungu alivyoacha kufanya kazi yake ya kuumba, akapumzika

siku ya Sabato na kuibariki, ndivyo mwanadamu anavyotakiwa kuacha shughuli za maisha yake ya kila siku, na kuzitumia saa hizo takatifu kwa ajili ya pumziko liletalo afya, ibada, na matendo matakatifu."—DA 207.

Programu ya shughuli zinazopatana na moyo wa ushikaji halisi wa Sabato itafanya siku hii yenye baraka iwe ya furaha na bora katika juma zima kwa ajili yetu na kwa ajili ya watoto wetu—kuonja ladha hasa ya pumziko letu la mbinguni.

**Kicho Mahali pa Ibada**

Wakristo wanaelewa uwezo wa Mungu wa kufanya cho chote, utakatifu wake na upendo wake, siku zote wataonesha moyo wa kicho cha kina kwa ajili ya Mungu, Neno lake na ibada yake. "Unyenyekevu na kicho havina budi kuwa bayana katika tabia ya wale wanaokuja mbele za Mungu."—PP 252. Tutatambua kwamba "saa na mahali pa maombi ni vitakatifu, kwa kuwa Mungu yupo hapo."—GW 178. Hatutakuja katika nyumba ya ibada kwa uzembe, bali tutakuja kwa moyo wa taamuli na maombi, na tutaepuka mazungumzo yasiyokuwa ya lazima.

Kama wazazi inatupasa kuwafundisha watoto wetu kwa kicho namna iwapasavyo kujiheshimu katika "nyumba ya Mungu." (1 Tim. 3:15). Maelekezo ya dhati na nidhamu kwa vijana nyumbani, katika shule ya Sabato, na katika ibada vitasaidia sana katika kudumisha utii wao katika miaka ya baadaye.

Wachungaji wanaohisi utakatifu wa ibada ya Mungu watadumisha kicho, usahili, utulivu na adabu kanisani kwa mfano, mafundisho, na tabia yao mimbarani.

**Afya na Kiasi**

Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu (1 Kor. 6:19). "Kwa sehemu kubwa nguvu za kiakili na kiroho zinategemea nguvu na shughuli za kimwili; kila jambo linalokuza afya ya kimwili husaidia ukuaji wa akili imara na tabia yenye ulingano sawia."—Ed 195.

Kwa sababu hiyo tunaishi kwa makusudi kulingana na kanuni za afya za mazoezi ya mwili, kuvuta hewa, mwanga wa jua, hewa safi, matumizi ya maji, kulala, na kupumzika. Kwa kusadiki tunaamua kula kiafya, kuvaa nguo zinazofaa, kuwa wasafi, kuwa na starehe

zifaazo, na tunaamua kwa hiari kuzifuata kanuni za afya, kujitawala, na chakula kiletacho afya. Kwa hiyo tunaepuka aina zote za pombe, tumbaku, na dawa za kulevya. Tunajitahidi kuhifadhi ulingano wetu wa kimwili na kiakili kwa kuepuka kuzidisha kitu cho chote.

Matengenezo ya afya na fundisho la afya na kiasi ni sehemu zisizoweza kutenganishwa na ujumbe wa Kanisa. Maelekezo yalitufikia kupitia kwa mjumbe wa Bwana "kwamba wale wanaozishika amri zake inawapasa kuingizwa katika uhusiano mtakatifu na yeye mwenyewe, na kwa kuwa na kiasi katika ulaji, hawana budi kuweka akili na miili yao katika hali nzuri kabisa kwa ajili ya utumishi."—CH 132. Pia, ni makusudi ya Mungu kwamba uwezo wa matengenezo ya afya uwezao kurejesha afya, uwe sehemu ya juhudi kuu za mwisho za kutangaza ujumbe wa injili."—MM 259.

Sisi ni mali ya Mungu, mwili, nafsi na roho. Kwa hiyo ni jukumu letu la kidini kuzifuata kanuni za afya, kwa ajili ya ustawi wetu na furaha yetu na kwa ajili ya huduma fanisi kwa Mungu na kwa jamii. Inatupasa kudhibiti uchu wetu. Mungu ametupatia vyakula vya aina nyingi vinavyotosha kukidhi kila hitaji la lishe. "Matunda, nafaka, na mboga vilivyoandaliwa katika njia sahili, … pamoja na maziwa na krimu, hufanya chakula kiletacho afya kuliko vyote."—CD 92.

Tunapofuata kanuni za kuishi kwa afya, hatutaona haja ya viburudisho. Kanuni za maumbile zinazuia matumizi ya vileo na dawa za kulevya za aina yo yote. Tangu siku za mwanzo za harakati hizi, kutokutumia pombe na tumbaku vimekuwa masharti ya kuwa mshiriki. (tazama uk. 47, 49, 62, 91, 163, 164.)

Mungu ametupatia nuru kubwa juu ya kanuni za afya, na utafiti wa kisasa wa sayansi umezithibitisha kabisa kanuni hizi.

**Mavazi**

Kama Wakristo wa dhehebu la Waadventista wa Sabato tumeitwa ili tujitenge na ulimwengu. Dini yetu haina budi kuwa na mvuto wa kujenga katika shughuli zetu zote. Tabia zetu hazina budi kujengwa katika kanuni na si katika mifano ya ulimwengu. Desturi na mitindo vinaweza kubadilika, lakini kanuni za tabia njema hubaki vile vile. Mapema katika historia yetu, Ellen G. White aliandika kwamba

kusudi la mavazi ya Kikristo ni "kuwalinda watu wa Mungu dhidi ya mvuto wa ulimwengu uletao uharibifu, pamoja na kuleta afya ya kimwili na kimaadili."—4T 634. Pia anashauri kwamba inatupasa kuepuka kujionesha kupita kiasi na kujipamba sana, mitindo ya kupita na fasheni, hasa zile zinazokiuka kanuni za staha, na kwamba ikiwezekana, mavazi yetu yawe bora, yenye rangi za kupendeza na yanayofaa kwa utumishi" "kuliko kujionesha." Mavazi yetu yanapasa kuwa ya adabu, "uzuri," "heshima," na kufaa kwa usahili wa kawaida."—MYP 351, 352.

Watu wa Mungu hawana budi kuwa miongoni mwa wahafidhina katika suala la mavazi, na hawataruhusu suala la mavazi litawale akili."—Ev 273.

Kuvaa kawaida, kuepuka kujionesha kwa vito na mapambo ya kila aina, vinakubaliana na imani yetu."—3T 366. Inafundishwa wazi katika Maandiko kwamba kuvaa vito ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Mtume Paulo anatuasa tuvae "mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani" (1 Tim. 2:9). Kuvaa mapambo na vito ni kutaka kuonekana kusikokubaliana na kujikana nafsi kwa Kikristo.

Katika baadhi ya nchi na utamaduni, desturi ya kuvaa pete ya arusi huchukuliwa kuwa ya lazima, na imekuwa ishara ya uadilifu katika akili za watu, na kwa hiyo haichukuliwi kuwa ni pambo. Katika hali hiyo hatuipingi desturi hiyo.

Tukumbuke kuwa mapambo ya nje hayaoneshi tabia ya kweli ya Kikristo, bali ni ule "utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu" (1 Pet. 3:3, 4). Inatupasa kuepuka utumiaji wa vipodozi visivyokubaliana na tabia njema na kanuni za adabu ya Kikristo.

Inatupasa kuzingatia usafi na mwenendo wa Kikristo tunapojitahidi kila wakati kumpendeza na kumwakilisha vyema Kristo Bwana wetu. Inawapasa wazazi wa Kikristo kuwaelekeza watoto wao wa kiume na wa kike kwa mifano, mafundisho na mamlaka, kuvaa kwa adabu na kwa hiyo kupata heshima na imani ya watu wanaowafahamu. Tuchukulie kuwa tumevaa vizuri tunapokidhi matakwa ya adabu kwa kuvaa mavazi ya kihafidhina yanayovutia.

**Usahili**

Usahili umekuwa sifa muhimu ya Kanisa tangu mwanzo wake. Inatupasa kuendelea kuwa watu walioitwa kuwa na maisha sahili. Kuongezeka kwa mbwembwe katika dini, siku zote huambatana na kuzorota kwa nguvu za kiroho. Kama "maisha ya Yesu yalivyokuwa yanaonesha tofauti kubwa" na maonesho na majivuno ya wakati wake (Ed 77), ndivyo usahili na nguvu ya ujumbe wetu inavyotakiwa kuwa na tofauti kubwa na maonesho ya siku hizi. Bwana anakataza "matumizi ya kufuja pesa yasiyo ya lazima kwa ajili ya ufahari na kujionesha."—TM 179. Sambamba na kanuni hizi, usahili na uangalifu katika matumizi ya pesa vinapasa kuambatana na mahafali zetu, arusi zetu na huduma zingine zote za kanisa.

**Vyombo vya Habari vya Kisasa**

Kama ilivyo miili yetu, utu wetu wa ndani unahitaji lishe bora kwa ajili ya kufanywa upya na kutiwa nguvu (2 Kor. 4:6). Akili zetu ndiyo kipimo cha utu wetu. Chakula cha akili zetu kina umuhimu mkubwa katika kujenga tabia na katika kutekeleza makusudi ya maisha yetu. Kwa sababu hiyo inatupasa kutathmini kwa makini sana mwenendo wa akili zetu. Mambo tunayoamua kusoma, kusikia, na kutazama iwe katika kitabu au jarida, redio au televisheni, intaneti au chombo kingine cha kisasa cha habari, huunda na kuathiri tabia zetu.

Vitabu na machapisho mengine ni kati ya nyenzo muhimu sana za elimu na utamaduni, lakini havina budi kuchaguliwa vyema na kutumiwa vizuri. Kuna machapisho mengi mazuri, lakini pia kuna mafuriko ya machapisho, mara nyingi yakiwa yanaonekana ya kuvutia sana, ambayo huharibu akili na uadilifu. Simulizi za visa vya hatari na ukosefu wa uadilifu, ziwe za kweli au riwaya, zikiwasilishwa kwa njia yo yote ile, hazifai kwa Mkristo wa umri wo wote.

Wale wanaoendekeza tabia ya kufuatila hadithi ya kusisimua wanalemaza tu uwezo wa akili zao na kuzifanya zikose sifa za kufikiri kwa kina na kufanya uchunguzi."—

CT 135. Pamoja na athari zingine mbaya zinazotokana na kusoma riwaya, tunaambiwa “huifanya nafsi isiweze kuyafikiria matatizo makubwa ya wajibu na hatima” na “huleta kutopenda majukumu muhimu katika maisha.”—CT 383.

Redio, televisheni na inteneti vimebadili kabisa hali yote ya dunia yetu na vimetufikisha mahali ambapo ni rahisi kukutana na maisha, mawazo na shughuli za ulimwengu mzima. Zinaweza kuwa nyenzo kubwa za elimu tunazoweza kuzitumia kukuza weledi wetu wa matukio ya ulimwengu na kufaidi mijadala muhimu na muziki bora kabisa.

Hata hivyo, kwa bahati mbaya vyombo vya siku hizi vya habari kwa umma vinaweza kuleta kwa hadhira zao takriban mfululizo wa maigizo na mambo mengine yenye mivuto isiyofaa na isiyoinua. Tusipokuwa na mipaka, vitaleta programu chafu katika nyumba zetu.

Usalama wetu na wa watoto wetu upo katika azma, ya kufuata ushauri wa mtume Paulo kwa msaada wa Mungu: “Hatimaye, … mambo yo yote yaliyo ya kweli … ya staha … ya haki … yaliyo safi kupendeza … yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo (Phil. 4:8).

**Starehe na Burudani**

Starehe ni kufanya upya uwezo wa mwili na akili kwa kukusudia. Akili yenye nguvu yenye afya haitahitaji burudani za kidunia bali itapata urejeshwaji wa nguvu katika burudani njema.

“Burudani nyingi maarufu katika ulimwengu siku hizi, hata kwa wale wanaodai kuwa Wakristo, zinatimiza makusudi yale yale yaliyokuwa yanatimizwa na zile za kipagani. Kuna chache sana kati ya hizo ambazo Shetani hazitumii kuangamiza watu. Kwa njia ya maigizo ameendelea kwa muda mrefu kuchochea tamaa na kutukuza tabia mbaya. Opera, pamoja na maonesho yake ya kupumbaza na muziki wa kutatanisha, dansi, meza ya karata, Shetani huvitumia vitu hivyo kuvunja vizuizi vya kanuni na kufungua milango kwa ajili ya kuendekeza anasa. Katika kila kusanyiko la anasa ambapo

ufahari huendelezwa au uchu huendekezwa, ambapo mtu hufanywa amsahau Mungu na kushindwa kuona maslahi ya milele, Shetani huizungushia roho mnyororo wake."—PP 459, 460. (tazama uk. 163, 164.)

Inatupasa kuepuka kila jambo linaloigiza, linalotumia vielelezo kuelezea au kudokeza dhambi na uhalifu wa mwanadamu—mauaji, uzinzi, unyanga'nyi na uovu kama huo ambao kwa sehemu kubwa umesababisha kuporomoka kwa maadili. Badala yake inatupasa kufurahia ulimwengu mkuu wa viumbe vya Mungu na uhusiano na mawakala wa kibinadamu na matendo ya Mungu.

Kucheza dansi kwa kujifurahisha ni aina nyingine ya burudani yenye mvuto mbaya. Burudani ya dansi … ni shule ya uharibifu, laana ya kutisha kwa jamii."—MYP 399. (Tazama 2 Kor. 6:15-18; 1 Yoh. 2:15-17; Yak. 4:4; 2 Tim. 2:19-22; Efe, 5:8-11; Col. 3:5-10.)

Burudani ni muhimu. Lakini badala ya kujiunga na idadi kubwa ya watu "wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu" (2 Tim. 3:4), hatuna budi kujitahidi kufanya urafiki wetu na burudani zetu ziwe za Kikristo na kikanisa.

**Muziki**

"Muziki uliwekwa kwa ajili ya kutimiza kusudi takatifu, kuinua mawazo kuelekea yale yaliyo safi, ya staha na yanayoinua na kuamsha katika moyo ibada na shukurani kwa Mungu."—PP 594. Yesu alikuwa akiwasiliana na mbingu kwa nyimbo."—DA 73.

Muziki ni moja ya sanaa za hali ya juu sana. Muziki mzuri hautupatii furaha tu, bali huziinua akili zetu na kukuza sifa zetu zilizo bora kabisa. Mara kwa mara Mungu amekuwa akitumia nyimbo za kiroho kugusa mioyo ya wenye dhambi kuwaleta katika toba. Kwa upande mwingine, muziki huvunja maadili na kututoa katika uhusiano wetu na Mungu.

Inatupasa kuwa waangalifu sana katika kuchagua muziki katika nyumba zetu, mikusanyiko ya kijamii, shule, na makanisa. Tuni yo yote, aina ya jazi, rock au aina mchanganyiko zinazohusiana na hizo, au lugha yo yote inayoelezea hisia za kijinga au zisizokuwa muhimu vitaepukwa.

**Hitimisho**

Tukisimama katikati ya hatari za siku za mwisho, tukibeba jukumu la kupeleka haraka ahadi ya wokovu kwa ulimwengu, na tukikabiliwa na hukumu ambayo itaishia kusimamishwa kwa haki Ulimwenguni, inatupasa kujitoa mwili, nafsi, na roho kwa Mungu, tukiazimu kudumisha viwango vya juu ya maisha ambavyo lazima vionekane kwa wale wanaongoja kurudi kwa Bwana wao.

SURA YA 13

# Ndoa, Kuachana na Kuoa/Kuolewa Tena

**Uhusiano wa Kijamii**

Mungu hutupatia silika yetu ya kijamii kwa ajili ya furaha na maslahi yetu. "Mawasiliano yetu ya pande mbili hupiga msasa uungwana wetu; kwa uhusiano wa kijamii, ujamaa hutokea na urafiki huanzishwa ambavyo husababisha umoja wa moyo na mazingira ya upendo ambayo hupendeza machoni pa Mungu.'—6T 172.

Uhusiano halali wa jinsia tofauti una manufaa kwa pande zote mbili. Uhusiano huo hauna budi kuendeshwa katika kiwango cha juu na kwa kuzingatia desturi zetu za kijamii zilizowekwa kwa ajili ya kutulinda. Shetani anakusudia kuzuia kila jambo jema, na upotoshaji wa mambo yaliyo bora kabisa, mara nyingi huleta yale yaliyo mabaya kabisa.

Sasa hivi viwango vinavyofanya uhusiano huu uwe salama na wa furaha vinaporomoka kwa kiwango cha kutisha. Ukiwa chini ya msukumo wa tamaa isiyodhibitiwa na kanuni za kimaadili na kidini, uhusiano kati ya jinsia tofauti kwa kiasi kikubwa umezorota na kuwa uhuru wa kila mtu kufanya anavyotaka, upotoshaji wa ngono, kujamiiana baina ya maharimu na unajisi wa watoto kingono.

Mamilioni wameviacha viwango vya tabia vilivyo katika Biblia na wanabadilisha hisia takatifu za ndoa kuwa matunda ya kusikitisha ya dhambi yaletayo majuto. Uovu huu hauharibu tu muundo wa jamii utokanao na familia, bali kusambaratika kwa familia pia huendeleza na kusababisha uovu huu na mwingine. Athari za kuharibika maisha ya watoto na vijana ni za kusikitisha. Athari zake kwa jamii huleta balaa na hujilimbikiza.

Uovu huu umekuwa wa wazi zaidi na unatishia viwango na makusudi ya nyumba ya Kikristo. Uzinzi, ponografia, udhalilishaji wa aina yo yote, (pamoja na udhalilishaji wa kingono kwa wanandoa,

watoto na wazee), kujamiiana baina ya maharimu, na desturi za ushoga na usagaji ni kati ya mambo yanayopotosha mpango wa awali uliowekwa na Mungu na yanaonesha kuporomoka kwa utu. Makusudi ya aya bayana za Maandiko (Tazama Kut. 20:14; Law. 18:22, 29; 20;13; 1 Kor. 6:9; 1 Tim. 1:10; Rum. 1:20-23) yanapokanushwa na maonyo yake yanapokataliwa kwa kuwekwa maoni ya wanadamu badala yake, wasiwasi na machafuko mengi hutokea. Tangu zama za kale na jamii za kale, siku zote mpango wa Shetani umekuwa kuwafanya watu wasahau kwamba Mungu ni Mwumbaji wao na kwamba alipowaumba wanadamu kwa mfano wake, aliwaumba wote "mwanamume na mwanamke" (Mwa. 1:27).

Ingawa Neno la Mungu linatuonya kuhusu athari zinazo zorotesha ulimwengu kupenda sana ngono na kutafuta anasa, Kristo alikuja kuzivunja kazi za Shetani na kuanzisha upya uhusiano wa wanadamu na Mwumbaji wao. Ingawa tulianguka katika Adamu na kuwa watumwa wa dhambi, tunapokuwa ndani ya Kristo tunapata msamaha kamili na haki ya kuchagua upya njia bora ya kufanywa upya kikamilifu. Kwa njia ya msalaba na uwezo wa Roho Mtakatifu, sote tunaweza kuwekwa huru dhidi ya nguvu ya desturi za dhambi tunaporejeshwa katika mfano wa Mwumbaji wetu.

Kama wazazi na viongozi wa kiroho wa vijana, inatupasa kuyaelewa matatizo yao kwa huruma, kujaribu kuwapa mazingira ya kijamii ambayo ni ya Kikristo, na kuwavuta kiroho ili tuweze kuwaambukiza viwango, msukumo na nguvu ya Ukristo.

Hata makosa ya wazazi wetu au watu wa rika letu yakiwa makubwa sana tuna wajibu na fursa ya kuvijua na kuvifuata viwango vya juu kabisa vya utu wa Kikristo. Tunaweza kujenga tabia ya Kikristo itakayotukinga na uovu na kutufanya tuwe na mvuto wa kutia moyo katika jamii kwa kusoma Biblia kwa kicho, kuelewa kwa kina mwenendo wa viumbe, kulinda kwa bidii nguvu na uwezo mtakatifu wa mwili, kuwa na azma thabiti, kudumu katika maombi na kuwatumikia wengine kwa dhati bila ubinafsi.

Mikusanyiko ya starehe ya vijana na hata wazee haina budi kuwa matukio ya ushirika wa furaha na uboreshaji wa nguvu za akili na nafsi, na siyo kwa ajili ya burudani za kipuuzi. Muziki mzuri, mazungumzo ya kutia moyo, kukariri mambo mema, picha au sinema zinazofaa, michezo iliyochaguliwa kwa uangalifu kwa ajili

ya umuhimu wake kielimu, na zaidi ya yote kuweka mipango na kuitumia kwa ajili ya kazi za kimisionari, vitabariki na kuimarisha maisha ya wote. Idara ya Huduma za Vijana ya Konferensi Kuu imechapisha mambo na mapendekezo ya vitendo yanayoweza kusaidia kwa ajili ya mwenendo wa mikusanyiko ya starehe na kwa ajili ya maelekezo katika uhusiano mwingine wa kijamii.

Kwa sehemu kubwa nyumba zetu ni mahali bora kabisa pa mikusanyiko ya starehe. Katika miji mikubwa ambapo haiwezekani kuwa na mikusanyiko ya aina hiyo majumbani na mahali ambapo hakuna kituo chetu wenyewe cha mambo ya jamii, inatupasa kuchagua mahali ambapo hapana mivuto inayoharibu viwango vya Kikristo, na si mahali ambapo kwa kawaida hutumika kwa burudani na michezo ya kibiashara, kama vile kumbi za starehe na viwanja vya kutelezea katika barafu, ambavyo vinaweza kuleta mazingira yaliyo kinyume na viwango vya Kikristo.

**Uangalizi**

Usimamizi, yaani kuchangamana kwa furaha na uchangamfu kwa watu wazima na vijana ni moja kati ya mivuto mizuri kabisa katika maisha ya watoto na vijana. "Kuna hatari kwamba wazazi na walimu … wanashindwa kuwa na uhusiano wa kutosha wa kijamii na watoto wao au wanafunzi."—CT 76. Ni wajibu wa kaya, shule na taasisi zetu zingine, kulinda maadili na sifa za wale waliowekwa chini yetu. Kama wazazi inatupasa kuunga mkono kwa nguvu sheria za taasisi zinazohudumia vijana na watoto wetu, na inatupasa kuweka ulinzi kama huo huo katika nyumba zetu. Kufanya jambo hilo liwezekane, inatupasa kujifunza kuwapokea marafiki wa watoto wetu. Lakini bado kwa sehemu kubwa ni wajibu wa vijana wenyewe kuufanya uangalizi uwe uhusiano wa heshima na furaha.

**Uchumba**

Uchumba unatambuliwa kama kipindi cha maandalizi ambapo mwanamume na mwanamke, waliopendana, hufahamiana zaidi wakijiandaa kwa ndoa tarajiwa.

"Wale wanaofikiria kuoana wapime kila hisia na kuangalia kila badiliko la tabia kwa yule wanayetaka kuunganisha naye hatima ya maisha yao. Kila hatua inayoelekea kwenye uhusiano wa ndoa

iambatane na adabu, usahili, uaminifu na makusudi ya dhati ya kumpendeza Mungu. Ndoa huathiri maisha ya baadaye katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao. Mkristo mwaminifu hawezi kufanya mipango ambayo Mungu hawezi kuiidhinisha."—MH 359.

Kutokufuata kanuni hizi katika uchumba wa Kikristo kunaweza kusababisha janga. Umoja wa mume na mke katika viwango na makusudi ni sharti la kuwa na ndoa yenye furaha na mafanikio. Tofauti za wahusika katika dini bila shaka zitaharibu furaha ya familia na kuleta machafuko, wasiwasi na kushindwa kulea watoto. Biblia inashauri, "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa" (2 Kor. 6:14).

Uhusiano wa familia ni wa karibu zaidi, ulio nyeti na mtakatifu zaidi kuliko mwingine wo wote duniani. Ulikusudiwa kuwa baraka kwa wanadamu. Na ni baraka kila mahali ambapo agano la ndoa hufanyika kwa kutumia akili, katika hofu ya Mungu, na kwa kuzingatia ipasavyo majukumu ya ndoa."—AH 18.

Ibada kwa Mungu, kushika Sabato, burudani, kujumuika, matumizi ya pesa, na ufundishaji wa watoto ni vipengele vya uhusiano wa familia wenye furaha. Kwa sababu tofauti katika maeneo haya mara nyingi zinaweza kuleta uzorotaji wa uhusiano huo, kuvunjika moyo, na hata kupoteza kabisa hali ya Ukristo, maandalizi ya kutosha ya ndoa hayana budi kujumuisha ushauri wa kichungaji kabla ya ndoa katika maeneo hayo.

"'Je! Watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?' Amo. 3:3. Furaha na mafanikio ya uhusiano wa ndoa vinategemea umoja wa wahusika; lakini kati ya anayeamini na asiyeamini kuna tofauti kubwa ya mambo wayapendayo, matakwa na makusudi. Wanatumikia mabwana wawili, ambao hawawezi kupatana. Hata misimamo ya mtu ikiwa safi na sahihi kiasi gani, mvuto wa mwenzi asiyeamini utakuwa na mwelekeo wa kumpeleka mbali na Mungu."—PP 174.

Kwa kawaida roho ya unabii inashauri dhidi ya ndoa kati ya "anayeamini na asiyeamini" na inatoa tahadhari zaidi dhidi ya kuungana na Wakristo wenzetu ambao "hawajaupokea ukweli wa wakati huu."—5T 364. Ndoa zina nafasi zaidi ya kudumu, na maisha ya ndoa kutimiza kusudi la Mungu kama mume na mke

wana umoja na wameunganishwa na maadili ya kiroho na mtindo wa maisha unaofanana. Kwa sababu hizo Kanisa linapinga ndoa kati ya Mwadventista wa Sabato na mshiriki wa dini nyingine na linataka wachungaji wake wasifungishe ndoa za aina hiyo.

Kanisa linatambua kwamba ni haki ya mtu binafsi kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu uchaguzi wa mwenzi wa ndoa. Hata hivyo, ni tumaini la Kanisa kwamba kama mshiriki atachagua mwenzi ambaye si mshiriki wa Kanisa, wenzi hao watatambua na kuelewa kuwa mchungaji wa kanisa la Waadventista wa Sabato aliyeahidi kusimamia kanuni zilizoelezwa hapo juu, hatatarajiwa kufungisha ndoa hiyo.

Mshiriki akiingia katika ndoa ya aina hiyo, kanisa halina budi kuonesha upendo na kujali kwa kusudi la kuwatia moyo wanandoa hao kuingia katika umoja kamili ndani ya Kristo.

## Ndoa

Ndoa ni jambo lililoanzishwa na Mungu mwenyewe kabla ya Anguko, wakati kila kitu, ikiwemo ndoa kilipokuwa "chema sana" (Mwa. 1: 31). "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja" (Mwa. 2:24). "Mungu alisherehekea ndoa ya kwanza. Kwa hiyo mwanzilishi wa deaturi hiyo ni Mwumbaji wa Ulimwengu. 'Ndoa na iheshimiwe'; ilikuwa moja kati ya zawadi za kwanza kabisa za Mungu kwa wanadamu, na ilikuwa moja kati ya desturi mbili ambazo Adamu alitoka nazo nje ya malango ya Paradiso baada ya kuanguka."—AH 25, 26.

Mungu alikusudia ndoa ya Adamu na Hawa kuwa mfano kwa ndoa za baadaye, na Kristo aliiunga mkono dhana yake ya mwanzo; "Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe" (Mat. 19:4-6). Ndoa, iliyoanzishwa na Mungu kwa njia hiyo, ni uhusiano wa watu wa jinsia tofauti kati ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja.

Ndoa ni azma ya maisha yote kwa mume na mke, kila mmoja kwa mwenzie na kati ya wanandoa hao na Mungu (Mk. 10:2-9); Rum. 7:2). Paulo anaonesha kuwa wajibu alionao Kristo kwa kanisa ni kielelezo cha uhusiano kati ya mume na mke (Efe. 5:31, 32). Mungu alikusudia ndoa iwe ya kudumu kama ulivo uhusiano wa Kristo na kanisa.

Kujamiiana katika ndoa ni zawadi takatifu ya Mungu kwa familia ya wanadamu. Ni sehemu muhimu ya ndoa, ambayo imehifadhiwa kwa ajili ndoa tu (Mwa. 2:24; Mit. 5:5-20). Kujamiiana kwa aina hiyo, ambako kumekusudiwa kufanyika kati ya mume na mke, huleta ukaribu, furaha, na usalama unaozidi kuongezeka siku zote, na huleta njia ya kukuza jamii ya wanadamu.

Umoja katika ndoa hupatikana kwa kuheshimiana na kupendana. Hakuna aliye juu ya mwingine (Efe. 5:5-28). "Ndoa, ambayo ni umoja wa maisha yote, ni ishara ya umoja kati ya Kristo na kanisa lake. Moyo ambao Kristo huuonesha kwa kanisa lake ndio moyo uwapasao mume na mke kuoneshana wao kwa wao."—7T 46. Neno la Mungu linakataza ghasia katika uhusiano baina ya watu (Mwa. 6:11, 13; Zab. 11:5; Isa. 58:4, 5; Rum. 13:10; Gal. 5:19-21). Nia ya Kristo ni kupenda na kupokea, kutafuta na kusaidia na kuwaimarisha wengine, kuliko kuwanyanyasa na kuwadhalilisha (Rum. 12:10; 14:19; Efe. 4:26; 5:28, 29; Kol. 3:8-14; 1 Thes. 5:11). Kwa wafuasi wa Kristo hakuna nafasi ya kudhibiti kwa vitisho na kutumia vibaya madaraka (Mat. 20:25-28; Efe. 6:4). Ghasia katika ndoa na familia ni machukizo. (Tazama AH 343).

"Mume au mke asidai kuwa mtawala. Bwana ameweka kanuni ya kuongoza katika suala hili. Inampasa mume kumpenda mke wake kama Kristo anavyolipenda kanisa. Na inampasa mke kumheshimu na kumpenda mume wake. Wote hawana budi kukuza moyo wa ukarimu, kudhamiria kutokumwudhi au kumkwaza mwingine."—7T 47.

Kuingia kwa dhambi kuriathiri sana ndoa. Adamu na Hawa walipofanya dhambi, walipoteza umoja ambao walikuwa wanaujua kati yao na Mungu na kati yao wao kwa wao (Mwa. 3:6-24). Uhusiano wao ukajaa hatia, aibu, lawama, na uchungu. Kila mahali ambapo dhambi inatawala, athari zake za kusikitisha kwa ndoa huwa

pamoja na faraka, kukosa uaminifu, dharau, unyanyasaji, upotoshaji wa ngono, ghasia, utengano, kuachana na talaka.

Ndoa zenye zaidi ya mume au mke mmoja pia ni ushahidi wa athari za dhambi kwa desturi ya ndoa. Ndoa kama hizo, japo zilikuwa zipo katika nyakati za agano la kale, hazipatani na mpango wa Mungu. Mpango wa Mungu kuhusu ndoa unataka watu wake wazishinde kawaida za utamaduni uliozoeleka zinazopingana na mtazamo wa Biblia.

Dhana ya Kikristo kuhusu ndoa inajumuisha mambo yafuatayo:

*Kiwango cha Mungu Kurejeshwa katika Kristo*—Katika kuukomboa ulimwengu kutoka katika dhambi na athari zake, Mungu anataka kurejesha ndoa katika kiwango chake cha awali. Jambo hili linatarajiwa katika maisha ya wale waliozaliwa mara ya pili katika ufalme wa Kristo, ambao mioyo yao inatakaswa na Roho Mtakatifu na ambao kusudi lao kubwa ni kumwinua Bwana Yesu Kristo (Tazama pia 1 Pet. 3:7; TMB 64.

*Umoja na Usawa Kurejeshwa katika Kristo*—Injili inasisitiza upendo na utii wa mume na mke kwa kila mmoja (1 Kor. 7:3, 4; Efe. 5:21). Kielelezo cha uongozi wa mwanamume ni upendo wa kujitoa mhanga na utumishi ambao Kristo huutoa kwa Kanisa (Efe. 5:24, 25). Petro na Paulo wote wanazungumzia hitaji la heshima katika uhusiano wa ndoa (1 Pet. 3:7; Efe. 5:22, 23).

*Neema Inapatikana kwa Wote*—Mungu anataka kuwarejesha katika uzima na kuwapatanisha na nafsi yake wote walioshindwa kufikia kiwango cha Mungu (1 Kor. 5:19). Hii ni pamoja na wale wenye uhusiano wa ndoa uliovunjika.

*Jukumu la Kanisa*—Musa katika Agano la Kale, na Paulo katika Agano Jipya walishughulikia matatizo yanayosababishwa na ndoa zilizovunjika (Kum. 24:1-5; 1 Kor. 7:11). Wote walishughulika na wale waliokuwa chini ya viwango vya Mungu kwa nia ya kuwasaidia na kuwaokomboa, huku wakidumisha na kuthibitisha kiwango. Vivyo hivyo, Kanisa la leo linatakiwa kudumisha na kuthibitisha kiwango cha Mungu kuhusu ndoa na wakati huo huo, kuwa jumuiya yenye kusamehe, kupatanisha, kuponya, likionesha huruma kunapotokea kuvunjika.

**Kuachana**

Kuachana ni kinyume cha makusudi ya awali ya Mungu katika kuanzisha ndoa (Mat. 19:3-8; Mk. 10:2-9), lakini Biblia haiko kimya kuhusu kuachana. Kwa kuwa kuachana kulitokea kama sehemu ya hali ya kuanguka ya mwanadamu, kanuni za Biblia zilitolewa ili kupunguza athari zilizosababishwa (Kum. 24:1-4). Kwa kawaida Biblia hujaribu kuiinua ndoa na kuzuia kuachana kwa kuelezea furaha ya upendo na uaminifu katika ndoa (Mit 5:18-20; Wim. 2:16; 4:9-5:1), kwa kuzungumzia uhusiano wa Mungu na watu wake unaofanana na ndoa (Isa. 54:5; Yer. 3:1), kwa kuzingatia uwezekano wa msamaha na kurejesha ndoa (Hos. 3:1-3), na kwa kuonesha chuki ya Mungu dhidi ya kuachana na mateso yanayosababishwa na kuachana (Mal. 2:15, 16). Yesu alirejesha mtazamo wa ndoa wa wakati wa uumbaji kuwa ndoa ni agano la maisha yote kati ya mwanamume na mwanamke na kati yao na Mungu (Mat. 19:4-6; Mk 10:6-9). Maelekezo mengi ya Biblia huunga mkono ndoa na hujaribu kurekebisha matatizo yanayoelekea kudhoofisha msingi wa ndoa (Efe. 5:21-33; Ebr. 134:4; 1 Pet. 3:7).

Ndoa imejengwa katika kanuni za upendo, uaminifu, upekee, kuaminiana, na kusaidiana kutoka kwa wanandoa wote wawili wakimtii Mungu (Mwa. 2:24; Mat. 19:6; 1 Kor. 13; Efe. 5:21-29; 1 Thes. 4:1-7). Kanuni hizi zikivunjwa, Maandiko yanakiri kwamba mazingira ya kusikitisha yanaweza kuharibu ndoa.

Neema ya Mungu ni tiba pekee ya athari za kuachana. Ndoa inapovunjika, wanandoa hao wa zamani hawana budi kuhimizwa kuchunguza hali yao na kutafuta mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yao. Mungu hutoa faraja kwa wale waliojeruhiwa. Mungu pia hupokea toba ya wale wanaofanya dhambi zinazoleta uharibifu mkubwa kabisa, hata zile zenye athari zisizorekebishika (2 Sam. 11; 12; Zab. 34:18; 86:5; Yoe. 2:12, 13; Yn 8:2-11; 1 Yoh. 1:9).

Maandiko yanatambua uzinzi na uasherati (Mat. 5:32) na kutelekezwa na mwenzi asiyeamini (1 Kor. 7:10-15) kama sababu za kuachana.

Hakuna fundisho la moja kwa moja katika Maandiko kuhusu kuoa/kuolewa tena baada ya kuachana. Hata hivyo, kuna kidokezo kikubwa katika maneno ya Yesu katika Mathayo 19:9 ambacho kinaweza kuruhusu kuoa/kuolewa tena kwa yule aliyekuwa

mwaminifu lakini mwenzi wake amekuwa si mwaminifu kwa nadhiri ya ndoa.

**Msimamo wa Kanisa juu ya Kuachana na Kuoa/Kuolewa Tena**

Kanisa, kwa kutambua fundisho la Biblia juu ya ndoa, linajua kuwa uhusiano wa ndoa uko chini ya kiwango katika ndoa nyingi. Tatizo la kuachana na kuoa/kuolewa tena linaweza kuonekana katika uhalisi wake likitazamwa kwa mtazamo wa Mungu na kulinganishwa na mambo yalivyokuwa katika Bustani ya Edeni.

Kusudi la mpango mtakatifu wa Mungu wa kuumba ulimwengu wetu lilikuwa kuumba viumbe katika mfano wake ambao wangezaliana na kuijaza nchi na kuishi pamoja katika usafi, mwafaka na furaha. Alimfanya Hawa kutoka katika ubavu wa Adamu na kumtoa kwa Adamu awe mke wake. Hivyo ndivyo ndoa ilivyoanzishwa—Mungu, mwanzilishi wa desturi hiyo na mfungishaji wa ndoa hiyo ya kwanza. Baada ya Bwana kumwonesha Adamu kuwa Hawa alikuwa mfupa katika mifupa yake na nyama katika nyama zake hasa, kusingeweza kutokea mashaka katika akili yake kuhusu wao kuwa mwili mmoja. Wala kusingeweza kutokea shaka kuhusu vile Mungu alivyokuwa amekusudia nyumba yao idumu milele.

Kanisa linashikilia mtazamo huo kuhusu ndoa na kaya bila kusita hata kidogo, likiamini kwamba kuushusha kwa namna yo yote mtazamo huu ni kushusha kiwango cha Mungu. Imani ya kwamba ndoa ilianzishwa na Mungu imejengwa katika Maandiko Matakatifu. Kwa sababu hiyo, fikra na hoja zote katika eneo hili linalosumbua la kuachana na kuoa/kuolewa tena hazina budi kulinganishwa na kiwango kitakatifu kilichooneshwa katika Edeni.

Kanisa linakubaliana na sheria ya Mungu na pia linakubaliana na rehema ya Mungu isameheyo. Katika hofu ya Mungu, Kanisa linaweka hapa kanuni na taratibu ambazo hazina budi kutumika katika suala hili la ndoa, kuachana na kuoa/kuolewa tena.

Ingawa ndoa ilifungwa kwa mara ya kwanza na Mungu peke yake, inatambuliwa kwamba sasa hivi watu wanaishi chini ya serikali za kiraia; kwa hiyo, ndoa ina mtazamo wa Mungu na wa kiserikali. Mtazamo wa Mungu unaongozwa na sheria za Mungu na ule wa serikali unaongozwa na sheria za nchi.

Sambamba na mafundisho hayo, matamko yafuatayo yanaonesha msimamo wa kanisa:

Yesu aliposema, "Mwanadamu asiwatenganishe," aliweka kanuni ya mwenendo kwa Kanisa, katika kipindi cha neema, ambayo haina budi kuwa juu ya sheria zote za serikali zitakazokwenda nje ya fasiri yake ya sheria hiyo ya Mungu inayoongoza uhusiano wa ndoa. Hapa alitoa kanuni ambayo wafuasi wake hawana budi kuifuata hata kama serikali au desturi iliyopo inatoa uhuru mkubwa zaidi. "Katika hubiri lake la mlimani Yesu alisema wazi kwamba haiwezekani kuwa na kuvunjika kwa uhusiano wa ndoa, isipokuwa kwa sababu ya uvunjaji wa nadhiri ya ndoa."—TMB 63. (Pia tazama Mat. 5:32; 19:9.)

Uvunjaji wa nadhiri ya ndoa kwa ujumla umechukuliwa kuwa na maana ya uzinzi au uasherati. Hata hivyo, neno la Agano Jipya linalomaanisha uasherati linajumuisha ukiukaji mwingine kadhaa katika ngono. (1 Kor. 6:9; 1 Tim. 1:9, 10; Rum. 1:24-27). Kwa hiyo, upotoshaji wa ngono, ikiwa pamoja na kujamiiana kati ya maharimu, kunajisi watoto kingono, na tabia za kishoga vinatambuliwa pia kama matumizi mabaya ya uwezo wa kujamiiana na ukiukaji wa kusudi la Mungu katika ndoa. Kwa hiyo mambo hayo ni sababu halali za kutengana au kuachana.

Ingawa Maandiko yanaruhusu kuachana kwa sababu zilizotajwa hapo juu, ikiwa ni pamoja na kutelekezwa na mwenzi asiyeamini (1 Kor. 7:10-15), kanisa pamoja na wale wanaohusika hawana budi kufanya juhudi za dhati kuleta mapatano, wakiwasihi wanandoa hao kuoneshana moyo kama wa Kristo wenye kusamehe na kurejesha. Kanisa linatakiwa kushughulika na wanandoa hao kwa moyo wa upendo na ukombozi ili kuwasaidia katika mchakato wa kupatana

Endapo mapatano hayatafikiwa, yule aliyekuwa mwaminifu kwa mwenzi aliyevunja nadhiri ya ndoa ana haki ya kibiblia kupata talaka na pia kuoa/kuolewa tena.

Mwanandoa aliyevunja nadhiri ya ndoa (Tazama sehemu ya 1 na ya 2 hapo juu) atastahili marudi toka kwa kanisa mahalia. (tazama uk. 61-67.) Akitubu kwa dhati, mwanandoa huyo anaweza kuwekwa chini ya karipio kwa muda utakaotajwa badala ya kuondolewa katika ushirika wa kanisa. Mwanandoa asiyeonesha ushahidi wa toba kamili na ya dhati ataondolewa katika ushirika. Kama kosa

hilo limeleta aibu kwa kazi ya Mungu, kanisa linaweza kumwondoa mtu huyo katika ushirika ili kudumisha viwango vyake vya juu na jina lake jema.

Yo yote kati ya aina hizo za marudi itatumika na kanisa katika namna ambayo itakuwa inajaribu kutimiza makusudi mawili ya marudi—kurekebisha na kukomboa. Katika injili ya Kristo, sehemu ya ukombozi katika marudi siku zote huhusiana na badiliko halisi la mkosaji na kuwa kiumbe kipya katika Yesu Kristo.

Mwanandoa akivunja nadhiri ya ndoa na akaachika, hana haki ya kimaadili ya kuoa/kuolewa na mtu mwingine wakati yule mwanandoa aliyekuwa mwaminifu kwa ndoa yao anaendelea kuishi bila kuoa/kuolewa na anaendelea kuwa safi. Mtu atakayefanya hivyo ataondolewa katika ushirika. Mtu atakayeoana naye akiwa mshiriki, pia ataondolewa katika ushirika.

Inatambuliwa kuwa wakati mwingine uhusiano wa ndoa unaweza kuzorota kufikia mahali ambapo ni bora kwa mume na mke kutengana. "Lakini kwa wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila ni Bwana, mke asiachane na mumewe; lakini ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, na apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe" (1 Kor. 7:10, 11). Mara nyingi utunzaji wa watoto, mpangilio wa haki za mali au hata ulinzi binafsi unaweza kulazimu badiliko la hali ya ndoa. Katika hali kama hizo inaweza kuruhusiwa, katika baadhi ya nchi, kutengana kisheria. Hata hivyo, katika maeneo kadhaa kutengana huko kunaweza kufanyika kwa talaka tu.

Kutengana au kuachana kutakakotokana na sababu kama vile kipigo, au ambapo "uvunjaji wa nadhiri ya ndoa" (Tazama sehemu ya 1 na ya 2 hapo juu) hauhusiki, hakumpi ye yote haki ya kimaandiko kuoa/kuolewa tena, isipokuwa kama wakati huo yule mwingine ameoa/ameolewa tena, amefanya uzinzi au uasherati, au amekufa. Mshiriki aliyeachana kwa njia hiyo akioa/akiolewa bila sababu hizi za kibiblia, ataondolewa katika ushirika, na yule atakayeoana naye, kama ni mshiriki, ataondolewa pia katika ushirika. (tazama uk. 61-64.)

Mwanandoa aliyevunja nadhiri ya ndoa na akaachika na kuondolewa katika ushirika na ambaye ameoa/ameolewa tena, au mtu ambaye ameachika kwa sababu tofauti na zile zilizoelezwa

katika sehemu ya 1 na ya 2 hapo juu na akaoa/akaolewa tena na ambaye ameondolewa katika ushirika, atahesabiwa kuwa hastahili kuwa mshiriki isipokuwa kama inavyoelezwa hapa chini.

Agano la ndoa si takatifu tu, bali pia linaweza kuwa changamano zaidi, kwa mfano, pale linapohusisha watoto. Kwa sababu hiyo, katika ombi la kurejeshwa katika ushirika, uwezekano alio nao mtu aliyetubu unaweza kuwa mdogo sana. Kabla ya uamuzi wa mwisho kufanywa na kanisa, ombi la kurejeshwa litaletwa na kanisa mbele ya kamati ya konferensi, kupitia kwa mchungaji au kiongozi wa mtaa kwa ajili ya ushauri na mapendekezo juu ya hatua ambazo aliyetubu/waliotubu anaweza/wanaweza kuchukua ili arejeshwe/warejeshwe.

Kurejeshwa katika ushirika kwa wale walioondolewa kwa sababu zilizotolewa katika sehemu zilizotangulia, kwa kawaida utafanyika kwa msingi wa kubatizwa tena. (tazama uk. 50, 66, 67.)

Mtu aliyeondolewa katika ushirika akirejeshwa katika ushirika, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 8, kuwe na uangalifu mkubwa kulinda umoja na mwafaka wa kanisa kwa kutokumpa mtu huyo jukumu la uongozi, hasa katika kazi inayohitaji kuwekewa mikono, isipokuwa kwa ushauri wa kina na uongozi wa konferensi.

Hakuna mchungaji mwenye haki ya kufungisha ndoa ya mtu ye yote anayeoa/anayeolewa tena, ambaye hana haki ya kimaandiko kulingana na maelezo ya ibara zilizotangulia.

**Huduma ya Kanisa Mahalia kwa Familia**

Kanisa kama chombo cha ukombozi cha Kristo halina budi kuhudumia washiriki wake katika mahitaji yao yote na kumlea kila mtu ili wote wapate kukua na kuwa na Ukristo uliokomaa. Jambo hili ni bayana hasa washiriki wanapokabiliwa na uamuzi wa maisha yote kama vile ndoa na matukio ya kusikitisha ya kuachana. Ndoa ya watu wawili inapokuwa katika hatari ya kuvunjika, kila juhudi ifanyike na wanandoa pamoja na wale wanaowahudumia kanisani au katika familia, kuleta mapatano yaliyo sambamba na kanuni za Mungu za kusuluhisha uhusiano ulioharibika. (Hos. 3:1-3; 1 Kor. 7:10, 11; 13:4-7; Gal. 6:1).

Machapisho yanayoweza kusaidia washiriki katika kujenga nyumba imara ya Kikristo yanapatikana kupitia kanisa au taasisi

zingine za kanisa. Machapisho hayo ni pamoja na: (1) programu za maelekezo kwa watu wanaochumbiana wakitarajia kuoana, (2) programu za mafunzo kwa wanandoa pamoja na familia zao, na (3) programu za kusaidia familia zilizovunjika na watu walioachika.

Msaada wa kichungaji ni muhimu katika eneo la mafunzo na maelekezo katika suala la ndoa, na kusuluhisha na kurejesha katika suala la kuachana. Jukumu la kichungaji katika suala la kuachana ni la kinidhamu na kusaidia pia. Jukumu hilo ni pamoja na kutoa taarifa husika, ambazo zinaweza kuwa nyeti na zinazotakiwa kushughulikiwa kwa busara kubwa. Hata hivyo, suala hili la kimaadili peke yake halitoshi kuwa kigezo cha kuepuka hatua za marudi zilizoelezwa katika sehemu 1-11 hapo juu.

Kama vile Mungu asamehevyo, washiriki wanatakiwa kusamehe na kuwapokea wale waliokosa (Isa. 54:5-8; Mat. 6:14, 15; Efe. 4:32). Biblia inahimiza uvumilivu, huruma na msamaha katika kuwalea Kikristo wale waliokosa (Matt. 18:10-20; Gal. 6:1, 2). Wakati watu fulani wakiwa katika marudi, ama kwa karipio au kwa kuondolewa katika ushirika, kanisa kama chombo cha Mungu cha utume, litafanya kila juhudi kudumisha mawasiliano ya kuwatunza na kuwalea kiroho

SURA YA 14

# Imani za Msingi za Waadventista wa Sabato

Waadventista wa Sabato wanaikubali Biblia kama kanuni yao pekee na wanashika imani kadhaa za msingi kama mafundisho ya Maandiko Matakatifu. Imani hizi, kama zinavyoelezwa hapa, zinaunda ufahamu na maelezo ya kanisa ya mafundisho ya Biblia. Mabadiliko ya maelezo haya yanaweza kutarajiwa katika kikao rasmi cha Konferensi Kuu wakati Kanisa linapoongozwa na Roho Mtakatifu katika weledi mkubwa zaidi wa ukweli wa Biblia au linapopata lugha bora zaidi ya kuelezea mafundisho ya Neno Takatifu la Mungu.

**1.** *Maandiko Matakatifu*

Maandiko Matakatifu, Agano la Kale na Jipya, ni Neno la Mungu lililoandikwa, lililotolewa kwa ufunuo wa Mungu kwa njia wa watu watakatifu wa Mungu ambao walinena na kuandika kama walivyokuwa wanaongozwa na Roho Mtakatifu. Katika Neno hili, Mungu amempatia mwanadamu ujuzi unaohitajika kwa ajili ya wokovu. Maandiko Matakatifu ni ufunuo wa mapenzi ya Mungu usio na makosa. Ni kipimo cha tabia, kipimo cha hali ya kiroho, na chombo cha kubainisha mafundisho na kumbukumbu inayoweza kuaminiwa ya matendo ya Mungu katika historia. (2 Pet. 1:20, 21; 2 Tim. 3:16, 17; Zab. 119:105; Mit. 30:5, 6; Isa. 8:20; Yn. 17:17; 1 Thes. 2:13; Ebr. 4:12.)

2. *Utatu*

Kuna Mungu mmoja: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, umoja wa Nafsi Tatu za milele. Mungu hapatikani na mauti, ni mwenye uwezo wote, anajua yote, yuko juu ya yote na yupo wakati wote. Yeye hana ukomo na yuko nje ya uwezo wa mwanadamu kuelewa,

lakini anajulikana kwa kujifunua yeye mwenyewe. Wakati wote anastahili kuabudiwa, kupendwa sana na kutumikiwa na viumbe wote. (Kum. 6:4; Mat. 28:19; 2 Kor. 13:14; Efe. 4:4-6; 1 Pet 1:2; 1 Tim. 1:17; Ufu. 14:7.)

**3.** *Baba*

Mungu Baba wa milele ni Mwumbaji, Chanzo, Mfadhili na Mtawala wa viumbe vyote. Ni mwenye haki na mtakatifu, mwenye huruma na amejaa neema, si mwepesi wa hasira, na amejaa upendo na uaminifu thabiti. Sifa na uwezo unaoonekana katika Mwana na Roho Mtakatifu, pia ni ufunuo wa Baba. (Mwa. 1:1; Ufu. 4:11; 1 Kor. 15:28; Yn. 3:16; 1 Yoh. 4:8; 1 Tim. 1:17; Kut. 34:6, 7; Yn. 14:9.)

***4. Mwana***

Mungu Mwana wa milele alifanyika mwili katika Yesu Kristo. Kwa njia yake, vitu vyote viliumbwa, tabia ya Mungu hudhihirishwa, wokovu wa wanadamu umefanyika, na ulimwengu unahukumiwa. Mungu wa kweli daima, alifanyika mwanadamu pia, yaani Yesu aliye Kristo. Alitungwa mimba na bikira Mariamu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Aliishi na kujaribiwa kama mwanadamu, lakini alionesha haki na upendo wa Mungu. Kwa miujiza yake alidhihirisha uwezo wa Mungu na alithibitishwa kuwa Masihi aliyekuwa ameahidiwa. Aliteseka na kufa msalabani kwa hiari kwa ajili ya dhambi zetu na kwa niaba yetu, alifufuliwa kutoka kwa wafu, na akapaa kwenda kuhudumu katika patakatifu pa mbinguni kwa ajili yetu. Atakuja tena katika utukufu kwa ajili ya ukombozi wa mwisho wa watu wake na kufanya upya mambo yote. (Yn. 1:1-3, 14; Kol. 1:15-19; Yn. 10:30; 14:9; Rum. 6:23; 2 Kor. 5:17-19; Yn. 5:22; Luk. 1:35; Flp. 2:5-11; Ebr. 2:9-18; 1 Kor. 15:3, 4; Ebr. 8:1, 2; Yn. 14:13.)

*5. Roho Mtakatifu*

Mungu Roho wa milele alishiriki pamoja na Baba na Mwana katika Uumbaji, kufanyika mwili na ukombozi. Aliwaongoza waandishi wa Maandiko. Aliyajaza uwezo maisha ya Kristo.

Huwavuta na kuwasadikisha wanadamu; na wanaochukua hatua huwafanya upya na kuwabadilisha wawe katika mfano wa Mungu. Alitumwa na Baba na Mwana ili awe na watoto wake, hutoa karama za roho kwa kanisa, hulipatia kanisa uwezo wa kumshuhudia Kristo na huongoza na kuwatia watu katika kweli yote sambamba na Maandiko. (Mwa. 1:1, 2; Luk. 1:35; 4:18; Mdo. 10:38; 2 Pet. 1:21; 2 Kor. 3:18; Efe. 4:11, 12; Mdo 1:8; Yn. 14:16-18, 26; 15:26, 27; 16:7-13.)

***6. Uumbaji***

Mungu ni Mwumbaji wa vitu vyote, na katika Maandiko ameelezea kisa halisi cha shughuli yake ya uumbaji. Kwa siku sita Bwana "alizifanya mbingu na nchi" na viumbe vyote hai vilivyo juu ya nchi, na akapumzika siku ya saba ya lile juma la kwanza. Kwa hiyo aliianzisha Sabato kama kumbukumbu ya kudumu ya kazi yake ya kuumba iliyokuwa imekamilika. Mwanamume na mwanamke wa kwanza waliumbwa kwa mfano wa Mungu kama kipeo cha kazi ya uumbaji, walipewa utawala wa ulimwengu na wakapewa jukumu la kuutunza. Dunia ilipomalizika kuumbwa ilikuwa "njema sana," ilikuwa inatangaza utukufu wa Mungu. (Mwa. 1; 2; Kut. 20:8-11; Zab. 19:1-6; 33:6, 9; 104; Ebr. 11:3.)

***7. Silika ya Mwanadamu***

Mwanamume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu wakiwa na ubainifu, yaani uwezo na uhuru wa kufikiri na kutenda. Ingawa waliumbwa kama viumbe huru, kila mmoja ni umoja wa mwili, akili na roho, akimtegemea Mungu kwa ajili ya uhai na kila kitu. Wazazi wetu wa kwanza walipomwasi Mungu, waliikana hali yao ya kumtegemea na wakaanguka kutoka katika cheo cha juu chini ya Mungu. Mfano wa Mungu ndani yao uliharibika na wakawa wanapatikana na mauti. Wazao wao wanakuwa na silika hiyo hiyo iliyoanguka pamoja na athari zake. Wanazaliwa wakiwa na udhaifu na mwelekeo wa uovu. Lakini Mungu aliupatanisha ulimwengu na nafsi yake katika Kristo, na kwa njia ya Roho wake, huwarejeshea wanadamu wanaotubu sura ya Mwumbaji wao. Wakiwa wameumbwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu wanatakiwa kumpenda na kupendana wao kwa wao, na kuyatunza mazingira

yao. (Mwa. 1:26-28; 2:7; Zab. 8:4-8; Mdo. 17:24-28; Mwa. 3; Ps. 51:5; Rum. 5:12-17; 2 Kor. 5:19, 20; Zab. 51:10; 1 Yoh. 4:7, 8, 11, 20; Mwa. 2:15.)

### *8. Pambano Kuu*

Wanadamu wote sasa wako katika pambano kuu kati ya Kristo na Shetani kuhusu tabia ya Mungu, Sheria yake, na utawala wake juu ya Ulimwengu. Mgogoro huu ulianzia mbinguni wakati kiumbe aliyekuwa ameumbwa, akiwa na uhuru wa kuamua, alipokuwa Shetani, yaani hasimu wa Mungu, kwa sababu ya kujikweza, akaongoza sehemu ya malaika katika uasi. Alianzisha moyo wa uasi katika ulimwengu huu alipowafanya Adamu na Hawa waingie dhambini. Dhambi hii ya wanadamu ilisababisha kuharibika kwa sura ya Mungu ndani ya wanadamu, kuharibika kwa utaratibu wa ulimwengu uliokuwa umeumbwa, na maangamizi yalitokea wakati wa gharika iliyokumba ulimwengu mzima. Ulimwengu huu, ukitazamwa na viumbe wote, ukawa uwanja wa pambano la Ulimwengu, ambalo katika matokeo yake, upendo wa Mungu hatimaye utathibitishwa. Ili kuwasaidia watu wake katika pambano hili, Kristo humtuma Roho Mtakatifu na wale malaika watiifu wawaongoze, wawalinde, na kuwadumisha katika njia ya wokovu. (Ufu. 12:4-9; Isa. 14:12-14; Eze. 28:12-18; Mwa. 3; Rum. 1:19-32; 5:12-21; 8:19-22; Mwa. 6-8; 2 Pet. 3:6; 1 Kor. 4:9; Ebr. 1:14.)

### *9. Maisha, Kifo na Ufufuo wa Kristo*

Katika maisha ya Kristo yaliyokuwa ya utii mkamilifu kwa Mapenzi ya Mungu, katika mateso, kifo na ufufuo wake, Mungu alitoa njia pekee ya upatanisho kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu, ili wale watakaoupokea upatanisho huo kwa imani wawe na uzima wa milele, na viumbe wote waelewe vizuri zaidi upendo mtakatifu wa Mwumbaji, usio na kikomo. Upatanisho huu mkamilifu huidhihirisha haki ya sheria ya Mungu na uzuri wa tabia yake, kwani huihukumu dhambi yetu na wakati huo huo hutoa njia ya msamaha kwa ajili yetu. Kifo cha Kristo ni cha badala na cha fidia, kiletacho upatanisho na badiliko. Ufufuo wa Kristo hutangaza ushindi wa Mungu dhidi ya nguvu za uovu, na kwa wale wanaoupokea upatanisho huo huwahakikishia ushindi wao wa mwisho dhidi ya

dhambi na mauti. Unatangaza ukuu wa Yesu Kristo, ambaye mbele yake kila goti, mbinguni na duniani, litapigwa. (Yn. 3:16; Isa. 53; 1 Pet. 2:21, 22; 1 Kor. 15:3, 4, 20-22; 2 Kor. 5:14, 15, 19-21; Rum. 1:4; 3:25; 4:25; 8:3, 4; 1 Yoh. 2:2; 4:10; Kol. 2:15; Flp. 2:6-11.)

***10. Kupata Wokovu***

Kwa sababu ya upendo na rehema zisizo na ukomo, Mungu alimfanya Kristo, asiye jua dhambi, kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili katika yeye tupate kufanywa wenye haki. Kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu huwa tunahisi hitaji letu, tunakiri hali yetu ya dhambi, tunatubu makosa yetu, na kumwamini Yesu kama Bwana na Kristo, kama mbadala na kielelezo. Imani hii ipokeayo wokovu huja kwa uwezo wa Mungu ulio katika Neno pamoja na karama ya neema ya Mungu. Kwa njia ya Kristo huwa tunahesabiwa haki, tunafanywa kuwa wana na binti za Mungu na tunakombolewa kutoka katika utawala wa dhambi. Kwa njia ya Roho Mtakatifu huwa tunazaliwa upya na kutakaswa; Roho huzifanya upya nia zetu, huiandika sheria ya Mungu katika mioyo yetu na huwa tunapewa uwezo wa kuishi maisha matakatifu. Tukikaa ndani yake tunakuwa washiriki wa silika ya Mungu na kuwa na uhakika wa wokovu sasa na katika hukumu. (2 Kor. 5:17-21; Yn. 3:16; Gal. 1:4; 4:4-7; Tit. 3:3-7; Yn. 16:8; Gal. 3:13, 14; 1 Pet. 2:21, 22; Rum. 10:17; Luk. 17:5; Mk. 9:23, 24; Efe. 2:5-10; Rum. 3:21-26; Kol. 1:13, 14; Rum. 8:14-17; Gal. 3:26; Yn. 3:3-8; 1 Pet. 1:23; Rum. 12:2; Ebr. 8:7-12; Eze. 36:25-27; 2 Pet. 1:3, 4; Rum. 8:1-4; 5:6-10.)

***11. Kukua katika Kristo***

Kwa kifo chake pale msalabani Yesu alizishinda nguvu za uovu. Yeye ambaye alizitiisha roho za pepo wakati wa huduma yake duniani amezivunja nguvu zao na kufanya maangamizi yao ya mwisho yawe ya uhakika. Tunapotembea naye katika amani, furaha na uhakika wa upendo wake, ushindi wa Yesu hutupatia ushindi dhidi ya nguvu za uovu zinazotaka kututawala. Sasa Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu na kutuwezesha. Tukijitoa wakati wote kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi wetu, tunawekwa huru dhidi ya matendo yetu ya nyuma. Hatuishi tena katika giza, hofu ya nguvu za uovu, ujinga, na kukosa maana katika maisha yetu

ya mwanzo. Katika uhuru huu mpya ndani ya Kristo, tunatakiwa kukua na kufanana naye katika tabia, tukiongea naye kila siku katika maombi, tukijilisha Neno lake, tukitaamali kuhusu Neno hilo na majaliwa yake, tukiimba sifa zake, tukikusanyika pamoja kumwabudu na kushiriki katika utume wa Kanisa. Tunapojitoa katika utumishi wa upendo kwa wanaotuzunguka na katika kushuhudia wokovu wake, kuwepo kwake pamoja nasi kila wakati kwa njia ya Roho huubadili kila wakati na kila kazi kuwa tukio la kiroho. (Zab. 1:1, 2; 23:4; 77:11, 12; Kol. 1:13, 14; 2:6, 14, 15; Luke 10:17-20; Eph. 5:19, 20; 6:12-18; 1 Thes. 5:23; 2 Peter 2:9; 3:18; 2 Kor. 3:17, 18; Flp. 3:7-14; 1 Thes. 5:16-18; Mat. 20:25-28; Yn. 20:21; Gal. 5:22-25; Rum. 8:38, 39; 1 Yoh. 4:4; Ebr. 10:25.)

### *12. Kanisa*

Kanisa ni jumuiya ya waumini wanaomkiri Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Sambamba na watu wa Mungu wakati wa Agano la Kale, tunatakiwa kutoka ulimwenguni; na kuungana pamoja kwa ajili ya ibada, kwa ajili ya ushirika, kwa ajili kujifunza Neno la Mungu, kwa ajili ya kuadhimisha Meza ya Bwana, kwa ajili ya huduma kwa wanadamu na kwa ajili ya kuitangaza injili ulimwenguni kote. Kanisa linapata mamlaka yake kutoka kwa Kristo, ambaye ni Neno aliyefanyika mwili, na kutoka katika Maandiko ambayo ni Neno lililoandikwa. Kanisa ni familia ya Mungu; iliyoasiliwa naye kama watoto wake, washiriki wake huishi katika msingi wa Agano Jipya. Kanisa ni mwili wa Kristo, jumuiya ya kiimani ambayo Kristo mwenyewe ni kichwa chake. Kanisa ni bibi arusi ambaye Kristo alimfia ili amtakase na kumsafisha. Atakaporudi na ushindi, atajipatia kanisa tukufu, yaani waaminifu kutoka vizazi vyote, walionunuliwa kwa damu yake, wasio na doa wala kunyanzi, bali watakatifu wasio na waa. (Mwa. 12:3; Mdo. 7:38; Efe. 4:11-15; 3:8-11; Mat. 28:19, 20; 16:13-20; 18:18; Efe. 2:19-22; 1:22, 23; 5:23-27; Kol. 1:17, 18.)

### *13. Waliosalia na Utume Wao*

Kanisa la Ulimwengu linaundwa na wote wanaomwamini Kristo kwa dhati, lakini katika siku za mwisho, kipindi ambacho ni cha uasi kila mahali, kuna watu waliosalia ambao wameitwa ili

wazishike amri za Mungu na imani ya Yesu. Watu hawa waliosalia hutangaza kuja kwa saa ya hukumu, hutangaza wokovu kwa njia ya Kristo na hutangaza kukaribia kwa ujio wake. Utangazaji huu unawakilishwa na wale malaika watatu wa Ufunuo 14; unakwenda sambamba na kazi ya hukumu kule mbinguni na huleta kazi ya toba na matengenezo duniani. Kila muumini anatakiwa kuwa na sehemu mahususi katika ushuhuda huu wa ulimwengu mzima. (Ufu. 12:17; 14:6-12; 18:1-4; 2 Kor. 5:10; Yud. 3, 14; 1 Pet. 1:16-19; 2 Pet. 3:10-14; Ufu. 21:1-14.)

### *14. Umoja katika Mwili wa Kristo*

Kanisa ni jumuiya moja yenye washiriki wengi walioitwa kutoka kila taifa, kabila, lugha na jamaa. Sisi ni viumbe vipya katika Kristo; tofauti za jamii, utamaduni, elimu na utaifa na tofauti kati ya walio juu na walio chini, matajiri na maskini, wanaume na wanawake haziwezi kutugawa. Tuko sawa katika Kristo ambaye, kwa Roho mmoja ametufunga katika ushirika na yeye, na sisi kwa sisi; inatupasa kuhudumu na kuhudumiwa bila upendeleo au kusitasita. Kwa njia ya ufunuo wa Yesu Kristo katika Maandiko tuna imani moja na tumaini moja, na hutoa ushuhuda mmoja kwa wote. Umoja huu unatokana na umoja wa Mungu wa utatu, ambaye ametuasili tuwe watoto wake. (Rum. 12:4, 5; 1 Kor. 12:12-14; Mat. 28:19, 20; Zab. 133:1; 2 Kor. 5:16, 17; Mdo. 17:26, 27; Gal. 3:27, 29; Kol. 3:10-15; Efe. 4:14-16; 4:1-6; Yn. 17:20-23.)

### *15. Ubatizo*

Kwa njia ya ubatizo huwa tunakiri imani yetu kwa kifo na ufufuo wa Yesu Kristo, na kushuhudia juu ya kifo chetu kwa dhambi na juu ya kusudi letu la kutembea katika upya wa uzima. Kwa hiyo tunamkiri Kristo kama Bwana na Mwokozi wetu, tunakuwa watu wake, na tunapokelewa na kanisa lake kama washiriki. Ubatizo ni ishara ya muungano wetu na Kristo, yaani msamaha wa dhambi zetu, na kumpokea Roho Mtakatifu. Ubatizo hufanyika kwa kuzamishwa katika maji na unategemea kukiri imani kwa Yesu na ushahidi wa toba ya dhambi. Hufuata baada ya kujifunza Maandiko Matakatifu na kuyakubali mafundisho yake. (Rum. 6:1-6; Kol. 2:12, 13; Mdo 16:30-33; 22:16; 2:38; Mat. 28:19, 20.)

### *16. Meza ya Bwana*

Meza ya Bwana ni kushiriki katika ishara za mwili na damu ya Yesu kama udhihirisho wa imani kwake, aliye Bwana na Mwokozi wetu. Katika tukio hili la ushirika, Kristo huwa anakuwepo kukutana na kuwatia nguvu watu wake. Tunaposhiriki, tunatangaza kwa furaha mauti ya Bwana mpaka atakapokuja tena. Maandalizi ya Meza hiyo ni pamoja na kujitathmini, toba na kuungama. Bwana alianzisha huduma ya kutawadhana miguu kuashiria kuoshwa upya, kuonesha utayari wa kutumikiana katika unyenyekevu kama wa Kristo na kuunganisha mioyo yetu katika upendo. Huduma ya ushirika mtakatifu iko wazi kwa Wakristo wote wanaoamini. (1 Kor. 10:16, 17; 11:23-30; Mat. 26:17-30; Ufu. 3:20; Yn. 6:48-63; 13:1-17.)

### *17. Karama za Roho na Huduma*

Mungu huwapatia washiriki wote wa kanisa lake katika kila kizazi karama za roho ambazo kila mshiriki hana budi kuzitumia katika huduma ya upendo kwa ajili ya maslahi ya jumla ya kanisa na ya wanadamu. Karama hizo, zitolewazo kwa njia ya Roho Mtakatifu, ambaye humgawia kila mshiriki kama apendavyo, hutoa uwezo na huduma zote zinazohitajika na kanisa kutimiza kazi lilizopewa na Mungu. Kulingana na Maandiko, karama hizi ni pamoja na huduma kama imani, uponyaji, unabii, kuhutubu, kufundisha, uongozi, upatanishi, huruma na utumishi wa kujitoa mhanga na msaada kwa ajili ya kusaidia na kutia moyo watu. Baadhi ya washiriki huitwa na Mungu na kujaliwa na Roho kwa ajili ya kazi zinazotambuliwa na kanisa katika huduma za uchungaji, uinjilisti, utume na ufundishaji zinazohitajika hasa kwa ajili ya kuwaandaa washiriki kwa ajili ya utumishi, kulijenga kanisa lifikie ukomavu wa kiroho na kudumisha umoja wa imani na kumjua Mungu. Washiriki wanapotumia karama hizi kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za Mungu, kanisa hulindwa dhidi ya mvuto mbaya wa mafundisho ya uongo, huwa linakua kwa ukuaji utokao kwa Mungu na hujengwa katika imani na upendo. (Rum. 12:4-8; 1 Kor. 12:9-11, 27, 28; Efe. 4:8, 11-16; Mdo. 6:1-7; 1 Tim. 3:1-13; 1 Pet. 4:10, 11.)

***18. Karama ya Unabii***

Moja kati ya karama za Roho Mtakatifu ni unabii. Karama hii ni alama ya kulitambua kanisa la waliosalia na ilidhihirika katika huduma ya Ellen G. White. Kama mjumbe wa Mungu, maandishi yake ni chanzo endelevu cha ukweli kilicho na mamlaka ambacho hulipatia kanisa faraja, uongozi, maelekezo, na marekebisho. Pia yanabainisha kwamba Biblia ni kipimo cha kupimia mafundisho yote na hali ya kiroho. (Yoe. 2:28, 29; Mdo. 2:14-21; Ebr. 1:1-3; Ufu. 12:17; 19:10.)

***19.Sheria ya Mungu***

Kanuni kuu za sheria ya Mungu ziko katika Amri Kumi na zinadhihirishwa katika maisha ya Kristo. Zinaonesha upendo, mapenzi na makusudi ya Mungu juu ya mwenendo wa uhusiano wa wanadamu na zinawahusu watu wote katika kila kizazi. Sheria hizi ni msingi wa agano la Mungu na watu wake na kipimo katika hukumu ya Mungu. Kwa huduma ya Roho Mtakatifu zinaonesha dhambi na kuamsha hisia za hitaji la Mwokozi. Wokovu ni kwa neema na si kwa matendo, lakini matunda yake ni utii kwa Amri. Utii huu huleta tabia ya Kikristo na husababisha hisia za hali njema. Ni ushahidi wa upendo wetu kwa Bwana na kuwajali wanadamu wenzetu. Utii wa imani huonesha uwezo wa Kristo kubadili maisha, na kwa hiyo huimarisha ushuhuda wa Kikristo. (Kut. 20:1-17; Zab. 40:7, 8; Mat. 22:36-40; Kum. 28:1-14; Mat. 5:17-20; Ebr. 8:8-10; Yn. 15:7-10; Efe. 2:8-10; 1 Yoh. 5:3; Rum. 8:3, 4; Zab. 19:7-14.)

***20. Sabato***

Baada ya siku sita za uumbaji, Mwumbaji mfadhili, alipumzika siku ya saba na kuanzisha Sabato kwa ajili ya watu wote kama kumbukumbu ya Uumbaji. Amri ya nne ya sheria ya Mungu isiyobadilika, inataka kuadhimishwa kwa Sabato hii ya siku ya Saba kama siku ya mapumziko, ibada, na huduma kulingana na mafundisho na desturi ya Yesu, ambaye ni Bwana wa Sabato. Sabato ni siku ya ushirika wa furaha na Mungu na sisi kwa sisi. Ni ishara ya ukombozi katika Kristo, ishara ya utakaso wetu, ishara ya utii wetu na mwonjo wa mustakabali wetu wa milele katika ufalme wa Mungu. Sabato ni ishara ya kudumu ya agano la milele kati yake na

watu wake. Kuadhimisha wakati huu mtakatifu kwa furaha kutoka jioni hata jioni, machweo hata machweo, ni kuadhimisha matendo ya Mungu ya uumbaji na ya ukombozi. (Mwa. 2:1-3; Kut. 20:8-11; Luk. 4:16; Isa. 56:5, 6; 58:13, 14; Mat. 12:1-12; Kut. 31:13-17; Eze. 20:12, 20; Kum. 5:12-15; Ebr. 4:1-11; Law. 23:32; Mk. 1:32.)

***21. Uwakili***

Sisi ni mawakili wa Mungu, tuliokabidhiwa naye muda na fursa, uwezo na mali na baraka za dunia na raslimali zake. Tunawajibika kwake kwa ajili ya matumizi mazuri ya vitu hivyo. Tunautambua umiliki wa Mungu kwa utumishi wa uaminifu kwake na wanadamu wenzetu, na kwa kurudisha zaka na sadaka kwa ajili utangazaji wa injili yake na kusaidia ukuaji wa kanisa lake. Uwakili ni fursa tuliyopewa na Mungu kwa ajili ya kukua katika upendo na ushindi dhidi ya ubinafsi na tamaa. Wakili hufurahia baraka zinazowajia wengine kama matokeo ya uaminifu wake. (Mwa. 1:26-28; 2:15; 1 Nya. 29:14; Hag. 1:3-11; Mal. 3:8-12; 1 Kor. 9:9-14; Mat. 23:23; 2 Kor. 8:1-15; Rum. 15:26, 27.)

***22. Mwenendo wa Kikristo***

Tumeitwa ili tuwe watauwa wanaofikiri, kujisikia na kutenda sawasawa na kanuni za mbinguni. Ili Roho aumbe ndani yetu tabia ya Bwana wetu inatupasa kujihusisha na mambo yanayoleta usafi kama wa Kristo, afya na furaha katika maisha yetu. Hii inamaanisha kwamba starehe na maburudisho yetu hayana budi kukidhi viwango vya juu kabisa vya tabia na uzuri wa Kikristo. Kwa kutambua tofauti za kitamaduni, mavazi yetu yawe sahili, ya adabu, na nadhifu, yanayowapasa wale ambao uzuri wao wa kweli hautokani na mapambo ya nje bali mapambo yasiyoharibika ya roho ya upole na utulivu. Inamaanisha pia kwamba, kwa kuwa miili yetu ni mahekalu ya Roho Mtakatifu, inatupasa kuitunza kwa akili. Pamoja na mazoezi na pumziko la kutosha, inatupasa kula chakula kiletacho afya kadiri iwezekanavyo na kutokula vyakula najisi vinavyotajwa katika Maandiko. Kwa kuwa vileo, tumbaku na matumizi mabaya ya dawa na dawa za kulevya huleta madhara kwa miili yetu, inatupasa kuviacha pia. Badala yake, inatupasa kufanya mambo yanayoelekeza mawazo na miili yetu katika nidhamu ya

Kristo ambaye anatamani tuwe na afya, furaha na hali njema. (Rum. 12:1, 2; 1 Yn. 2:6; Efe. 5:1-21; Flp. 4:8; 2 Kor. 10:5; 6:14-7:1; 1 Pet. 3:1-4; 1 Kor. 6:19, 20; 10:31; Law. 11:1-47; 3 Yoh. 2.)

### *23. Ndoa na Familia*

Ndoa ilianzishwa na Mungu katika Edeni na kuthibitishwa na Yesu kuwa ni muungano wa maisha yote kati ya mwanamume na mwanamke katika urafiki wa upendo. Kwa Mkristo ahadi ya ndoa ni kwa Mungu pia kama ilivyo kwa mwenzi, na haina budi kutolewa kati ya watu wenye imani moja tu. Upendo wa pamoja, heshima, staha na uwajibikaji ni vipengele muhimu vya uhusiano huo, ambao unatakiwa kuakisi upendo, utakatifu, ukaribu, na uendelevu wa uhusiano wa Kristo na kanisa lake. Kuhusu kuachana, Yesu alifundisha kuwa mtu amwachaye mwenzi wake na kuoa/kuolewa na mwingine, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, afanya uzinzi. Ingawa baadhi ya uhusiano wa familia unaweza kuwa chini ya kiwango, wanandoa wanaojitoa kikamilifu kwa kila mmoja katika Kristo wanaweza kufikia umoja wa upendo kwa kuongozwa na Roho na malezi ya kanisa. Mungu hubariki familia na anakusudia wanafamilia wasaidiane kufikia ukomavu kamili. Inawapasa wazazi kuwalea watoto wao katika kumpenda na kumtii Bwana. Kwa mfano na maneno yao, hawana budi kuwafundisha kuwa Yesu ni mdhibiti wa nidhamu mwenye upendo, mpole na anayejali kila wakati, anayewataka wawe viungo vya mwili wake, yaani familia ya Mungu. Kuongezeka kwa uhusiano wa kifamilia ni moja kati ya alama za ujumbe wa mwisho wa injili. (Mwa. 2:18-25; Mat. 19:3-9; Yn. 2:1-11; 2 Kor. 6:14; Efe. 5:21-33; Mat. 5:31, 32; Mk. 10:11, 12; Luk. 16:18; 1 Kor. 7:10, 11; Kut. 20:12; Efe. 6:1-4; Kum. 6:5-9; Mit. 22:6; Mal. 4:5, 6.)

### *24. Huduma ya Kristo Patakatifu pa Mbinguni*

Kuna patakatifu mbinguni, hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu. Kristo anahudumu katika hema hiyo kwa niaba yetu, akifanya iwezekane kwa waumini kunufaika na dhabihu yake ya upatanisho iliyotolewa mara moja pale msalabani. Alisimikwa kuwa Kuhani wetu Mkuu na kuanza huduma yake ya uombezi wakati wa kupaa kwake. Mwaka 1844, mwishoni mwa

kipindi cha unabii cha siku 2300, aliingia katika awamu ya pili na ya mwisho ya huduma yake ya upatanisho. Ni kazi ya hukumu ya upelelezi ambayo ni sehemu ya kuondolewa kabisa kwa dhambi, ikiwakilishwa na kutakaswa kwa patakatifu pa kale pa Waebrania katika Siku ya Upatanisho. Katika huduma hiyo kielelezo, patakatifu palitakaswa kwa damu ya dhabihu za wanyama, lakini mambo ya mbinguni hutakaswa kwa dhabihu kamilifu ya damu ya Yesu. Hukumu ya upelelezi inawadhihirishia wenye akili wa mbinguni ni akina nani miongoni mwa waliokufa wamelala katika Kristo na kwa hiyo, ndani yake wanaonekana kuwa wanastahili kuwa na sehemu katika ufufuo wa kwanza. Pia inadhihirisha ni akina nani miongoni mwa walio hai wanaokaa ndani ya Kristo, wakizishika amri zake na imani ya Yesu, na kwa hiyo, katika yeye wako tayari kwa ajili ya kubadilishwa na kuingia katika ufalme wake wa milele. Hukumu hii itathibitisha haki ya Mungu katika kuwaokoa wale waliomwamini Yesu. Itatangaza kwamba, wale walioendelea kuwa waaminifu wataupokea ufalme. Kukamilika kwa huduma ya Kristo kutakuwa mwisho wa kipindi cha rehema kabla ya Ujio wa Pili. (Ebr.. 8:1-5; 4:14-16; 9:11-28; 10:19-22; 1:3; 2:16, 17; Dan. 7:9-27; 8:13, 14; 9:24-27; Hes. 14:34; Eze. 4:6; Law. 16; Ufu. 14:6, 7; 20:12; 14:12; 22:12.)

### *25. Ujio wa Pili wa Kristo*

Ujio wa Pili wa Kristo ni tumaini lenye baraka kwa kanisa, kilele cha kuvutia cha injili. Ujio wa Mwokozi utakuwa halisi, wa kimwili, unaoonekana, na wa ulimwengu mzima. Atakaporudi, wafu wenye haki watafufuliwa, na watatukuzwa pamoja na wenye haki walio hai na kupelekwa mbinguni, lakini wasio haki watakufa. Utimilifu wa karibu vipengele vyote vya unabii, pamoja na hali ya sasa ya ulimwengu, vinaonesha kuwa ujio wa Kristo uko karibu. Wakati wa tukio hilo haujadhihirishwa, na kwa hiyo tunaaswa kuwa tayari wakati wote. (Tit. 2:13; Ebr. 9:28; Yn. 14:1-3; Mdo. 1:9-11; Mat. 24:14; Ufu. 1:7; Mat. 24:43, 44; 1 Thes. 4:13-18; 1 Kor. 15:51-54; 2 Thes. 1:7-10; 2:8; Ufu. 14:14-20; 19:11-21; Mat. 24; Mk. 13; Luk. 21; 2 Tim. 3:1-5; 1 Thes. 5:1-6.)

### *26. Kifo na Ufufuo*

Mshahara wa dhambi ni mauti. Lakini yeye ambaye peke yake hapatikani na mauti, atawapa uzima wa milele watu wake waliokombolewa. Hadi siku hiyo kifo ni hali ya kutokuwa na fahamu kwa watu wote. Kristo ambaye ni uzima wetu, atakapoonekana, wenye haki waliofufuliwa na wenye haki walio hai watatukuzwa na kunyakuliwa kwenda kumlaki Bwana wao. Ufufuo wa pili, yaani ufufuo wa wasio haki, utatokea miaka elfu moja baadaye. (Rum. 6:23; 1 Tim. 6:15, 16; Mhu. 9:5, 6; Zab. 146:3, 4; Yn. 11:11-14; Kol. 3:4; 1 Kor. 15:51-54; 1 Thes. 4:13-17; Yn. 5:28, 29; Ufu. 20:1-10.)

### *27. Milenia na Mwisho wa Dhambi*

Milenia ni miaka elfu moja ya utawala wa Kristo na watakatifu wake kule mbinguni kati ya ufufuo wa kwanza na ule wa pili. Katika kipindi hiki, waovu waliokufa watakuwa wanahukumiwa; dunia itakuwa ukiwa kabisa, bila ya wanadamu walio hai, lakini itakuwa inakaliwa na Shetani na malaika zake. Mwishoni mwa milenia, Kristo na watakatifu wake watashuka kutoka mbinguni kuja duniani, pamoja na ule Mji Mtakatifu. Wafu wasio haki watafufuliwa wakati huo, na watauzingira ule mji wakiwa na Shetani na malaika zake; lakini moto kutoka kwa Mungu utawala na kuitakasa dunia. Kwa njia hiyo, Ulimwengu utakuwa umeondolewa dhambi na wenye dhambi milele. (Ufu. 20; 1 Kor. 6:2, 3; Yer. 4:23-26; Ufu. 21:1-5; Mal. 4:1; Eze. 28:18, 19.)

### *28. Nchi Mpya*

Katika nchi mpya, ambamo haki inakaa, Mungu atatoa makazi ya milele kwa waliokombolewa na mazingira makamilifu kwa ajili ya uzima wa milele, upendo, furaha, na kujifunza mbele zake. Kwani hapo, Mungu mwenyewe atakaa na watu wake, na mateso na kifo vitakuwa vimepita. Pambano kuu litakuwa limekwisha, na dhambi haitakuwapo tena. Vitu vyote, vilivyo hai na visivyo hai vitakiri kwamba Mungu ni pendo; naye atatawala milele. Amina. (2 Pet. 3:13; Isa. 35; 65:17-25; Mat. 5:5; Ufu. 21:1-7; 22:1-5; 11:15.)

**Maelezo**

*Maelezo haya yana ufafanuzi kuhusu kanisa linavyoweza kufanya katika suala fulani mahususi. Kanisa linaweza kutumia njia zingine za kushughulikia mambo hayo. Njia hizo badala hazina budi kukubaliana na kanuni zinazokubalika za muundo na uendeshaji wa Kanisa.*

**Maelezo ya SURA YA 8**

1. ***Sherehe ya Ndoa*** (tazama uk. 74)—Katika baadhi ya nchi au majimbo, mchungaji hana budi kuteuliwa rasmi na kusajiliwa ili aweze kuendesha huduma ya ndoa. Katika nchi nyingi mchungaji anaweza kuendesha huduma ya ndoa kanisani lakini mkataba huo husainiwa kisheria na msajili wa wilaya, ambaye kwa kawaida hukaa katika chumba cha kujiandalia na kusikiliza aina ya tamko la ndoa lililoidhinishwa. Na katika nchi zingine mchungaji hawezi kabisa kuendesha sherehe ya ndoa kwa kuwa inatambuliwa kuwa ni jukumu la serikali na inachukuliwa kuwa ni mkataba wa kisheria. Katika hali kama hiyo, washiriki kwa kawaida huwa wanarudi nyumbani au kwenye nyumba ya ibada ambapo mchungaji huendesha huduma maalum kuomba baraka za Bwana kwa wanandoa husika. (tazama uk. 146-154.)

2. ***Kufundisha na Kuandaa Wazee*** (tazama uk. 75)—Licha ya mchungaji kuwa na wajibu wa kwanza wa kufundisha wazee, konferensi zinahimizwa kupanga mikutano ya mara kwa mara kwa ajili ya kuwafundisha. Ili kuboresha uhusiano wa timu ya mchungaji na wazee, inawapasa wachungaji kuhudhuria mikutano hiyo ya mafunzo. Viongozi wa makundi wanaofanya kazi mahali pa wazee hawana budi kualikwa pia.

3. ***Utunzaji na Ukarabati wa Mali za Kanisa*** (tazama uk. 78, 79)—Mashemasi wa kiume na wa kike hawana budi kuhakikisha kuwa jengo la kanisa linasafishwa na kukarabatiwa wakati wote na kwamba maeneo ya nje yanasafishwa na kuwa ya kuvutia wakati wote. Hii ni pamoja na kuhakikisha kazi ya ulinzi inafanywa. Katika makanisa makubwa ambapo ni lazima kuajiri mlinzi, inawapasa mashemasi kupendekeza kwa baraza

la kanisa mtu anayefaa na baraza litapiga kura ya kumwajiri, au baraza linaweza kuidhinisha mashemasi kuajiri mlinzi. Ni lazima idhini ya baraza itolewe kwa ajili ya pesa zote za ukarabati mkubwa. Bili zote za matengenezo, na gharama za kudumu, kama vile za maji, umeme na fueli hupelekwa kwa mhazini kwa ajili ya malipo.

4. ***Karani Hutunza Kumbukumbu*** (tazama uk. 79)—Kumbukumbu za vikao vya baraza hazina budi kuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za kanisa, au katika mfumo mwingine wa kumbukumbu unaofaa uliokubaliwa na kanisa, zikieleza wakati na tarehe ya mkutano, idadi ya waliohudhuria na taarifa ya uamuzi wote uliofanyika. Karani hana budi pia kuandika orodha ya kamati zilizoteuliwa katika kikao, kumpatia mwenyekiti orodha ya wajumbe wa kila kamati pamoja na hadidu za rejea na muhtasari wa kazi ambayo kamati imeombwa kufanya. Kitabu cha kumbukumbu za kanisa kinaweza kupatikana katika Duka la Vitabu vya Kiadventista au katika nyumba ya uchapishaji katika baadhi ya nchi.

   Kitabu cha kumbukumbu za kanisa kina mahali pa kuandika washiriki, pamoja na sehemu ya kuonesha jinsi na wakati washiriki wanavyopokelewa na kuondolewa. Kumbukumbu hizo hazina budi kufuata wendo, na inapasa kuonesha ushahidi wa kila ingizo katika sehemu inayoandikwa uamuzi unaohusu washiriki. Kumbukumbu za washiriki hazina budi kutunzwa kwa usahihi na kuboreshwa kila wakati ili kuonesha hali rasmi ya washiriki.

5. ***Kuwasiliana na Washiriki*** (tazama uk. 80)—Inampasa karani kuwasiliana mara kwa mara na washiriki wasioonekana kanisani na inampasa kuwapatia habari za maendeleo ya kanisa, kuwatia moyo, na kutoa taarifa ya shughuli zao za Kikristo kila robo.

6. ***Pesa za Oda Binafsi za Vitabu*** (tazama uk. 82)—Mahali ambapo hakuna Duka mahalia la Vitabu vya Kiadventista, washiriki wanaweza kuweka pesa za oda binafsi za maandiko mbalimbali, vitabu, makabrasha, magazeti, na pesa za kuagizia

majarida yatolewayo kwa kipindi maalum katika bahasha pamoja na fomu ya oda iliyojazwa ipasavyo na kuzikabidhi kwa katibu wa huduma binafsi. Mhazini atawasilisha oda hizo pamoja na pesa kwenye Duka la Vitabu vya Kiadventista au nyumba ya uchapishaji, kulingana na mfumo uliokubaliwa na konferensi. Mwishoni mwa kila robo, katibu wa huduma binafsi atatoa taarifa kwa kanisa katika mkutano wake mkuu wa kila robo kuhusu akaunti ya kanisa katika Duka la Vitabu vya Kiadventista na/au nyumba ya uchapishaji na atampatia nakala mhazini. (tazama uk. 97, 98.)

7. ***Kulinda Watoto—***Inalipasa kanisa kuwa mahali salama pa kuleta watoto wetu. Kila anayehusika na watoto wadogo hana budi kukidhi vigezo vya Kanisa na vya kisheria. Ili kuwalinda watoto wetu, makanisa yanahimizwa kuweka sera zitakazotoa hali ya usalama na ulinzi unaofaa kwa watoto. Sera hizo hazina budi kuwa pamoja na:
    - *a.* *Kanuni ya Watu Wazima Wawili*—Hakisha kuna watu wazima wawili katika madarasa au shughuli za watoto.
    - *b.* *Mlango Wazi*—Zuia mawasiliano ya faragha au ya mtu na mtu na himiza kanuni ya mlango wazi katika hali zote. Mahali ambapo kuwa na mlango wazi haiwezekani, weka mtu mzima mwingine mlangoni.
    - *c.* *Kuhakiki Wanaojitolea*—Hakikisha wanaojitolea wote wanajaza fomu ya taarifa ya mtu anayejitolea, chunguza historia zao na inapotakiwa na sheria, chunguza taarifa zao polisi.
    - *d.* *Sera ya Miezi Sita*—Weka kipindi cha kusubiri cha miezi sita kwa watu waliiotoka kubatizwa au kuhamia ambao wameonesha kuwa wanataka kuhudumia watoto.
    - *e.* *Mafunzo*—Toa mafunzo mara kwa mara kwa walimu na waliojitolea kuwasaidia kuwaelewa na kuwalinda watoto na jinsi ya kuwalea katika imani.

    Viongozi wa kanisa mahalia hawana budi kushauriana na konferensi ili kuwa na uhakika juu ya taratibu na matakwa ya konferensi, pamoja na matakwa mahalia ya kisheria kwa watu wanaohudumia watoto. Miongozo ya

ziada inapatikana kutoka Adventist Risk Management kwenye www.adventistrisk.org.

8. ***Miongozo ya Huduma za Watoto*** (tazama uk. 86)—*The Children's Ministries Handbook: A Step-by-Step Guide for Children's Leaders Around the World (2005); The Children's Ministries Coordinator: A Step-by-Step Guide for Organizing Children's Ministries in the Local Church (2005); and Pastor's and Elder's Handbook for Children's Ministries (2005). Silver Spring, Md.*: Huduma za Watoto, Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na mkurugenzi wa huduma za watoto wa konferensi yako mahalia na www.gcchildmin.org.

9. ***Miongozo ya Huduma za Familia*** (tazama uk. 91)—*Caring for Families Today: A Guide for Family Ministries (2009). Silver Spring, Md.*: Huduma za Familia, Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato. Kwa taarifa zaidi, wasiliana na mkurugenzi wa huduma za familia wa konferensi yako mahalia na www.adventistfamilyministries.org.

10. ***Miongozo ya Huduma za Afya*** (tazama uk. 92)—*CELEBRATIONS* (muhtasari wa programu 12 za masomo muhimu ya huduma za afya, pamoja na maelezo na PowerPoint), *CHARTERS* (mfululizo wa mihadhara yenye PowerPoint kwa ajili ya masomo kwa hadhira za walei), *Misingi ya Huduma za Afya* (Mihadhara 84 juu ya afya ya msingi kwa ajili ya viongozi wa huduma za afya), *Breath Free* (mtaala wa kuacha kuvuta), *Youth Alive* (programu ya kujenga uwezo wa kurudi katika hali ya kawaida kwa vijana wetu), *Vegetarian Cuisine Instructor's Course* (Mwongozo namna ya kufanya), *Birthing Companions* (kusaidia wanawake vijana wajawazito katika ujauzito wao), *Regeneration* (programu ya hatua 12 za kutoka katika utegemezi), na *My Vegetarian Food Pyramid* (mabango makubwa au madogo).

11. ***Miongozo ya Mambo ya Jamii na Uhuru wa Kidini*** (tazama uk.

93)—Kwa maelezo zaidi, wasiliana na mkurugenzi wa mambo ya jamii na uhuru wa kidini wa konferensi yako mahalia au tembelea www.irla.org.

12. ***Miongozo ya Huduma za Uchapishaji*** (tazama uk. 94)—*Literature MinistryTraining Manual* (vitabu namba 1-3 pamoja na masomo ya PowerPoint); *The Publishing Ministry* (kijitabu); *Student Literature Evangelism Manual; Miracles of Grace* (kitabu chenye shuhuda 365 za wainjilisti wa vitabu ulimwenguni); *The Literature Evengelist* (Jarida la kila robo la idara ya Huduma za Uchapishaji ya Konferensi Kuu. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na mkurugenzi wa huduma za uchapishaji wa konferensi yako mahalia au mkurugenzi wa union yako. Unaweza pia kwenda kwenye www.publishing.gc.adventist.org.

13. ***Miongozo ya Shule ya Sabato na Huduma Binafsi* (tazama uk.** 97, 99)—Miongozo ya kusoma Biblia ya Shule ya Sabato kwa ajili ya umri mbalimbali *(CQ, Cornerstone Connections, Real-Time Faith, Vijana Wadogo, Msingi, Chekechea, and Awali); Mwongozo wa Shule ya Sabato; Keys for Sabbath School and Personal Ministries Leaders* (mfululizo wa vitini); *Reaching and Winning* (mfululizo wa vijitabu kwa ajili ya huduma binafsi kwa watu wa mifumo mbalimbali ya imani); *Adventist Community Services Handbook: The sharing)* (barua ya taarifa). Kwa maelezo zaidi, wasiliana na mkurugenzi wa shule ya Sabato au wa huduma binafsi wa konferensi yako mahalia. Unaweza pia kwenda kwenye www.sabbathschoolpersonalministries.org au kwenye GraceLink.net, JuniorPowerPoints.org, RealTimeFaith.net, CornerstoneConnections.net, CQBibleStudy.org, au SabbathSchoolU.org.
14. ***Miongozo ya Huduma za Uwakili*** (tazama uk. 99)—*Steps to Discipleship* (2009). Silver Spring, Md.: Huduma za Uwakili, Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na mkurugenzi wa idara ya huduma za uwakili wa konferensi, union au divisheni yako mahalia au tembelea www.adventiststewardship.com

15. ***Miongozo ya Huduma za Wanawake*** (tazama uk. 100)—Uthibibitisho wa viongozi ngazi ya 1-4; miongozo ya Siku ya Maombi, Siku Maalum ya Wanawake, na Siku ya Kupinga Udhalilishaji; *Mwongozo wa Huduma za Wanawake kwa Wachungaji na Wazee.* Kwa maelezo zaidi wasiliana na mkurugenzi wa huduma za wanawake wa konferensi yako mahalia na tembelea www.adventistwomensministries.org.

16. ***Mpango wa Uundaji wa Chama cha Vijana wa Kiadventista*** (tazama uk. 102)—Maelezo ya kina kuhusu mpango wa uundaji wa Chama cha Vijana wa Kiadventista yanapatikana kwa mkurugenzi wa huduma za vijana wa konferensi. Kila kanisa halina budi kuchunguza taswira ya vijana na familia zake, miongozo, watendakazi, vitendea kazi na uhusiano na shule, likianzisha huduma bora ya vijana kulingana na vigezo hivyo.
Katika maeneo mengine linaweza kutumika neno lingine badala ya "chama," kama vile "ushirika" au "harakati" lakini jina "Vijana wa Kiadventista" halina budi kutumika kila wakati ili kukibainisha chama.

17. ***Miongozo ya Huduma za Vijana*** (tazama uk. 105)—Tembelea tovuti yetu kwa ajili ya masomo zaidi na maelezo zaidi katika www.gcyouthministries.org au andika barua pepe kwenda youth@gc.adventist.org.

**Maelezo ya SURA YA 9**

1. ***Orodha Kielelezo ya Viongozi wa Kanisa*** (tazama uk. 108). Kamati ya mapendekezo itachagua washiriki watakaotumika kama maofisa katika nafasi mbalimbali. Kanisa dogo linaweza kuwa na orodha ndogo ya maofisa. Kanisa kubwa linaweza kuwa na orodha ndefu ya maofisa. Orodha hii inaweza kufikiriwa:

Mzee/wazee
Shemasi/mashemasi wa kiume
Shemasi/Mashemasi wa kike
Karani

Mhazini na msaidizi/wasaidizi
Mratibu wa waliovutiwa
Baraza la kanisa
Bodi ya shule ya kanisa
Kiongozi wa Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista na msaidizi/wasaidizi
Kiongozi wa Chama cha Vijana wa Kiadventista
Mdhamini wa Chama cha Vijana wa Kiadventista
Katibu-mhazini wa Chama cha Vijana wa Kiadventista na msaidizi/wasaidizi
Mkurugenzi wa muziki wa Chama cha Vijana wa Kiadventista
Mpiga piano au ogani wa Chama cha Vijana wa Kiadventista
Mkurugenzi wa Klabu ya Wavumbuzi
Mkurugenzi wa Klabu ya Mabalozi
Mratibu wa shule ya Biblia
Mkurugenzi wa huduma za watoto
Mwimbishaji wa kanisa au kiongozi wa nyimbo au mratibu wa muziki
Mpiga ogani au piano wa kanisa
Katibu wa mawasiliano au kamati ya mawasiliano
Mkurugenzi wa Huduma za Jamii
Kiongozi wa Chama cha Dorkas
Katibu-mhazini wa Chama cha Dorkas
Katibu wa elimu
Kiongozi/viongozi wa huduma za familia
Kiongozi wa huduma za afya
Mratibu wa huduma kwa walemavu
Mkurugenzi wa Klabu ya Watafuta Njia na naibu mkurugenzi
Kiongozi wa huduma binafsi
Mkurugenzi wa huduma za maombi
Mkurugenzi wa huduma za uchapishaji
Kiongozi wa uhuru wa kidini
Mrakibu/warakibu wa shule ya Sabato na msaidizi/wasaidizi
Katibu wa shule ya Sabato na msaidizi/wasaidizi
Viongozi wa vitengo vya shule ya Sabato, pamoja na viongozi wa utandaaji kwa watu wazima

Katibu wa uwekezaji wa shule ya Sabato
Kiongozi wa huduma za uwakili
Mkurugenzi wa Shule ya Biblia Wakati wa Likizo
Kiongozi wa huduma za wanawake
Watenda kazi wa ziada wanaoonekana kuwa wa lazima
Maofisa wa Chama cha Kaya na Shule (kiongozi na katibu-mhazini).

Kama kanisa moja peke yake linasimamia shule, kamati ya mapendekezo ya kanisa hupendekeza kwa baraza ambalo nalo hufanya uteuzi. Kama makanisa zaidi ya moja yanasimamia shule moja, bodi ya shule itaendesha mchakato huo. (Tazama uk. 88, 89.)

**Maelezo ya SURA YA 10**

*1)* ***Shule ya Sabato*** (tazama uk. 117)—Muda wa kawaida wa Shule ya Sabato ni saa moja na dakika kumi. Hata hivyo jambo hilo haliizuii konferensi kuamua kutumia muda mrefu au mfupi zaidi, ingawa ni muhimu kuwa na muda wa kutosha kuhamasisha mara kwa mara shughuli za umisionari na majukumu ya kanisa la ulimwengu, pamoja na sadaka ya utume na angalau dakika thelathini za kusoma Biblia.

2) ***Mfumo wa Ibada*** (tazama uk. 117, 118)—Mifumo ya ibada hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine na utamaduni mmoja hadi mwingine. Mifumo ifuatayo inapendekezwa:

*Mfumo Mrefu wa Ibada*

Muziki wa Utangulizi
Matangazo
Kuingia wahudumu
Wimbo wa sifa
Ombi
Kusoma fungu la Maandiko
Wimbo wa sifa
Ombi
Wimbo wa sifa au muziki maalum
Sadaka

Wimbo wa kujiweka wakfu
Hubiri
Wimbo
Baraka
Kanisa kusimama au kukaa kwa muda mfupi kwa ajili ya sala ya kimyakimya
Muziki wa kumalizia

*Mfumo Mfupi wa Ibada*

Matangazo
Wimbo
Ombi
Sadaka
Wimbo au muziki maalum
Hubiri
Wimbo
Baraka
Kanisa kusimama au kukaa kwa ajili ya ombi la kimyakimya

***1)3)*** ***Mfumo wa Ibada*** (tazama uk. 118)—Wahudumu wanapoingia na kupiga magoti, kanisa halina budi kuinamisha vichwa likiomba kuwepo kwa Mungu na baraka zake. Ukimya wa kicho kuandaa njia kwa ajili ya zoezi linalofuata. Sehemu kuu mbili za ibada ni:

a. Mwitikio wa kanisa kwa njia ya sifa na heshima ambavyo hufanyika kwa nyimbo, maombi na matoleo.b. Ujumbe kutoka katika Neno la Mungu.

Yule anayewaongoza waumini mbele za Mungu kwa ombi la kichungaji pengine hufanya jukumu takatifu kuliko zote katika huduma na inampasa kutambua kwa kicho umuhimu wa huduma hiyo. Kwa kawaida yule anayeomba hupiga magoti akiwaelekea washiriki, na washiriki wakipiga magoti kwa kadiri inavyowezekana, humwelekea yule anayeomba. Ombi halina budi kuwa fupi lakini lazima liwe na heshima na upendo, shukurani, na kutaja mahitaji mahususi ya waumini pamoja na eneo lote ulimwenguni.

Sadaka ni sehemu nyeti ya wakati wa ibada. Wakati tunashauriwa kumwabudu "Bwana kwa uzuri wa utakatifu," pia tunahimizwa

kuleta “sadaka [tu]kaziingie nyua zake” Zab. 96:9, 8). Kwa hiyo utoaji wa sadaka zetu kwa Mungu kwa kawaida huchukua nafasi kama sehemu ya huduma ya ibada.

Itakuwa vyema kukiwa na Muziki maalum au wimbo wa ibada.

Kisha litafuata jambo ambalo ni moja ya sehemu muhimu kabisa za muda wa ibada—kulilisha kundi la Mungu. Matokeo yenye heri kwa utukufu wa Mungu hufuata kila mara kanisa linapolishwa kweli kweli na kujisikia kwamba “Mungu amewaangalia watu wake” (Luka 7:16). Yule anayeleta ujumbe hana budi kuona utakatifu wa kazi hii na inampasa kujiandaa kikamilifu.

Mzee hushirikiana na mchungaji katika kupanga utaratibu wa ibada. Kama kanisa halina mchungaji wa kudumu, mzee ndiye msimamizi wa ibada na inampasa kuiendesha au kupanga mtu wa kufanya hivyo. Wakati mwingine unaweza kufanyika mkutano wa ushuhuda na sifa, au unaweza kutolewa muda kwa washiriki kadhaa kuelezea mambo waliyokutana nayo katika kazi zao za utume.

4. ***Muda wa Mikutano*** (tazama uk. 118)—Ili kuimarisha na kuhamasisha moyo wa umisionari miongoni mwa washiriki, mikutano ya ziada ya huduma binafsi inaweza kufanywa katika njia moja au zaidi ya hizi zifuatazo:
   a. Mkutano wa dakika kumi wa huduma binafsi unaofanyika kila Sabato, kwa kawaida mara baada ya kufunga shule ya Sabato na kabla ya huduma ya mahubiri.
   b. Mkutano wa katikati ya juma unaoambatana na mkutano wa maombi wa kila juma. Wakati huo, sehemu ya kwanza ya huduma inaweza kuwa kwa ajili ya ujumbe wa ibada, ukifuatiwa na kipindi cha maombi, ikikumbukwa kwamba ibada ni muhimu katika ukuaji wa kiroho na kujianda kwa ajili ya huduma. Muda unaobaki unaweza kutumika kwa kufundisha huduma ya wainjilisti walei. Mafunzo ya mbinu za uongoaji wa roho hutolewa, na washiriki hupewa nafasi ya kuwasilisha na kujadili matatizo waliyokutana nayo katika uinjilisti wa walei.

Mikutano ya huduma binafsi haina budi kufanyika wakati unaofaa kulingana na hali mahalia. Baraza la huduma binafsi halina budi kupanga kwa uangalifu kuifanya mikutano ya huduma

binafsi ya kanisa iwe ya uamsho wa kiroho na mafunzo ya vitendo, na kuhakikisha kwamba inafanyika kwa wakati wake na kudumu kama mikutano mingine ya kanisa.

5. ***Kutawadhana Miguu*** (tazama uk. 121)—Wanaume na wanawake hawana budi kutengewa maeneo tofauti kwa ajili ya kutawadhana miguu. Mahali ambapo ngazi au umbali ni tatizo, ifanyike mipango maalum kwa ajili ya wenye ulemavu. Mahali ambapo inakubalika kijamii na ambapo mavazi hayataondoa staha, mipango maalum ifanywe kwa ajili ya mume na mke au wazazi na watoto waliobatizwa kushirikiana katika kaida ya kutawadhana miguu. Ili kuwatia moyo watu wenye hisia za karibu au wenye haya wanaoweza kuona aibu kuchagua mtu wa kutawadhana naye, viongozi wa kanisa wawekwe kwa ajili ya kuwasaidia watu wa aina hiyo kupata watu wa kutawadhana nao.

   Inawapasa watu wote kunawa mikono yao vizuri kabla ya kurudi kushiriki Meza ya Bwana. Wale wanaoongoza katika huduma hawana budi kufanya hivyo hadharani kwa sababu za kiafya.

6. ***Mkate na Divai*** (tazama uk. 121)—Wakati washiriki wanarudi kanisani, unaweza kuimbwa wimbo wakati wachungaji au wazee wanakaa katika sehemu zao karibu na mkate na divai (juisi ya zabibu isiyotiwa chachu) na mashemasi wa kiume na wa kike wanakaa katika sehemu zao.

   Kitambaa kilichofunika mkate huondolewa.

   Fungu linalofaa kutoka katika Maandiko linaweza kusomwa, kama vile 1 Wakorintho 11:23, 24; Mathayo 26:26; Marko 14:22; au Luka 22:19; au hubiri fupi linaweza kutolewa wakati huu badala ya kabla ya meza ya Bwana. Jambo hilo linaweza kuwa na mguso kama hubiri litasisitiza maana ya mkate na divai ili ujumbe wake uendelee kuwa katika akili za washiriki wakati mkate na divai vinagawiwa.

   Kwa kawaida wahudumu hupiga magoti wakati ombi la kubariki mkate linatolewa. Washiriki wanaweza kupiga magoti au kuendelea kukaa.

Kawaida sehemu kubwa ya mkate unaogawiwa unakuwa umekatwakatwa mapema, isipokuwa sehemu kidogo inayoachwa katika kila sahani kwa ajili ya wazee na/au wachungaji kumega. (Watu wote waaoshika ule mkate lazima waoshe mikono yao vizuri kabla ya kurudi kwa ajili ya ushirika mtakatifu.) Wachungaji na wazee huwapa mashemasi wa kiume zile sahani zenye mkate ambao huwagawia washiriki ingawa katika makanisa madogo wachungaji na wazee huwagawia washiriki wote.

Wakati huo unaweza kuchaguliwa muziki maalumu, shuhuda, muhtasari wa hubiri, kusoma mafungu yaliyochaguliwa, kuimba kanisa zima, au muziki wa kutaamali.

Inawapasa washiriki kushikilia vipande vyao vya mkate mpaka wachungaji au wazee wanaohudumu wamegawiwa. Wakati kila mtu amekwisha kukaa, viongozi huwaeleza watu wote kula mkate kwa pamoja. Wakati mkate unaliwa maombi ya kimya kimya hutolewa.

Kisha mchungaji husoma fungu linalofaa kama vile, 1 Wakorintho 11:25, 26; Mathayo 26:27-29; Marko 14:23-25 au Luka 22:20. Viongozi hupiga magoti wakati divai inaombewa. Kwa mara nyingine mashemasi wa kiume ihuwagawia washiriki. Mambo kama yale yaliyopendekezwa wakati wa kugawa mkate yanaweza kuendelea wakati huu. Baada ya wachungaji au wazee wanaohudumu kugawiwa, washiriki wote hunywa divai kwa pamoja.

Njia nyingine ni ya mkate kubarikiwa na kumegwa; kisha mkate na divai kuwekwa katika trei moja na kupitishwa kwa washiriki. Mshiriki huchukua vyote wakati huo huo kutoka katika trei. Mkate huliwa na kufuatiwa na maombi ya kimya kimya. Kisha baada ya kuombea divai, divai hunywewa na kufuatiwa na maombi ya kimya kimya. Mahali ambapo mabenchi yana mahali pa kuweka glasi, ukusanyaji wa glasi si wa lazima mpaka baada ya huduma.

7. ***Mkutano Mkuu*** (tazama uk. 123, 124)—Taarifa zinaweza kuwa na mambo yafuatayo:

a. Taarifa kutoka kwa karani ikionesha washiriki wa kanisa

waliopo na idadi ya washiriki waliopokelewa na waliohamia makanisa mengine. Pia idadi ya wale walioondolewa katika ushirika mwaka huo ielezwe bila kutaja majina yao, pamoja na wale waliokufa. Maelezo mafupi ya uamuzi wa baraza la kanisa katika mikutano yake yanaweza kuwa na manufaa kwa washiriki.

b. Taarifa kutoka kwa kiongozi wa huduma binafsi akitoa maelezo ya shughuli za umisionari, pamoja na shughuli za Huduma za Jamii, pamoja na mipango ya kazi ya siku za usoni. Taarifa hii ifuatiwe na taarifa kutoka kwa katibu wa huduma binafsi.

c. Taarifa kutoka kwa mhazini ikionesha kiasi cha zaka iliyopokelewa na kutumwa konferensi, taarifa ya sadaka za utume zilizopokelewa na kutumwa, na taarifa inayoonesha pesa za kanisa mahalia zilizopokelewa na kutumika.

d. Taarifa kutoka kwa mashemasi wa kiume na wa kike kuhusu kutembelea washiriki, shughuli zao kwa ajili ya maskini, na kazi zingine za kulea.

e. Taarifa kutoka kwa katibu wa chama cha vijana ikieleza shughuli za umisionari na mambo mengine yanayofanywa na vijana wa kanisa.

f. Taarifa kutoka kwa katibu wa shule ya Sabato ikielezea idadi ya washiriki na mambo mengine yanayohusu shule ya Sabato

g. Taarifa kutoka kwa mhazini kuhusu hali ya kifedha ya shule ya kanisa, ikielezea mahitaji yake ya vifaa na masuala mengine.

h. Taarifa kutoka kwa mkuu au mwalimu wa shule ya kanisa ikielezea masuala kama ya udahili, maendeleo ya shule kitaaluma, ubatizo wa wanafunzi, na matokeo ya juhudi za watoto katika shughuli za kanisa.

i. Taarifa kutoka kwa Kiongozi wa Chama cha Kaya na Shule ikielezea shughuli na mahitaji ya jumuiya hiyo.

j. Taarifa kutoka kwa katibu wa mawasiliano kuhusu vyombo vya habari, redia, televisheni na shughuli zingine za mawasiliano yanayohusu kanisa na jamii.

8. ***Kamati Zingine za Baraza*** (tazama uk. 127)—Viongozi wa kamati zingine zinazoteuliwa na baraza hawana budi kutoa taarifa kila mara. Kwa mfano katika kanisa kubwa, baraza la kanisa linaweza kuteua kamati ya kupanga uinjilisti yenye wakuu wa idara zinazoshughulika na umisioanari, pamoja na mzee mmoja kama mwenyekiti. Kamati hii itatoa taarifa kwa baraza na pia itachukua jukumu la kuratibu programu za umisionari za idara mbalimbali.

9. ***Miongozo ya Chama cha Vijana wa Kiadventista*** (tazama uk. 128)—Miongozo ya kuwasaidia viongozi wa Chama cha Vijana wa Kiadventista inapatikana katika idara ya huduma za vijana katika divisheni, union na konferensi. Katika miongozo hii kuna *Youth Ministry Accent,* jarida la kila robo linalochapishwa na Idara ya Huduma za Vijana ya Konferensi Kuu. Vitini vilivyopo vinavyoelezea mada nyingi za kusaidia katika huduma za vijana vinaweza kupatikana kutoka katika idara ya huduma za vijana ya konferensi na duka la vitabu vya Waadventista.

10. ***Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista*** (tazama uk. 128)—Kama Chama cha Vijana Wadogo wa Kiadventista ni sehemu ya programu ya shule ya Kiadventista, kila darasa litakuwa chama pekee, na mwalimu akiwa kiongozi na wananafunzi kuchaguliwa kama maofisa wa chama. Mahali pasipo na shule ya kanisa, vijana wadogo hawana budi kujumuishwa katika programu nzima ya vijana inayohusisha familia.

**Maelezo ya SURA YA 11**

1. ***Miongozo ya Huduma za Uwakili*** (tazama uk. 131)—*Steps to Discipleship* (2009). Silver Spring, Md.: Huduma za Uwakili, Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na idara ya uwakili ya konferensi, union, au divisheni yako mahalia au tembelea www.adventiststewardship.com.

## *2. Mfano wa Bajeti ya Mwaka** (tazama uk. 133.

*Mapendekezo ya Bajeti ya Uendeshaji wa Kanisa*

**Makadirio ya Mapato—**

| | | |
|---|---|---|
| Michango ya Matumizi ya Shule ya Sabato | 1,500.00 | |
| Mfuko wa Kanisa kwa ajili ya Wahitaji | 375.00 | |
| Sadaka ya Kanisa Itolewayo kwa Mpango | 27,055.00 | |
| Mfuko wa ustawi wa Jamii | 300.00 | |
| Jumla ya Mapato | | 29,230.00 |

**Makadirio ya Matimizi-**

| | | |
|---|---|---|
| Matengenezo na Kupaka rangi Kanisa | 2,250.00 | |
| Mafuta | 2,350.00 | |
| Mlinzi n Vifaa | 1,475.00 | |
| Bima ya Jengo na Samani | 750.00 | |
| Mfuko wa Kanisa kwa wahitaji | 1,450.00 | |
| Vifaa vya Shule ya Sabato | 1,250.00 | |
| Matumizi ya Dharura | 2,000.00 | |
| Umeme | 3,220.00 | |
| Maji | 360.00 | |
| Gesi | 550.00 | |
| Vifaa vya Ofisi | 500.00 | |
| Kufua | 75.00 | |
| Ruzuku kwa Shule ya Kanisa | 8,000.00 | |
| Gharama za Ustawi wa Jamii | 1,000.00 | |
| Uinjilist na Kuanzisha Makanisa | 4,000.00 | |
| Jumla ya Makadirio ya Matumizi | | 29,230.00 |
| Salio | | 0 |

*Safu za ziada (kama vile bajeti ya mwaka uliopita na hali halisi ya mwaka huo) hazina budi kuwekwa kwa ajili ya kulinganisha, lakini zimeachwa katika mfano huu kwa sababu ya ufinyu wa nafasi.

# Vifupisho

AA The Acts of the Apostles
AH The Adventist Home
CD Counsels on Diet and Foods
CG Child Guidance
CH Counsels on Health
CM Colporteur Ministry
COL Christ's Object Lessons
CSW Counsels on Sabbath School Work
CT Counsels to Parents, Teachers, and Students
CW Counsels to Writers and Editors
DA The Desire of Ages
Ed Education
Ev Evangelism
FLB The Faith I Live By
GC The Great Controversy
GCB General Conference Bulletin
GW Gospel Workers
HP In Heavenly Places
MH The Ministry of Healing
MM Medical Ministry
MYP Messages to Young People
PK Prophets and Kings
PP Patriarchs and Prophets
RH Review and Herald
SC Steps to Christ
T Testimonies for the Church
TM Testimonies to Ministers and Gospel Workers
TMB Thoughts From the Mount of Blessing

# Nyongeza ya Iliyokuwa Divisheni ya Mashariki mwa Afrika

Ndoa
Mahari
Ndoa ya Kikristo
Mamlaka ya Kufunga Ndoa
Vizuizi vya Kutofungwa Ndoa
Huduma na Utaratibu wa Kufunga Ndoa
Kuandikisha Ndoa
Mapambo katika Harusi
Jamii ya Kikristo
Talaka
Ndoa za Wake Zaidi ya Mmoja
Desturi za Tohara
Ugomvi Kati ya Ndugu
Utunzaji wa Pesa za Kanisa
Kitabu cha Orodha ya Majina ya Washiriki
Vyeti vya Ushirika
Madarasa ya Ubatizo
Darasa la Mafundisho ya Biblia
Kuanzisha Kanisa
Huduma ya Kutawadha Miguu
Huduma ya Meza ya Bwana
Jinsi ya Kutengeneza Divai Isiyochachuka
Utunzaji wa Vyombo
Utaratibu wa Ibada ya Meza ya Bwana
Kuketi Wakati wa Kuomba
Huduma ya Idara ya Huduma za Washiriki
Mikutano ya Maombi
Mikutano ya Makambi
Mazishi
Huduma Kanisani
Huduma Kaburini
Pesa za Kundi
Pesa za Shule za Kanisa

SURA 15

# Nyongeza ya Iliyokuwa Divisheni ya Mashariki Mwa Afrika

Mambo yafuatayo yameongezwa kutokana na ushauri wa Konferensi Kuu kwamba kila divisheni iandae na kupitisha nyongeza za kanuni zitakazotumika katika divisheni hiyo tu; na kwamba nyongeza hizo ziwe sehemu ya mwongozo wa kawaida wa Kanisa. Hii ni kuwasaidia na kuwaongoza wachungaji, maofisa wengine na makanisa katika masuala ya kanisa katika nchi za Mashariki mwa Afrika.

***Ndoa***—Pamoja na mambo yaliyoelezwa katika sura ya 15 ya *Mwongozo* huu wa *Kanisa*, ni vyema kusisitiza maswala yafuatayo kuhusu ndoa:

***Mahari***—Desturi ya kudai mahari kutoka kwa mtu anayetaka kuoa ni utamaduni na mila za kale zinazoendelea miongoni mwa watu wasiomjua Mungu katika makabila mengi. Kwa asili mahari ilikuwa ni dhamana kwamba atakayeolewa atathaminiwa na kuhesabiwa kuwa mke halisi na hivyo kutendewa vizuri. Kwa kadiri mahari ilivyokuwa kubwa, ndivyo mke alivyojiona wa thamani zaidi. Lakini tangu Ukristo ulipokuja mambo yamebadilika. Msingi wa ndoa ya Kikristo ni upendo. Upendo huo ni wa thamani kubwa sana na wa kudumu kuliko mifugo, pesa, au vitu vyo vyote vitolewavyo kama mahari. Hivyo Wakristo wanaooana kwa upendo wa kweli hawana haja ya kuwa na dhamana nyingine ya usalama wa ndoa yao.

Ni jambo la kusikitisha kwamba bado kuna Wakristo wanaoona kuwa desturi hii ya kale ya kulipa mahari ni njia ya kujipatia mali

kwa kutumia watoto wao. Mahari ya kubwa sana hudaiwa kutoka kwa mtu anayetaka kuoa. Vijana wengi hawawezi kumudu mahari Bila msaada wa ndugu zao. Vijana wengine huamua kupita njia za mkato, na kukosa idhini ya wazazi na baraka za Mungu na kanisa. Hivyo dhamana ya mahari imepoteza nguvu yake, na kusababisha ugumu kanisani badala ya kuuondoa.

Kwa hiyo tunawashauri Wakristo wote walio na nuru na kukomaa waache kudai mahari kwa ajili ya binti zao.

Pamoja na hayo kanisa linapinga kabisa vijana wa kiume na wa kike wa Kikristo kutumia njia za mkato za kutoroshana au kuoana bila idhini ya wazazi. Wachungaji na wazee wa kanisa wanatazamiwa kuwafundisha vijana juu ya kawaida na taratibu bora za kuoana na kuwaongoza katika njia nzuri kwa mashauri ya kiroho, na ikibidi, wazungumze na kuwashauri wazazi washupavu ili waondoe vizuizi vya ndoa visivyo vya lazima.

***Ndoa ya Kikristo***—Kwa sababu tunakubali kwamba kanisa hupimwa kutokana na kawaida zake za mema na mabaya, na kwamba ndoa ya Kikristo inayokubalika na wengi inafaa kwa Wakristo wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, tunasisitiza ushauri kuwa makanisa yetu yote yawafundishe washiriki wao kupata huduma ya ndoa ya kisheria na kikanisa, ambapo watu wanaooana hupatana kuzishika kanuni zinazotawala ndoa ya Kikristo.

Inashauriwa kwamba mshiriki akioa au kuolewa na mtu aliye katika darasa la ubatizo, apate pia huduma hiyo ya kisheria na kikanisa. Kama watu walio katika darasa la ubatizo wameoana kwa ndoa ya kimila, basi inashauriwa wafanyiwe huduma ya kisheria na ya kikanisa kabla hawajabatizwa.

***Mamlaka ya Kufungisha Ndoa***—Miongoni mwa Waadventista wa Sabato, wachungaji waliowekewa mikono ndiyo wanaoruhusiwa kufungisha ndoa. Hakuna njia nyingine. Katika nchi nyingine wachungaji huruhusiwa kisheria kufungisha ndoa. Pengine ni lazima jina lake lipelekwe kwanza serikalini, ili kupata kibali cha kuwa msajili wa ndoa kwa mujibu wa sheria ya nchi. Ni wajibu wa kila mchungaji kuzifahamu sheria za nchi anayokaa, na kuhakikisha, kabla hajaendesha huduma ya ndoa, kwamba amesajiliwa na serikali

au mamlaka husika na kwamba ana mamlaka kufanya huduma hiyo kwa mujibu wa sheria. Ni lazima ahakikishe pia kuwa matangazo yanayotakiwa kwa mujibu wa sheria yametangazwa na kwamba hakuna pingamizi lo lote dhidi ya kufungwa kwa ndoa husika.

***Vipingamizi vya Kufungwa kwa Ndoa*—**Mchungaji asikubali kufungisha ndoa ya namna isiyofaa, au iliyofanywa kwa haraka kupita kiasi, au yenye utata. Maisha yetu yametufundisha kwamba kutozingatia ushauri wa Mungu juu ya kuoana na watu wasioamini au wasio wa madhehebu yetu, mara nyingi huleta huzuni, uchungu, na kupoteza imani katika Neno la Mungu. Kwa hiyo wachungaji wasifungishe ndoa kati ya asiyeamini na aaminiye.

Kanisa la Waadventista wa Sabato haliafiki haki ya kuoa au kuolewa tena kwa wale waliovunja ndoa kwa sababu yo yote isipokuwa kwa yule asiye na hatia katika kuvunjika kwa ndoa kutokana na sababu zilizoelezwa katika sura a 15 ya *mwongozo* huu. (Kwa maelekezo mengine tazama sura ya 15 ya Kanuni na Kawaida za Kanisa).

Mchungaji hana mamlaka ya kufungisha ndoa ya mtu aliyeachana kama kuachana kwake hakuruhusiwi na Maandiko Matakatifu. Kama wanaotaka kufunga ndoa ni wageni kwa mchungaji, yeye atachunguza habari zao kwa makini, ili ahakikishe kwamba hakuna vipingamizi dhidi ya ndoa hiyo kulingana na Biblia.

***Huduma na Utaratibu wa Ndoa*—**Bibi arusi atasimama kushoto kwa bwana arusi, na wote wawili wakimkabili mchungaji. Huduma inaweza kuanza kwa wimbo, na baadaye mafungu kutoka katika Maandiko Matakatifu yasomwe. Maneno yafaayo ni Waefeso 5:15-33. Kisha ombi la kuwepo kwa Bwana na baraka zake juu ya huduma hiyo hutolewa.

Kisha Mchungaji Atasema, “Wapenzi, tumekusanyika hapa mbele za Mungu na mbele ya mkutano huu, ili kuwaunganisha mwanamume huyu na mwanamke huyu katika ndoa takatifu, ambayo jambo la heshima, lililoanzishwa na Mungu wakati wanadamu walipokuwa hawana hatia, nalo linafananishwa na mwungano wa Kristo na kanisa lake. Jambo hili takatifu alilibariki na kuliheshimu

kwa kuwepo kwake, na kwa mwujiza wake wa kwanza alioufanya katika mji wa Kana ya Galilaya; na ndoa imesifiwa zaidi na mtume Paulo akisema kwamba haina budi kuheshimiwa na wote na imekusudiwa kuleta umoja zaidi na Bwana. Kwa hiyo isichukuliwe wala kufanuyika kwa namna isiyofaa, wala kwa haraka au kwa uzinifu na uasherati, bali kwa heshima, na kicho kwa Mungu, na ikumbukwe kwamba ndoa iliwekwa na Mungu kwa ajili ya kusaidiana na kufarijiana kwa kadiri ya mahitaji ya kila mmoja, katika siku za kufanikiwa na katika siku za taabu."

"Katika hali hiyo takatifu watu hawa wawili waliopo hapa mbele yenu wamekuja wapate kuunganishwa sasa kwa kicho cha Mungu, ili wakae pamoja siku zote bila kutengana. Kwa ajili hiyo, mtu ye yote akiweza kuonesha sababu inayoweza kufanya wasiunganishwe kihalali katika ndoa aseme sasa; vinginevyo, anyamaze milele."

Kama hakutakuwa na kipingamizi, mchungaji atawaambia bwana na bibi arusi:

"Ninawaagiza ninyi wawili, mjibu sasa kama mtakavyojibu siku ya hukumu, ambapo siri zote za mioyo zitafunuliwa, kama mmoja wenu anajua sababu au kipingamizi cho chote cha kuunganishwa kihalali katika ndoa, basi aseme sasa. Mjue hakika kwamba watu wo wote wanaofunga ndoa kinyume na vile ilivyoruhusiwa katika Neno la Mungu hawaunganishwi na Mungu; na ndoa yao si halali."

Kisha bwana arusi atatoa tamko hili kwa sauti ya kusikika akimfuatisha mchungaji:

*Nashuhudia kweli kwamba sijui pingamizi lo lote dhidi ya mimi (majina yote—fulani fulani bin fulani) kuunganishwa katika ndoa na (majina yote—fulani fulani binti fulani,).

Kisha bibi arusi naye atatoa tamko hili:

*Nashuhudia kweli kwamba sijui pingamizi lo lote dhidi ya mimi (majina yote—fulani fulani binti fulani) kuunganishwa katika ndoa na (majina—yote fulani fulani bin fulani).

Kisha mchungaji atamwuliza bwana arusi:

"Je, unamkubali mwanamke huyu kuwa mke wako uliyemwoa kihalali, na.kuishi naye katika hali takatifu ya ndoa kama ilivyoamriwa na Mungu? Je, utampenda, na kumfariji, na kumheshimu, na kumtunza, katika ugonjwa na katika afya; na kuwaacha wengine wote, ukidumu na yeye tu siku zote mtakazoishi?

Bwana arusi atajibu:

“Ndiyo, namkubali”

Kisha mchungaji atamwuuliza bibi arusi:

“Je, unamkubali mwanamume huyu kuwa mume wako aliyekuoa kihalali, na kuishi naye katika hali takatifu ya ndoa kama ilivyoamriwa na Mungu? Je, utampenda, na kumfariji, na kumheshimu, na kumtunza, katika ugonjwa na katika afya; na kuwaacha wengine wote, ukidumu na yeye tu siku zote mtakazoishi?”

Bibi arusi atajibu:

“Ndiyo, namkubali.”

Kisha mchungaji atauliza;

“Ni nani anayemtoa mwanamke huyu awe mke wa mwanamume huyu?”

Baba wa bibi arusi, au mlezi alivechaguliwa ataonesha ukubali wake kwa kusema—“Ni mimi.”

Ndipo bwana arusi atamshika mkono yule bibi arusi nao watafuatisha maneno yanayosemwa na mchungaji kama ifuatavyo:

*Nawasihi watu wote waliopo hapa, washuhudie kwamba mimi(majina yote—fulani fulani bini fulani) nakutwaa wewe (majina yote—fulani binti fulani) uwe mke wangu halali wa ndoa; niwe nawe na kuambatana nawe tangu sasa hata siku zote, katika hali njema na katika hali mbaya, latika utajiri na katika umaskini, katika ugonjwa na katika afya, nikupende na kukutunza, mpaka mauti itakapotutenganisha kulingana na amri takatifu ya Mungu; na katika mambo hayo nakupa ahadi yangu.”

Ndipo bibi arusi naye atafuatisha maneno yanayosemwa na mchungaji kama ifuatavyo:

* Nawasihi watu wote waliopo hapa, washuhudie kwamba mimi(majina yote—fulani fulani bini fulani) nakutwaa wewe (majina yote—fulani binti fulani) uwe mume wangu halali wa ndoa; niwe nawe na kuambatana nawe tangu sasa hata siku zote, katika hali njema na katika hali mbaya, latika utajiri na katika umaskini, katika ugonjwa na katika afya, nikupende na kukutunza, mpaka mauti itakapotutenganisha kulingana na amri takatifu ya Mungu; na katika mambo hayo nakupa ahadi yangu.”

*Maneno yenye alama hii (*) ni ya lazima katika kufunga ndoa kulingana na sheria ya nchi. Kisha mchungaji ataweka mkono wake juu ya mikono ya bwana na bibi arusi ambao watakuwa wameshikana mikono, na kusema:

"Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe. Kwa sababu (majina yote fulani fulani bin fulani) na (majina yote fulani fulani binti fulani) wamekubaliana kuishi katika hali ya maisha matakatifu ya ndoa, nao wameyashuhudia haya mbele za Mungu na mbele ya mkutano huu, na katika mambo haya wametoa ahadi na kujifunga kila mmoja kwa mwenzake, na wameyatangaza mambo hayo kwa kushikamana mikono, sasa mimi natangaza kwa mamlaka ya Neno la Mungu na sheria ya nchi kwamba wamekuwa mume na mke. Kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amina."

**Sala ya Baraka**

"Bwana awabariki, na kuwalinda; Bwana awaangazie nuru ya uso wake, na kuwafadhili; Bwana awainulie uso wake na kuwapa amani, sasa na hata milele, Amina."

***Kusajili Ndoa*****—**Katika nchi nyingine baada ya kufanya huduma ya ndoa, mchungaji hana budi kisheria kuandika maelezo ya ndoa hiyo katika hati ya serikali. Hati hii, pamoja na malipo yake haina budi kupelekwa serikalini katika muda uliowekwa kisheria.

Katika nchi nyingi inampasa mchungaji kuwapa hati zao za ndoa watu aliowafungia ndoa.

Katika nchi ambazo kisheria ndoa hufungwa na maofisa wa serikali walioteuliwa kwa kazi hiyo, baada ya kusajili ndoa, maarusi waende kanisani, na mchungaji atawafanyia huduma ya Kikristo kama ilivyoelezwa hapo juu.

***Mapambo kwenye Arusi*****—**Ingawa arusi ni jambo la furaha, shangwe/vigelegele vipatane na kawaida za kanisa. Ndugu wasishindane kwa mapambo ya gharama kubwa au kuandaa vyakula vingi kwa shughuli nyingi. Wachungaji waonyeshe mifano mizuri katika jambo hilo. Maarusi wasitumie jambo hili kama fursa ya kujitajirisha kutoka kwa rafiki zao.

Kwa sababu ya shughuli nyingi zinazoambatana na maandalizi na sherehe za arusi, ndoa zisifungwe siku ya Sabato.

***Familia ya Kikristo*—**Familia ya Kikristo ndiyo msingi wa Kanisa. Wachungaji na viongozi wa kanisa wahimize mafundisho yaliyotolewa kwa maarusi kuhusu familia ambayo Kristo anaweza kukaa ndani yake. Sala za asubuhi na jioni zidumishwe kama majukumu yao ya kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu na kanuni za kanisa.

Kushika Sabato kwa uangalifu kusisitizwe, pamoja na haja ya kumaliza kazi zote siku ya Ijumaa kabla jua kuchwa. Mwanzo na mwisho wa siku takatifu wawe na maombi nyumbani au kanisani.

***Talaka*—**Familia ya Kikristo ndiyo moyo wa kanisa. Kuwe na juhudi za kulinda familia zilizojengwa juu ya kanuni za Kikristo. Ikijulikana kwamba hali kati ya mume na mke imezorota, kutokana na makosa ya mmoja wao au ya wote wawili, basi mchungaji atafute kwa ushauri wenye busara kuwakumbusha juu ya ahadi zao mbele za Mungu na maombi, na kurudisha amani na mapatano nyumbani kwa kusameheana. Ikiwa juhudi zote zimeshindwa kuwapatanisha, basi jambo hilo litaletwa katika baraza la kanisa. Katika masuala ya talaka, kanisa lifuate maelezo yaliyo katika sura ya 15 ya *mwongozo* huu na mafundisho ya Biblia juu ya kutangua ndoa, kisha wahusika wataruhusiwa, kwenda mahakamani.

***Ndoa za Zaidi ya Mke Mmoja*—**Kusudi dhahiri la Mungu ni mtu kuwa na mke mmoja tu. Uasi wo wote dhidi ya kusudi hili huleta machafuko na kuhafifisha kanuni za Biblia zinazotawala jamii ya wanadamu, na hasa kanisa la Kikristo. Desturi ya kuwa na wake wengi miongoni watu wasio Wakristo tunaowahubiria injili katika makabila mengi, hupingana na kanuni za Kikristo, na huleta uharibifu ikiruhusiwa katika Kanisa la Kikristo. Kwa hiyo Kanisa letu limeshika maelekezo yafuatayo:

1. Mtu akiwa na wake wengi wakati injili inapomfikia, akibadilika moyo, basi atatakiwa kuitengeneza hali yake kwa kuwaacha wake zake wote na kubaki na mmoja tu, kabla hajahesabiwa kustahili ubatizo na kuingia katika ushirika wa kanisa.

2. Watu wanaowaacha wake zao hivyo, watatazamiwa kuwapatia mahitaji yao ya vitu vyote, pamoja na mahitaji na malezi ya watoto wao, kwa kadiri wanavyoweza kufanya.
3. Tunafahamu kwamba injili ikiwafikia watu katika nchi fulani waliooa wake wengi au pale ambapo desturi za mila na utamaduni humfanya mke aliyeachwa kuwa dhalili siku zote za maisha yake, na hata kuchukuliwa kuwa ni malaya, na kwa sababu hiyo pia watoto wake hudhalilishwa. Kwa masuala yote kama hayo, kanisa litashirikiana na yule mume katika kuwaandalia wale wake na watoto wao riziki zao za kuwatunza, na kuwalinda dhidi ya fedheha na mateso hayo.
4. Tunatambua na kukubali haki ya mke, aliyeachwa na mume mwenye wake wengi, kuolewa tena.
5. Wake za mtu walioolewa naye walipokuwa hawamjui Mungu, ambao baada ya kupokea imani ya Kikristo hawawezi kuachana na mume wao kutokana na sababu na desturi za kimila/utamaduni, wakipata kibali cha kamati ya konferensi, au union wanaweza kubatizwa na kupokelewa katika ushirika wa kanisa. Lakini mwanamke aliye mshiriki akiolewa kama mke wa pili au zaidi, ataondolewa katika ushirika wa kanisa, na hatapokelewa tena katika ushirika wa kanisa mpaka aachane na yule mume.

***Desturi za Tohara*****—**Ingawa katika desturi za tohara kuna mafundisho ya kawaida za kikabila, ili kuwandaa wavulana na wasichana kwa majukumu ya maisha yao watakapokuwa watu wazima, kwa sababu ya desturi na mila mbaya zinazoambatana na ushirikina wa kipagani, si vyema kabisa kwa vijana wa Kikristo kushiriki katika mambo hayo.

Kama ni lazima wavulana wetu watahiriwe kwa sababu za kiafya, basi waende kwa madaktari hospitalini. Kwa wasichana tohara ni desturi, mila, na utamaduni mbaya kabisa, nasi tunatamka kwamba tunakataza kabisa jambo hilo.

Mafundisho yaliyotolewa kwa vijana wetu wa kiume na wa kike katika Chama cha Vijana wa Kiadventista yatawaandaa wavulana na wasichana wetu kutimiza wajibu wao katika jamii.

**Viongozi wa Kanisa**

Viongozi wa kanisa huchaguliwa kila mwaka. (Taz. sura ya 6 ya *mwongozo* huu). Hakuna sababu ya mtu kuchaguliwa ili adumu katika kazi fulani siku zote bila kubadilishwa. Ili kuhakikisha kwamba kazi ya kanisa inatendeka vizuri, inashauriwa kuwa viongozi wote waliochaguliwa upya wapewe semina kuhusu nyadhifa na kazi zao kabla hawajaanza kuzitenda. Wajibu wa kuendesha semina hizo ni wa konferensi.

**Ugomvi Kati ya Ndugu**

Tabia ya washiriki wa kanisa kwenda kwenye mahakama za kiraia kwa sababu ya matatizo kati yao, ni kinyume cha mafundisho ya mtume Paulo. “Je, mtu wa kwenu akiwa ana daawa juu ya mwenzake athubutu kushitaki mbele ya wasio haki, wala si mbele ya watakatifti? ... basi imekuwa upungufu kwenu kabisa kwamba mnashitakiana ninyi kwa ninyi” (I Wakorintho 6:1,7).

Washiriki wasioweza kutatua matatizo kati yao, wasihiwe sana kupeleka masuala yao kanisani na kukubali uamuzi wa ndugu zao.

**Utunzaji wa Pesa za Kanisa**

Inashauriwa kwamba wote watumiao pesa za Bwana watunze pesa za kanisa kwa uangalifu sana. Mhazini wa kanisa afundishwe vizuri namna ya kuandika taarifa zake na kuzituma kwa viongozi wa konferensi kama inavyotakiwa.

Ni lazima stakabadhi zitolewe kwa pesa zote zinazopokelewa na kanisa, na pawe na nakala moja inayowekwa tayari kwa ajili ya ukaguzi. Kama ofisa ye yote au mtu mwingine atachukua pesa za kanisa bila idhini, basi ataachishwa wadhifa wake mara moja. Kama ni mtumishi wa kanisa, jina lake litapelekwa kwenye kamati ya konferensi. Ni wajibu wa mzee wa kanisa au kiongozi wa kundi, kuhakikisha kwamba sadaka maalum zinatangazwa na kukusanywa kwa wakati wake. Wakati zaka na sadaka zinapokusanywa na mashemasi siku ya Sabato, sala fupi maalum itolewe kabla au baada ya kukusanywa, kumshukuru Mungu kwa baraka zake. Kuwe na mashemasi katika kila kundi kwa ajili ya kupokea zaka ya Bwana. Zaka za vitu kama vile ng’ombe, kondoo, mbuzi, kuku, nafaka

na mazao ya shambani, zihesabiwe kuwa takatifu kwa Bwana sawasawa na pesa. Kanisa liandae mahali pazuri pa kutunzia zaka za namna hiyo, kama vile ghala au zizi. Mashemasi wawili au zaidi washirikiane katika kuuza zaka za aina hiyo kwa bei iliyo katika soko wakati huo. Mtu asitumie hii kama nafasi ya kununua zaka ya Bwana kwa bei ya chini.

Sadaka za Shule ya Sabato zithibitishwe na kiongozi wa Shule ya Sabato na katibu wake, na ikiwa kuna tofauti kati ya pesa na hesabu iliyoandikwa na mwalimu katika taarifa ya kikosi, suala hilo lichunguzwe mara moja.

Vyombo maalum vinavyofaa viandaliwe kwa ajili ya mashemasi kukusanyia sadaka za watu wa Mungu siku ya Sabato. Tabia ya kukusanya sadaka kwa kuziweka juu ya kitabu au ndani ya kofia haifai katika nyumba ya Bwana. Ofisa, shemasi, au mwalimu wa Shule ya Sabato asiiweke sadaka katika mifuko yake. Mhazini wa kanisa awe na shemasi mmoja au zaidi kama mashahidi wakati wa kuhesabu pesa zote zilizokusanywa.

Sadaka ya Mavuno ipelekwe kwa mhazini wa kanisa mara moja. Ni wajibu wa kiongozi Huduma mahususi kuhakikisha kwamba vishina vya stakabadhi zote za sadaka hiyo na vipeperushi vinavyotumiwa, vinarudishwa kanisani baada ya muda ulioruhusiwa kuomba Sadaka ya Mavuno kumalizika.

**Kitabu cha Orodha ya Washiriki**

Ushauri umetolewa kwamba kitabu kilichoandaliwa na Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati ndicho kitumiwe kwa ajili ya kuorodhesba majina ya washiriki wa Kanisa. Ikiwezekana majina yachapwe, na kama haiwezikani kuchapa, yaandikwe kwa herufi kubwa, kwa mfano, PAULO MASHAURI. Kitabu hiki kitunzwe katika sanduku au kabati lenye kufuli. Mara kwa mara majina yakaguliwe na mkuu wa konferensi, au katibu wake, kuhakikisha kwamba idadi ya washiriki iliyo katika kitabu ni sawa na ile iliyotumwa konferensi.

Mshiriki akiondolewa katika ushirika wa kanisa kwa kura ya kanisa, karani wa kanisa atamwarifu kwa kumwandikia barua.

**Vyeti vya Ushirika**

Mtu anapoingia katika madarasa ya kujiftinza Biblia au katika ushirika wa kanisa, atapewa moja kati ya vyeti vifuatavyo:

1. Cheti cha darasa la ubatizo.
2. Akibatizwa, Cheti cha Ubatizo.
3. Kadi ya Ushirika.

Baadhi ya vyeti hivi vina sehemu ya kuandika kumbukumu ya zaka ya mtu kwa nyuma. Cheti cha ubatizo kina imani za msingi au ahadi zilizotolewa na mtu aliyebatizwa. Kadi ya ushirika ni ya miaka miwili. Wataradhia wa ubatizo wataweka sahihi zao katika vyeti mbele ya washiriki, kabla ya kubatizwa.

***Madarasa ya Ubalizo***—Imeonekana kwamba mtu anayetaka kuwa mshiriki wa kanisa anahitaji kufundishwa kwa takriban miaka miwili hivi, lakini si lazima kwa watu waliokuwa Wakristo kwa muda mrefu, ambao wameyajua mafundisho makuu ya Kanisa kwa njia ya masomo ya Sauti ya Unabii au kwa kusoma vitabu na magazeti yetu. Inashauriwa kwamba, mtu abatizwe wakati ameandaliwa vyema.

Wale walio katika madarasa ya kujifunza Biblia hawana budi kutumia kitabu cha mafundisho ya Biblia kinachofaa kwa darasa lao. Kiongozi wa mtaa afuatilie mara kwa mara jinsi madarasa haya yanavyoendeshwa na kuona maendeleo ya wanafunzi.

Kila mwanafunzi anayejua kusoma atiwe moyo wa kununua kitabu chake mwenyewe cha mafundisho ili apate kuyaelewa mafundisho darasani kwa kujifunza mwenyewe nyumbani.

***Darasa la Mafundisho ya Biblia kwa Washiriki***—Inashauriwa kwamba baada ya ubatizo, washiriki wapya waingie darasa maalum kuwasaidia kuelewa zaidi wajibu wao kama washiriki. Mchungaji au mzee wa kanisa asimamie mafundisho haya naye afuatishe masomo yaliyoandaliwa kwa kusudi hili.

**Kuunda Kanisa**

Washiriki wafahamu kwamba maombi ya kuunda kanisa huambatana na majukumu fulani. Waelekezwe kujenga jengo la kanisa litakalodumu miaka mingi kulingana na majengo mengine

yanayotumiwa katika nchi yao na kwa gharama wanazoweza kuimudu. Ramani za majengo hayo zitumwe kamati ya union ili ziidhinishwe.

Makanisa yaliyoundwa ipasavyo yasikusanyike katika madarasa ya Shule kwa ajili ya ibada, isipokuwa kama hali inalazimu.

Kabla kanisa halijaundwa, mchungaji au kiongozi wa mtaa atoe semina kwa wale watakaokuwa viongozi wa kanisa. Washiriki wachange pesa kwa ajili ya kununulia vyombo na vitu vingine vinavyohitajika kwa huduma ya Meza ya Bwana. Ikiwa kanisa lao litagawanyika kuwa makanisa mawili, basi kila kanisa lipewe mgawo wa sehemu ya vyombo vya kutumia. Utaratibu wa kuunda kanisa umeelezwa katika *Mwongozo* huu sura ya 5.

**Huduma ya Kutawadhana Miguu**

Kristo alianzisha huduma hii kuwaandaa watu kwa ajili ya Meza ya Bwana. Huduma hii husaidia washiriki kuondoa kiburi, fitina, na kupenda makuu; maana tukiwa na mambo hayo moyoni, hatuwezi kushirikiana na Kristo. Huduma hii pia ni ukumbusho wa jinsi Mwokozi alivyojinyenyekeza, naye ameifanya kuwa huduma takatifu.

**Huduma ya Meza ya Bwana**

Huduma ya Meza ya Bwana ilianzishwa na Kristo kuwasaidia wafuasi wake waikumbuke na kufahamu vizuri dhabihu yake ilyotolewa kwa ajili yao. “Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu” (Luka 22:19). Waadventista wa Sabato hawakatazi washiriki wa madhehebu mengine ya Kikristo kushiriki Meza ya Bwana wakitaka kushirika. Hii inamaanisha kuwa tunaamini Meza ya Bwana ni kwa ajili ya Wakristo wote.

Kwa msingi huo huo, hatuwakatazi washiriki wetu walio katika karipio kushiriki Meza ya Bwana kama wataonesha toba ya kweli.

Kwa kawaida watu walio katika darasa la ubatizo, ambao hawajawa washiriki, hawawezi kushiriki Meza ya Bwana.

Ili kudumisha moyo wa kicho kwa Mungu, inashauriwa kwamba mahali ambapo kuna watu wengi wasio washiriki huduma ya Meza ya Bwana ifanyike mchana au wakati mwingine unaofaa.

Mashemasi wa kike wanatarajiwa kutengeneza mkate na divai, na kuandaa Meza. Baada ya huduma mkate na divai ilyobaki vitamwagwa kwa staha.

**Jinsi ya kutengeneza mkate usiotiwa chachu (kwa kanisa dogo).**

vifaa:

Vikombe vitatu vya unga (ngano) mweupe, nusu kikombe cha maziwa au maji, chumvi kidogo na maji kidogo mengine.

Weka unga katika sahani, ongeza chumvi, changanya sana na maziwa au maji; kisha nyunyiza maji baridi juu yake, mpaka umekuwa mzito.

Kanda kwa dakika kumi na tano hivi. Kisha sukuma kuwa na mraba wa takriban sentimeta 10 x 10. Chora mistari kwa kisu au uma na kutengeneza miraba midogo ya sentimeta 1 x 1 kurahisisha uvunjaji na kuzuia malengelenge. Weka juu ya sahani za chuma zilizonyunyiziwa unga, na kuoka kwa moto mkali na angalia usiunguze.

**Jinsi ya Kutengeneza Divai Isiyochachuka**

Nunua zabibu mbichi au kavu. Tabua zabibu kutoka shina, na tokosa zabibu katika sufuria mpaka zichemke. Chuja kwa kitambaa. Kisha chemsha kwa dakika tano. Kabla kuchemka kabisa, engua povu lote lililopanda juu. Baada ya kuchemka kabisa, weka katika chupa safi ya kioo isiyo na chachu, na zilizopashwa moto ili zisivunjike. Acha kiasi cha sentimeta moja kabla ya juisi kufika kwenye kizibo, kisha funika vizuri. Kata kipande cha kizibo kikichotokeza juu na usilibe kwa nta. Hifandhi mahali penye baridi, bila kuzihamisha hamisha mara nyingi.

**Utunzaji wa Vyombo**

Ni wajibu wa kila kanisa lililoundwa, kununua vyombo vinavyofaa kwa huduma ya Meza ya Bwana.

Ni kazi ya mashemasi wa kike kufua na kupiga pasi vitambaa vya meza na vitambaa vya kufutia miguu na mikono. Vifaa vyote vitakaushwa vizuri na kuhesabiwa kuona kama vyote vipo kabla ya kuwekwa katika sanduku lenye kufuli.

**Utaratibu wa lbada ya Meza ya Bwana**

Kwa kawaida saa moja inatosha kwa ibada ya asubuhi siku ya Sabato. Mambo yake yaandaliwe vizuri na mzee wa kanisa au kiongozi. Washiriki wasicheleweshwe kwa kungojea mwanzoni mwa ibada kwa sababu ya kushauriana juu ya masuala ya huduma katika chumba cha maandalizi kanisani. Kila inapowezekana matangazo yatolewe kabla ya ibada kuanza. Jitihada zifanywe kuanza huduma kwa saa yake kamili. Utaratibu huu wa ibada ufuatao hufaa kwa mahitaji ya watu wa Mungu katika ibada yao:

1. Ombi la moyoni wahudumu wanapoingia mimbarani
2. Wimbo wa kumsifu Mungu, watu wote wakisimama
3. Sala fupi
4. Wimbo wa kufungua huduma
5. Somo la Maandiko Matakatifu
6. Sala
7. Wimbo wa Kwaya au muziki wa pekee
8. Zaka na Sadaka (Ziwekwe katika bahasha
9. Sala fupi ya shukrani kwa baraka ya Mungu
10. Hubiri
11. Wimbo wa kufunga ibada
12. Ombi la mwisho
13. Kanisa kusimama au kukaa kwa muda mfupi na kuomba kimyakimya
14. Mashemasi wafanye bidii kuona kwamba pana utulivu na kumcha Mungu, watu wasitembee-tembee kanisani.

**Kuketi Wakati wa Kuomba**

Maneno haya yafuatayo yanaonesha utaratibu wa kuomba, isipokuwa mahali ambapo watu wamebanana au mahali penye majimaji. "Katika ibada ya pamoja au ya binafsi, inatupasa kupiga magoti mbele za Bwana tunapopeleka maombi yetu kwake. Yesu ambaye ni kielelezo chetu, alikuwa anapiga magoti na kuomba. (Luk. 22:41) Paulo alisema, "Kwa hiyo nampigia Baba Magoti. … (Efe. 3:14) Daniel alikuwa anapiga "magoti mara tatu kila siku, akasali, akashukuru mbele za Mungu wake." (Dan. 6:10) Prophets and Kings, uk.48.

**Kipindi cha Idara ya Huduma Mahususi**

Inatarajiwa kwamba mzee wa kanisa au kiongozi wa idara hii atahakikisha kuwa dakika kumi zimetengwa kati ya mwisho wa shule ya Sabato na mwanzo wa mahubiri kwa ajili ya idara ya huduma mahususi. Kipindi hicho ni cha kupokea taarifa ya huduma mahususi, na kutoa fursa kwa watu kutoa ushuhuda mfupi wa jinsi walivyoshuhudia katika kuongoa watu wengine. Pia malengo na mipango ya idara siku za usoni itangazwe, na kama kuna vijizuu na magazeti vitolewe kwa ajili ya kuwagawia watu wengine.

**Mkutano wa Maombi**

Maelezo yaliyotolewa katika *mwongozo* huu kuhusu mkutano huo yazingatiwe sana. Mkutano huo si wa mahubiri. Hivyo juhudi nyingi zifanyike kuwafanya washiriki wahudhurie. Kuwe na muda wa kutosha wa maombi na ushuhuda.

**Kuhamisha Washiriki**

Mara kwa mara washiriki waelekezwe wajibu wao wa kuhakikisha kwamba ushirika wao uko katika kanisa la mahali wanapoishi. Maelezo ya kuhamisha washiriki yapo katika *mwongozo* Huu. Yazingatiwe sana.

Endapo mshiriki atakuwa hajaelewa na kuona haja ya kuomba kuhamisha ushirika, kanisa lenye ushirika wa mtu aliyehamia mahali pengine, ikipita miezi sita lifanye mwasiliano naye kuwezesha barua ya uhamisho itolewe.

Inawapasa makarani wa kanisa kuhakikisha kwamba maombi ya uhamisho yanafanywa upesi. Barua ipelekwe kwa njia ya posta na isichukuliwe na mshiriki mwenyewe. Vivyo hivyo sehemu ya pili ya barua hio inayoonesha kupokelewa kwa mshiriki huyo irejeshwe upesi kwa lile kanisa analotoka. Baada ya kukamilisha mchakato wote huu barua za uhamisho zote zitunzwe na karani wa kanisa kwa ajili ya ukaguzi wa mchungaji au kiongozi wa konferensi mwisho wa mwaka.

Kila mshiriki anaposafiri hana budi kuwasiliana na kanisa lake mara kwa mara na kutuma zaka na sadaka zake.

Juhudi za kila aina zifanyike kuwatafuta washiriki wasiojulikana

walipo na kuwasiliana na makanisa waliyo karibu nayo. Kama mshiriki hajulikani alipo baada ya miaka miwili kanisa linaweza kupendekeza jina lake liondolewe, na kuandika katika kumbukumbu kwamba haiwezekani kujua mahali alipo.

***Mwenendo wa Kikristo*****—**Wakristo waepuke na mionekano mibaya katika uhusiano kati ya wa wanaume na wanawake. Watenda kazi na viongozi wa kanisa wana wajibu wa pekee katika kulinda na kuimarisha destri njema na usafi wa kanisa. Mchungaji ye yote akianguka katika zinaa, hastahili tena kuwa katika jamii ya wachungaji. Lakini anaweza kupewa kazi nyingine isiyo kichungaji au uinjilisti akionesha badiliko la moyo na mwenendo kwa muda wa kutosha.

**Mikutano ya Makambi**

Mikutano ya watu wa Mungu kila mwaka hufuata desturi ya Biblia katika zama za kale. Mikutano ya makambi ikusudiwe kuamsha roho za watu na kuliamsha kanisa. Ni vyema mahubiri ya uinjilisti yafanyike kabla ya makambi ili waumini wapya wapate kushiriki katika karamu hii ya kiroho.

Eneo la makambi lichaguliwe kwa uangalifu na maandalizi yafanywe ili watu wazingatie mafundisho ya Neno la Mungu bila kuvsumbuliwa na mambo mengine. Ni vizuri kujenga ua wa mabua au majamvi ili watu wahudhurie siku zote.

Ili kufanikisha makambi mambo yafuatayo yafanyike:

Kipindi cha maombi ya asubuhi katika vikosi vya maombi na kutoa ushuhuda.

Mafundisho ya Biblia asubuhi na alasiri. Kipindi kimoja kwa ajili ya kila idara kanisani k.m. Shule ya Sabato, huduma mahususi, Chama cha Vijana wa Kiadventista, Uinjilisti wa Vitabu, Elimu, Sauti ya Unabii, Afya na Kiasi. Kipindi cha wazazi, vijana na watoto. Banda la kuonesha na kuuza vitabu na magazeti litayarishwe. Na pia muda wa wahudumu kutoa ushauri kwa washiriki binafsi, ili kuwasaidia katika masuala nyeti ya kiroho, uwekwe katika ratiba ya makambi.

**Huduma ya Mazishi**

(Mchungaji, mzee wa kanisa, au shemasi anaweza kufanya huduma hii). Ushauri umetolewa kwamba, kadiri inavyowezekana, mazishi yafanywe siku isiyo ya Sabato. Lakini kama ni lazima kufanya mazishi siku ya Sabato, basi watu waangalie ili mazishi yasizuie huduma za kawaida katika nyumba ya Mungu. Washiriki na watu walio katika madarasa ya ubatizo wafundishwe kwamba wakati wa huduma ya mazishi ya Kikristo tunaweza kuonesha kwa utulivu imani yetu katika ahadi ya siku ya ufufuo wakati wa kuja kwa Bwana Yesu Kristo; na kwa hiyo haifai, wala si vizuri kufuata mila na desturi za wasioamini katika kuomboleza kwa ajili ya marehemu.

***Huduma Kanisani*—**Watu wakiisha kuketi kanisani omba sala fupi ya kwamba Mungu afariji kila mtu kwa ahadi yake ya ufufuo, na hivyo kuondoa giza liletwalo na mauti. Kisha mafungu ya Maandiko Matakatifu yatasomwa, machache ama mengi, kwa kadiri ya umri na maisha ya marehemu. Kwa kawaida somo litakuwa na mafungu yafuatayo:

"Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke, siku zake za kuishi si nyingi, naye hujaa taabu. Yeye huchanua kama vile ua, kisha hukatwa; hukimbia kama kivuli, wala hakai kamwe ... Mtu akifa, je, atakuwa hai tena? Mimi nitangoja siku zote za vita vyangu, hata kufunguliwa kwangu kunifikilie. Wewe ungeita, nami ningekujibu; ungekuwa na tamaa ya kazi ya mikono yako" (Ayubu 14:1,2,14,15).

"Wewe, Bwana, umekuwa makao yetu, kikazi baada ya kizazi. Kabla haijazaliwa milima wala hujaiumba dunia, na tangu milele hata milele ndiwe Mungu. Wamrudisha mtu mavumbini, usemapo, rudini, enyi wanadamu. Maana miaka elfu machoni pako ni kama siku ya jana ikiisha kupita, na kama kesha la usiku ... Siku za maisha yetu miaka sabini, na ikiwa tuna nguvu miaka themanini, na kiburi chake ni taabu na ubatili, maana chapita upesi tukatokomea mara ... Basi, utujulishe kuzihesabu siku zetu, tujipatie moyo wa hekima" (Zaburi 90:1-4,10,12).

"Angalieni nawaambia ninyi siri, hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu

watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa Mauti imemezwa kwa kushinda. Ku wapi, Ewe mauti kushinda kwako? U wapi, ewe mauti uchungu wako? Uchungu wa mauti ni dhambi na nguvu za dhatnbi ni torati. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo" (I Wakorintho 15:5157).

Ni vyema kutoa historia kidogo ya marehemu. Baada ya hapo kuwe na hubiri fupi. Simulia maisha ya Kikristo ya marehemu kuwasaidia walio hai, ukionesha tumaini lenye baraka na hakika ya kumshinda adui wa mwisho ambaye ni mauti. Sisitiza ahadi za injili zinazowafariji wenye huzuni na tangaza ujio wa pili wa Kristo kama "tumaini lenye baraka" la vizazi vyote.

Kisha sala fupi ifuate, yenye shukurani kwa wema wote wa Mungu kwa marehemu, kwa matumaini kwamba hakuna cho chote katika vipawa vizuri vya Mungu kitakachopotea, ya kuwa katika siku ya ufufuo vitu vyote vyema vinavyoondolewa sasa vitarudishwa, na kwamba mateso yote ya hapa duniani yakoma kabisa. Omba kwamba watu wote watambue ufupi wa maisha, wakiona kweli ubatili wa mambo yote ya dunia, na uhakika wa ufufuo, ukionesha mambo ya hakika ya milele, ili watu wote waliopo ambao wangali dhambini waamke. Ombea familia ya marehemu na ndugu zake waliobaki; tena ombea kazi ya injili duniani iishe na mwenye kutoa uzima arudi upesi na kuleta kutokufa. Kisha kuwe na wimbo, na ombi la baraka na kufunga huduma.

***Huduma ya Mazishi Kaburini—***Maiti inaposhushwa kaburini mhudumu atasoma Maandiko Matakatifu yafuatayo:

"Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi ajapokufa atakuwa anaishi" (Yohana 11:25).

"Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai, nami nalikuwa nimekufa, na tazama ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu" (Ufunuo 1: 17,18).

"Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao" (Ufunuo 14:13).

"Lakini ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake, Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya Malaika mkuu na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo" (I Thes.4:13-18).

***Kuweka Maiti Kaburini*—**Mhudumu atasema maneno haya: "Kwa sababu imempendeza Mwenyezi Mungu katika upendo wake na hekima yake kumruhusu ndugu yetu mpenzi alale katika Kristo, nasi kwa moyo wa huruma twaweka mwili wake ardhini; udongo kwa udongo, majivu kwa majivu, mavumbi kwa mavumbi; katika tumaini la hakika, lisilo na shaka katika ufufuo wa uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu; ambaye wakati wa ufunuo wake wa utukufu "ataubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake" (Wafilipi 3:21).

Kisha mhudumu atatamka: "Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile, kiti cha enzi ikisema, Tazama, masikani ya Mungu ni pamoja na wanadainu, naye atafanya masikani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufunuo21:3,4). Kisha ataunga kwa ombi.

**Muundo wa Kanisa**

Kulingana na maneno yaliyotangulia yanayotoka katika Roho ya Unabii, inaeleweka kwamba mahali ambapo makanisa katika fildi moja hayajafikia hadhi ya kuwa konferensi, yaani, yakiwa-yangali

katika hadhi ya fildi hayawezi kuchagua mwenyekiti, katibu wala mhazini wa fildi. Maofisa hawa huchaguliwa na kamati ya 'Union' yao ambapo wao kama fildi huwa na wajumbe kwenye kamati hiyo kwa mujibu wa sera.

Lakini ni vyema fildi ziwe konferensi mara zinapoweza kubeba jukumu la madaraka ya uongozi wa kanisa ambalo kwa kawaida hubebwa na konferensi.

**Pesa za Kundi**

Mhazini wa kundi ataandika kwa uangalifu hesabu za pesa zote za mapato na matumizi. Mwishoni mwa kila mwezi atatuma zaka na sadaka zote pamoja na michango yote iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya kanisa kwa mhazini wa kanisa, naye atazituma kwa njia inayokubalika kwa mhazini wa konferensi, ambaye pia ni mhazini wa kanisa la konferensi.

***Pesa za Shule ya Kanisa*—**Katika fildi ambazo bado hazijawa konferensi zinazoendesha shule ya kanisa, pesa zote za shule ya kanisa hutumwa moja kwa moja kwa mhazini wa fildi kwa ajili ya malipo ya baadaye kulingana na maelekezo ya kamati ya fildi.